**3 JUNI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 3 Juni, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Ifuatayo Iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Tunaendelea.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali. Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 501

### Mafunzo kwa Vijana Wanaokopa Mfuko wa Maendeleo

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa mafunzo ya ujasiriamali kwa kiasi gani kwa vijana kabla hawajapatiwa mikopo kutoka kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Patrick.

**SPIKA:** Mheshimiwa subiri kidogo, naambiwa kisemeo chake wakati akiuliza kilikuwa kimezimika.

Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, uliza upya swali lako, rudia.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, naomba nipate majibu ya swali langu, Namba 501, kutoka Serikalini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuwaandaa vijana kabla ya kupatiwa mikopo, vijana wamekuwa wakipatiwa mafunzo ya ujasiriamali, uanzishaji wa miradi, usimamizi na uendelezaji, urasimishaji na pia, kuunganishwa na huduma wezeshi kupitia taasisi za fedha na benki, mamlaka za kodi, mamlaka za uendeshaji viwanda vidogovidogo *(SIDO)*, huduma za udhibiti usalama na viwango *(TBS, OSHA* na *TMDA)* na huduma za hifadhi ya jamii. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 jumla ya vijana 2,685 walipatiwa mafunzo haya katika Mikoa ya Dodoma, Kagera, Manyara, Kigoma, Shinyanga, Mwanza na Arusha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Prof. Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Vijana wetu ni nguzo muhimu sana katika Taifa letu. Je, ni kwa nini Serikali isitenge fedha nyingi za kutosha na kuziweka katika mfuko huu, ili zisaidie vijana wetu kutatua changamoto zao ambazo wanakabiliana nazo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, kuna mfumo gani wa kufuatilia vijana wanaopata fedha katika mfuko huu kuangalia kama wamepata changamoto gani au mafanikio gani kutokana na fedha wanazopatiwa katoka katika mfuko huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, ni kweli kwamba, kuna umuhimu ambao tuliuona, kama Serikali, kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba, kundi la vijana ndio nguvu kazi ya Taifa kwa mujibu wa majibu ya sensa ambayo tuliyapata. Katika kufanya hivyo, Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja ni kuhakikisha kila Wizara inakuwa na fungu maalum, kwa ajili ya shughuli za vijana na kwa kuanza na Ofisi ya Waziri Mkuu tunayo shilingi bilioni moja kila mwaka wa fedha kuweza kuhakikisha vijana hawa wanakopeshwa. Tunayo Wizara ya Madini ambayo imeanzisha program maalum ya *Mining for Better Tomorrow* ambayo nayo inalenga katika kuwasaidia vijana wachimbaji wadogowadogo na kuwawezesha kimtaji.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo, Wizara ya Michezo kuna fedha ambazo Watanzania wote ni mashihidi kupitia Dkt. Samia Suluhu Hassan na Bunge hili zimekuwa zikipitishwa, kwa ajili ya kuwakopesha vijana walio kwenye kazi za sanaa. Hata kwenye michezo mmeona timu zetu zilikuwa zinapata mkono wa mama kwa namna mbalimbali na mmeona jinsi ambavyo, Simba imefanya vizuri zaidi na Yanga nao walikuwa wanufaika wa fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, pia, katika Wizara nyingine ipo Wizara ya Kilimo nayo pia, ina programu maalum ya *Building Better Tomorrow,* kwa ajili ya vijana. Katika fedha, sasahivi tumeenda kutenga bajeti zaidi ya shilingi trilioni moja ambayo wanufaika ndani ya bajeti hiyo ni vijana.

Mheshimiwa Spika, pia, katika kila Wizara zimewekwa fedha, kwa ajili ya vijana kwa sababu, tuliona ukiziweka kwenye kapu moja hauwezi kuwasaidia kwa urahisi zaidi. Kwa hiyo, mahususi tumeweka kwenye Wizara za Kisekta, ili kuweza kuwafikia walio wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ameuliza kuhusiana na…

**SPIKA:** Kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa kifupi. Kuhusiana na kama tunafanya ufatiliaji; la kwanza ipo, ndio kwenye mwongozo tunafanya ufatiliaji, kwanza, kuwajengea uwezo kabla ya kuwakopesha.

Pili, baada ya kuwajengea uwezo tunawashauri pia, kwenye maandiko yao ya mradi ni namna gani ambavyo tunaweza tukawapa fedha na tatu tunatoa hiyo mikopo na mwisho tunafanya tathmini na ufatiliaji, ili kuweza kuona kwamba, wanakidhi yale matakwa waliyoombea ile fedha na kuweza kuwasaidia. Tunafanya kazi ya *mentorship* kuweza kuwasaidia vijana hawa waweze kujitegemea, kujiajiri, kuajiriwa na zaidi kuweza kuchangia katika Pato la Taifa na uchumi kwa sababu, Serikali ya Awamu ya Sita inaheshimu sana nguvu kazi ya Taifa ambayo ni vijana kwa sehemu kubwa. Kwa hiyo, mipango iko mingi na mikakati, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 502

**Kupandisha Hadhi Mji Mdogo wa Mbalizi**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi ya Mji Mdogo wa Mbalizi kuwa Halmashauri ya Mji wa Mbalizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mahitaji na umuhimu wa kuanzisha maeneo ya kiutawala, ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Aidha, uanzishaji wa maeneo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287 na Mamlaka za Miji, Sura ya 288, pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo, ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadae kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa, ikiwemo mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ina watumishi wote katika idara zote kama ilivyokuwa Halmashauri na pia, kuna vitongoji kama Kitongoji cha Mbalizi chenyewe kina watu zaidi ya 54,000. Je, Serikali haioni umuhimu wa kupandisha hadhi na kuipa Mbalizi kipaumbele inaposubiria mipangilio ya maeneo mengine?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, ni kwa nini Serikali isifanye marekebisho ya mipaka ya vitongoji vya Utengule, Usongwe, ambavyo haviingiliani vinakuwa vinaingiliwa na vijiji vya kata nyingine? Je, Serikali haioni umuhimu wa kurekebisha mipaka hasa tunapoelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Njeza kwa namna ambavyo amefuatilia suala la kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kuwa Halmashauri ya Mji. Namhakikishia kwamba, Serikali inatambua sana umuhimu wa Mamlaka ya Mji

Mdogo wa Mbalizi kuwa, Halmashauri ya Mji wa Mbalizi. Ndio maana ilianzisha mamlaka hii, lakini tunafahamu kwamba, pia, inakidhi vigezo kwa idadi ya watu pia, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia kwamba, tumeweka kipaumbele kama Serikali kwamba, tukamilishe kwanza maeneo ya utawala yaliyopo kwa sababu, bado yana mapengo mengi ya ofisi za utawala pia, yana mapengo mengi ya watumishi, wakuu wa idara, nakadhalika. Baada ya kukamilisha tutahakikisha kwamba, tunatoa kipaumbele cha hali ya juu kwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kupata hadhi ya kuwa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kuhusiana na changamoto ya mipaka katika vijiji hivyo, natumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuchukua hatua za kuitisha Kikao cha *DCC,* kupitia Mheshimiwa *DC* wa Mbeya, pamoja na kuanzisha *RCC* na kuleta Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ajili ya marekebisho ya mipaka hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mamlaka ya Mji Mdogo Namanyere ilikidhi vigezo na vimepitia hatua zote. Ni lini mtatekeleza takwa la kisheria kuipandisha hadhi kuwa, Halmashauri ya Mji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba, tunafahamu Mamlaka ya Mji Mdogo Namenyere walishafikia hatua za kuleta taarifa rasmi na vikao rasmi vilikaa. Kwa hiyo, nawaomba

wanannchi wa Namenyere pamoja na Mheshimiwa Mbuge tuwe na subira kwa sababu, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na Halmashauri ya Mji Mdogo Namanyere ni suala la muda, tukifika hatua za utekelezaji, basi tutatoa kipaumbele pia, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Swali la 503 tutalirejea. Mheshimiwa Nikodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, sasa aulize swali lake.

Na. 504

**Kuwapatia Bodaboda Mikopo**

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuwapatia Bodaboda mikopo midogomidogo itakayowasaidia kuwainua kiuchumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kundi la waendesha pikipiki kibiashara wanaojulikana kwa jina la bodaboda tayari lilianza kunufaika na mikopo ya asilimia 10 inayoratibiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambapo katika mwaka 2022/23 Mamlaka za Serikali za Mitaa zilitoa mikopo kwa vikundi 5,217 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Aidha, kati ya vikundi hivyo, vikundi 589 vilikuwa ni vikundi vya bodaboda venye jumla ya wanachama 3,096 sawa na asilimia 11 ya vikundi vyote vilivyonufaika na mkopo wa shilingi bilioni 8.63

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuratibu na kuhakikisha wafanyabiashara ndogondogo, wakiwamo bodaboda, wanajisajili kupitia mfumo wa wafanyabiashara ndogo pamoja na kuhakikisha mwongozo wa uratibu na usimamizi wa wafanyabiashara

ndogondogo (machinga) na huduma zisizo rasmi unasambazwa kwenye mamlaka za Serikali za mitaa kote nchini ifikapo Julai, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini Mwaka 2022 na 2023 Mbogwe bodaboda hawakupata hii mikopo. Sasa wewe kwa kuwa, ni msimamizi mkuu wa hizi Halmashauri kauli yako ni ipi, ili kusudi bodaboda walio na vikundi Mbogwe waweze kunufaika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Upo tayari kuongozana na mimi baada ya Bunge hili, ili kusudi ukakutane na changamoto iliyopo Wilayani Mbogwe kwa vikundi vya watu wenye ulemavu na akina mama, ambavyo havinufaiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Maganga amefuatilia mara kwa mara kuhusiana na mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu yakiwemo makundi ya bodaboda.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kutoa ufafanuzi kidogo kwamba, mikopo hii haijawa *specific* kwamba, bodaboda ni lazima wakopeshwe, lakini kama wanaangukia kwenye kundi la vijana, basi wanakopa kama vijana kupitia kundi lao la bodaboda. Kwa hiyo, natumia nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbogwe kama kuna vikundi vya bodaboda ambavyo vinakidhi sifa ya kupata mikopo ya asilimia 10 wahakikishe wanawapa mikopo hiyo, ili vikundi vya bodaboda viweze kunufaika kama ilivyo malengo ya Serikali na kama ambavyo imenufaisha katika Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili. Niko tayari kufuatana na wewe Mheshimiwa Mbunge. Tutakubaliana kipindi hiki tupange ratiba, ili baada ya Bunge tuweze kwenda kukagua vikundi hivyo pia, kuhamasisha vikundi vile ambavyo vinahitaji mikopo ya asilimia 10. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, bodaboda wengi wananufaisha matajiri, wao hawana bodaboda hizo ni wafanyakazi tu. Serikali haioni umuhimu wa kuwatambua wasiokuwa na pikipiki na mkawapa mikopo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba, baadhi ya bodaboda wanafanya kazi hiyo kwa kutumia pikipiki za watu wengine, wameajiriwa, lakini wako bodaboda ambao wanamiliki pikipiki zao. Dhamira ya Serikali ni kuwakopesha bodaboda madereva wenyewe kuwa na uwezo wa kununua pikipiki wao wenyewe na kufanya biashara wao wenyewe. Ndio maana tunaendelea kuwahamasisha kwamba, watumie nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kutoa wito kwa madereva wa bodaboda wote katika Halmashauri kujiunga katika vikundi, ili waweze kupata mikopo ya kununua bodaboda zao wenyewe na waweze kufanya biashara kwa ufanisi mkubwa zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri sasa umesahau kumsifia Mbunge leo, naona uliamua kusifia Wabunge wote. Umesahau kumsifia Mbunge kumsifia kwamba, anafanya kazi nzuri.

Haya, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Eeh, ndio utaratibu ukiamua kusifia, sifia wote, kama hutaki kusifia usifie Mbunge yeyote.

Tunarejea kwenye swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, Swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika.

Na. 503

**Ujenzi wa Barabara za Lami Jimbo la Lupembe**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA K.n.y. MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza:-

Je, Serikali kupitia *TARURA* ina mpango gani wa kujenga barabara za lami katika Jimbo la Lupembe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kupitia *TARURA,* imepanga kuanza ujenzi wa barabara katika Jimbo la Lupembe ambapo katika bajeti ya mwaka 2024/25 imetenga shilingi milioni 500, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Barabara itakayoanza kujengwa ni ya Lunguya – Soko la Mbao yenye urefu wa kilomita 1.0 ambayo pia, inapita katika Kituo cha Afya cha Mtwango.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na kwa jitihada hizo, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Barabara ya Mtwango kupitia Kichiwa hadi Ikuna mpaka Nyombo, barabara hii ni ya kimkakati kwa maendeleo ya Jimbo la Lupembe. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, huko nyuma nimeuliza humu ndani na tukapata majibu ya Serikali kwamba, tutaanza kuwa na utaratibu tofauti wa kugawa fedha za kujenga barabara za *TARURA* kwa kuangalia maeneo mbalimbali, milima, udongo ulivyo na mvua, ili kusiwe na mgao ambao uko sawa kwa kila jimbo. Je, Serikali inaanza lini utaratibu huu kwa maana bajeti hii nimeona haioneshi kama kuna huo mgao unaoonesha hali kama hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ahsante, katika mwaka wa bajeti 2024/2025, Serikali imetenga shilingi milioni 500, kwa ajili ya kujenga kipande cha Barabara ya Mtwango – Kichiwa – Ikuna – Nyombo kwa kiwango cha lami kwa mita 300 na kukiunganisha kipande hicho na kipande kingine cha Barabara ya Lunguja – Sokola.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha inajenga barabara za lami katika Jimbo la Lupembe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na jinsi ya ugawaji wa fedha za *TARURA,* nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na nimpe habari njema kwamba Serikali iko katika hatua za mwisho za kutengeneza *formula* hii mpya ambayo itatumika kugawa fedha hizi zinazotengwa kwa ajili ya barabara za *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge siku hii ya leo tutakuwa na kikao ambacho ni cha kuhitimisha jinsi ya kutengeneza *formula* hiyo mpya ambayo pamoja na vigezo vingine itazingatia umuhimu wa barabara katika kilimo lakini urefu wa mtandao wa barabara katika jimbo husika. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko kazini na itahakikisha kwamba katika Mwaka wa Bajeti 2024/2025 *formula* hii mpya inaanza kutumika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimwa Spika, ahsante, kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuendelea kujenga kilometa moja ya lami kwenye Mji wetu wa Kharumwa na tumeahidiwa kukabidhiwa Ilani hiyo tarehe 10 mwezi huu wa sita. Je, Serikali imejipanga vipi kutupatia taa za barabarani kwa kilometa hiyo moja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kama Serikali ilivyoanza kuhakikisha kwamba imejenga miundombinu ya lami katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mikakati ya kuhakikisha miundombinu hiyo inaambatana na miundombinu mizuri ya kuwa na taa itafanyika. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali itafanya jitihada ili kuweza kupata taa na barabara hiyo iweze kupendeza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 505

**Kulipa Fidia Wananchi Wanaopitiwa na Njia ya Umeme Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza: -

Je, lini Wananchi wa Kata za Yombo na Kiromo wanaopitiwa na mradi wa njia ya umeme kutoka Chalinze hadi Bagamoyo watalipwa fidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* inakamilisha zoezi la uthamini wa mali za wananchi wanaopitiwa na Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220, kutoka Chalinze hadi Bagamoyo yenye urefu wa kilometa 90.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya awali yanaonesha gharama za fidia kwa mradi huu ni shilingi bilioni 4.2 ambapo Kata za Yombo na Kiromo wananchi 243 watalipwa fidia ya kiasi cha shilingi billioni 1.57. Zoezi la uthamini linatarajiwa kukamilika ndani ya miezi mitatu kuanzia sasa. Aidha, zoezi la kulipa fidia litaanza baada ya uthamini kukamilika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimwia Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina swali moja tu la nyongeza kwa sababu majibu yake ni mazuri sana.

Je, ni lini sasa atatembelea Bagamoyo kukutana na Wananchi wa Kiromo pamoja na Yombo ili kufanya nao mkutano, kuwaelezea mazuri yaliyofanywa na Serikali kuhusu sekta ya umeme pamoja na huo mradi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa mwaliko wa kunikaribisha Bagamoyo na mimi ninamhakikishia kwa niaba ya Naibu Waziri Mkuu na Naibu Wa Nishati nitawasiliana na wewe Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kupanga tarehe ya kwenda Bagamoyo na kufanya mkutano huo na wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Ninaomba niiulize Serikali, ni lini Kituo cha Kupozea Umeme kinachojengwa Eneo la Uhuru Wilayani Urambo kitakamilika ili kuondoa matatizo ya umeme tuliyonayo ya kukatika kila wakati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake. Kituo cha Kupooza Umeme cha *Uhuru Substation* kimeshafikia zaidi ya 92%. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tunasimamia kituo hiki kwa weledi mkubwa sana ili kuhakikisha kinakamilika ndani ya muda wa mkataba wa mkandarasi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalumu, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe.

Na. 506

**Lengo la Asilimia 80 ya Watanzania Kutumia Nishati Safi ya Kupikia Ifikapo 2033/2034**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE K.n.y. MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kupunguza gharama ya gesi ili lengo la kufikia asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2033/2034 ifikiwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya jitihada kuhakikisha bei ya nishati safi ya kupikia inapungua. Kwa upande wa mitungi ya gesi

inayopatikana kutoka kwenye viwanda vya kusafishia mafuta *(Liquified Petroleum Gas - LPG))*, ruzuku imetolewa kwa mitungi 83,500 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.5. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itatoa ruzuku kwa mitungi 452,445 yenye thamani ya shilingi bilioni 10.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa gesi asilia, Serikali inaendelea na uwekezaji wa ujenzi wa mabomba ya kusafirisha na kusambaza gesi majumbani. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ina mpango wa kuongeza miundombinu ili kupokea meli kubwa za Gesi ya *LPG* na hivyo kushusha gharama za bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi zinazojihusisha na usambazaji na uuzaji wa Gesi ya *LPG* na Gesi Asilia pamoja na kuwekeza katika ujenzi wa vituo vya kujaza gesi vinavyohamishika na visivyohamishika kwa kila wilaya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaishukuru Serikali kwa kuweka ruzuku kwenye ununuzi wa mitungi awali lakini mwananchi anapokwenda kujaza mtungi awamu ya pili, bei ya gesi iko juu sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kushusha bei ya gesi ili wananchi wengi waweze kumudu ununuzi wa gesi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa miongoni wa sababu zinazosababisha bei gesi na mtungi iwe juu ni mtungi wenyewe, je, Serikali iko tayari sasa kuwavutia wawekezaji wa ndani ili waje wajenge viwanda vya kutengeneza mitungi hapa ndani na bei ya gesi iweze kushuka na wananchi wengi waweze kumudu bei hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mhesimiwa Spika, ahsante, ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kupunguza gharama ya kujazia gesi, tayari yalikuwa ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwamba tuwekeze katika kupata teknolojia itakayorahisisha kupunguza bei. Sisi tumeshaanza kufanya hivyo na tayari tumeanza mazungumzo na wadau mbalimbali kwa ajili ya kuwekeza teknolojia kadha wa kadha katika kununua gesi (kujaza ile kwa mara ya pili) ili mwananchi asiweze kununua gesi ile kwa gharama ya jumla, kama ni mtungi wa kilo 7 au ni mtungi wa kilo 23, bali aweze hata kununua kidogo kidogo ili kuweza kumrahisishia matumizi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tayari pamoja na mikakati ya ruzuku kuongeza miundombinu, tunao mkakati wa kuongea na wadau kwa ajili ya kuwekeza kwenye eneo la teknolojia ili mwananchi aweze kupata gesi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la pili, tayari Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati amefanya kikao na wadau katika eneo hili la *LPG* kuweza kuona ni kwa namna gani wanakuja na mikakati yao ambayo sisi kama Serikali tuitaifanyia kazi, ikiwemo suala la kuwa na viwanda kwa ajili ya kutengeneza mitungi ya kuwekea gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, suala la nishati safi ya kupikia kwenye Serikali ya Awamu ya Sita ni kipaumbele na tutahakikisha tunafanya kila liwezekanalo kuhakikisha mwananchi anapata gesi kwa bei nafuu lakini vilevile kuboresha mazingira kwa ajili ya kuhakikisha Watanzania wengi wanatumia gesi hii, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, swali fupi la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inasambaza miundombinu ya gesi yetu asilia ambayo ina gharama nafuu katika Halmashauri za Mkoa za Dar es Salaam?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, tayari tulishaanza kwa Dar es Salaam kwa maeeo ya Mikocheni na Mbezi na kupitia Shirika letu la Maendeleo la Petroli *(TPDC)*, tunayo mikakati kwa ajili ya kuongeza uwekezaji wa miundombinu hususan katika Mkoa wa Dar es Salaam ili wananchi wengi waweze kupata miundombinu hii ya gesi na hivyo kupunguza gharama ya matumizi majumbani. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, lipo katika mikakati ndani ya Wizara yetu na tunaendelea kulifanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake. Mbunge anayetoka Manyara.

Haya, Mheshimiwa Monni nimekuona lakini kuna Mbunge kule nyuma alitangulia. Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray. *(Makofi)*

Na. 507

**Hitaji la Mabwawa ya Umwagiliaji Kata za Mbulu Vijijini**

**MHE. REGINA N. QWARAY K.n.y. MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga mabwawa ya umwagiliaji katika Kata za Eshkesh, Yaeda Chini, Geterer, Gidhimu, Masqaroda na Maretadu – Mbulu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa mbalimbali nchini, ikiwemo mabwawa ya Tumati, Dongobesh na Dirim, kwa kutumia Mshauri Elekezi wa *M/S CCL – Multi-Netwas JV*. Aidha, Mshauri Elekezi anaendelea na kazi ya usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji katika Kata ya Gidhimu yenye vijiji vitatu ikiwemo Dumanang, Guye na Ng'orat. Katika Kata za Maretadu na Masqaroda Serikali imepanga kuchimba visima ambapo wakulima 760 watanufaika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kuendelea kubaini maeneo mbalimbali nchini yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na ujenzi wa mabwawa. Wataalamu kutoka Tume watatembelea na kufanya tathmini katika maeneo ya kata za Eshkesh, Yaeda Chini na Geterer, ndani ya Halmasauri ya Mbulu ili kuyaingiza katika mpango wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kabla ya kuingizwa katika mpango wa ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa ... haya Mheshimiwa Regina amekaa. Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Kijiji cha Ndoroboni na Babayu tayari wameshafanya usanifu kwa ajili ya mabwawa hayo lakini ninaomba kujua, ni lini sasa ujenzi utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni kwamba, tukishamaliza usanifu maana yake tunaingia katika mpango wetu wa utekelezaji kwa maana ya fedha halafu *then* tunatangaza mkandarasi. Kwa hiyo, hatua iliyopo sasa hivi ni kumtafuta mkandarasi ili sasa aweze kutekeleza kazi ya ujenzi katika maeneo hayo Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; ninaomba kuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri. Skimu ya Umwagiliaji ya Mang'onyi ilishaelekezwa ijengwe toka mwaka wa fedha uliopita na taratibu za mkandarasi zilikuwa zinaendelea. Ninaomba nijue ni lini sasa ujenzi wa Skimu ya Mang'onyi utaanza rasmi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba kwenye Skimu ya Mang'onyi tuko katika hatua za mwisho; tuko kwenye upekuzi ili sasa baada ya hapo tumkabidhi mkandarasi *site* aanze kufanya kazi. Maana yake hii hatua ambayo tunaimalizia sasa ndani ya muda mfupi, mkandarasi atakuwepo *site* na ujenzi utaendelea, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kunipa nafasi. Wilaya ya Songwe tuna mradi mkubwa wa Bwawa la Nanjembo katika Kata ya Kanga na Mwambani. Ni miaka mingi sasa yapata miaka 15 tumekuwa tukiandikia na usanifu ulishaisha tumeshapeleka Wizarani. Ni lini Serikali itatupatia fedha tuweze kujenga mradi huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni kwamba, katika Skimu ya Nanjembo kilichokuwa kinafanyika sasa hivi ni usanifu wa kina ambao sasa umeshamalizika. Kwa hiyo sasa hivi tuko katika hatua za kutafuta mkandarasi ambaye atakuja kujenga katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, jukumu hili tunalifanya kwenye maeneo yote ambayo tumeainisha katika mwaka wa fedha unaokuja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ninakuthibitishia tu kwamba Skimu hii itajengwa

na tutaisimamia kuhakikisha Wananchi wa Songwe wanapata huduma hii ya umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond.

Na. 508

**Tozo ya Ziada Kwenye *Form* ya *PF3* katika Hospitali za Serikali**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza: -

Je, kwa nini watu waliopata ajali wanapokwenda Hospitali za Serikali na form za *PF3* hulipa gharama za kumwona daktari na kugonga muhuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Sera ya Afya ya Mwaka 2007 imeweka utaratibu wa wagonjwa wote wa dharura kupatiwa huduma za afya za dharura. Kwanza, pasipo kikwazo cha kulipia hadi hapo changamoto za kiafya za dharura zitakapokwisha.

Mheshimiwa Spika, ninatoa wito kwa Waganga Wakuu wa vituo vyote kuhakikisha wagonjwa wa dharura wanapata huduma wanazostahili kwanza ili kuokoa maisha yao na taratibu nyingine zifuate baada ya kuwa wamehudumiwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inafanya kazi kwa maandishi na jambo hili amelitoa hapa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kunena, je, ni lini sasa andiko hilo litatoka lisambae kote kwenye hospitali kuu mpaka kule kwenye vituo vya afya, kwa sababu wagonjwa wengine waliopata ajali huwa wanafia *causality*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa wagonjwa wengi wa ajali na hususan Moshi ni vijana waliopata ajali za bodaboda na wakati mwingine ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mbunge, anayezungumza yuko nyuma yako, kwa hiyo rudi kidogo kule nyuma. Rudi kule nyuma amalize kuongea kwanaza, rudi tu.

Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ... na kwa kuwa takwa hilo linafanya vijana waliopata ajali kwa bodaboda wajifiche ili wasiende tu mikononi mwa askari, ni lini elimu itatolewa kwa vijana hao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mawili mazuri muhimu sana yanayogusa maisha ya watu...

**SPIKA:** Subiri kidogo Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Naibu Waziri ana kiti hapo mbele. Kwa hiyo, pita hapo mbele ukae dakika mbili zako uende.

Aa, nenda hapo mbele. Si ulikuwa unaongea naye? Ndiyo, pita huku pita huku. Ndiyo, usimwongeleshe kwa nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna nzuri ambavyo amekuwa aking'amua matatizo ya msingi yanayokabili Watanzania lakini Wana-Kilimanjaro. Kwanza, moja, kuna Maandiko kwa sababu ni Sera ya Afya ya 2007, inatamka hivyo. Kwa hiyo, inatakiwa itekelezwe na sisi kwa pamoja tufuatilie. Ninaendelea kuwaasa watumishi wote na hasa viongozi wanaosimamia vituo vyetu kuhakikisha kwamba wanasimamia hilo na wanaweka utaratibu ambao ni mwafaka kuhakikisha wagonjwa wanaokuja kwa namna hii wanahudumiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, la pili, moja hili ni kwa kusema *PF3* na mambo mengine, kwa kweli sidhani kama sasa hivi kuna hilo tatizo. Kwamba mtu akiumia ni lazima apitie apate *PF3* halafu ndiyo aende hospitalini lakini tutaendelea kufuatilia, tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani tuone namna ya kuliweka hilo vizuri, likae vizuri kama ambavyo umeshauri ili tuweze kuokoa maisha ya watu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 509

**Hitaji la Mashine za Watoto Njiti katika Hospitali za Mikoa na Wilaya**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kupeleka mashine za watoto njiti katika hospitali zote za mikoa na wilaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imepeleka vifaa vya kusaidia watoto njiti kwenye vituo vya kutolea

huduma za afya 241, vyenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 2.6 hadi kufikia Machi 2024.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2024/2025, Serikali imepanga kutumia shilingi bilioni 30 kuimarisha huduma za watoto wachanga katika hospitali 100 kwa kujenga wodi maalumu za watoto wachanga, watoto njiti na ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba ikiwemo mashine za kuwasaidia watoto wachanga njiti kupumua.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninataka kujua, mpaka sasa ni hospitali ngapi za mkoa na hospitali ngapi za wilaya ambazo zimepelekewa mashine za watoto njiti?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa changamoto ya watoto njiti ni kubwa sana, watoto wengi wanapoteza maisha kwa sababu ya kukosa huduma muhimu na wazazi wengi kutokuwa na elimu namna ya kuwatunza watoto hawa. Ninataka kujua mpango wa Serikali ni upi ili kuhakikisha Watoto hao wanaishi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la kwanza linahitaji takwimu. Kama unazo unaweza kumjibu Mheshimiwa Mbunge, kama huna ukazitayarishe umkabidhi Mbunge. Unaweza kujibu swali la nyongeza la pili.

Majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimwia Spika, hebu ninaomba arudie swali lake la pili la nyongeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Ninasema, kwa kuwa changamoto ni kubwa sana, watoto njiti wengi wanapoteza maisha kwa sababu ya kukosa huduma muhimu na wazazi wengi kutokuwa na elimu namna ya kuwatunza watoto hao, ninataka kujua mpango wa Serikali ni upi ili kuhakikisha watoto hao njiti wanaishi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ameona kwamba hapa tumezungumzia hospitali 241, vituo 241 lakini kama unavyojua kwenye nchi hii kuna Majimbo 214, maana yake *almost* hospitali zote za Mikoa sasa zipo *covered* lakini kuna Majimbo machache kwa kweli siweze kukwambia hapa lakini ni machache mno ambayo siyo vifaa havipo ni zile wodi lakini maeneo yametengwa kwa ajili ya kusaidia hao Watoto. Ndiyo maana tunaenda sasa kwenye Majimbo haya 100 kwenda kujenga na kuweka vifaa.

Mheshimiwa Spika, hivyo nikuhakikishie tu kwamba kwenye hospitali zetu za Wilaya nyingi tunazo hizo *facility* kwa maana ya vifaa lakini kuna hospitali za Wilaya ambazo hazina majengo ndiyo tunaenda kujenga haya majengo 100.

**SPIKA:** Sawa, sasa kwenye hilo la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri, utampa takwimu kwa sababu anataka kujua ni ngapi, kwa hiyo utampelekea takwimu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, sawa nitampa takwimu.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye swali lake la pili ni kweli kama unavyosema, asilimia 48 ya vifo vya watoto vinachangiwa kwenye eneo hili la watoto njiti lakini baada ya mapinduzi makubwa ambayo Mheshimiwa Rais wetu amefanya kwenye ujenzi lakini pia kwenye

kupeleka vifaatiba na ninyi mnajua kule Wilayani hata leo ukiangalia eneo la *cancer* utaona jinsi ambavyo kuna *improvement* kubwa sana, badala ya watu asilimia 80 kwenda pale *Ocean Road* wakiwa kwenye *terminal stage,* sasa hivi asilimia 70 wanaenda wakiwa na *early stage* kwa sababu vifaa vipo huku chini.

Mheshimiwa Spika, hili eneo la kuokoa maisha ya watoto kwa kweli limefanyiwa kazi kubwa na elimu tunaendelea kutoa. Elimu ambayo tunaitoa siyo kwamba wakina mama wawaangalie watoto wao lakini waende kliniki wakati wote wanapopata ujauzito, wakati wa ujauzito wahudhurie zile dalili za mwanzo ziweze kuonekana ili atakapokuwa hospitalini basi mtoto awe chini ya uangalizi wa wataalam badala ya kubakia kule nyumbani.

Mheshimiwa Spika, nihakikishe wewe na mimi na kila myu tuendelee kutoa hiyo elimu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya swali fupi la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni haja ya kuleta mashine za watoto njiti katika kituo cha afya Bukundi, kwa kuwa wastani wa watoto 15 kuzaliwa kwa mwaka wakiwa njiti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninamuomba Mheshimiwa Mbunge nikimaliza kujibu hili swali lake tukae pamoja na yeye chini halafu tupige *MSD* vifaa vipelekwe kule kwa sababu Mheshimiwa Rais wetu ameshanunua vipo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge sasa aulize swali lake.

Na. 510

**Biashara ya Vipepeo Zanzibar**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani kufanya mazungumzo ya pamoja kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara juu ya zuio la usafirishaji wanyama hai nje ya nchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali iliweka zuio la biashara ya ukamataji na usafirishaji wa wanyamapori hai nje ya nchi kutokana na dosari kadhaa zilizokuwa zimejitokeza katika uendeshaji wa biashara hii. Kufuatia zuio hilo, Serikali iliunda Kamati ya wataalam kwa ajili ya kufanya tathmini ya zuio na kuwasilisha mapendekezo kuhusu mustakabali wa biashara hii. Kamati hiyo ilipokea maoni kutoka pande zote mbili za Muungano kwa kuwa masuala ya wanyamapori yanasimamiwa na sheria mbili tofauti kwa Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Spika, suala la biashara ya vipepeo ni miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa katika vikao rasmi vya mashirikiano kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya Zanzibar. Kwa sasa wataalam wanakamilisha taarifa na mapendekezo ili yaweze kuwa msingi wa kufanya maamuzi ya mustakabali wa biashara hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, swali la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa utekelezaji na ufanyaji maamuzi wa mikataba ya kikanda na mikataba ya kimataifa inajumuisha pande mbili za Muungano ikiwa ni pamoja na mkataba huu wa *CITES* ambao Mheshimiwa Waziri ameuzungumza hapo.

Je, Serikali haioni haja ya kuwa na dawati maalum la uratibu kule Zanziba ili kuweza kusaidia kufanikisha uratibu wa shughuli za utekeleza wa *CITES*? *(Makofi)*

Swali la Pili, je, Serikali haioni haja ya kuwa na kamati maalumu ambayo itashirikisha pande mbili za muungano ili kuweza kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa mikataba hii ambayo inazungumzia masuala ya muungano, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, baada ya zuio hili tulipata fursa nzuri ya kujadili kuhusiana na mwenendo wa biashara hii jinsi unavyofanyika na changamoto ambazo zimejitokeza. Katika vikao vyetu vya mashauriano mambo haya yamekuwa yakijadiliwa kwa kina na kwa msingi, kwa hiyo ninamuomba Mheshimiwa Mbunge atupe fursa mambo haya yanafanyiwa kazi naamini tutafika pazuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kwa niaba yake Mheshimiwa Dorothy Kilave. *(Makofi)*

Na. 511

**Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Ngarenanyuki – Arumeru Mashariki**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE K.n.y. MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga majengo ya Mahakama ya Mwanzo Ngarenanyuki na katika maeneo jirani ambayo hayana huduma ya Mahakama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Mahakama kwa muda mrefu imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya uhaba na uchakavu wa majengo, hususani kwa Mahakama za Wilaya na za Mwanzo. Aidha, Mahakama ya Mwanzo Ngarenanyuki ni miongoni mwa Mahakama zenye majengo chakavu ambapo inahitajika kujengwa jengo jipya. Kwa sasa, Mahakama hii haifanyi kazi na wananchi wa eneo hilo wanapata huduma za Mahakama katika Mahakama ya Mwanzo King'ori iliyopo umbali wa takribani kilomita 28 kutoka Ngarenanyuki.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka wa fedha 2023/2024 tunajenga Mahakama ya Mwanzo Maji ya Chai iliyoko Jimbo la Arumeru Mashariki. Aidha, kadri fedha zitakavyopatikana Mahakama ya Ngarenanyuki pia itajengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Je, mpo tayari kufuatana na Mheshimiwa

Pallangyo kwenda kuangalia umbali uliopo kutoka Mahakama moja kwenda Mahakama nyingine?

Je, ni lini sasa Jimbo la Temeke au Wilaya ya Temeke mtajenga Mahakama ya Mwanzo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Pallangyo, japo nimeshamwambia kilometa zilizopo ni 28 lakini tuende tukajiridhishe kwamba umbali ule je, unakidhi wananchi kuendelea kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Temeke kujenga Mahakama za mwanzo, kwanza tuishukuru Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo imetoa fedha kwa kujenga kituo jumuishi cha Mahakama eneo la Temeke na kinaanza kufanya kazi hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadri hali ya fedha itakavyoruhusu tutaweza kujenga Mahakama ya Mwanzo ya Temeke ili kusogeza huduma za mwanzo karibu na wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mahakama ya Tarafa ya Matemanga hali yake ni mbaya sana lakini pia imejengwa pembezoni mwa barabara. Je, ni lini Serikali itatujengea Mahakama yenye hadhi nzuri kama siyo kukarabati Mahakama ile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tunakiri uwepo wa uchakavu wa miundombinu za Mahakama ngazi ya mwanzo kama hii Mahakama

ya Tarafa aliyoirejea ya Matemanga. Ninamuahidi tu kadri hali ya fedha itakavyokuwa nzuri Mahakama itaendelea kutekeleza mpango wake wa ukarabati na ujenzi wa Mahakama ikiwemo Mahakama hii ya Matemanga, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Waheshimiwa Wabunge swali hili nimeletewa taarifa hapa kwamba lilishapata kujibiwa hapa Bungeni, kwa hiyo tunaliondoa kwenye orodha.

*(Swali Na. 512 la Mhe. Husna J. Sekiboko Liliondolewa)*

**SPIKA:** Tunaenda na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 513

**Ujenzi wa Barabara ya Nanjoka – Mtwara Pachani**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Nanjoka – Nalasi - Mchoteke – Njenga – Mjimwema – Magozini - Mtwara Pachani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Tunduru – Nanjoka – Nalasi – Mchoteke - Njenga – Mjimwema – Magozini hadi Mtwara Pachani yenye urefu wa kilometa 300. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika

mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imesaini mkataba wa ujenzi wa kilometa 1.5 katika Mji wa Tunduru na kazi za ujenzi zinatarajiwa kukamilika Septemba, 2024. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa sehemu iliyobaki, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nyoka, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Namtumbo kwenda Likuyuseka kwa kiwango cha lami?

Swali la pili, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya kutoka Mtonya, Mgombasi hadi Naikesi Kata ya Kitanda kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mjibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hizi mbili, Mkoa wa Ruvuma wameshaomba tuweze kuzifanyia usanifu na kwa sasa tunachofanya ni kuijenga kwa kiwango cha changalawe, kuimarisha maeneo korofi na kupanua madaraja ambayo ni madogo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshapokea maombi kwa maana ya kuanza kufanya usanifu kwa barabara ya Namtumbo, Mtonya kwenda Likuyu na kutoka Mtonya, Mgombasi kwenda Naikesi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Ikombe kilichopo kwenye Wilaya ya Kyela, wananchi wanapata shida sana wanapokwenda kupata mahitaji yao kwenye Kata ya Matema, hasa

wajawazito wanapokuwa na uchungu wanapanda kwenye mitumbwi, wanapata matatizo ambayo yanapelekea vifo. Wanakufa kwa sababu ya uchungu wapo ndani ya mtumbwi kwenye Ziwa Nyasa.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ambayo haihitaji daraja? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tupo kwenye utaratibu wa kuijenga barabara lakini jambo la kwanza kubwa ilikuwa ni kuanza kulijenga daraja lenyewe la Ikombe ambalo limeshajengwa na lile la Bujode linasanifiwa, kinachofuata ni kujenga barabara yenye tuta ili kuondoa changamoto ambayo ipo kwa sasa, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa kifupi Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Hii ni pamoja na dharura iliyojitokeza siku ya Ijumaa usiku, pale kwenye lile daraja tunaloomba kila siku la Mitomoni, kile kivuko chao walichokuwa wanatumia kimeharibika na kikataka kuleta maafa makubwa juzi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutusaidia kwa dharura kupata tu injini itakayowezesha kuvusha hicho kivuko kilichopo. Sasa hivi wananchi wa upande wa Mitomoni hawawezi kabisa kuvuka kuja upande wa Mkenda ambako ndiko wanapata mahitaji yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninatoa pole kwa changamoto hiyo kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa eneo hilo la Mitomoni. Tayari tulishapata hiyo taarifa na kupitia Bunge hili niagize Mtendaji Mkuu wa *TEMESA* ambaye vivuko vipo chini

yake, pamoja na Meneja wa *TEMESA* Mkoa wa Ruvuma wafike eneo na waweze kuona namna ya kutatua hiyo changamoto haraka inavyowezekana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Mtwara - Pachani kwenda Magazini mpaka Nalasi ni barabara ambayo kama ulivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba ilishafanyiwa upembuzi yakinifu muda mrefu na ipo ndani ya ilani ya uchaguzi. Ni barabara ambayo inatusumbua sana, kwanza ni barabara ambayo ni ya kiusalama zaidi, inatumika sana na Majeshi yetu.

**SPIKA:** Swali lako Mheshimiwa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, sasa je ni lini hasa Serikali miaka mitano inaenda kuisha sasa ipo kwenye Ilani, ni lini Serikali itaiweka kwenye bajeti kuanza kuijenga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tumeshakamilisha usanifu lakini kikubwa kabla hatujapata fedha ya kuanza kuijenga yote, Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi kwamba tunachofanya ni kuhakikisha kwamba yale maeneo yote ambayo yanafanya barabara isipitike tutahakikisha kwamba tunaendelea kuyakarabati ili barabara yote iweze kupitika wakati tunatafuta fedha kuijenga yote, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Benardeta Mushashu, swali la nyongeza.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ni lini sasa barabara ya Kyaka, Katoro, Kanazi, Ketema kilometa 60.7 itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika bajeti ambayo tumeipitisha barabara hiyo tumeiweka kwenye mpango wa kuanza kuijenga kwa mwaka unaokuja ikiwa ni pamoja na daraja kubwa katika hiyo barabara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Ulinzi kutoka Lumesule kupitia Chamba mpaka Mbamba *Bay* ambayo ilikuwa inatumika tangu enzi ya ukoloni, sasa hivi haipitiki.

Je, ni lini Serikali itaifungua barabara hii kwa ajili ya ulinzi wa nchi yetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara nyingi kama tumekuwa tunasema, nyingi zilikuwa zimefunga kwa sababu ya hali ya mvua na tayari tumeshawapa maelekezo mameneja nadhani wapo *site* kuhakikisha kwamba barabara zote zilizokuwa zimefunga ziweze kufunguliwa na nimuagize pia Meneja wa Mkoa wa Ruvuma aweze kuhakikisha kwamba barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge pia inafunguliwa kama barabara zingine ambazo tumeahidi kuzifanyia kazi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi sasa aulize swali lake.

Na. 514

**Ujenzi wa Barabara ya Bihawana – Manyoni Kupitia Itigi**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Bihawana, Mpalanga, Chidilo, Chali hadi Manyoni kupitia Itigi kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Bihawana – Mpalanga – Chidilo – Chali hadi Manyoni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2024/2025. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niipongeze Serikali kwa majibu mazuri na kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya katika kuiweka vizuri barabara hii ya kutoka Bihawana mpaka Chali na hususani katika eneo la Chali, Makulu na Chali Isanga ambapo pale wanajenga madaraja manne.

Swali langu la nyongeza ni kwamba *TANROADS* walitangaza kujenga barabara ya lami kutoka Bahi Mwanachugu mpaka *Station* ya Bahi lakini mpaka sasa hatujui hatima ya barabara ile itaanza lini pamoja na kwamba ilishatangazwa kwa ajili ya kujengwa, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa pongezi za Serikali kwa kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika suala la miundombinu.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeamua kujenga barabara

zote ambazo zinaunganisha Miji yote na vituo vyote vya *station* vya *SGR* na hii barabara ndiyo anayoisema.

Mheshimiwa Spika, barabara zote zilitangazwa kwa pamoja ikiwemo hii Barabara, lakini hii barabara kabla ya *TANROADS* kuanza kuihudumia ilikuwa ipo chini ya *TARURA* kwa hiyo ilikuwa haijafanyiwa usanifu. Kinachofanyika sasa hivi ni kukamilisha usanifu ili ujenzi uanze, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kinachofanyika sasa hivi ni kukamilisha usanifu halafu tutaanza kuijenga kwa haraka sana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Barabara ya Nyoni-Maguu iliyopo kwenye Ilani ya 2020/2025, ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli barabara aliyoitaja ya Nyoni-Maguu ipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na tunachofanya bado tunaendelea kwa kweli kutafuta fedha ili tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami. Katika kipindi hiki bado nimhikikishe Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kuikarabati na kujenga maeneo yale korofi hasa, kwa sababu ni barabara ambayo inapita kwenye miinuko mingi sana. Tutaijenga kwa zege ama kwa lami kuhakikisha kwamba, yote inapitika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, sasa aulize swali lake.

Na. 515

**Hitaji la Malambo – Momba**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Malambo ndani ya Tarafa ya Ndalambo na Msango pamoja na kukarabati malambo ya Mkomba, Kasanu na Kamsamba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali imeendelea kuwekeza katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji kwa mifugo kutokana na changamoto kubwa iliyopo ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo Jimbo la Momba. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kujenga malambo na kuchimba visima virefu kwa ajili ya maji ya mifugo bado mahitaji ya miundombinu ya maji kwa mifugo ni makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea na uchimbaji wa kisima kirefu cha Kapele-Kasinde katika Halmashauri ya Wilaya ya Momba kwa ajili ya maji ya mifugo. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa malambo katika Tarafa ya Ndalambo na Msangano, pamoja na ukarabati wa malambo ya Mkomba, Kasanu na Kamsamba kulingana na upatikanaji wa fedha ili yaweze kutumika kwa ajili ya maji ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kutoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Momba kufanya usanifu *(design)* wa malambo hayo na kuwasilisha gharama zake Wizarani ili yaweze kujumuishwa kwenye mpango na bajeti ya Wizara ya mwaka 2025/2026 kadri ya upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa, Serikali bado inajipanga kutafuta pesa ili kuweza kunusuru hali ya mifugo ndani ya Jimbo la Momba, ni upi mkakati wa haraka na wa dharura  kwa ajili ya kunusuru mifugo yetu ili iweze kupata maji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ni upi mkakati wa Serikali mkiwa mnaendelea kutafuta hela ya malambo kutujengea majosho kwenye Kata ya Kapele, Nzoka, Mpapa, Kamsamba pamoja na Mkomba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, moja ya mikakati ya haraka ambayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inaifanya sasa ni kuchimba visima virefu.

Mheshimiwa Spika, shukrani kubwa ambazo tunatoa ni kwa Bunge lako Tukufu kupitisha bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa kuiongeza maana yake kuna fedha nyingi. Kwa hiyo, nilipokuwa ninazungumza na Katibu Mkuu, ameniambia kwamba, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, haraka tutakayoifanya sasa ni kuchimba visima ambavyo vipo ndani ya uwezo wetu ili kupunguza adha ya maji kwa mifugo nchini hususan katika eneo la Jimbo la Momba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la kujenga majosho la lenyewe litawekwa katika mpango hususan maeneo yote ambayo Mheshimiwa Mbunge, ameainisha. Kwa hiyo, hili limeshafika na Wizara naamini tutalifikisha kama lilivyo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu

kutoka upande wa Serikali. Tutaleta kwenu tangazo la wageni waliopo hapa Bungeni asubuhi hii.

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika, hawa ni wageni watatu wa Mheshimiwa Anton Mwantona ambao ni Mabalozi wa Mazingira kutoka Mkoa wa Mbeya; yupo Chifu Rocket Masoko Mwanshinga ambaye ni Chifu Mkuu wa Mbeya, ahsante sana; yupo pia Chifu Joel Burton Mwakatumbula, huyu ni Chifu Mkuu Rungwe na yupo pia, Ndugu Ezekiel Gwatengile, ambaye ni Afisa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine ambao ni wageni wetu sisi Wabunge wote. Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii; hawa ni Kamati ya Shindano la Kimataifa la Kutangaza Utalii Duniani, *Miss Travel World 2024* wakiongozwa na Ndugu Samwel Malugu ambaye ni Mratibu na Mwanzilishi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 86 wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na hawa ni wanafunzi na wafanyakazi wa Shule ya Sekondari *St. John Vianney*. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi ambaye ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na huyu ni Mkurugenzi kutoka Taasisi ya *Maikovin Events Company Work* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ghati Chomete ambaye ni mume wake kutoka Mkoa wa Mara, karibu sana shemeji yetu, wote ni shemeji yetu. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Kata ya Kawe kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Suleiman Haroub; hee jamani, kuna Mheshimiwa Mbunge anaitwa Suleiman Haroub? Jina lake la mwisho ni nini? Mbona inaonekana.., haya wageni wawili wa Mheshimiwa Suleiman Haroub ambao ni marafiki zake kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Haya Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Masache Kasaka ambaye ni Katibu na Mjumbe kutoka Chama cha Mabucha na Wafugaji wa Wanyamapori Nchini. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Riziki Lulida ambaye ni mtumishi kutoka Taasisi ya Waandishi *(The Media Climate Change Conversations)*. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Joseph Tadayo ambao ni wapigakura wake kutoka Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi ambao ni wakulima kutoka Malinyi wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Kata ya Njiwa, Ndugu Issa Matekula. *(Makofi)*

Wapo wageni 14 wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu ambao walimu kutoka Shule ya Msingi Kirangi, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Tunao wageni 49 wa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta ambao ni Kwaya ya Upendo kutoka Urambo Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 100 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Machwa iliyopo Kata ya Murieti, Halmashauri ya Jijini la Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao hapa Bunge asubuhi hii. Wengine watatangazwa kadiri watakavyokuwa wanapata nafasi ya kuingia.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, Jambo la Dharura.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa.

## JAMBO LA DHARURA

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nimesimama kwa Kanuni ya 54, nadhani kwa sababu ya ku-*save* muda sina haja ya kuisoma. Usiku wa tarehe 01 saa 7.00 katika Kata ya Kalenge Wilayani Biharamulo, Kijiji cha Rusenga na Kitongoji cha Rogwe kuna magari mawili yanayosemekana ni magari ya polisi; moja, ni *Pick Up* zile ambazo zinatumiwa na polisi *Land Cruiser*, lakini gari jingine la pili, lilikuwa ni gari la kawaida.

Mheshimiwa Spika, walifika katika familia ya Mzee Ruyoho Bugangati, wakaivamia nyumba ile usiku saa saba wakidai kwamba, kuna mhalifu walikuwa wanamtafuta aliyekuwa ametokea Mkoa jirani wa Geita na ikasemekana yupo kwenye nyumba ile. Baada ya kutokumkuta walianza kufanya adhabu kwa nyumba ile, kwa kuwasulubu na kuwafanyia mateso usiku ule saa saba na walifika bila kuongozana na mtu.

Mheshimiwa Spika, baba mwenye nyumba akavunjwa mguu, akachomwa singe kwenye mguu, lakini kijana wake wa kiume aliyekuwepo akavunjwa mkono na baada ya hapo wale watu waliachwa pale hawakuchukuliwa. Sasa nilipopata taarifa nikaanza kufuatilia nikajiuliza kama hawa watu walikuwa ni askari polisi nadhani wanapofanya adhabu kama ile na wale watu kama ni wahalifu ilibidi wapelekwe kituo cha polisi wakashtakiwe.

Mheshimiwa Spika, nikafuatilia kwa *OCD* wa Biharamulo mpaka jana anasema hatambui hilo gari wala hao watu na hakutuma askari. Sasa yeye mwenyewe akawa bado anafuatilia kujua wale watu walitokea sehemu gani. Mpaka sasa bado hatutajua, lakini inaonekana ni askari kwa mujibu wa taarifa tulizokuwepo nazo, kwa sababu walikuwa na silaha nzito za moto wakitafuta yule mtu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimesimama hapa? Nimesimama hapa kuomba Mwongozo wako, lakini pia tupate majibu ya Serikali na endapo sitaridhika kwa majibu ya Serikali nitatoa hoja Bunge linisaidie kujadili hii hali, kwa sababu hawa ni Watanzania ambao wamevamiwa nyumbani kwao saa saba usiku. Watu wameingia pale bila kuwa na Kiongozi wa Kijiji wala Kiongozi yeyote.

Mheshimiwa Spika, sisi ni Watanzania kama Watanzania wengine. Wananchi wangu katika Kata ya Kalenge wana taharuki, kwa sababu hata Serikali au Jeshi la Polisi halijui hawa watu walitokea wapi? Kwa hiyo, ninaposimama hapa, hili jambo nadhani bado linaendelea, kwa sababu hatujui kesho wataamkia kwenye kata ya nani au kwenye familia ya nani katika Jimbo langu?

Mheshimiwa Spika, sasa nikaomba tupate majibu ya Serikali ni nini utaratibu? Vinginevyo, ikishindikana nitoe hoja Bunge linisaidie, kwa sababu yametokea Biharamulo, kesho yatatokea Majimbo mengine. Kwa hiyo, lazima Watanzania sisi kama Wabunge tunaowawakilisha tuweze kuwalinda, tujue wanalindwaje na maisha yao yanaendeleaje.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, kwa sababu wamama mpo hapa najua akina mama hamzai mioyo ya watu mnazaa watoto. Hata kama yule mtu alikuwa ni jambazi sidhani wazazi wake kama wanahusika kumlea awe jambazi.

**SPIKA:** Umeeleweka.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba kutoa hoja ili Wabunge wenzangu waniunge mkono

tuweze kulijadili hili jambo endapo hatutapata majibu mazuri ya Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, akitutaka tutumie Kanuni ya 54, kwamba, ana jambo la dharura ambalo angetamani Bunge liweze kulijadili na kutoa maamuzi pengine ama kuazimia jambo fulani kuhusu hilo ambalo amelieleza ili Serikali iweze kuchukua hatua.

Waheshimiwa Wabunge, matumizi ya Kanuni ya 54, yanataka masharti ya Kanuni ya 55, yawe yametimizwa. Kwa maelezo ya awali aliyoyatoa Mheshimiwa Mbunge, ambayo ukirudi kwenye Kanuni ya 54, yanataka mimi niwe nimeridhika hapa kama ni jambo ambalo linaweza kutolewa kama hoja ya dharura ili nimpe nafasi sasa aweze kueleza kwa mapana na marefu ili atoe sasa hoja ndio Wabunge tuweze kumuunga mkono na kama hakuungwa mkono basi hoja inakuwa imekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, kama hao watu wamevunjika mkono, mwingine amevunjwa mguu ni dhahiri wananchi wamepata madhara. Kwa hiyo, tunakupa pole sana Mheshimiwa Mbunge, lakini pia na wananchi wa Biharamulo kwa ujumla na Kata uliyoitaja kwa madhila hayo ambayo wameyapata. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa maana ya Bunge kuweza kulichukua jambo hili kama la dharura na maadamu na wewe katika maelezo yako umesema polisi wamekupa taarifa kwamba, hawana taarifa hiyo na waendelea kufuatilia. Maana yake sisi hatuna uhakika kama ni jambo la uhalifu ule ambao unaweza kutokea kwenye familia yoyote au ni uhalifu ambao umefanywa na polisi. Kwa hiyo, mazingira hayo Bunge halitaweza kujadili jambo hili, kwa sababu hali taarifa ambazo zitalifanya lifikie mahali pa kujua kama jambo hili linakidhi masharti ya Kanuni ya 55 au hapana, kwa sababu tutakuwa tunaazimia kwa nani? Nani ili afanywe nini? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, maana yake ni nini? Kanuni ya 55, inataka yale ambao ambayo yanaweza kufanywa na Serikali kwa utaratibu wa kawaida huwa yanafanywa kwa utaratibu wa kawaida. Yale ambayo yanahitaji hatua za ziada basi ndio Bunge linachukua jambo hilo kama la dharura na linaweza sasa kujadili na kuilekeza Serikali nini cha kufanya.

Kwa hiyo, katika mazingira haya ni kweli watu wamepata madhara na tunawapa pole na kwa kweli Mheshimiwa Mbunge, pole sana. Natumai walipoenda hospitali wamepata pengine vipimo na matibabu ndio maana mmeweza kujua kwamba, wamevunjika, lakini kwa maana ya tukio lenyewe namna ulivyolieleza hainipi mimi fursa ya kuamua kwamba, ni jambo la dharura linaloweza kujadiliwa na Bunge ili kuilekeza jambo lolote Serikali. Kwa hiyo, kwa muktadha huo kama ulivyosema umeongea na upande polisi kwa maana ya *OCD* basi waendelee kufuatilia ili hawa wahalifu waweze kukamatwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyu atakuwa Mbunge wa mwisho kuzungumza kuhusu mambo haya ya utaratibu, kwa sababu majina yapo mengi sana ya Wabunge mnaotaka kuchangia. Mheshimiwa Esther Matiko. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimesimama kwa Mwongozo Kanuni ya 76 kwa jambo ambalo limetokea hapa. Pamoja na kwamba, umetoa maelezo, lakini nimesimama kwa kile ambacho amekileza Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa, hapa. Kumekuwa na mtiririko wa matukio ambayo aidha unapata unaambiwa wamekuja askari…

**SPIKA:** Mheshimiwa Matiko, kwanza kaa. Maamuzi yakishatolewa na Kiti, ni maamuzi yameshatolewa. Sasa ukisema umesimama kwa jambo la Mheshimiwa *Engineer* Ezra limeshafungwa saa hizi. Kwa hiyo, sasa ukianza kurejea huko ni kama unanirejesha kwenye maamuzi ambayo nimetoka kuyatoa mwenyewe hapa mbele. Kwa hiyo, hilo jambo kikanuni haliruhusiwi.

Waheshimiwa Wabunge, wanaweza kuwa wengine Kanuni wamezisahau kidogo. Ukiwa hujaridhika na maamuzi Kanuni zetu zinaeleza; Kanuni ya 5, ambaye hajaridhika unatumia Kanuni ya 5, hapo unaweza kupeleka taarifa kwa Katibu, halafu tunayapitia tena yale ambayo yalitolewa hapa mbele. Baada ya kusema hayo Waheshimiwa tunaendelea. *(Kicheko)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI.**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na hapa mbele nipo na orodha ya majina ambao wameomba kuchangia na majina kwa kweli ni mengi na kwa wingi wa majina, tunarejea kwenye uamuzi ambao niliutoa Siku ya Ijumaa Wachangiaji mtachangia kwa dakika nane.

Tutaanza na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, ningependa nichangie kwenye eneo la misitu; eneo ambalo lina wachangiaji wachache sana. Sekta hii ni Sekta muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu na Sekta hii ina uwezo mkubwa sana wa kuiongezea Serikali mapato na ina uwezo mkubwa sana wa kuongeza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa pekee ni moja ya Sekta chache inayoweza kusaidia sana kupunguza umasikini wa kaya kwenye maeneo ya vijiji vyetu. Kwa umuhimu zaidi Sekta hii inaweza ikawa ni kichocheo kikubwa sana cha viwanda katika maeneo ya vijiji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, subiri kidogo. Mheshimiwa Mbunge wa Urambo, anayechangia yupo nyuma yako.

Mheshimiwa Deo Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, muda wangu utalindwa, kutokana na umuhimu huu ndiyo maana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alikubaliana na Baraza la Biashara lilipopeleka mapendekezo ya namna bora ya kuhakikisha kwamba sekta hii inapewa umuhimu mkubwa na ikaundwa Kamati pale ambayo ilikuwa chini ya Baraza la Biashara pamoja na Wizara yetu ya Maliasili na Utalii. Wao wakaunda *steering committee* ambayo ingesaidia kuona ni kwa namna gani sekta hii inaweza ikapewa kipaumbele katika kuhakikisha mazao ya misitu yanakuwa na thamani zaidi na kunakuwa na uongezaji wa thamani.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi sekta hii imekuwa ni sekta ambayo tunapoteza kwa kupasua mbao peke yake kwa sababu *recover rate* ya mbao ni ndogo sana ni kama 40% tu, mabaki mengine yote yanatupwa. Kwa hiyo, wenzetu kwenye *steering committee* wakikuja na *proposal* na moja ya *proposal* kubwa ilikuwa

ni kuangalia ni kwa namna gani wawe na utaratibu wa kitu kinaitwa mazao ya misitu yaani kuwa na mkakati wa mazao ya misitu yaliyohandisiwa ili kuongeza thamani.

Mheshimiwa Spika, sasa mazao haya ya misitu yamekuwa yakiongeza thamani kwa kiasi kidogo sana, lakini Kamati hii ilitakiwa ndiyo itoe mikakati namna gani inatuvusha kwenye jambo hili. Sisi tunawapongeza kwanza kwa kuanza na hiyo *framework* lakini Tanzania tunaheshimika sana duniani na Afrika kwa kuwa wazuri wa kuandika. *Framework* hiyo mpaka leo bado haijaanza utekelezaji wake ambao unaweza ukatupeleka huko ambako tunatakiwa tuende.

Mheshimiwa Spika, mimi nipende kusema, wakati haya yanatokea kuna jambo limejitokeza kubwa sana ambalo ni makampuni kutoka nje na hasa kutoka nchi ya Uchina na nchi nyingine ambayo yamekuja katika nchi yetu kama wawekezaji wa kuja kuchukuwa mazao yetu ya misitu kwa namna ambayo wao wamepewa vibali na Serikali.

Mheshimiwa Spika, niseme wazi, hao wawekezaji wamejenga viwanda vingi sana, ni viwanda ambavyo kwa mimi ambaye nafahamu kiwanda, tunasema sio viwanda ni mabanda na wana mashine ambazo unaweza ukazihamisha hapa, ukazihamishia pale na walianza Mafinga, wameendelea wanakwenda maeneo mengi na sasa wapo Njombe. Nini kinatokea? Sekta hii kupitia wawekezaji hawa inaendelea kuwatia umaskini wananchi wetu, wanaendelea kuwa na hali mbaya kuliko kule walivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, nilivyokuwa mdogo tulikuwa tunapasua mbao, tunajaza lori, tunapata pesa, tunalipa ada, leo hii wananchi wa Njombe na maeneo mengi ya Nyanda za Juu Kusini wamekuwa na hali mbaya kwa sababu wawekezaji wa Kichina wao ndiyo wanaoamua bei, wao ndiyo wanaoamua ubora, wao ndiyo wanaosema huu mzigo unafaa au haufai, lakini sio hilo tu, kuna utaratibu mzima wa soko ambao haueleweki, sisi tunasema

wawekezaji hawa inatakiwa Wizara ichukue hatua za haraka sana kuiokoa misitu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kinachotokea ni uchakataji na umalizaji wa misitu bila kuwa na mpango mahususi wa upandaji. Sio hilo tu, lakini wananchi wanauza hayo magogo kwa kampuni za Kichina hawapati manufaa kwa sababu wanapewa bei ndogo sana. Inasikitisha kwamba kenta ndogo au kenta ya tani tatu mtu ambaye amelima miti kwa miaka saba mpaka kumi anapata kiasi cha shilingi 130,000, ni fedha ndogo, hazimsaidii yeye, hazisaidii uendelezaji wa misitu na pia hazileti mapato, kibali cha kusafirisha *semi-trailer* wenzetu hawa wanalipwa 15,000 hiyo ndiyo *income* inayokwenda Serikalini, lakini halmashauri wanapata kati ya shilingi 150,000 hadi shilingi 200,000. Kwa hiyo, ukiangalia kwa ujumla wake uwekezaji wa namna hii hauna tija katika nchi yetu na haukubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimwombe sana Mheshimiwa Waziri achukue hatua za dharura na za haraka, tunafahamu mawili; suala la kwanza walikuwa wamepewa muda wa mwaka mmoja wakaongezewa miaka miwili na sasa vibali vyao vinatakiwa viishe itakapofika mwezi wa sita mwaka huu. Sisi Wana-Njombe tunasema hatutegemei Serikali itatoa vibali zaidi bila kufanya utaratibu utakaohakikisha ongezeko la thamani linawafaidisha wananchi wa Njombe na maeneo mbalimbali ya Tanzania ambao kwa sababu ya shida zao wamelazimika kuuza magogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho la muhimu zaidi, katika hali hii tunaona sasa misitu inateketea kwa hiyo, suala zima la kutunza mazingira ambalo nchi yetu ndiyo inalipigania kwa kiasi kikubwa linaonekana kwamba halipewi umuhimu unaotakiwa. Hawa Wachina/hawa wawekezaji wanachofanya wamekaa kwenye kiwanda ambacho ni mabanda wanangojea waletewe magogo, hawajali nani anatoka wapi, nani anapanda miti, wakati gani wanachotaka wao ni pesa; na tuna taarifa za kutosha kuonesha kwamba wawekezaji wa aina hiyo walianzia Congo, Uganda na huko kote walifukuzwa aidha kwa kuondolewa au kwa kuona *materials*

zimekwisha. Sasa wamekuja kwetu na sisi Wananjombe hatukubali kuwa kichwa cha mlevi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali iingilie suala hili na ifanye tathmini ya haraka ikiwezekana ndani ya miezi mitatu ili kuhakikisha kwamba wananchi, mfumo mzima wa bei, upangaji wa bei pamoja na kuona wananchi wanafaidika namna gani uangaliwe wakati vibali hivi vinafanyiwa tathmini. Kama halitafanyika hili katika hii miezi mitatu, hatuoni sababu kwa nini wawekezaji hawa ambao hawana tija waendelee kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wawekezaji hawa wana mambo yale ambayo huwezi kutegemea mwekezaji atakuwa nayo. Masuala ya *safety* kwao ni *almost zero,* masuala ya mikataba ya ajira ni kama hakuna, masuala ya malipo ni ya kinyonyaji. Tuombe sana Serikali yetu sikivu ilichukue hili na ndiyo maana *steering committee* iliamua kuanzisha huo utaratibu na ku-*focus* kwenye mazao ya misitu yaliyohandisiwa ili kuongeza thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilitegemea leo hii Serikali tungekuwa tumefika mahali tunasema tunakwenda eneo kama katikati ya Mufindi na Njombe – Makambako tunakuwa na *industrial park* kubwa, tunaanza kuleta mazao ya mbao pale, tunajenga viwanda pale, tunaweka *incentives* watu wajenge viwanda pale, tunaanza ku-*export* mazao yaliyohandisiwa kwenda nchi nyingine kutoka Tanzania kwenye *yard* kubwa ambayo itakuwa inaendeshwa na wawekezaji wa ndani wanaojiamini wa ndani na wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninasema kwamba jambo hili nalichukulia *very serious* na nitaomba maelezo kwa Mheshimiwa Waziri wakati tunakuja kwenye Kamati ya Matumizi, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi nianze kuungana na Waheshimiwa Wabunge waliompongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Serikali nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye Sekta ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Spika, naomba leo nijikite Madaba pekee katika mchango wangu kwa sababu ya fursa pana ambayo Madaba tunayo kwenye sekta hii ya utalii hasa na misitu. Kwenye sekta hizi mbili ya utalii kwa maana ya wanyamapori na sekta ya misitu.

Mheshimiwa Spika, ikolojia ya uchumi wa Madaba katika muktadha wa maliasili na utalii kwa sasa tuna maeneo mawili makubwa ambayo yanaweza kuleta mapinduzi ya kiuchumi Madaba. Eneo la kwanza ambalo tunalo nitaeleza kwa kina ni fursa kwenye uwekezaji wa mazao ya misitu na tayari Madaba kama halmashauri tumefanya jitihada ambazo nitazieleza hapa na nitaomba Serikali itusaidie na Watanzania wanaoishi Madaba waungane na Mbunge wao kuhakikisha kwamba hili tunalifanikisha.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa uwekezaji mkubwa uliofanyika na *Sao - Hill* Mafinga, uwekezaji unaofuata kwenye sekta ya misitu upo Madaba. Madaba tuna sehemu iliyopandwa miti inayozidi hekta 100,000, hekta 100,000 zimeshapandwa miti na ndani ya kipindi hiki kuanzia sasa mpaka miaka mitano tutaanza uvunaji mkubwa sana. Kwetu sisi Madaba kuna upekee kwenye hii sekta, ukiondoa ule uwekezji wa *Sao - Hill* ambao kwa sehemu kubwa ni *parastatal* kwa maana ya, ni uwekezaji wa Serikali. Asilimia kubwa ya uwekezaji wa Madaba ni kupitia sekta binafsi, kwa hiyo, mchango wa uchumi utakaotokana na uwekezaji kwenye misitu Madaba utakuwa mkubwa sana kwa mtu mmoja mmoja kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa Njombe hapa lakini pia kwa mapato ya Serikali yanayohusiana na kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Madaba tumeshachukuwa hatua, tayari tumeshaandaa mpango maalum wa kongani kujenga kongani la viwanda vya bidhaa za mbao. Tumeshatengeneza mpangokazi huo, tayari tumeshawekeza kwenye ardhi kwa maana tumeshatoa

hekari 25 kwa ajili ya hilo kongani; na kongani hili litazalisha bidhaa mbalimbali za viwandani ambazo Mheshimiwa Waziri anazifahamu zikiwemo nguzo za umeme, nguzo za kujengea, *marine boats*, *ply woods* na bidhaa nyingi ambazo nikizitaja hapa zitanichukulia muda lakini ndiko ambako tumeamua kwenda.

Mheshimiwa Spika, matokeo yatakayotokana na uwekezaji huu Madaba, kwanza ni uwekezaji ambao utatoa ajira kwenye mnyororo mzima wa thamani wa zao la misitu. Ninaposema mnyororo mzima maana yake toka kwenye uzalishaji wa miche mpaka kwenye uzalishaji wa bidhaa za mbao. Tunatarajia zaidi ya watu 150,000 mpaka 200,000 wataajiriwa kwenye mnyororo huu wa thamani wa mazao ya msitu na ninavyosema 150,000 mpaka 200,000 ninamaanisha ni zaidi ya mara tatu ya wakazi wote wa Madaba watakuwa wameajiriwa na uwekezaji huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake *population* ya Madaba ongeza mara tatu zaidi utapata watu ambao watafanya kazi kwenye sekta hii. Kwa hiyo, Watanzania wote wanaoishi Madaba watakuwa na fursa ya ajira, uwekezaji huu Mheshimiwa Waziri ninatamani uwe uwekezaji wa wewe na mimi. Tuache *legacy* kubwa kwenye nchi hii, tuache *legacy* kubwa kwa Wanamadaba kuhakikisha kwamba Wanamadaba na Watanzania 150, 000 au zaidi wanapata ajira kupitia uwekezaji wa kongani la viwanda vya mbao Madaba, kongani ambalo tutalijenga kwenye kijiji cha Kipingo ardhi ipo Mheshimiwa Waziri naomba utusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo mawili ambayo Mheshimiwa Waziri naomba unisaidie kwenye hili, jambo la kwanza naomba unisaidie tupate *feasibility study* upembuzi yakinifu na wa kina wa uwekezaji huu. Hatuna fedha halmashauri tunaomba Wizara mtusaidie, tuna maslahi mapana kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, ombi letu la pili tunaomba tukishamaliza *feasibility study* utusaidie kutangaza kupata wawekezaji wenye tija ambao tutawekeza nao kwenye mradi huu, hatupendi aina ile ya uwekezaji ambayo Mheshimiwa Deo Mwanyika hapa amesema.

Hatutaki aina ya wawekezaji ambao watawanyonya Watanzania, tunataka tunufaike na uwekezaji mkubwa ambao tumeufanya Madaba kwa miaka mingi. Kwa hiyo, tunaomba sana kwenye hili nimepewa marekebisho nimeambiwa ni kongani la viwanda sio kongano la viwanda niliongea Kingoni zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili nimesema ni uwekezaji kwenye maliasili za wanyamapori, pale Madaba pia tuna mradi mkubwa wa uwekezaji kwenye wanyamapori (*WMA*) pale kijiji Cha Ifinga. Tumemaliza hatua zote za awali Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana umetusaidia. Sasa tulipokwama, kwanza ule ni uwekezaji mkubwa hekta 37,000 za ardhi zimewekezwa kwenye maliasili ya wanyamapori, eneo ambalo litatoa fursa ya uwindaji kwa maana ya utalii wa uwindaji, tunao utalii wa picha lakini tutakuwa na utalii wa uvuvi (*sports fishing*) na utalii mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshafanya hiyo *analysis* na tumeridhika na Wizara imejiridhisha kwamba ule uwekezaji unawezekana. Hatua nyingine ambayo tumepiga ni hii ambayo sasa tumempata mdau ambaye yupo tayari kutusaidia kufanya *resource zone management plan* (*plan* ya ukanda ile ya uwekezaji). Mheshimiwa Waziri tunachoomba hapo, maombi yetu kwanza ni kuwezesha hii *resource zone management plan* ifanikiwe kwa haraka lakini pili kumpata mwekezaji mwenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili pamoja na kwamba hamjali gazzete tayari kwa ajili ya uwekezaji, tunaye mwekezaji ambaye anafanya kazi pale na tayari alishalipa zile *fees* mbalimbali; na moja kati ya fedha ambazo zimelipwa ni zile zinazohusu kwenda kwenye kijiji, mpaka sasa ni kama dola 20,000 Kijiji cha Ifinga kinaidai Serikali. Fedha zimelipwa kupitia Wizara kwa maana ya Hazina na Mheshimiwa Waziri wa Fedha nadhani atanisikia alipo, zimeshalipwa kupitia Wizara miaka minne mfululizo zimeendelea kulipwa lakini hazijafika kwa wananchi wa Ifinga.

Mheshimiwa Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri katusimamie hii fedha ni ya Watanzania, wananchi maskini wa

Madaba, dola 20,000 wakizipata wataenda kuboresha huduma zao pale. Fedha hii ni nyingi tunaomba sana utusaidie, manufaa mengine ni mengi nisingependa kuyafafanua hapa kwa sababu ninahofia muda.

Mheshimiwa Spika, mimi nikuombe tu Mheshimiwa Waziri utusaidie katika haya mambo mawili, uwekezaji wa Ifinga kwa maana ya *WMA* na changamoto zake zilizopo; na pale ambapo Serikali mnapaswa kufanya naomba mtusaidie kwa sababu italeta mapinduzi makubwa sana ya kiuchumi kwa Wanaifinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa pili, ni kongani la viwanda Madaba ambalo litaajiri zaidi ya watu 150,000 kwenye mnyororo mzima wa thamani wa mazao ya misitu. Haya mambo mawili yakifanikiwa yataleta mapinduzi makubwa sana ya kiuchumi ndani ya Madaba, ndani ya Mkoa wa Ruvuma na yatakuwa *model* ya uchumi kwa nchi yetu kama ambavyo Mheshimiwa Deo amesema hapa tumewekeza sana kwenye misitu. Hatuna *model* nzuri ambayo tunaweza tukaiiga, tukai-*copy* na kui-*paste*, nataka Madaba tutengeneze *model* ya kiuchumi ambayo maeneo mengine wataitumia kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi na Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, atafutatiwa na Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga ajiandae.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa mawazo yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya kwa ajili ya kulijenga

Taifa letu na tunaona hata juzi yupo Korea kwa ajili ya kupambana kuleta maendeleo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Angellah Kairuki na Naibu wake Mheshimiwa Dunstan Kitandula pamoja na Watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii wakiongozwa na Dkt. Hassan Abbas pamoja na Naibu wake Katibu Mkuu CP Benedict. Kwa kweli hawa watu wanafanya kazi kubwa sana ambayo inaleta tija katika maendeleo yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda mbali sana, juzi wakati tumeenda na Timu ya Wizara ya Maliasili na Utalii China niliona jinsi Mheshimiwa Angellah Kairuki alivyokuwa anahangaika pamoja na Katibu Mkuu Abbas walivyokuwa wanahangaika kutafuta makampuni ya kuleta utalii katika nchi yetu hii ya Tanzania. Walikuwa hawapumui, hata muda wa kunywa chai walikuwa wanaukosa kabisa, naomba niwape maua yao kwa kazi nzuri wanayoifanya na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuwaona wanafaa na hakika wanafaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali yangu kwa kutupa Mkoa wa Kagera hifadhi, tuna hifadhi tatu ambazo ni Burigi - Chato, Rumanyika, Karagwe na Ibanda - Kyerwa. Kwa kweli hizi hifadhi ni nzuri sana lakini kinachonisikitisha hazitangazwi hizi hifadhi zetu. Nilikuwa naomba Serikali yetu Tukufu iweze kutangaza hizi hifadhi kwa sababu kuna vitu vingi vya utalii katika zile hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa naomba sana Serikali yangu Tukufu, watu wa *immigration* wanasumbua sana watalii wanapoingia nchini. Kwa mfano watalii wanaoingilia Uganda, Entebe na Kigali wakiwa wanakuja Bukoba kuna *barriers* nyingi sana, wanahojiwa mpaka watalii wanakuwa hawana hamu tena ya kuja katika utalii wetu wa Mkoa wa Kagera. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Angellah Kairuki na timu yako muangalie hili muweze kutusaidia kuondoa hizi changamoto katika Mkoa wetu wa Kagera na miundombinu pia haipo vizuri sana katika hifadhi zetu, nilikuwa naomba na hilo mliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine katika Mbunga yetu ya Burigi, Chato, nakumbuka kuna hoteli ambazo *TANAPA* walizijenga pale, lakini hazina *facilities*. Hakuna vitanda hakuna nini, kwa hiyo, watalii wakienda pale hawawezi kukaa kwa muda mrefu, ili waweze kutalii.

Mheshimiwa Spika, Kagera kuna vitu vingi vizuri vya utalii na kuna kila aina ya utalii. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali yetu iweze kuangalia miundombinu mizuri katika hifadhi zetu za Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni mwaka wa tano kwa hizi hifadhi zetu, lakini hatuna sehemu ya kulaza wageni. Ninaomba sana kama kuna wawekezaji, basi wanaweza kuja kuweka hoteli katika Mkoa wetu wa Kagera, wanaweza wakajenga katika fukwe za Ziwa Victoria, ili wageni wetu wakija wapate sehemu zuri ya kulala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kama Kagera hoteli ambayo ni ya hali ya juu ni shilingi 120,000 ambayo kwa *USD* ni kama *dollar* 45 hivi. Sasa mtalii akija pale anakuwa na uwoga, anajiuliza hii ni hoteli gani ambayo ninalipa *dollar* 45? Anakuwa na woga anahisi labda hakuna usalama. Kwa hiyo, tukipata wawekezaji ambao wanaweza kuja kuwekeza katika Mkoa wetu wa Kagera, wakaweka hoteli nzuri za viwango vizuri *(Standard)*, itakuwa ni nzuri sana. Kwa hiyo, nawakaribisha sana wawekezaji katika Mkoa wetu wa Kagera, waje wawekeze katika fukwe za Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tuna changamoto katika hoteli zatu za Mkoa wa Kagera, hazina *Wi-fi* za kutosha. *Wi-fi* ambazo zipo katika hoteli nyingine ni za kusuasua, zina-*connect* na ku-*disconnect* kwa hiyo, naomba sasa hata ambao wana hizi hoteli waweke *Wi-fi* ambayo inaeleweka. Maana yake ni mgeni akitoka nje anataka aweze kuwasiliana na ndugu zake na familia kwa ujumla ambao amewaacha huko kwa hiyo, asipopata mawasiliano inakuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, naomba niongelee hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Shigongo juzi, kuhusu watu walioliwa na mamba. Kiukweli

ile hoja iliniumiza, yule mama aliyeenda kuchota maji, ili aje kupikia uji watoto, lakini hakuweza kurudi akapitilizia huko huko kwa kweli, imeniumiza sana. Sasa Mheshimiwa Waziri nakuomba sana wewe na Mheshimiwa Aweso mtatue hizi changamoto. Nimeona umesema kuna vizimba 50 mtaweka, kwa ajili ya kutega mamba na viboko. Sasa nakuomba wewe na Mheshimiwa Aweso mkae mchimbe visima sehemu ambazo kuna changamoto ya mamba na viboko, ili wale watu wapate maji wasiweze kwenda kule kwenye ziwa wakaliwa na hao mamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkifanya hivyo mtakuwa mmeokoa kizazi chetu. Mheshimiwa Angellah Kairuki wewe ni mama, unajua uchungu kama yule mama amewaacha watoto nyumbani, wamebaki wanamsubiri mama, kumbe mama maskini ya Mungu ameshaondoka, inasikitisha sana. Kwa hiyo, mkichimba hivyo visima itatusaidia sana katika kuondoa hayo madhara ya watu kupoteza maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kununua helikopta mbili ambazo zimekuja kusaidia kutoa wanyama wakali ambao ni tembo. Kwa kweli, nampongeza sana katika hili kwa sababu, kabla ya kununua hizi helikopta mbili Wizara ilikuwa inakodi kwa saa moja walikuwa wanatumia shilingi milioni tano, ambayo ilikuwa ni hasara kubwa kwa Serikali, lakini mama yetu kipenzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu ameweza kuliona hilo, akawapa Wizara hela ya kununua helikopta mbili, kwa ajili ya kuokoa binadamu dhidi ya hao wanyama ambao wanaleta madhara kwa binadamu na mali zao. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hiyo nzuri aliyoifanya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia, ninaipongeza sana Serikali yangu katika kuleta utalii katika nchi yetu ya Tanzania. Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu na Dkt. Ally Hassan Mwinyi wamefanya hiyo *Royal Tour* pamoja na *Amazing Tanzania*, kiukweli wakati ile *Amazing Tanzania* inafunguliwa nchini China, wale Wachina walifurahi sana wakasema lazima waje Tanzania kutalii. Kwa hiyo, ni kitu kikubwa sana ambacho

Marais wetu wamekifanya na kizuri zaidi ni walikuwa wanaongea kwa lugha yetu ya Tanzania. Kwa kweli, ilikuwa ni raha sana na mimi mwenyewe nilifurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu nyingine ambazo sijawahi kufika Zanzibar na humu Tanzania, vivutio ni vingi sana. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ninaomba mfuatilie *Amazing Tanzania*, kweli ni *real Amazing Tanzania,* inavutia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Dkt. Mwinyi aliweza kuonesha vivutio vingi sana kwa Zanzibar. Kwa kweli, naipongeza sana Serikali yangu na ninawahamasisha Watanzania tuendelee na sisi kufanya utalii wa ndani, siyo mpaka Wazungu ndiyo watoke nje waje kufanya utalii na sisi wenyewe tupende kufanya utalii katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Naipongeza sana Wizara ya Maliasili na Utalii.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga. Mheshimiwa Minza Simon Mjika, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi uliyonipatia ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Maliasili na Utalii. La kwanza, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan kwa umuhimu anaoipa hii Wizara na pia, kwa *commitment* aliyoiweka katika Wizara hii kwa sababu, amefanya mengi na tunayajua. Pia naomba niipongeze Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji Wakuu wakiongozwa na Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitakuwa na mambo matatu, la kwanza ni suala zima la tembo katika Mkoa wangu wa Singida. Kuna muda najiuliza thamani ya mwanadamu na thamani ya mnyama, sijui kama vinaendana, lakini kuna muda najiuliza maswali mengi na kutokana na majibu tofautitofauti yanayotolewa na Wizara, hasa jibu kubwa

likiwa kwamba, wale tembo wanapita kwenye eneo la mkondo wake wa njia ambayo huwa wanapita. Tunaelewa, lakini *population growth* pia, ipo kila siku kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, walipoweka *game reserve* Mwaka 2010 au 2005 siyo sawa na sasa hivi, *population* inakuwa makazi yanaongezeka na watu wanaongezeka. Sasa kama walikuwa wanalifahamu hilo na kama wanalijua, wanachukua *mechanism* gani, ili kuepusha haya madhara makubwa?

Mheshimiwa Spika, mimi niseme ukweli, kwenye Wilaya yangu ya Manyoni na Ikungi imekuwa ni taharuki kubwa, kwanza kwa wakulima wetu wa korosho, tembo wanapita wanaharibu mazao na usalama wa wananchi wetu umekuwa ni mdogo. Hasa tukizingatia vijijini wanatumia sana pikipiki kama *means of transport*. Sasa kama mtu ana dharura ya kwenda hospitali usiku ataendaje? Kwa hiyo, wananchi wetu wamekuwa waoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninaomba niiombe Wizara wajitahidi kwa sababu, najiuliza pia, kwani nchi za wenzetu hawana hizi hifadhi? Na kama wanazo, wao wame-*control* vipi na sisi tunashindwa vipi? Kwa hiyo, ni lazima tujifunze pia, kwa wenzetu wamefanyaje kwa sababu, haya mambo yapo hata kwa wenzetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, mimi ninaomba, hili suala ni muhimu na ni *sensitive*. Unapomfanya mwananchi anakuwa na uoga, hawezi kuamka asubuhi kwenda shambani na hawezi kufanya mambo ni kama giza limeingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tulikuwa na Mkutano na Katibu Mkuu, watu walipata madhara ya tembo na wanahofu usiku watarudije majumbani. Kwa hiyo, hilo liko chini yako na ninaamini kwa sababu, unafanya kazi nzuri, basi utaenda kutusaidia sisi Mkoa wa Singida kwenye suala zima la tembo.

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili ni utalii. Kwa kuwa, tumeona sekta ya utalii na tunajua ni sekta muhimu kwa nchi yetu. Inachangia Pato la Taifa, lakini pia, ni sekta ambayo ni *income*

*generation* ambayo inatusaidia, tunapata pesa kwa ajili ya zahanati, elimu yetu na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, hapa nazungumzia suala zima la *returning visitors*. Pamoja na juhudi zilizofanywa na Mheshimiwa Rais mwenyewe, Wizara wanafanya kazi kubwa sana ya kutangaza utalii na watalii wameongezeka kwa kiasi kikubwa, lakini hoja yangu hapa ni jinsi gani sasa hao *returning visitors* watarudi tena Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninachotaka kukiongelea zaidi ni uzalishaji wa watoa huduma. Ni jinsi gani tunavyozalisha na tunavyowatengeneza wanaotoa huduma, ili wamvutie yule mtu kuja kwa sababu, tutawaleta wengi, lakini *rate* ya wanaorudi ikoje?

Mheshimiwa Spika, sijajua tathimini yake ikoje, lakini isije kuwa wanakuja halafu hawarudi. Sasa kama wanakuja halafu hawarudi, katika *long term planning* za kipato cha taifa itafika mahali tunaanza kuona watu wanapungua, lakini kwa sababu, labda hatujajua tufanyeje, ili namba ya *returning visitor* iwe kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna nchi ambayo mtu anataka kwenda kila mwaka. Ni kwa nini isiwe Tanzania, anataka kuja kila mwaka? Kwa hiyo, suala la uzalishaji wa watoa huduma liwe chini ya Wizara, wana chuo kinachotoa mafunzo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ni uhifadhi, wako vizuri, wako *intact*. Ukiongelea misitu wako vizuri, lakini utalii mmeacha soko huria la watoa huduma na mbaya zaidi mmewaachia *VETA* ndiyo wanasimamia kutoa huduma. Sasa Mheshimiwa Waziri wewe ndiyo unaesimamia kutangaza na kuendeleza utalii, ukimuachia *VETA,* yeye ni mafunzo ya ufundi, hawezi kujua *feeling* ya mlaji wa mwisho ikoje. Wewe mwenye Wizara ndiyo unajua mlaji wa mwisho ambaye ni mtalii anataka *satisfaction* gani, ili aweze kurudi tena Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninaomba uzalishaji wa watoa huduma iachiwe Wizara *100 percent* kwa sababu, hiyo ndiyo inayojua uchungu. Ni sawa na uchungu wa mwana anaujua mzazi. Wewe

ndiyo unajua kwamba, watalii wanataka nini. Sasa *VETA* ni ufundi. Kwa hiyo, kama unavyo-*control* chuo chako, *control* na uzalishaji wa *private sector* wanazotoa kwa wahudumu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hawa *tour guide, tour chef, waiter* na *waitress*, kuna muda hata *mood* zao siyo nzuri na kuna muda ni mapokea. Mheshimiwa Oliver amesema mmeenda nje, hata hamjalala mnatangaza, wewe na Katibu Mkuu wako, lakini mwisho wa siku haumpokei wewe *airport* wala humpokei wewe popote, watoa huduma ndiyo wanaokusaidia baada ya ile kazi kubwa ya kutangaza utakayokuwa umeifanya. Kwa hiyo, hilo jukumu ipewe Wizara kwa asilimia 100, ili mlaji na mtumiaji ajue na mwisho yeye ndiye atakayejua matokeo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilisema niliseme hilo kwa sababu, ni muhimu na kuna *gap* kubwa sana la *returning visitors,* hasa kwa watoa huduma. Mimi kwa uchunguzi ninavyoona ni jinsi tunavyowapokea na kuwahudumia wanapokuwa hapa. Mheshimiwa Waziri kwa hiyo naomba ulichukue hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni suala zima la masoko ya utalii. Sekta ya utalii, kama nilivyosema, ni muhimu sana na ni *income generation* katika nchi yetu na inaongeza Pato la Taifa. Wizara ya Maliasili kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje, wangeweka hawa waambata katika Wizara zetu za Maliasili na Utalii. Kama kuna Idara ya Usalama na Idara ya Uhasibu, kwa nini hamna mtu anayeshughulikia utalii katika balozi zetu au ofisi zetu za ubalozi?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, yule ndiyo ataweza kuwa na *daily activities* ya kuainisha ni kongamano gani katika nchi hiyo na ni sehemu gani katika nchi hiyo ninaweza nikatangaza utalii kuliko kusubiri Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu watoke Tanzania waende sijui Uturuki ndiyo waanze kuainisha na kufanya. Kama kutakuwa na mtu anayekaa ofisini kazi yake ndiyo hiyo utampa *target, KPI* utampima *target* zake, lakini pia, utaangalia ni jinsi gani amefanya kazi kwa kutokana na hiyo *target*. Hiyo ndiyo itakuwa *daily operation* ya kwake. Kwa hiyo, kama zilivyo *department* nyingine zilizopo kwenye

balozi zetu na kwa sababu, sekta hii inaingiza kipato cha Taifa na ni sekta muhimu tunayoitegemea, nayo iwe na waambata hawa wa maliasili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, balozi anakuwa mhasibu, au balozi mwingine ameteuliwa, lakini yeye ni daktari, au balozi hana ile *exact knowledge* ya utalii kwa hiyo, *the way* atakavyoelezea au *commitment* atakayokuwanayo haitakuwa sahihi, lakini hawa wakiwekwa watakuwa chini ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii,. Ataweza kuwasimamia, ataweza kufanya *checklist* na ataweza kuwapa *commitment* na *target* za ku-*archive*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naona hilo likifanyika ni muhimu sana kwa sababu, hii ni sekta muhimu ya kutuingizia Pato la Taifa, itatusaidia kupata watalii wengi na itatusaidia pia, kujua tatizo ni nini hasa kwa wale *returning visitors,* wamekutana na changamoto gani Tanzania au kuna jambo gani? Yaani kutakuwa na dawati *special* ambalo ataweza kuwa-*accomodated* na tukapata hayo makosa yetu, ili tujirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninatoa pongezi nyingi. Naomba kushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Minza Simon Mjika.  Soud Mohammed Jumah, ajiandae.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nami niungane na wenzangu kwanza kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu yao yote kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Utalii kwenye hotuba yake kwamba, tokea kuzinduliwa kwa Makala ya Tanzania *the Royal Tour*, tumeona utalii umeendelea kuimarika nchini

kwetu, watalii wameongezeka na Pato la Taifa limeongezeka. Kwa idadi hiyo, basi tumeona watalii wa kimataifa wameongezeka kutoka 620,000 mwaka 2020 hadi kufikia watalii 1,800,000 mwaka 2023 sawa na asilimia 191.

Mheshimiwa Spika, vilevile Pato la Taifa limeongezeka kutoka dola za Kimarekani bilioni 0.7 kwa mwaka 2020 mpaka kufikia dola bilioni 3.3 kwa mwaka 2023 sawa na asilimia 371. Hii ni kazi nzuri iliyofanywa na Wizara kwa kushirikiana na Serikali yetu, hususan kupitia Filamu ya *Tanzania the Royal Tour,* ambayo imeongeza watalii wengi mpaka kufikia idadi hii ya kuongeza pato na kuongeza watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee pia, kuipongeza Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 walijiwekea lengo la kukusanya mapato ya shilingi bilioni 773, lakini mpaka kufikia Februari, 2024 waliweza kukusanya shilingi bilioni 664, sawa na 86%. Wizara imefanya kazi nzuri, wanastahili pongezi kwa hilo. Tunaendelea kuwatia moyo, lakini waendelee kuongeza bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa wito na rai kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na timu yake waendelee kuongeza ubunifu katika sekta hii na waangalie namna ya kutafuta vivutio vingine, ili kuendelea kuongeza watalii na Pato la Taifa. Kwenye Wizara hii tumeona vipaumbele vyao vinne, ambavyo ni wanyamapori, mambo ya kale, misitu na nyuki na sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye misitu na nyuki, imeweza kufanya vizuri kupitia akinamama. Tumeona Mkoa wa Arusha na Manyara kuna vikundi 109 ambavyo vimenufaika na sekta hii, vikundi hivi vimeweza kupatiwa elimu kuboresha na kuongeza thamani ya zao la asali. Wanatengeneza *lotion*, mafuta ya kupaka na sabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatamani kuona elimu hii isiishie Manyara na Arusha. Kuna akinamama hapa Dodoma wanavuna asali, kuna akinamama Tabora wanavuna asali na Iringa kote wanavuna asali. Tunatamani kuona Wizara inawekeza nguvu kuwasaidia akinamama

hawa ambao wanashughulika na mazao ya asali, wawape elimu, ili waongeze thamani mazao haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara hii ikae na kundi la kinamama ambao wanashughulika na zao hili la asali wawaunganishe na *GS 1* na *TBS,* kwa ajili ya kupata *barcode,* ili tuanze kuziona bidhaa hizi kwenye ma-*super market*. Tunatamani kuona bidhaa hizi zinazunguka Tanzania nzima hata watalii wanapokuja zifike kwenye hoteli, lakini *package* ziwe nzuri zaidi na waweke nembo ya Tanzania pale. Hata wale watalii wanaponunua na kwendanazo huko ni njia ya kutangaza bidhaa zetu na mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namuomba pia, Mheshimiwa Waziri wa Utalii na timu yake waangalie sasa namna ya kuongeza watalii wa ndani kwenye Taifa letu. Tumeona watalii wa nje wanafanya vizuri sana, lakini kwa idadi ya Watanzania ambao tuko zaidi ya milioni 60 na idadi ya Watanzania ambao wanafanya utalii wa ndani bado hailingani, uwiano hauko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona kipindi Mheshimiwa Rais anafanya Makala ya *Tanzania the Royal Tour,* vikundi vingi vya kinamama na vijana vilihamasika kufanya utalii, lakini ikafika mahali ile hamasa ikapotea. Ni lazima sasa Wizara iangalie ni nini kimesababisha hamasa ile kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmojawapo ambaye nilihamasisha vikundi vya vikoba vya kinamama Dar es Salaam kwenda kufanya utalii. Tukifika kule tunatamani kuona Wizara inatambua mchango wa wanawake wajasiriamali wanaojikusanya kwa fedha zao wanakenda kufanya utalii, wapate hata *certificate of appreciation.* Kwamba, vikundi hivi vilikuja, vikasajiliwa, kukawa na kitu cha ziada cha kuwafanya siku nyingine warudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vikundi vya kinamama Tanzania vimegawanyika kwenye makundi matatu. Kuna vikundi ambavyo vinajiweza sana, kuna vikundi ambayo viko kati na kuna vikundi vidogo sana vya chini ambavyo mitaji yao ni midogo sana. Vile

vinavyojiweza vipatiwe elimu na Wizara ya namna gani wanaweza kuwekeza kwenye sekta ya utalii. Tunatamani kuona wanawake wawekezaji kwenye sekta hii kutoka Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakuta Wizara hii inaandaa makongamano, hususan ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam. Kuna kuwa na makongamano mengi makubwa, lakini ukiangalia namba ya waalikwa na makundi, huoni makundi ya wanawake wa *VIKOBA* ambao wana mitaji kuitwa kuona pale kuna nini na wakajifunza nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii kwa kweli inasikitisha sana na haileti afya. tuna Kijiji cha Makumbusho pale Dar es Salaam, mule ndani kuna nyumba za makabila yote, kuna ngoma za asili za makabila mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam ni mkoa ambao una watu wengi kuliko mikoa yote, kuna watoto wanazaliwa Dar es Salaam ame- cram-ishwa tu kwamba wewe ni Muhaya, wewe ni Mnyiramba, wewe ni Mchaga, lakini yaani amekariri tu kwamba akiulizwa wewe kabila gani anaitaja kabila lake hajui mababu na mababu huko nyuma walikuwa wanaishi nyumba za aina gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto shuleni wanasoma kwamba mahindi yalikuwa yanavunwa yanawekwa kwenye vihenge anakiona tu wenye kitabu hajui kinafananaje lakini mule ndani vipo. Tunaomba sasa Wizara iweke nguvu kubwa kutangaza kile kijiji *at least* hata mara moja kwa mwezi kuwe na utaratibu yaani kama hamasa fulani ifanyike mara moja kwa mwezi, kuwe na ngoma zinacheza mule, vyakula vya asili vinapikwa mule watu wakawa wanaenda kwa wingi wanabeba na watoto kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukienda pale wikiendi ukipita nje unasikia kuna ngoma zinalia ndani hakuna watu unaweza ukapita nje *parking* zimejaa hakuna hata pakuweka gari watu wote wapo *bar*

pale wanakunywa pombe wanaangalia mpira ndani hakuna watu. Tunaomba Wizara iongeze nguvu kutangaza kile kijiji kina vivutio vingi na vizuri. Kuna kina mama pale wanabiashara zao lakini hakuna wateja watu wengi wakija wakishuka wanakaribishwa wote wanaishia *bar* hakuna anayeenda mule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama matangazo yakiwa ya kutosha watu wakawa wanaenda kwa ajili ya maonesho wataweza kuwasaidia na wale wakina mama ile sehemu sasa imekuwa maarufu kwa ajili ya ile *bar* na vikao vya harusi, nje pote pamejaa yani ni vikao tu vya harusi lakini ndani kwenye makumbusho hakuna watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu lingine kwa Wizara wajaribu kuweka utaratibu wa kupata walimu wazuri lakini Wizara hii yani iungane ikae na Wizara ya Uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji waangalie namna ya kuanisha fursa kwa ajili ya wakina mama kuwekeza katika sekta ya utalii. Wakina mama wana mitaji wanatamani kuwekeza lakini bado hawana upeo na ile elimu ya kuwa wawekezaji kwenye sekta ya utalii, hii sekta ina fedha. Wakina mama mitaji kama nilivyosema tayari wanayo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri na timu yako kaeni na watu wawekezaji ainisheni zile fursa piteni kwenye mikoa kutaneni na vikundi vile vikubwa na vya kati muhamasishe namna ya kufanya uwekezaji katika sekta ya utalii hili linawezekana kabisa na mkianza hiyo *program* niwakaribishe sana kwenye Mkoa wa Dar es Salaam nitawakutanisha na vikundi vikubwa ambavyo vinatamani kuwekeza Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, niombe mnapokuwa na makongamano mbalimbali ya sekta hii ya utalii tunaomba mialiko kwa ajili ya vikundi vya wakina mama waje wajue nini mnafanya wanaweza kuwekeza wapi lakina pia na vijana. Tuna vijana wengi wamemaliza vyuo wana *idea* nzuri sana, wanatamani kutangaza utalii wa ndani wanapokuwa na maandiko yao na *idea* zao kaeni nao wasikilizeni hawa watakuwa mabalozi wazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumieni vijana na wakina mama hawa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Minza Simon Mjika, atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege ajiandae.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi nzuri kama hii kuingia ndani ya Bunge hili. Pia, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyofanya kazi nzuri sana katika nchi yetu tunampongeza Mama yetu tumpe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maliasili mdogo wangu Mheshimiwa Angellah Kairuki kwa kazi nzuri ambayo anafanya, sekta hii ina changamoto sana lakini tunaona ni jinsi gani anavyopambana. Nampongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Kitandula kwa kazi nzuri ambazo anafanya pamoja na Mheshimiwa Waziri wake.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla nishukuru sana Katibu wa Maliasili pamoja na Naibu Katibu na viongozi wote wa Maliasili hongereni kwa kazi nzuri ambazo mnafanya. Napenda niingie moja kwa moja katika Mkoa wangu wa Simiyu napenda nimpongeze kuna mwekezaji ambaye anaitwa *Mwiba Company Limited* huyu mwekezaji wetu kwa kweli ana tija katika Mkoa wetu wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, kwanza katika Kijiji cha Makao amefanya wanafunzi wanapata chakula, wanafunzi 850 katika Shule ya Msingi Makao wanapata chakula kila siku. Hii imeleta ufanisi katika upande wa elimu wanafunzi wameacha kabisa utoro wanahudhuria shule,

wanapata chakula na masomo yanaenda vizuri. Si hapo tu amepeleka baiskeli 200 sekondari kwa wanafunzi wa Makao kwa hiyo zina thamani ya shilingi milioni 40 tunamshukuru sana huyu muwekezaji wetu. Amejitahidi amejenga nyumba za walimu, amekamilisha madarasa, amejenga nyumba za wafanyakazi wa afya, kwa hiyo tunampongeza sana kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Mkoa wetu wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, vilevile nisisahau kumpongeza Mkuu wetu wa Mkoa wa Simiyu *Mr.* Nawanda kwa kweli anafanya kazi kubwa sana, tunamwona anavyokimbia huku na huku anahamasisha maendeleo, anasimamia maendeleo kweli Mheshimiwa Rais hakukosea amutupa kijana mchapakazi Mungu ambariki sana na kuendelea kumpatia afya njema.

Mheshimiwa Spika, ninapenda niende katika upande wa Kijiji cha Makao, Kijii cha Makao kimepakana na Hifadhi ya Ngorongoro kwa kweli ni wadau wapekana ni pua na mdomo, lakini kuna mambo ambayo sasa nilikuwa nataka nimshauri dada yangu Mheshimiwa Angellah Kairuki (ndugu yangu) aweze kunisikiliza kwa makini. Moja wale Wanakijiji wa Makao huwa wanapita katika ile Hifadhi ya Ngorongoro wakielekea Enduleni, Sinoni na Hospitali *KCMC* na sehemu zingine zote kwa ajili ya kupata mahitaji yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni moja kunakuwa na tozo ambazo ni lazima mtu atoe ndiyo apite pale hata kama anaenda kununua mahitaji yake ya kila siku, si kwamba anaingia kutalii mule hapana anapita tu kwenda kupata mahitaji yake ya kila siku. Tozo zenyewe zimekaa kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 0 – 5 wanapita bure, miaka 6 – 15 ni shilingi 2,360 kwenda na kurudi unalipia mara mbili lakini kuna kuanzia miaka 16 mpaka mpaka 100 ni shilingi 11,800 wananchi hawa kwa kweli wanalalamika sana. Wakati mwingine unaweza ukakuta mzazi anapelekwa hospitali anapita pale ana watu watatu, wanane pengine anahitaji kuongezwa damu lakini lazima wale watu watozwe pesa mimi naona hiyo kama vile haijakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna mzazi anapeleka mtoto shule anaenda kununua mahitaji yake ya kila siku lazima atozwe ile pesa. Nilikuwa naomba sana nina ombi langu Mheshimiwa Waziri unisikilize mimi kwa maoni yangu niliona kwamba wale wakazi wa Kata ya mwisho ya Makao wanapotaka kuingia kwenye ile hifadhi kwa sababu wanapita tu kwenda kununua mahitaji yao, nilikuwa naomba waandaliwe hata kama ni kadi maalumu. Kwamba hii kadi inamtambulisha kuwa huyu ni mkazi wa Kijiji cha Makao anapopita basi anaonesha ile kadi anapita, anaenda na anarudi kwa sababu si mtalii.

Mheshimiwa Spika, watu wa kule wana maisha ya chini ni wakulima na wafugaji wadogo. Wale watu wanalalamika sana nimeshakaa nao zaidi ya mara mbili na baada ya Bunge hili nitakuomba sana dada yangu na mdogo wangu Mheshimiwa Kairuki twende katika Kijiji cha Makao tukakae na wanakijiji kule utawasikia wanavyoeleza changamoto zao, wanaomba msaada sana kwa hilo. Hatukatai kwa magari ambayo yanapita pengine yanaenda Arusha wale tunakubali wachangie lakini kwa wale wanakijiji wa kata ya pembezoni hapo tunaomba muwasamehe kwa hilo, hilo ndilo lilikuwa ombi langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaenda upande mwingine kwamba katika hiyo barabara ya kutoka Makao kuingia Ngorongoro mpaka Arusha sasa hivi ni barabara ya *TANROADS,* barabara ile kwa kweli ni mbovu sana haifai kabisa hata magari yakipita mule ni shida. Wakati mwingine mnakwama njiani yaani ni hivi na hivi barabara ile imeharibiwa sana, miundombinu imeharibika kwa ajili ya maji. Tunaomba basi muangalie hilo, hii barabara iweze kutengenezwa na baadaye ikae vizuri ili hata watalii wetu wanapopita wapite bila shida tupate watalii ambao ni wazuri kesho na kesho kutwa tena warudi. Si mtalii anafika sehemu shuka tembea kwa mguu, shuka tembea kwa mguu haipendezi. Tunaomba barabara kama ile iweze kukamilishwa na watu wale waweze kuishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nishukuru sana kwamba huyu Mwiba amekuwa ni msaada mkubwa sana katika Mkoa wa Simiyu. Kwanza kama nilivyosema kwamba katika Kijiji cha Mwajimoso

wamejenga madarasa mawili na nyumba moja ya walimu *two in one* yenye thamani ya shilingi milioni 20,800,000 walimu wanakaa pale vizuri na madarasa yamejengwa vizuri kwa hiyo mimi nazidi kumpongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna kijiji kingine kinaitwa Mwamhongo yeye amejenga nyumba ya *three in one,* wanakaa mule wafanyakazi wa afya kwa kweli nyumba ile ni nzuri sana nimeshafika pale na nimeiona. Kwa kweli ni nyumba ambayo inapendeza sana wanakaa wafanyakazi watatu ipo vizuri, imejengwa vizuri ina geti safi. Kwa hiyo tunamshukuru sana huyo mwekezaji kwa ajili ya huduma nzuri ambazo anazifanya katika Mkoa wetu wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingine nazidi kuzileta kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri anazoendelea kufanya. Sasa hivi tunaona jinsi watalii walivyoongezeka nchini, watalii wanaongezeka kila kukicha hii ni kwa sababu mama yetu amekuwa mtu wa kwanza katika *Royal Tour* amehamasisha vizuri, watu wengi wamependa, nchi nyingi zimependa zinakuja kuangalia hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kingine ambacho napenda niongee sasa ukielekea katika hicho Kijiji cha Kakesio kwenda hospitali kwenye matibabu. Mtu anaelekea labda hospitali kwenye matibabu, kupeleka huduma mbalimbali za kiafya wanafunzi wanaenda kutibiwa kule kama nilivyokwambia, wanaendelea kutozwa pesa hicho kitu wanalalamika sana. Hata sasa hivi nimepata meseji nyingi kwamba Wizara ya Maliasili inaendelea kutoza, tunaomba mlisemee hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nilikuwa na mambo machache sana ya kuongea, mengi niliyaongea ninaomba sana dada yangu na mdogo wangu Mheshimiwa Angellah Kairuki fuatilia jambo hili ili tuondoe kero kwa Wananchi wa Mkoa wetu wa Simiyu. Vinginevyo maliasili mnaenda vizuri mnajitahidi. Kingine ambacho nataka niwapongeze sana maliasili ni hili la kugundua hili bomu la machozi baridi sasa hivi hatuna shida kivile tembo wapo ndiyo lakini tumepata mabomu baridi

mikoani; halmashauri zetu ziweze kununua na baadaye wananchi wetu waweze kuishi vizuri.

Mheshimiwa Spika, mabomu yale yakipigwa yana mlio mkubwa kwa mfano lile bomu la nyuki, nyuki wale wanavyopoga kelele hakika tembo lazima akimbie kwa sababu hapendi mlio wa nyuki. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri napenda nikupongeze sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nashukuru leo nilikuwa na hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na uchangiaji wapo wageni waliyoingia hapa watatangazwa ili watoe nafasi kwa wageni wengine waliopo nje wanaotaka kuingia humu ndani.

Tunao wageni 45 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ambaye ni Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo hawa ni wanafunzi, walimu na wazazi kutoka Shule ya Sekondari Daora ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 42 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni Taasisi ya Mtetezi wa Mama kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo wanafunzi 105 wa Shule ya Msingi Cannosa ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 90 na walimu 10 ya Shule ya Msingi; sasa sijajua hii ni *mount* au Mtakatifu haya Mt. Mary Goreti, nadhani Mtakatifu Mt. Mary Goreti ya Jijini Arusha, karibuni sana maana naona ma-*sister* pale itakuwa ya Mtakatifu Mary Goreti ya Jijini Arusha karibuni sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nilishamtaja Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, na mimi kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii na kuanza tu ningependa kumshukuru *Allah Subhanahu Wa Ta'ala* kwa kutujalia kuamka kuwa wazima na kutufikisha katika Bunge lako hili na kuendelea na shughuli hizi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika ningependa kuwasilisha shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake ikiongozwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa sekta mbalimbali zinazotengeneza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, nafikiria sote ni mashahidi wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha Bajeti yake hapa amezungumza mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa watalii karibu kwa 50% lakini hali kadhalika ukusanyaji wa maduhuli umeongezeka kwa asilimia kubwa. Hali kadhalika tukiangalia hata ile tansia au sekta ya nyuki ambayo kwa kipindi kirefu tumekuwa tuki-*struggle* kuipandisha hadhi sasa hivi tumeanza kuona kuna dalili kubwa ya kuweza kuleta ufanisi na hatimaye kutoa mchango mkubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kwa kweli na watendaji wako mnahitaji sifa na mnafanya kazi nzuri. Sambamba na hayo mchango wangu ningeanza kwenda moja kwa moja kwenye suala zima la utafiti na elimu. Hapa ningeanza kwa kuwapongeza wenzetu wa *TAWIRI* kwa kufanikisha kongamano la nne kama sikosei au la tano lile ambalo limefanyika mwezi wa Disemba mwaka jana na kwa kweli Mheshimiwa Waziri una timu nzuri ya watafiti kwa sababu wameweza kuwaleta watafiti kutoka maeneo mbalimbali duniani na wakakusanyika Arusha takribani kwa siku tatu na kuweza kuja na maazimio mbalimbali ambayo nategemea maazimio yale tutafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika ningependa vilevile kuwapongeza wenzetu wa *TAFORI* nimeona tangazo lao limetoka kwamba na wao watakwenda kuwa na kongamano la Kimataifa la kisayansi ambalo linaenda kufanyika mwezi Disemba mwaka huu.

Kwa hiyo niombee kila la kheri lakini pia kumwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba bajeti inatengwa ya kutosha ili kongamano hilo likawe kongamano la maana kwa sababu linakwenda kuwajumuisha watafiti kutoka maeneo mbalimbali ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika ombi langu hapa tujitahidi kuwahamasisha vijana wetu wa vyuo vikuu: *SUA*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *SUZA* na vyuo vikuu mbali mbali ili tuhakikishe kwamba wanleta *paper* zao na wanapata nafasi kuweza kufanya uwasilishaji na yale maazimio ambayo yatatokana na kongamano hilo basi tuyafanyie kazi. Pia niwapongeze pia wenzetu wa *Tanzania Association of Foresters (TAF)* na wao wamefanya mkutano wa mwaka mwezi uliopita na pia walikuwa na kongamano la siku moja na lile kongamano lilikuwa la maana sana kwa sababu suala zima la hewa ukaa ambayo sasa hivi ndiyo *topic* ya mjini limezungumzwa na mikakati mbalimbali ilikuwa imepangwa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, kuna vyuo vyetu hivi: Chuo cha Misitu Olmotonyi Arusha pamoja na Chuo cha Mweka cha Wanyamapori kweli hzi ndiyo chemichemi za elimu kwa Tanzania katika masuala mazima ya elimu ya misitu na elimu za wanyamapori. Maprofesa wengi, madaktari wengi na wataalamu wengi wakubwa wametokana na vyuo hivi hata wale ambao wameenda *SUA* wengine kwanza walianzia *either* Mweka au walianzia *FTI* Olmotonyi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hivi sasa uingiaji wa wanafunzi katika vyuo vile umepungua sana na zaidi kwa sababu sasa hivi ili mtoto asome katika vyuo vile inabidi mzazi aangalie mfuko wake akamsomeshe lakini ukiangalia mahitaji yetu ni makubwa kwa ajili ya wale vijana. Sasa ningeomba tu Mheshimiwa Waziri utenge fedha maalumu kama ilivyokuwa zamani ili wale ambao wanaenda kusoma katika Vyuo vya Misitu Olmotonyi, Mweka, *FIT* na chuo cha Nyuki Tabora basi angalau kuna unafuu Wa ada wazazi wachangie kiasi lakini Serikali ikiwezekana ibebe huu mzigo ili wanafunzi wengi zaidi waweze kusoma kule na kuweza kupata nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ni suala zima la uharibifu wa misitu. Uharibifu wa misitu ni mkubwa na kama wataalamu wanavyosema kwamba karibu hekta laki tatu kwa mwaka zinapotea za misitu na sababu kubwa za upoteaji ni uvamizi wa maeneo ya misitu, uchomaji wa moto hovyo au moto kichaa lakini pia ukataji wa misitu hovyo.

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba kuuliza tu nini tufanye ili kuweza kusitiri hali hii? Kwa sababu kama unavyojua kila Mheshimiwa Mbunge anayesimama hapa anawalaumu Askari Usu au Askari wa Jeshi la Uhifadhi. Tunasema tembo wametoka misituni lakini ukweli hii misitu ambayo tunahifadhi ndiyo vyanzo vya maji, vyanzo vya nishati, vyanzo vya utalii tunaouzungumza ndiyo vyanzo vya kila kitu tunachokizungumza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tutaruhusu misitu hii itoweke tunakwenda kuhatarisha maji, tunakwenda kuhatarisha nishati, tunakwenda kuhatarisha vyanzo vya utalii. Kwa hiyo niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu wakati tunachangia basi tuweke mizani sawa au tuweke *balance* ya kujua kwamba hii misitu ambayo inaharibika au inahifadhiwa au inavamiwa basi ndiyo umeme ambao tunautegemea ambapo kila mtu angependa aunganishe umeme kutoka kwao.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala zima la Jeshi Usu, Jeshi USU tumeambiwa hapa na Mheshimiwa Waziri kwamba kuna askari wetu wanne walifariki katika kipindi cha mwaka huu, zaidi ya askari arobaini wamejeruhiwa. Sasa unaweza ukaona tatizo ambalo linawakabili askari wetu wa Jeshi la Uhifadhi. Tulishazungumza hapa maslahi ya hili Jeshi bado hayajakaa sawa. Kwa hiyo, ile sheria ya *scheme* ya kuboresha maslahi ya hawa maaskari wa Jeshi USU au Askari wa Jeshi la Uhifadhi tuletee tuipitishe ili hawa vijana wetu wanapoteza maisha, wanakuwa vilema, wanaacha wajane, wanaacha wazazi, wanafariki lakini maslahi yao bado yako duni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ningeomba ukalishughulikie hili. Maslahi yao bado ni duni lakini kazi wanayoifanya ni ngumu nani ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala zima la uratibu wa masuala mazima ya maliasili kule Zanzibar, na hili ningeomba ukaliangalie kwa sababu kuna kipindi hapa Mr. Ambwene alifanya kazi nzuri sana, alijaribu ku-*facilitate* utayarishaji wa kanuni kwa ajili ya kuweza kuratibu masuala mazima ya maliasili ya wanyamapori kule Zanzibar. Sasa naona kama suala limekwama njiani, sasa tusaidie ili tupate dawati na tuunde Kamati ya wataalam ya usimamizi na uratibu ili tuweze kuhakikisha kwamba masuala yale ambayo yanahusu mikataba ya kimataifa kama *CITES* yanaratibiwa vizuri baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. *(Makofi)*

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege atafuatiwa na Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga ajiandae.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza niitumie kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoinyanyua juu sekta hii ya utalii. Kwa mfano, yeye binafsi ameshiriki kikamilifu katika kuitengeneza filamu ya *royal tour* ambayo imefaulu sana katika kuitangaza nchi yetu huko nchi za nje, vilevile kuleta watalii wengi nchini, hongera sana Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri Kairuki na timu yake yote kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii. Pia nitumie fursa hii kuipongeza TAWA kwa jinsi ambavyo tunashirikiana nao vizuri katika Jimbo langu na kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizi, bado tuna tatizo kubwa sana la mamba katika Jimbo langu la Mwibara, watu wanaendelea kuuawa. Kwa mfano, katika wiki moja iliyopita watu wawili wameuawa na mamba, sasa kwa vile mashambulizi haya yanaendelea na watu wanaendelea kufa, ni lazima tukiri kwamba

kwanza tatizo ni kubwa kuliko tunavyoliona, pili ni kwamba mikakati ya Serikali inayoendelea sasa hivi haijafaulu kwa hiyo tuna haja ya kubadili mikakati ili tuweze kupambana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwanza naishauri Wizara ijaribu kushirikiana na Idara zingine za Serikali, kwa mfano katika yale maeneo ambayo mamba wanashambulia tatizo kubwa ni kwamba wananchi wengi wanakwenda labda kuogelea majini, kwa hiyo tunahitaji kuweka maji ya bomba au visima.

Mheshimiwa Spika, kingine wananchi wengi wanakamatwa wanapokwenda kuvua samaki, kwa hiyo tunahitaji kuwajengea vizimba vya kufugia samaki, vilevile boti za kisasa ambazo zitaweza kuhimili mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, Mwibara tumechoka, kila siku tunazika watu, watu wanauawa, watu wanakuwa walemevu na Serikali ipo, tunaomba Serikali ije na mwarobaini ambao utasaidia sana kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwanza nataka ni-*declare interest,* kuna kesi ya Jaji Edward Mwesiumo, huyu Jaji ni Baba Mkwe wangu, nimeoa binti yake, amekuwa na kesi na Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzia mwaka 1998. Kuna kesi alibambikiwa ikaenda Mahakamani, Mahakama ikaamua aweze kulipwa, lakini mpaka tunavyoongea sasa hivi bado hajalipwa, kuanzia mwaka 1998 mpaka leo ni muda mrefu sana umepita.

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mwanasheria, unajua kwamba *justice delayed, is justice denied* na MAMA ameshasema hataki kumdhulumu mtu na sasa huyu ameshakuwa mzee, ametumikia sana nchi hii, alikuwa Jaji, akawa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani. Huyu Mzee sasa amekuwa mtu mzima sana, haiwezekani Serikali ya Mama Samia ikamuacha huyu Mzee akafa kabla ya kupata haki yake, naomba Bunge lako hili vilevile liisukume Serikali imlipe huyu Mzee haki yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache mimi naunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kajege hebu ngoja, Mheshimiwa Mgungusi subiri kidogo.

Hebu nielewe hiyo kesi, aliyebambikiwa kesi ni aliyekuwa Jaji kabla ama?

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, unajua kulikuwa na mambo ya kisiasa, sasa akasingiziwa kwamba amekutwa na nyara za Serikali katika gari lake na gari likakamatwa, lakini walipokwenda katika kesi akashinda.

Mheshimiwa Spika, sasa miaka imekwenda muda mrefu sana hajalipwa haki yake mpaka leo hii tunapozungumza na ukiniruhusu baadaye nikuletee kesi nzima na hukumu iliyotolewa.

**SPIKA:** Kwa hiyo, wanaodaiwa kutekeleza hiyo hukumu ni Wizara?

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ni Wizara na Mheshimiwa Kairuki anaijua na hata juzi nimeleta *copy* ya hukumu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, kwa hiyo Serikali inafahamu jambo hili.

**SPIKA:** Hebu tafadhali tusaidie hiyo nakala.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, sawa nitakuletea, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara ajiandae.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi kwa sababu ya muda mambo ni mengi ya Wizara hii lakini

nimechagua machache tu mambo mawili, nitachangia suala la mgogoro wa ardhi baada ya upandishaji hadhi Pori la Akiba la Kilombero na pia kuna suala la kutaka Jeshi la Uhifadhi kwa maana taasisi za Wizara *TANAPA* na Ngorongoro pengine baadae na *TAWA* waweze ku-*retain* mapato yao ambayo wanaingiza wakati wa shughuli za utalii, uwindaji na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, kabla ya hayo kuna *hints* kidogo tu nataka nimpe Mheshimiwa Waziri kwa sababu sisi watu wa Malinyi tumezungukwa na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, tumezungukwa na Pori la Akiba la Kilombero kwa maana ya *TAWA*, lakini kwa mazingira hayo na sisi tunahitaji kuangaliwa kwenye kipengele cha ujirani mwema kwa maana ya *CSR*. Nimeona kwenye taarifa yao hapa ya hotuba ya Waziri karibia bilioni 40 kadhaa zimetumika maeneo mbalimbali kuweza kuchangia jamii, lakini sasa ni wakati wa watu wa Malinyi kuweza kupata keki ya kuwepo jirani na hifadhi na kama ndiyo wahifadhi namba moja. Kwa hiyo, hili jambo nasi tuangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la watu wa Ngombo, iliamuriwa kwamba watu wa Ngombo wahame pale na tathmini imefanyika, fidia iweze kulipwa lakini mpaka leo watu bado hawajalipwa. Kwa hiyo, nilikuwa namkumbushia Mheshimiwa Waziri analifahamu hili na tuna uhusiano wa ukaribu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba lifanyiwe kazi kwa uharaka ili msimu wa kulima unapofika Oktoba tusianze kuvutana vutana.

Mheshimiwa Spika, pia suala la *TFS* wanafanya kazi nzuri sana kwa nchi nzima kwa ujumla wake, lakini hata kwangu Malinyi. Mheshimiwa Waziri, naomba unisikilize.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kule Malinyi *TFS* hawana Ofisi ya Wilaya mpaka sasa hivi tunavyozungumza wanatumia Ofisi ya Mbunge, kwa maana ya Ofisi yangu nimewapa vyumba viwili ndiyo wanatumia kama Ofisi ya *TFS* Wilaya, Meneja Wilaya yuko pale na timu yake. Kwa hiyo niseme hawanisumbui sana, ni wenzangu tunafanya nao kazi vizuri, lakini naomba muangalie. Najua mtaweka bajeti pengine mmeweka lakini kipaumbele kwa sasa kiwe pale, kwa

sababu mimi nikijisikia kuanza kuwa *busy* tena na wasaidizi wangu watakosa sehemu ya kutumia. Najua mmeweka bajeti lakini bajeti huwa haitolewi asilimia mia kulingana na mazingira tofauti, basi kipaumbele iwepo Malinyi waweze kusaidiwa na ofisi iweze kujengwa kwa uharaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uvuvi kwenye maeneo ya TAWA kwa maana ya Bonde la Kilombero. Sisi watu wa Malinyi, Mlimba, Ifakara na Ulanga wananchi wetu wavuvi wanendelea na shughuli zao, wana leseni za halmashauri lakini kuingia kule TAWA maeneo yale ambayo yana samaki wengi unatakiwa kulipa shilingi elfu tano kwa siku, unakwenda unavua lakini saa kumi na mbili uwe umeshatoka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri usaidie, shilingi elfu tano kwa siku kwa maana mvuvi akiwepo kule kila siku kwa mwaka karibia milioni moja laki nane na hamsini inakaribia milioni mbili. Mvuvi wa kawaida ambaye anavua kienyeji analipa kiwango hicho kwa mwaka ni gharama kubwa sana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hii gharama ipunguzwe lakini zaidi muda wa mtu kuvua uwe *extended*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani mnafahamu kwenye mambo ya uwindaji, kwenye vitalu kuna uwindaji wa siku 21, siku kadhaa, ningeomba hata uvuvi wasiingie na kutoka siku hiyo hiyo, kuwe na vibali vya siku saba mtu akate, vibali vya siku 21 au vya mwezi kuwepo na mazingira hayo. Mtu anaweza akalipa hela anaenda kule mtoni anavua, anatega, kuvua siyo kuokota ni kutega maana unaenda kubahatisha, anaweza kutwa nzima asipate kitu hata siku tatu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba mtengeneze utaratibu vibali vya vipindi hivi ambavyo nimevitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa zaidi ambalo nataka nichangie sasa ni *issue* hii ya mgogoro mkubwa wa ardhi kule Malinyi kwa maana baadhi ya vijiji vyetu maeneo yao yamechukuliwa na ninazungumza hapa Bungeni mara ya pili yameingizwa kwenye *GN*. mpya ya 64 baada ya kupandisha hadhi hili Pori la Akiba la Kilombero.

Mheshimiwa Waziri naomba tu ili mambo yasiwe mengi hili jambo ulichukue. Tumezungumza, umeniahidi unalifanyia kazi lakini naomba sana lifanyiwe kazi kwa uharaka majawabu yaweze kutoka.

Mheshimiwa Spika, hapa kwenye taarifa yenu imeoneshwa ukurasa wa 37 na 38 kuna baadhi ya maeneo kule wenzetu Mkungunero na maeneo mengine, maeneo ya hifadhi yamemegwa kurudishwa kwa wananchi, maeneo kadhaa. Kwa mfano, pale Mpanga Kipengele karibia hekari elfu 51 zimerudishwa kwa wananchi ili waweze kutumia, lakini Wami Mbiki hekari 17,000, Mkungunero hekari 12,000 na maeneo mengine yanayofanana na hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi watu wa Malinyi hatujasema imegwe hifadhi tupewe maeneo tulime, tunasema yale ya kwetu maeneo ya Kijiji, ramani ya Kijiji inataja kwamba yapo kijijini na taarifa mbalimbali za Serikali na vikao vimekiri maeneo yameingizwa ndani, tunaomba yale maeneo yarudishwe na kama itaonekama kama baadhi ya maeneo kati ya hayo yana *sensitivity* kubwa ya uhifadhi na kadhalika bado inaeleweka, pengine tungeweza kusema Serikali ifanye inavyofanya. Sasa watu wanatoka kwa utaratibu gani? Hakuna mtu anayezungumzia suala la kuwafidia watu, hakuna anayezungumzia suala la kuwarudishia. Kwa hiyo, hayo mawili naomba yaweze kufanyika kwa uharaka ili mambo yasiwe mengi baadae Bunge la Septemba.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo niligusia kuhusu Jeshi la Uhifadhi ku-*retain* fedha zake. Bahati nzuri, mimi nimehudumu Wizara hiyo miaka kadhaa unafahamu na baadae kule *TANAPA* miaka kadhaa, na bahati nzuri sekta ya uhifadhi ndiyo nilikuwa naifanyia kazi moja kwa moja. Tendo la Wizara ya Maliasili hasa hizi taasisi kuendesha shughuli zake kwa kutumia *OC* kama Halmashauri kama Wizara zingine hatuwezi kutoboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnakumbuka tulifunga shughuli za uhifadhi karibia miaka miwili kutokana na athari za *COVID,* maana yake tumerudi miundombinu ilikuwa ni hovyo, angalau kidogo baada ya mambo kukaa vizuri hali imerudi ya uchumi na mambo mengine

ambayo yamefanyika jitihada angalau utalii umeanza kufunguka. Hatujapona vizuri tumepigwa na mafuriko makubwa nchi nzima mnafahamu, barabara zetu tumekuwa tukilia hapa kila siku Malinyi na kwingine, lakini hifadhini shida ni kubwa zaidi. Wageni ambao tunatangaza sasa hivi wanafikaje hifadhini? Kwa hiyo, hali ya miundombinu kwenye mapori yetu yote iwe ya *TANAPA*, *TAWA*, Ngorongoro hali ni mbaya sana, sasa huwezi kufanya marekebisho ya barabara kwa kiwango kikubwa kwa kutumia fedha za *OC*.

Mheshimiwa Spika, changamoto, utakuta sehemu zingine za huduma *camps* zile za watalii uchafu, kuna shida ya madawa na kadhalika huwezi kusubiri *OC* ndiyo ufanye marekebisho. Watu wanapiga picha wapinzani wetu wanatuma mitandaoni, wanasema mnaona hizi hifadhi za Tanzania ni chafu na nini? Kwa hiyo, kwenye *trip advisor* kule wageni wanatupiga kwa sababu ya mazingira haya, hatuwezi kutegemea *OC* ku-*run* utalii, hatuwezi kutoboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme kwa sababu naona Serikali kwa sababu ipo hapa waweze kuchukulia hili kwa uzito watu wa *TANAPA*, Ngorongoro, angalau *TFS* wana-*retain,* waweze ku-*retain* mapato yao na kama kuna jambo Serikali inahitaji basi bora wawambie gawio wawe wanapeleka lakini siyo kuwapa *OC* kama zwatu wengine hatuwezi kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TAWA* kwa sasa hawaja-*break even* kwa hiyo hawawezi kujiendesha kwa muda huo mchache. Kwa hiyo, kipindi hiki angalau wanahitaji msaada wa Hazina waendelee kuwabeba lakini watakapotengemaa basi waachiwe na wao waweze ku-*retain* mapato yao, lakini kwa sasa naomba hili jambo Serikali ilichukulie kwa uzito mkubwa, ahsante kwa leo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, hili alilosema la hifadhi kuwa chafu pengine kwa kukosa msamiati, kule Mlima Kilimanjaro kuna vile vituo havina vyoo. Mimi nimeshapanda ule mlima sijui watu wangapi wameshapanda humu ndani, lakini ule Mlima kuna njia mojawapo ambayo kuna maeneo kabisa ya kupumzika na hayana sehemu ya watu kujihifadhi.

Kwa hiyo, ni muhimu iwepo kwa sababu kwa kweli ukifika pale mazingira kidogo siyo, Mheshimiwa Waziri sijui kama wewe umepanda Mlima lakini ile hali iliyopo kule, halafu ukikutana na hali nyingine inakuwa haipendezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae. Mheshimiwa Hawa, nimeletewa majina mawili hapa kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo na leo mna mtu mmoja, kwa hiyo ni dakika tano tano.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru, daa! dakika tano shughuli. Mimi ninakushukuru kwa kunipa nafasi na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama hapa nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kupitia taarifa ya Kamati na nimeona vitu vingi lakini kutokana na muda mimi naomba nishauri Serikali. Nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba mahusiano mazuri na Kamati kwa maana ya Bunge ni mazuri sana kwa sababu ukiangalia taarifa ya Kamati vipo vitu vingi sana ambavyo wameshauri, lakini vitu vingi sana bado havijafanyiwa utekelezaji na ndiyo maana unakuta tumekuwa tukirudia yale yale ya miaka ya nyuma tunaendelea kuyazungumza kwa sababu hayajafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nishauri kwenye eneo la huu utalii. Utalii upo zaidi kwenye maeneo ya Kaskazini, kila siku hapa tunasikia Ngorongoro, tunasikia Serengeti, tunasikia Manyara, tunasikia Tarangire, lakini kuna maeneo mengi sana nchini kwetu ya utalii, ni utalii mzuri kabisa hayana fukwe, hayana nini lakini yana utalii mzuri ambao kama Wizara itachukua ushauri wa Wabunge na ushauri wa Kamati basi tutakwenda kuwa na utalii wa hali ya juu kuliko kutegemea zaidi maeneo ya Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sisi watu wa Tabora tuna utalii mzuri sana, tuna utalii wa malikale, kwa sababu ukizingatia Tabora ni moja kati ya Mikoa ya kihistoria na ni Mkoa ambao una mambo

mengi sana ya malikale. Kwa hiyo, wakiamua kuwekeza kwenye malikale si kwa Tabora tu na maeneo mengine basi tutakuwa na utalii ambao ni wa kipekee kabisa kwa sababu tuna vitu vingi ambavyo vinaweza kuwa ni vivutio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwenye hilo, ninawashukuru maliasili wameweza kutusaidia mapori yetu kuweza kuwa ni maeneo ya kivutio kwa sababu wameweza kutengeneza vivutio ambavyo vinaweza kusaidia Watanzania wanaoishi Tabora na wengine wanaofika pale Tabora kuweza kupata vivutio.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu jambo moja kuhusiana na huu uzinduzi wa *Presidential Village.* Sijui kuna Waheshimiwa Wabunge wangapi ambao wanafahamu hili jambo na hili jambo linamhusisha moja kwa moja Mheshimiwa Rais. Hii *Presidential Village* sijui ni kitu gani kwa sababu kwanza haijatangazwa kama ilivyokuwa imetangazwa *royal tour* ama ni kwa sababu Mheshimiwa Rais hajaamua kuingia mwenyewe *front* ili kuweza kutangaza kama alivyofanya kwenye *royal tour* na Je, Wizara mnasubiri Mheshimiwa Rais ndiye aje afanye hii kazi badala ya ninyi kuangalia ni namna gani ambavyo mnaweza kutangaza kupitia hii? Kwa sababu tumeona kwenye mitandao kuna hili jambo linaitwa *Presidential Village* ambalo amefanya pamoja na watu wa Jamhuri ya China?

Mheshimiwa Spika, nimeona, sasa nauliza nijue hii ni kitu gani na je kwetu sisi inahusu na kama Mheshimiwa Rais yupo ina maana ni moja kati ya sehemu ya utalii wetu kutangazwa. Sasa kama Wizara mna mpango gani wakufanya jambo hili ili liende likawe ni kivutio kama ambavyo tumefanya kwenye *royal tour* badala ya kusubiri Mheshimiwa Rais afanye hebu fanyeni ninyi ili muweze kwenda sawa.

Mheshimiwa Spika, pia tumeona kwenye suala zima la haya mabomu baridi. Kwanza niwapongeze Jeshi la Wananchi kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ili kuweza kusaidia kuzuia wanyama wakali wasiweze kushambulia ama kuingia kwenye mashamba. Pamoja na kazi nzuri ambayo imefanyika hili janga sasa hivi linapelekwa kwenye

Halmashauri zetu kwamba sasa halmashauri ndizo zinatakiwa zinunue haya mabomu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu tumeshapitisha bajeti ya Halmashauri, leo bajeti hii inakuja inataka Halmashauri ndiyo iende ikanunue haya mabomu. Huu siyo mzigo unaokwenda kuongezwa kwenye Halmashauri zetu? Pili, kama hili lilikuwa ni jambo ambalo walikuwa wamelipanga kwa nini wasizungumze kwanza hata na Kamati tu inayoshughulika na hizi Halmashauri ili kushirikiana na TAMISEMI kuona namna bora ya kuweza kusaidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni changa la macho kwa sababu ina maana halitatekelezwa kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025 sijui litatekelezwa mwaka gani. Kwa hiyo, mimi ninawaomba sana Wizara badala ya kutegemea Halmashauri zetu pelekeni kwanza mabomu yenu ya mifano halafu baadae mkae na Serikali kuona namna gani Halmashauri zinavyoweza kuchangia ili kuweza kununua haya mabomu kwa ajili ya kusaidia.

Mheshimiwa Spika, upi mkakati wa Wizara, maana haya mabomu yanasaidia mnyama akishaingia pale akipigwa harudi, mkakati madhubuti wa Serikali wa kupunguza hawa wanyama kabla hawajatoka kwenye maeneo yao kwenda kufika kule kwa wananchi. Nini mkakati wao wa kuwazuia huku? Hatujauona huku kwenye taarifa yao. Kwa hiyo, tunataka watuambie mkakati wao kabla hawajaenda kukutana na hayo mabomu baridi ili tuweze kujua na tuweze kunusuru wananchi wetu na mazao yao lakini na kuuwawa na hao wanyama wakali ambao wamekuwa wakiingia kwenye maeneo yetu ya wananchi ambako wanaishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda bado upo? *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja, malizia.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, jamani dakika tano ni mtihani. Pia, tumekuwa tukizungumza kuhusiana na malazi kwa watalii, hii ni changamoto kubwa sana. Ndiyo maana nimesema Wizara kama hamjakaa na Kamati kwa maana ya Wabunge, kukaa na kukubaliana nini kiwe kipaumbele tutaendelea kuzungumza mambo haya na watalii watakuwa wanakuja hawarudi tena kwa sababu ya changamoto ambazo wanakutana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niwaambie, tunataka kwenda kuwapitishia bajeti. Tunawapitishia namna gani bajeti ambayo mwisho wa siku Kamati wamesema huku nyuma kuna changamoto ambayo mnatakiwa mkae mzungumze? Tutaonana jioni tujue tunapitisha ama hatupitishi, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi kwa sababu ya muda naomba niende moja kwa moja kwenye kuchangia. Kwanza, nipongeze sana Makala ya *Tanzania The Royal Tour* lakini pia na filamu ya *Amazing Tanzania* ambayo ilifanya tukashinda Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo niseme na niiombe sana Wizara tujitahidi sana kutunza uoto wa asili na kurekebisha barabara, malazi na usafiri unaokwenda kwenye hizo hoteli. Kwa mfano pale Ziwa Nyasa kuna yale maeneo mazuri sana ya fukwe kutalii lakini changamoto ni njia ya kufika huko kwenye hizo fukwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vema Wizara itoe fedha kidogo ili kufungua hizo njia. Mkiachia halmashauri peke yake zinashindwa. Kwa hiyo, hii itakuwa ni pamoja na ile ya uoto na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, pia niwaombe Wizara; Mheshimiwa Rais aliweza kuigiza ile filamu na ndiyo ikatuletea sifa zote hizo, sasa na ninyi msibweteke. Mkae chini na ninyi muanze kubuni filamu

itakayopaa kama ile *Royal Tour* ya Mheshimiwa Rais. Muanze kubuni filamu na kuwaweka watu maana, (mashuhuri) wa kuigiza hizo filamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo watu wanaoweza kuigiza hizi filamu na hata humu ndani ya Bunge wapo. Pia, msituwekee wale watu ambao wakienda wanafanya zile filamu zinakuwa ni vichekesho. Tunataka watu watakaofanya watu wakaangalia filamu kama alivyofanya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye jambo lingine. Mheshimiwa Waziri, kuna vikundi mbalimbali vinapenda na vinaweza kutembelea vivutio vyetu. Hata hivyo, kuna kundi moja naomba uwasaidie. Kundi la wanafunzi wenye ulemavu na vijana walemavu wanatamani sana kwenda kuviona vivutio na wao ni sehemu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakuta wale wenye ulemavu wa miguu, hao wanaotumia *wheelchair*, wasiosikia (watu wasiokuwa na uwezo wa kusikia), watu wenye ualbino na vijana wa vyuo vikuu wanatamani. Hebu tengenezeni hilo kundi mkawachukue.

Mheshimiwa Spika, kule karibu na maeneo ya Arusha na Kilimanjaro kuna vyuo vingi. Pia, wakiunganika na wanafunzi wenzao wa mikoa mbalimbali ya Dar es Salaam, Dodoma na mikoa mingine wapelekeni wanafunzi wasio na uwezo waende wakatalii. Hiyo ni haki yao. Sasa huko msiwasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine niseme kuhusu uharibifu wa mazao, kuua watu na suala la tembo. Mimi ningeshauri, tembo wanazaliana sana *mating* yao ni kuanzia Desemba mpaka Machi. Hebu tufanye *culling* kabla ya Desemba. Maana yake Wanyama hawa wana muda wao wa ku-*mate*. Wale wenzangu mliosoma kidogo kama mimi kuhusu *animal behavior*. Wale *mating* ina muda siyo kama binadamu. Sasa ninyi mjipange muwe mnafanya *culling* kupunguza kabla hawajaingia ule msimu wa *mating*. Kwa sababu mkifanya culling katika kipindi kile cha Desemba – Machi mtaweza kuua mpaka wanyama wenye mimba. Sasa mjitahidi kufanya *culling*. Vilevile,

Mheshimiwa Waziri suala la tembo Ruvuma tunakula sana nyama ya tembo.

Mheshimiwa Spika, hebu niwaombe kama mnafikiria kuwapunguza muwachinje (sijui niseme kuwaua) muwachinje halafu tengenezeni hizo nyama kisha pelekeni katika mikoa ambayo tembo analiwa. Vilevile, hizi nyama nyingine mimi najiuliza, hivi hawa wananchi wa kawaida wanapata hizo nyama za pori? Mheshimiwa Waziri, kweli wanapata? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wanyama wanatoka vijijini huko lakini nyama zinaliwa mjini. Mimi naomba mniambie au mkiweza tengenezeni masoko hata wenzetu wa vijijini waipate hiyo nyama. Tujue kuna masoko mangapi vijijini huko ili watu wapate hiyo nyama. Ndiyo maana wanaingia huko kuwaua hovyo. Mnawashika wakina mama na kilo 10 za nyama pori; na wao wanatamani. Kwa hiyo, hilo mjipange kabisa kuhusu hawa wanyama wanaoua hawa muwapunguze sisi tuko tayari kula hiyo nyama.

Mheshimiwa Spika, halafu pia kuna suala la majangili. Mheshimiwa Waziri nikuulize, hivi hawa majangili wanatoka nje au wako ndani? Jangili atatoka Kenya au Uganda kweli anakuja huku? Lazima kuna jangili mkubwa ndani ya nchi na ndiye anayewaita wale majangili kule nje. Hebu tujipange, majangili wapo tunakaa nao. Majangili waondoke, haiwezekani. Jamani hatuna ulinzi? Ninaposikia suala la majangili mimi nashangaa.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho; hili nalisema kwa masikitiko. Wote tunafahamu Chuo cha Utalii kilikuwepo pale Kivukoni. Pia, wenzetu walikiweka pale makusudi kwa sababu hoteli nzuri zote ziko sehemu ile. Leo kile Chuo wanakiondoa pale na majengo wanawapatia Mahakama halafu Chuo wanakiambia kiende Temeke. Wakati nilitegemea Mahakama ndiyo iende Temeke kwenye wateja wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hebu nisaidie. Wanawatoa Chuo pale kwenye ofisi zao wanawapeleka Temeke wakati Temeke ndiko kuna

wadau wa Mahakama wamejaa huko. Leo mnawanyang'anya wale Chuo halafu Mahakama ndiyo wanakuja wanakaa mjini. Mjini kuna mambo ya vurugu kweli? *(Makofi)*

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, sasa hata hivyo mmekwisha wanyang'anya; naomba nimalizie kidogo.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ntara kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Temeke.

**TAARIFA**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante lakini labda nimpe tu taarifa kwamba, sisi hatuna wadau wengi kiasi hicho, unatuambia tuwe na Mahakama. Hata utalii kwetu upo na kile Chuo cha Utalii ni kikubwa sana. Nadhani vibaki kama vilivyopangwa kwa ajili ya maslahi mazima ya nchi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, yaani siipokei. Wamewapeleka kule kwenye bandari. Kule ndiko kuzuri, Chuo cha Bandari kiko karibu na Temeke kinaendana kabisa na mambo ya Bandari. Hata hivyo, hawa wa utalii hoteli ziko pale, waliojenga siyo kwamba hawakuwa na akili. Waliweka lile jengo pale ili wale watoto waende kufanya *field* kwa sababu hoteli zote ziko pale. Hata hivyo, yale majengo sasa yamebaki wazi kwa sababu Serikali imekuja Dodoma na majengo mengi yako kule. Basi hii Wizara ya Utalii sasa wawape yale majengo yaliyobaki wazi kule ili wafanye hoteli na ikiwezekana hata ofisi.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kuwahamisha kwa kweli hawakuwatendea haki. Mahakama ihame iende kule kule Temeke ikakake kule. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imekwishagonga.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Utalii, dada yangu Mheshimiwa Angellah Kairuki, Naibu Waziri Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Katibu Mkuu Dkt. Hassan Abbas, Naibu Katibu Mkuu Kamishna Wakulyamba na Wenyeviti wote wa taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hii, Ma-*general* na *Major Generals* wote walio Wenyeviti; hongereni sana kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Spika, pili napongeza sana kwa Tanzania kuwa *Vice Chairman* wa *UN-WTO*. Ni jambo jema sana na litaendelea kutupatia heshima nchi yetu. Pia, Wizara hii ni tegemeo kubwa la kuingiza mapato hasa mapato ya fedha za kigeni. Kwa hiyo, kazi mnayoifanya sisi tunaitambua na tunawapongeza sana. Endeleeni hivyo hivyo kuongeza juhudi za kuongeza watalii tulionao.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda mbele naomba pia nipongeze juhudi na umahiri wa Shirika la Mzinga walioshirikiana na *TAWIRI* kutengeneza bomu hili la baridi la kufukuza tembo. Kazi ya kufukuza tembo nimeiona imeanza. Wameanza kazi hii kule Same na Meatu na imeonesha mafanikio na ufanisi. Kwa hiyo, tunaomba sana pia wafike na Namtumbo kwa sababu Namtumbo ni waathirika wakubwa sana wa tembo. Mheshimiwa Waziri unafahamu nimewaletea kesi nyingi za tembo na nimezungumza sana. Pia, tuna waathirika hawa kwenye mazao na bindadamu. Vilevile, tumekwishapoteza binadamu watatu. Kwa hiyo, tunaomba sana lile zoezi lifike na kwetu.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba vile vifuta jasho vifike kwa sababu walioliwa mazao maafisa maliasili walishafika, wamekwishakagua, wamefanya tathimini na wameleta Wizarani lakini wananchi bado hawajalipwa fidia zao.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Wananchi wa Likuyu, Nambecha, Mandepwende, Kitanda, Magazine, Lusewa huko nao wote hao walipata athari za kuliwa kwa mazao yao na taarifa zao ziko Wizarani. Tunaomba sana muwafanyie haraka walipwe fedha zao.

Mheshimiwa Spika, sisi eneo lingine la pili ambalo tunashukuru sana ni kwamba mmetuwekea lango la kuingilia katika Hifadhi ya Mwalimu Nyerere. Sasa, tunaomba mje Namtumbo mtupatie elimu ya mara kwa mara kwa wananchi. Sisi Namtumbo ni wakulima na biashara yetu ni mazao ya kilimo na kilimo chenyewe. Hii biashara ya utalii kwetu ni mpya. Tunaomba mtupe elimu ya mara kwa mara ili mtujenge kisaikolojia na sisi tufanye biashara hii ya utalii ili na sisi tuungane katika uchumi huu wa utalii. Tusije kuwa sisi ni waangaliaji tu pale kwa kuwa hatuifahamu, wanaoifahamu ndio wao tu wafanye biashara ile ya utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba sana wataalamu waje mara kwa mara ili kutupatia elimu ya umma ili watu waweze kwa sababu wananchi wanazo fedha za mazao ili waweze kwenda kwenye biashara hii ya utalii.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu Selous ilianza kuwa *protected area* toka mwaka 1896. Pia, eneo hili mwaka 1940 liliongezwa na likawa na ukubwa wa kilometa za mraba ($km^2$) 54,600. Hata hivyo, mwaka 2019 tukaligawa kilometa za mraba ($km^2$) 30,000 likawa *National Park*. Ni eneo kubwa sana na ni *National Park* ya pili Afrika. Ukiondoa ile *Naukluft Park* ya Namibia, sisi ya kwetu ni ya pili.

Mheshimiwa Spika, hii imehifadhiwa tangu 1896, ina vitu vingi vya hifadhi vilivyohifadhika, wanyama wengi, *varieties* za wanyama, ina vitu vingi kabisa vya asili, misitu na ikolojia nzuri kabisa. Kwa hiyo, tunaomba sana bado kuna changamoto ya njia ya kufikia yale

maeneo ya vivutio vya kiutalii. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali iongeze fedha za kufungua njia ya kufikia kwenye yale maeneo ya utalii ili yale wanayoona tunapo *promote* kwenye *TV* na kwenye *social media,* basi watalii wanapofika waweze kwenda kuona.

Mheshimiwa Spika, pia idadi ya watalii wanaofika bado ni wachache. Wale wageni wa nje mpaka mwaka 2023 ni 4.4% ambao walifika karibu 39,000. Vilevile, wa ndani ni 21,684 sawa na 2.4% ya watalii wote waliofika katika *National Park* ya Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, bado kuna *potential* kubwa sana. Kwa hiyo tuongeze nguvu ya kushawishi kuleta watalii.

Mheshimiwa Spika, vilevile miundombinu yake, *camps*, hoteli ni lazima yajengwe katika eneo lile. Tusitegemee watalii wote tunawapeleka Kaskazini. Eneo lile bado bichi sana, kama ni nanii bado ni kigoli yaani eneo lile bado ni bichi. Kwa hiyo, tuleteeni watalii wa kutosha. Mtengeneze miundombinu, washawishini *investors* waje waweke vitegauchumi katika eneo lile la Selous.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kutoka mwisho; Nchi yetu hii kwenye watalii waliokuja, *Maliasili Statistical Bulletin* anatuambia kwamba, ile *trend* ya watalii wa nje waliotembelea mbuga zetu mwaka 2023 ni 888,506. Hawa wa nje toka 2020 walikuwa 218,760. Kwa hiyo mmefanya kazi nzuri sana toka mwaka 2020 tulipopata ile shida ya *Pandemic* ya *Covid* wakashuka chini lakini wameongezeka mpaka 888,506. Hizi ni taarifa kutoka *Maliasili Statistical Bulletin.* Vilevile watalii wa ndani wameongezeka kutoka 361,000 mpaka 902,000 kwa ujumla wake. Hao ndio waliotembelea mbuga zetu. Kwa hiyo jumla yake unakuta ndiyo hiyo milioni moja laki saba na zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa bado hawa wa nje. Tusibweteke tusije tukasema tu 1,800,000; hawa ni wa ndani na wa nje. Tuongeze juhudi za kuwashawishi wa nje wafike kwa wingi. Wenzetu leo ukienda pale Egypt kutembelea zile *Pyramids;* wanakwenda kutembelea *Pyramids* na kwenda kumuona Firauni na magofu yale wanaingiza watalii zaidi ya milioni tano kwa mwaka. Sisi wa kutoka nje bado tuko kwenye laki

nane, tuseme laki tisa. Kwa hiyo, bado kuna juhudi za kufanya. Tusibweteke bado watu wa nje hawajaja wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, tuongeze juhudi ya watalii wa nje ambao wanatuletea fedha za kigeni na sisi tuna shida ya fedha za kigeni…

**SPIKA:** ahsante sana, kengele ya pili imekwishagonga.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nianze moja kwa moja kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Leo hii ametunukiwa shahada (*degree* ya heshima) nchini Korea katika maeneo ya anga. Ameongeza idadi kubwa ya ndge nchini na ameweza kujenga na kukarabati viwanja vingi katika nchi yetu. Kwa hiyo, tunampongeza sana kwa juhudi hiyo ambayo ameifanya na kuendelea kutunukiwa *degree* katika nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kumpongeza kwa kutangaza kupitia *Royal Tour.* Kwa kweli ameweza kuongeza idadi kubwa sana ya watalii nchini zaidi ya milioni mbili. Vilevile, niendelee kumpongeza hata Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi ambaye pia kwa Zanzibar utalii umeongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Ukienda Zanzibar wazungu wamejaa, watalii ni wengi kiasi kwamba kwa kweli nawapa maua yao Marais wote wawili wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri wetu Mheshimiwa Angellah Kairuki, hongera sana. Wanasema kwamba mzigo mzito usimpe mnyamwezi, mpe mwanamke na mwanamke anaweza mizigo yote na tumeamini sasa hivi mambo yanakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nimpongeze Mheshimiwa Dunstan Kitandula. umekwenda kuongeza nguvu kubwa sana katika utalii wetu nchini, hongera sana. Niwapongeze Makatibu Wakuu wote na Wakuu wote wa taasisi zote zilizopo katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia kuhusiana na uendelezaji wa eneo la Kihesa pale Kihesa – Kilolo. Eneo hili lilitengwa katika Sekta ya Utalii ili kukuza utalii mikoa ya Kusini. Miongoni mwa waliopewa viwanja hivi, kwanza tulipewa viwanja vya *TTB*, *TAWIRI*, *MWEKA*, Chuo cha Utalii cha Taifa, *TFS* pamojana na *ISCC*. Pia, pamoja na kupewa maeneo hayo tumeona tu *TTB* na *TAWIRI* ndio ambao wameanza kuendeleza maeneo hayo. Je, wengine lini mtaendeleza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tulijua kwamba, kama mtayaendeleza, utalii wa Kusini ndiyo utafanya vizuri zaidi. Pia, tulitegemea kwamba Serikali ilikuwa na mpango mzuri kabisa kwamba, Mikoa ya Kusini ina vivutio vingi vizuri lakini havitangaziki. Sasa tulijua kwamba kutakuwa na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba vinatangazika ili kuweza kuongeza uchumi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niombe, bila ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa, ujenzi wa Barabara ile ya Msembe inayokwenda mbuga za Wanyama *Ruaha National Park* ambayo ni mbuga ya pili kwa ukubwa bado tutakuwa hatujawatendea haki Mikoa ya Kusini kwa sababu tukishajenga vile viwanja watalii wengi wataweza kuja katika maeneo yetu. Kwa hiyo, niombe sana lazima mkakati uwepo kuhakikisha kiwanja cha Iringa kinajengwa haraka sana pamoja na ile Barabara inayokwenda *Ruaha National Park*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nielezee kuhusiana na maonesho ya karibu kusini, yanayofanyika katika kile Kiwanja cha Kihesa, Kilolo. Tunatambua kwamba Iringa ni kitovu cha utalii kwa mikoa ya ukanda wa kusini ikiwemo Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Ruvuma, Songwe, Rukwa na Katavi. Mwaka 2019 wewe Mheshimiwa Spika ulikuja kama

Mgeni Rasmi pale Iringa na ulijionea jinsi Wakuu wa Mikoa walivyokuwa wanasema vivutio vingi, vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maonesho yale yalifanyika kwa sababu Wizara iliweza kuandaa yale maonesho na yakawa mazuri sana. Lakini mwaka 2023 Wizara haikuweza kutoa chochote mikoa yote iliweka *OC* zao tu ndio wakaweza kufanya yale maonesho, na Mheshimiwa Waziri ulikuja kama Mgeni Rasmi, kwa kweli walikuomba sana na maonesho hayakuwa mazuri, nia na madhumuni ya kuhakikisha yale maonesho yanafanyika? Ni kuhakikisha Wizara inatia nguvu pale. Sasa *TTB* mnafanya nini? Kwa nini msichukue yale maonesho mkakuza utalii wetu uliopo katika Nyanda za Juu kusini?

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Anjela, Waziri wa Maliasili na Utalii, hebu sasa maonesho yajayo tunaomba Wizara ichukue hili jukumu ili kuhakikisha yale maonesho yanakuwa na tija yanatangaza vile vivutio vya mikoa yetu iliyopo katika Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuzungumza kuhusiana na fidia za wananchi kutokana na wanyama pori, wananchi wanapata shida sana, wananchi wamepoteza maisha, mazao yanapotea, watoto wamekuwa yatima, mifugo yao imeliwa. Ukiangalia katika Mkoa wetu wa Iringa utakuta kuna maeneo kwa mfano Idodi, Mlowa, Mlenge, Pawaga watu wanapata shida lakini tena ukienda Kilolo unakuta kuna Msosa, Magana, Ilula, Mtangika, Nyanzwa watu hawa bado wanaendelea kulia na vifutajasho ambavyo hawapatiwi na pengine hata wakipatiwa siyo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pengine ije sasa sheria tuboreshe kwa sababu watu wanapata mateso lakini vifuta jasho haviwasaidii chochote. Mtu amepoteza mazao yake yote hajui atakula nini kifutajasho hapatiwi, sasa mimi naomba kuwe na mkakati maalum kuhakikisha kwamba watu wanapopatiwa majanga kama haya basi mapema inafanyika wanapewa fidia siyo vifuta jasho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kujua Wizara ina mkakati gani wa kutambua maeneo ya utalii au makumbusho mapya? Kwa mfano mimi nawapongeza sana Magereza pale Kihesa Mgagawo. Wametunza maeneo mazuri sana vyumba alivyolala Nelson Mandela, vyumba alivyolala Walter Sisulu, vyumba alivyolala Thabo Mbeki mimi nilitegemea sasa hivi vile vyumba vingekuwa vya utalii. Wangeweka watu wakaja wakatalii na ingeweza kusaidia sana hata wananchi wanaokaa katika maeneo yale wakapata vitu vingi kutokana na watalii kuja pale, barabara nzuri zingejengwa kusaidia wananchi ambao wako katika maeneo yale. Mimi nina imani kabisa hawa Marais kwenye nchi zao wanatamani waje waone yale maeneo lakini sasa haiwezekani kwa sababu hakuna mkakati ulioweka kuhakikisha kwamba hivi vyumba vinatunzwa. *(Makofi)*

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Justine Nyamoga.

**TAARIFA**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napongeza sana mchangiaji anavyoendelea kuchangia vizuri sana lakini nilitaka kuongezea taarifa kwa suala la Kihesa Mgagao ambapo pale kuna gereza na tulishaiomba Wizara ya Maliasili iiombe Wizara ya Mambo ya Ndani kurudishiwa lile eneo ili kuweka sehemu za kumbukumbu na kuweka Taasisi rafiki ambayo itafanya watalii waweze kwenda badala ya kwenda gerezani na hadi leo Wizara hii haijafanya, nilitaka tu kumjulisha taarifa hiyo ili pia na Waziri asikie, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati inaipokea taarifa hiyo?

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, mimi ninaipokea kabisa umoja ni nguvu na ninaamini kabisa tukishirikiana mambo yatakwenda vizuri na mzigo mzito mpe mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, biashara ni matangazo, sisi Mkoa wetu wa Iringa una vivutio vizuri mno lakii havitangaziki miundombinu ni mibaya sana. Kwa hiyo, mimi naomba Wizara hebu ije Mkoani kwetu Iringa tuwaonyeshe vivutio vizuri mno ambavyo vipo lakini miundombinu yake ni mibovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, namshukuru sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ajiandae

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ya kupambania utalii katika nchi yetu. Pia nampongeza Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri hususani kanda ya kusini hawa kanda ya kusini wanafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi unapata athari kubwa kutokana na Wanyama tembo, kuna athari kubwa, kuna vifo vinatokea kila wakati na sasa hivi ni zaidi ya watu 15 wameshafariki kuanzia mwaka jana, lakini pia kuna ulemavu wa kudumu na uharibifu wa mazao unaosababisha kuwa na njaa kali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hata huduma za jamii watoto hawaendi shule, shughuli za Uchumi hazifanyiki vizuri kwa sababu ya wanyama tembo, inabidi watu mbaki majumbani kwenu kwa kuhofia wanyama ndovu wanaosumbua sana katika mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la kifuta jasho na kifuta machozi bado jambo hili hafanyiki vizuri kwa Mkoa wa Lindi. Nikitolea mfano Wilaya ya Nachingwea taarifa niliyoipata hapa hadi Septemba mwaka 2022 ndio imelipwa mwisho hapo. lakini kuanzia hapo walipolipwa hadi leo bado hakuna kifuta machozi wala kifuta jasho, hii ni hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa inafanyika na Wizara hii ya Maliasili na Utalii na imefanya kazi kubwa ya kupeleka helkopta kule kuwasaka wale tembo kuwapeleka kule kwenye mbuga. Lakini na sasa hizi jitihada kubwa ilizofanya Wizara ya Maliasili na Utalii wakishirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kutengeneza hili bomu baridi, ni jambo jema sana lakini bado ni kazi inayoenda kufanyika kwa muda tu yaani ni suluhisho la muda mfupi. Sisi Wanalindi na Wanachingwea tunalilinganisha hili suala kama vile helkopta ilivyofanya kazi kubwa ya kuwafukuza wale tembo, imetumia gharama imewapeleka kule kwenye mbuga lakini bado wamerudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata hili bomu baridi litaenda kufanya hivyohivyo inakuwa tembo wako Nachingwea kwa mfano, unawafukuza na lile bomu sana sana wataenda Rwangwa au wataenda Liwale au wataenda Tunduru au wataenda huko Namtumbo kwa ndugu yangu Mheshimiwa Vita Kawawa. Bado watakuwa wanazunguka zunguka pale pale lakini hata wakienda mbugani bado kule kwenye hifadhi hawatachelewa wanarudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nawaomba Wizara, kutumia Taasisi yao ile ya *TAWIRI* waendelee kufanya bado utafiti ili tupate suluhisho la kudumu. Wanapoenda kule mbugani kuna nini kule? kwanini kinachowafanya wale tembo warudi tena kwenye jamii, kwenye makazi ya watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo tunayoishi sisi kule Nachingwea, Liwale, Mchinga, Rwangwa maeneo yale bado hata babu na babu waliendelea kuishi maeneo yale hatujaenda kuwashambulia, hatujaenda kukaa makazi ya wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanyama ndio wanakuja maeneo yetu kuna nini kule kwenye mbuga wanachokimbia? Kuna njaa, kuna ng'ombe wengi wameenda kule mbuga zao zimeshambuliwa. Kwa hiyo, hili suala la bomu mimi naliafiki ni zuri sana vijana wetu wametafiti

vizuri sana na wamekuja na suluhisho, lakini suluhisho hili siyo la kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini sasa kifanyike? Watafute mbinu mbadala wapate suluhisho la kudumu la kuwafanya wale tembo ama ndovu wabaki maeneo yao siku zote. Lakini pia sisi Wanalindi tunaomba kifuta jasho na kifuta machozi kitolewe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kule nyumbani siyo shwari hali Mkoa wa Lindi kwa wilaya zake zote siyo shwari. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wako naomba twende, Bunge hili likiisha twende mkatoe neno kule kwa wananchi wetu wawasikie nyinyi wenyewe wawaone. Kwa sababu kila tunapoenda wanasema sisi hatuwafikishi taarifa jambo hili, angalau mkienda kule inaleta faraja kidogo mnapoonekana. Wale wananchi kule walioathirika na wanyama ndovu angalau wanapata faraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu fikiria tu Mheshimiwa Waziri familia yako imemkosa mtu ambaye alikuwa anatafuta chakula ndani ya familia, familia yako imekosa mazao, hawana kitu unategemea hao watu watakuwaje? Lakini mnapokuwepo pale Mheshimiwa Waziri unaposema sasa leo nimekuja ndugu zangu kuwasikiliza angalau wanafarijika kuliko wanakuona tu kwenye *TV* kubwa hivi Mheshimiwa Angellah Kairuki hawakuoni, Mheshimiwa Kitandula hawakuoni sasa hapa tunafikia wapi watu hawa wanakosa imani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hakutakuwa na jambo la kutuambia sisi Wanalindi kuhusu fidia kihusu kifuta machozi kwa kweli mimi kama tutafunga hii hiyo jioni mjadala huu mimi kwa kweli sitaunga mkono hoja, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, ajiandae.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi niweze leo kuchangia kwenye Wizara hii

muhimu ya Utalii. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyojitoa kuutangaza utalii wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu amekuwa akiutangaza utalii wa nchi yetu kupitia filamu yake ya *Royal Tour* na *Amazing Tanzania*, lakini hiyo tu haitoshi Mheshimiwa Rais wetu amekuwa akiutangaza utalii wa nchi yetu kila anapokwenda au anaposafiri, Mheshimiwa Rais wetu yeye ni alama ya nchi yetu ya Tanzania na anaendelea kuitangaza Tanzania popote duniani anapotembelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Angellah Kairuki mtoto wangu nakupongeza sana kwa kazi kubwa unayoifanya, lakini pia nimpongeze Naibu Waziri Kitandula unafanya kazi kubwa tuko na nyinyi pamoja. Kipekee niwapongeze Watendaji wa Wizara hii Mheshimiwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya, mnafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuwapongeza kwangu nawapongeza kutokana na kazi kubwa iliyofanyika kutokea mwaka 2021 inaonyesha hapa idadi ya watalii walioingia Tanzania walikuwa ni 922,692, lakini kufika mpaka mwaka 2023 watalii walioingia nchini mwetu wamefikia 1,808,205, ni idadi kubwa sana sana lakini pia kwenye watalii walioangalia vivutio mwaka 2021 watalii 788,733 waliingia kuangalia vivutio, lakini kufika mwaka 2023 watalii 1,985,707 waliingia kwenye nchi yetu kuangalia vivutio mbalimbali, idadi hiyo ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa mapato mwaka 2021 tulipata bilioni 1.3 na mwaka 2023 bilioni 3.4 kwa utalii wa kimataifa lakini utalii wa ndani mwaka 2021 tulipata bilioni 46.3 na mwaka 2023 tulipata bilioni 175.3 ni kiasi kikubwa sana sina budi kuwapongeza sana Wizara hii kwa kazi kubwa mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaongelea katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam, kwenye Mkoa wa Dar es Salaam umejikita pia kwenye utalii wa fukwe lakini pia utalii wa malikale. Dar es Salaam tuna *National Museums* au Makumbusho ya Taifa, tuna Kunduchi *Ruin*s (Magofu ya Kunduchi), tuna *Botanic Garden*, tuna Nyumba ya Mwalimu Nyerere Magomeni, Makao Makuu ya TANU, Mbwa maji Geza Ulole kuna chanzo pale cha vyombo vya mabaki ya watu wa kale, Kijiji cha Makumbusho, Uwanja wa Uhuru, Feri Soko la Samaki na *Railway Station* pamoja na *City Boma* au pale *City Council,* Pori la Pande na Kisiwa cha Mbuji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yote ya kitalii bado hayana taarifa sahihi, mimi ninayeongea hapa kwa kuwa ni mdau na nimesomea *Cultural Heritage and Tourism* katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nayatambua kutokana na elimu niliyoipata lakini hayana *information* yoyote kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali hivi vivutio vya malikale vilivyopo katika Mkoa wa Dar es Salaam viwekewe mabango makubwa ili Watanzania wajue kwamba hapa tunapozungumzia Makao Makuu ya TANU ile nyumba ndogo pale kwenye Uhuru pale *Press* watu wanaangalia leo kama Makao Makuu ya CCM, wakati pale palikuwa ni Makao Makuu ya *TANU* ile nyumba ndipo ilipozaliwa Chama cha *TANU*, Chama kilichopigania uhuru wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watoto wetu wanatakiwa wajifunze wajukuu zetu wajifunze wajue chanzo cha uhuru wa nchi hii ulipiganiwa na Chama cha *TANU* ambacho kilikuwa pale Lumumba kwenye ile nyumba ndogo. Nikipongeze Chama Cha Mapinduzi kwa kuthamini hilo kwani kibanda kile cha Makao Makuu ya *TANU* ile nyumba iko vilevile inakarabatiwa tu kwa kawaida ambayo ni Kanuni katika Malikale unaweza ukaikarabati kwa vile unavyotaka lakini usiibomoe niwapongeze sana chama changu kwa kuweka hiyo historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika Magofu ya Kunduchi, Magofu ya Kunduchi yale yapo katika kujifunza makaburi ya watu maarufu Masheikh na Masharifu. Kwa hiyo, pale kuna eneo tumepata

nashukuru katika kuongea Serikali hii ni sikivu imetenda angalau ilipeleka pesa kidogo mazingira yale sasa yamekuwa yanafikika vizuri. Lakini bado tunahitaji ukumbi pale kidogo ili wanafunzi wanapokuja kujifunza wakae sehemu waweze kuelezwa vizuri historia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Makumbusho ya Taifa; tuna Makumbusho ya Taifa, makumbusho ile ni chanzo cha elimu kwa wanafunzi mimi nimekuwa Mwalimu kwa miaka kadhaa tena Mwalimu mkuu kwa miaka kadhaa sijawaona watu wa Makumbusho ya Taifa wakafanya semina kwa walimu kuwaeleza umuhimu wa makumbusho hayo vyanzo vya historia ya Tanzania ili wale walimu waweze kuleta wanafunzi wao pale kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme pia bado tunahitaji kupata Makumbusho au *Plantation Museum* tunakolekea wanafunzi na watoto wetu wajukuu zetu wanaoishi Dar es Salaam wanasoma kwenye vitabu vyao mahindi *maize* lakini ukimuuliza mche huu ni nini na hii ni nini? Haya ni mahindi au hizi ni karanga anashindwa kutambua anasoma kwenye vitabu laki haelewi uhalisia wake. Hivyo basi, tukipata hii *Plantation Museum* ambayo itajengwa na watatengeneza pale mazao ya aina mbalimbali watalima hapo karanga, chai kila aina ya zao litakuwepo kwenye eneo hilo hiyo itasaidia wanafunzi kujifunza kwa vitendo. Mwanafunzi anapojifunza wa kugusa kitu na kukiona anaelewa zaidi kuliko anaposoma kwa nadharia tu bila vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna Uwanja wa Uhuru pale Temeke, ule uwanja una Historia kubwa ya Uhuru wa Tanzania lakini watu wanaona kana kwamba ni uwanja wa kwenda kucheza tu, ni uwanja tukutane Uhuru, tukutane kwa Mkapa lakini ule Uwanja wa Uhuru una historia kubwa ya Uhuru wa Tanzania na ni sehemu ya utalii wa nchi hii. Je, Serikali pamoja na kuweka kuwa chanzo hicho mmeweka matangazo gani au tangazo gani linaloonesha kwamba huu Uwanja wa Uhuru ndiyo wenye historia ya Tanzania. Bendera mkoloni ilishushwa kwenye uwanja ule?

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Mbunge kabla ya kuendelea na mchango wako, wageni walioingia Bungeni baada ya matangazo ya awali.

Wapo wageni 40 wa Mheshimiwa Angellah Kairuki ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii. Hawa ni kutoka Chuo cha Biashara, Kampasi ya Dodoma, karibuni sana.

Wengine ni wageni 50 wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu, ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Uuguzi Peramiho kutoka Songea, karibuni sana.

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Michael Mwakamo ambao ni walimu wa Shule ya Msingi ya *Saint* Gemma kutoka Mlandizi, Kibaha, Jijini Dar es Salaam. Haya, sijui wamekaa upande gani?

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Vita Kawawa, ambaye ni Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Namtumbo, karibu sana.

Wageni 44 wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo cha Biashara, Kampasi ya Dodoma, wanaotokea Makete, karibuni sana. Vilevile tunao wageni 146 wa Mheshimiwa Muharami Mkenge ambao ni walimu nane na wanafunzi 134 kutoka Shule ya Sekondari Baobab. Najua inaitwa Baobab, ila hapa naona imeandikwa Baobao; sasa, haya, Shule ya Sekondari Baobab kutoka Bagamoyo, Mkoani Pwani, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni walioingia.

Sasa tunaendelea, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimshukuru Mungu ambaye ameendelea kutupa uzima na uhai, tunaendelea kupata pumzi yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ya kuendelea kuitangaza nchi yetu, kwa ajili ya utalii. Naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu. Naomba nimpongeze kamishna wa *TANAPA* kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu. Nampongeza kamishna wa *TAWA* na ninampongeza Kamishna wa *TFS*.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii ya kumshukuru sana Kamishna wa *TANAPA* pamoja na wahifadhi wote kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya. Naomba niwashukuru sana wamenijengea bweni katika Kata ya Stalike, Shule ya Sekondari Stalike, wamenipa shilingi milioni 120 na bweni limekamilika. Naomba niwashukuru sana *TANAPA,* lakini ukishukuru unaendelea kuomba. *TANAPA* mmeniahidi kuwa mtanijengea bwawa, kwa ajili ya wananchi wangu kuvua samaki katika Kata ya Stalike, naomba niwakumbushe, nategemea katika bajeti hii mtakuja kunijengea. Naomba niwashukuru sana. mlikuja katika kata yangu mkaongea na wananchi katika matatizo ambayo walikuwanayo Wananchi wa Kata ya Stalike. Ninawashukuru sana *TANAPA* kwa unyenyekevu mkubwa sana na pia, naomba nimshukuru sana Kamishna wa *TAWA,* naye alikuja katika Jimbo langu la Nsimbo tukafanyanae ziara.

Mheshimiwa Spika, ninaomba, katika Kata ya Ugala tuna Ziwa Ugala ambalo mamba wameongezeka. Naomba *TANAPA* waende wakafanye uwindaji kwa sababu, wananchi wengi wanakufa, kwa ajili ya mamba.

Mheshimiwa Spika, vilevile ndani ya Mkoa wetu wa Katavi kulikuwa kuna uwindaji, kwa ajili ya bucha za nyama ya wanyamapori na wananchi wengi walihamasika kutokana na Hayati Rais Dkt. Magufuli, alikuja Mwaka 2019 akafanya ziara, akahamasisha wananchi wawe na bucha za nyamapori. Wengine wakakopa na kweli, bucha zile zilikuwepo, lakini sasa hivi zile bucha na uwindaji ule haupo tena. Naomba sana watu walikuwa wanaifurahia nyamapori na ilikuwa inaenda vizuri tena siyo kwa magendo kwa sababu, bucha zilikuwepo na shughuli ilikuwa inaenda vizuri. Naomba zile bucha, kupitia *TAWA,* basi zirudi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni *TAWA* ofisi yao iko Inyonga, Makao Makuu ya Mlele. Naomba sana ndani ya Jimbo la Nsimbo tunapata tabu, waweke ofisi ndani ya Wilaya ya Mpanda, ili wananchi waweze kupata leseni zao kwa urahisi, kwa ajili ya uwindaji.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Itenka, Mto wa Katuma, kuna viboko wengi. Kwenye Ofisi za Halmashauri zetu kuna vitengo vya maliasili, naomba sana wapate uwezeshwaji wa magari, ili waweze kwenda kuwafukuza wale viboko.

Mheshimiwa Spika, vilevile ndani ya Kata ya Stalike kutokana na wanyama wanavyoongezeka kwa wingi, hususan tembo kwa sababu, tumepakana kabisa na Mbuga ya Katavi, naomba pale Stalike tuweke kituo kidogo cha maliasili, ili wanyama wakizagaa waweze kurudishwa katika maeneo yao kwa sababu, sasahivi wanyama wengi wanazagaa wanafika katika Kata mbalimbali za Kapalala, Mtapenda na Uruwira. Sasa tukiweka kituo cha maliasili katika Kata ya Stalike itatusaidia sana kuweza kurudisha hawa wanyama katika eneo lao la uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kifuta jasho. Tunashukuru mwaka jana kifuta jasho kilitoka, lakini kwa asilimia ndogo sana. Tunaomba kwa sababu, athari wanayopata wananchi kupitia mashamba yao ni kubwa, naomba kifuta jasho kiongezwe. Wananchi wanapata hasara kubwa, wanalima halafu mazao yao yanaharibiwa.

Mheshimiwa Spika, naenda *TFS*. Ninaomba nimpongeze sana Kamishna wa *TFS* kwa lazi kubwa na nzuri anayoendelea kuifanya na vilevile ameendelea kuwa msikivu sana. Kulikuwa na matatizo mengi makubwa, tulikuwa tunamlalamikia kuhusu vijana wake wanavyowapiga wananchi, yale matatizo yamekwisha kabisa. Naomba nimshukuru kwa sababu, amekubali kuja kwenye Jimbo la Nsimbo. Naomba aje kwa sababu, yeye katika Jimbo la Nsimbo ndiye mdau wangu mkubwa, aje tuoneshane mipaka ya *TFS* na wananchi, ili tatizo hili liweze kufutika kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Kamishna Silayo kwa kazi kubwa, ni msikivu. Tunakuombea kila la heri kwa kazi kubwa ambayo unaendelea kuifanya. Ndani ya Jimbo langu la Nsimbo nina Mbuga ya Katavi, bado hatujafanya hamasa ya utalii katika mbuga ya Katavi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa sana, amehangaika, Wabunge wengi wamezungumza humu ndani.

Mheshimiwa Spika, Mbuga ya Katavi ndiyo yenye wanyama wakubwa na twiga mweupe anapatikana kwenye mbuga hii. Ninaomba sana tufanye hamasa au kuitangaza Mbuga ya Katavi iweze kuwa na watalii wengi kwa sababu, ya mazingira ya Mkoa wa Katavi, sisi sasa hivi tuna uwanja wa ndege, tuna barabara ya lami, hatuna shida. Vilevile, tunawapongeza wawekezaji mbalimbali wameendelea kujenga hoteli, ina maana hata watalii sasa hivi wakija hawawezi kupata shida.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru na ninaunga mkono hoja 100%. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, atafutiwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza,

kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai tuko hapa tunachangia Wizara ya Maliasili. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Angellah Kairuki na Naibu wake Mheshimiwa Kitandula na watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi wanazoendelea kufanya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, ninayo mambo ya kuchangia kwenye Wizara hii. Kwanza kabisa, napenda ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuboresha utalii nchini Tanzania, kuitangaza Tanzania, imefahamika Kidunia, kwa ajili ya ile Filamu ya *Royal Tour.* Mheshimiwa Rais baada ya Filamu ya *Royal Tour* matokeo yake ni watalii wengi wamekuja nchini na watu wengi wamekuwa na mvuto wa kuja kuiona Tanzania ikoje.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo sasa hivi tumekuwa na watalii wengi, lakini tuna uhaba wa vitanda na hoteli. Itakumbukwa huko nyuma Tanzania ilikuwa na hoteli za kitalii, tulikuwa tuna hoteli nyingi kwenye hizo mbuga zetu za wanyama. Hoteli hizi zilikuwa zinamilikiwa na Serikali, lakini ilipokuja Sera ya Ubinafsishaji Serikali ilizibinafsisha hoteli hizo. Hoteli hizo ziko katikati ya Mbuga zetu za Wanyama, labda kwa kuzitaja, naweza nikatumia kishikwambi ili kuweza kuzitaja; ziko hoteli kule Serengeti ambazo zilibinafsishwa na hazifanyi kazi vizuri, lakini ziko hoteli kule Ngorongoro ambazo pia, zilibinafsishwa na hazifanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Kamati yalikuwa ni Serikali kuzirudisha hoteli hizo, ili ziweze kutumika na kuangalia uhitaji wa hoteli wa sasa ulivyo. Iko Hoteli ya Lobo na Seronera, lakini pia, kule Srengeti zipo hoteli hizo, jumla Serikali ilibinafsisha hoteli 23, katika hizo hoteli sita hazijaweza kutimiza masharti ya ubinafsishaji, bila kuisahau *Mikumi Wildlife Lodge*. Vilevile zipo hoteli za *Kunduchi Beach* pamoja na *Embassy* ambazo toka zimebinafsishwa hazijawahi kufanya kazi. Ombi la kamati lilikuwa ni kuzirudisha hizi hoteli na lilikuwa kwenye Azimio la Bunge. Naiomba Wizara ya Maliasili na Utalii itekeleze Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo ninapenda kulizungumza ni Mradi wa Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali

*(Destination Digital Marketing Commanding Centre)*. Mradi huu uko Dar es Salaam na umetumia shilingi 1,372,256,210.07. Mradi huu umejengwa ukiwa una miundombinu yote ya kutangaza utalii nchini Tanzania, upo pale Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, ni nini hoja yangu ninayotaka kusema hapa? Hoja yangu ni kwamba, ndiyo maana kamati haikukubaliana na zile shilingi bilioni mbili zilizokuwa zimetengwa, kwa ajili ya kujenga mfumo mwingine wakati tayari tuna mfumo ambao upo.

Mheshimiwa Spika, kuna zile shilingi bilioni 19 ambazo ziliongezwa kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii. Katika hizo shilingi bilioni 19, shilingi bilioni mbili zilikuwa imetengwa, kwa ajili ya kujenga huo mfumo. Kamati iliangalia ikaoanesha kwamba, tayari tuna mfumo ambao tungeweza kuuendeleza na mfumo huo kazi yake ni kutangaza vivutio vilivyopo nchini kwetu Tanzania kidijitali. Hivyo basi, hatukuona sababu ya kuja na mfumo mpya. Sisi, kama kamati, tungeomba kama mapendekezo yalivyopendekeza katika zile shilingi bilioni 19 ambazo ziliongezwa kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii, shilingi bilioni 10 ziende kwenye fedha ya maendeleo na shilingi bilioni tisa ziweze kwenda...

**SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo, subiri kidogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, haya.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge punguzeni sauti kidogo. Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, hivyo basi, kama kamati, tulikaa tukaona kwamba, kwa vile pesa zimeongezwa shilingi bilioni 19, basi zingeweza kutumika kwenda kupunguza matatizo ya tembo na wanyama waharibifu. Sasahivi kumekuja huu ugunduzi wa bomu baridi kufukuza tembo. Hizi ni *temporary measures, they are not permanent solution,* kwa ajili ya tembo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili kupitia Taasisi ya *TAWIRI* mje na *solution* ya hawa tembo. Inawezekana hawa tembo

wanahama kule porini kwa sababu ya njaa. Tembo wanakula viazi na matunda mbalimbali. Naomba nitoe ushauri kwenye suala la tembo, ilkiwezekana iletwe kanuni hapa, hayo maeneo wanayokaa tembo vipandwe hivyo viazi na pia, muangalie ni mazao gani mengine ambayo tambo wanakula.

Mheshimiwa Spika, tembo wako milioni 60, sasa hivi wanazidi kuongezeka. Sasa baada ya miaka 10 au 20 tutakuwa na tembo wangapi na sisi hatuwavuni? Tunawashughulikiaje hawa tembo? Tuwapandie mazao wanayopenda kula huko huko porini, ili waweze kula kwa sababu, tembo kama atapandiwa viazi atakula hivyo viazi na kama atapandiwa hayo matikiti maji atakula hayo matikitimaji.

Mheshimiwa Spika, haya maeneo ambayo tembo wanakaa hawa *TAWIRI* waje na utafiti wa kudumu, wakapande mazao ambayo tembo wanakula, ili tembo wakae kulekule msituni. Ninachokiona hapa ni tembo anatoka porini kuja kwa wananchi, kwa ajili ya njaa. Njaa inamuuma ndiyo maana anatoka porini, kiu inamshika ndiyo maana anatoka porini kwa sababu, hata mabwawa ukiwauliza Wizara ya Maliasili na Utalii, hawajaweza kuchimba mabwawa ya maji kwenye kila hifadhi. Nitolee mfano kule Katavi, bwawa liko kule limejaa matope, tembo ni lazima atavuka kuja kutafuta maji.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni mabwawa yachimbwe na mazao wanayokula tembo yapandwe huko huko kwenye hifadhi.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Taska Mbogo. Umesema tembo wako milioni 60?

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, samahani niweke *data* vizuri zisije zikarikodiwa vibaya. Tembo wapo 60,000, simba 17,000, chui 24,000 na nyati 225,000. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile ajiandae.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Nianze kwa kupongeza Serikali zetu zote mbili kwa maana ya Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu na Serikali ya Dkt. Hussein Mwinyi, kule Zanzibar kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika ku-*promote* sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nimpongeze Waziri wa Wizara hii, Dada Angellah Kairuki pamoja na Naibu Waziri ndugu yangu Dunstan Kitandula kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika sekta hii ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukupongeza wewe kwa kuwa mdau mkubwa wa utalii katika Nyanda za Juu Kusini. Tulia *Marathon* na tamasha lako la ngoma ni maeneo muhimu sana ambayo yanatuonyesha ushiriki wa mtu mmoja mmoja kama mdau katika kukuza utalii hasa katika maeneo ya Kusini, eneo ambalo limesahaulika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nakitegemea, baada ya miaka yote hii ya wewe kuandaa *marathon* pamoja na tamasha la ngoma, ule ushiriki sasa wa Serikali ku-*promote* matamasha haya, siyo tu kuwa ya kitaifa lakini kwenda katika ngazi ya kimataifa hilo sijaliona. Pia kuna jitihada nyingi ambazo zinafanywa na wadau wengine ambao wanafanana na wewe katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ambayo yanahitaji msukumo wa Serikali ili matamasha hayo na *event* mbalimbali ambazo zinaweza zika-*promote* utalii siyo tu kwenda katika ngazi za Kitaifa lakini na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachokiona ni kwamba Serikali imehodhi utalii, wananchi hawana *ownership* ya utalii wao na wale ambao wana-*engage* kwenye ku-*promote* utalii hawapati msaada ama ushiriki wa Serikali katika kuwavusha kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo naliona pia ni uratibu wa sekta ya utalii ndani ya Wizara za Serikali na taasisi za Serikali. Kwa mfano, Wizara ya Elimu ni muhimu sana kushirikiana na Wizara ya Utalii katika kutengeneza mitaala kufundisha vijana wetu ili wawe *competent* katika sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia unaweza kuona, kwa mfano pale *VETA* - Mikumi, kile chuo kinatoa kozi za utalii na pale kuna mgahawa mzuri tu ambao una-*train* vijana wetu lakini sasa hivi tunavyozungumza ni mwezi wa saba uko kwenye ukarabati ambao hatujui unaenda kuisha lini. Sasa vitu kama hivyo ambavyo vina-*train* vijana wetu kuwa *competent* kwenye sekta ya utalii vinatia shaka kama tunaweza kufikia malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mikumi mpaka sasa haina umeme na ukiuliza kwanini, *TANESCO* wamewapelekea bili kubwa miaka yote hii hawawezi kulipa kwa hiyo wame-*opt* kutumia majenereta jambo ambalo linaongeza gharama ya uendeshaji. Hivi kama Wizara ya Nishati imeshindwa kukaa na Wizara ya Utalii kupeleka umeme pale kuna jambo gani lingine ambalo wanaliweza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili siyo tu linaongeza gharama ya uendeshaji lakini pia ni ndwele ambayo inaashiria kwamba kuna changamoto ya mawasiliano na uratibu kati ya sekta ambazo ni muhimu kushirikiana pamoja ili ku-*promote* utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Uchukuzi sasa hivi tuna *SGR train* ambayo inaenda kuanza kazi, kutoka pale ni kilomita 20 tu kufika Kilangali kufungua geti kuingia mbugani. Tumeshazungumza sasa hivi hii ni bajeti ya tatu, hakuna kinachofanyika. Mteja au mtalii ambaye anaondoka Dar es Salaam kwa *SGR* mpaka Kilosa, kusafiri kilomita 120 kwa vumbi mpaka kuingia kwenye geti la Mikumi ni sawa sawa na kuweka kiraka cha batiki kwenye suruali ya *jeans*. Haipendezi, haifurahishi wala haitamanishi, wakati Wizara ya Ujenzi inaanza miradi mipya, inaacha barabara hii ambayo ni ya msingi sana katika ku-*promote* utalii na suala zima la uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ushirikishwaji wa wananchi ni muhimu lakini ku-*militarize* utalii ni jambo lingine ambalo tunapaswa kulizungumza. Haifurahishi mtalii anapoingia *airport* anakutana na askari wamevaa kijeshi na nyota zao kwa ajili ya kumgongea *passport* ni jambo jema, lakini anapotoka pale anakutana na trafiki kibao ambao wanamsimamisha barabarani na anapofika kwenye hifadhi zetu anakutana na wengine ambao wamevaa kijeshi na bunduki. Sasa kuna watalii wengine wamekuja kupumzika wana *trauma* zao. Wametoka kwenye vita huko wamekuja kupumzika wanakutana na wanajeshi kila sehemu, mpaka sehemu ya kupumzika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sasa tukaona ni jinsi gani sekta nzima ya utalii, askari wanabaki kulinda usalama wa watalii lakini tuwe na vionjo vya kiraia hasa kwenye eneo la huduma. Mtu ambaye anakutana na mtalii anamhudumia mtalii, anapoingia pale kwenye mbuga au anapoingia kwenye hifadhi akutane na watu ambao wamevaa kiraia ambao wanaweza wakampokea vizuri na huyu mteja akafurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo napenda kuunga mkono suala ambalo sisi Wabunge tumelipigania sana, sehemu ya malipo au mapato ya utalii kubakia hifadhini. Hili linaweza kuboresha sana uendeshaji wa hifadhi zetu zikaongeza ufanisi na kuimarisha miundombinu ambayo imeharibika sana na mvua za El Nino. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu za kuchukua hizi fedha mwanzoni kupeleka Mfuko Mkuu wa Serikali bado zingalipo. Hata maamuzi haya ya kuziacha fedha hizi kwenye hifadhi ni kwa sababu ya changamoto ambazo tunazi-*face* katika hifadhi zetu. Sababu ambazo zilipelekea kuchukua fedha hizi ni ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha. Sababu hizi bado zipo na urejeshaji wa fedha hizi kwa ajili ya matumizi ya kuendesha hifadhi zetu ni lazima kuwe na udhibiti wa matumizi ya fedha hizo ili ziende kwenye malengo ambayo Bunge linadhamiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilio cha Bunge na msukumo wa Bunge kuhakikisha hifadhi zetu zinapata fedha hizi ni lazima Serikali iende

kusimamia fedha hizi kwenda kuboresha na kutangaza sekta ya utalii na maeneo mengine na siyo kurudi tena kule ambako tulitoka, kwenye ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia kilimo, tunazungumzia ruzuku ya mbegu na pembejeo kwenye mifugo na maeneo mengine. Hata kwenye nishati kuna ruzuku ya kujenga vituo vipya vya mafuta katika maeneo ambayo hayafikiki. Ni lini Serikali italeta ruzuku kwenye Sekta ya Utalii kwa ajili ya kuwawezesha vijana kujenga makazi, vyumba na malazi kwa ajili ya watalii wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kuna sekta ngumu ya kuwekeza ni hii lakini ni sekta mbayo inalipa sana. Ni vizuri Serikali ikaja na mpango wa kuwezesha vijana wetu wawekeze kwenye malazi kwa ajili ya watalii hasa wale ambao wamekuwa *trained* na wamemaliza kozi mbalimbali ambazo zinahusiana na utalii. Kwa kufanya hivi tutatengeneza ajira lakini tutaboresha mazingira na sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwezi kumaliza bila ya kuzungumzia changamoto za migogoro hasa kati ya hifadhi na wananchi au vijiji. Kule Mikumi tuna changamoto ya hifadhi, utakuta mpaka mmoja una *GN* zaidi ya tatu. Mamlaka ambazo zinatoa *GN* hizi ni Serikali hiyo hiyo. Utakuta kuna *GN* ya sitini na ngapi, kuna *GN* ya sabini na ngapi, kuna *GN* ya 2000. Je, ni mazingira gani ambayo taasisi zetu na mamlaka zetu zinatoa *GN* mbalimbali ambazo zinaenda kupelekea migogogro kwa wananchi wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina tutamalizia na Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi uliyonipa na mimi niweze kuchangia Wizara hii muhimu, Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza, ninaunga mkono mapendekezo ya

Kamati ya nyongeza ya bajeti ya shilingi bilioni 16 ili kwenda kuimarisha utafiti wa misitu na wanyamapori. Kwa kweli hapo ndiyo hasa eneo lenyewe ambalo kama tunataka kuweka uhifadhi wa kweli ni lazima tuwekeze kwenye sekta zetu za utafiti kwa maana ya *TAFORI* pamoja na *TAWIRI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Wizara kwa kufanya vizuri sana katika ukusanyaji wa mapato kwa sababu ni kama sasa asilimia 97.12 na muda bado, kwa hiyo ina maana watavuka malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa makumbusho wa Marais hapa Dodoma pia ni jambo zuri sana la kupongezwa kwa ajili ya kujenga makumbusho ya Marais wetu na shilingi bilioni moja imetengwa kwa shughuli hiyo, tunawapongeza Wizara, wafanye haraka, wajenge makumbusho ya hawa viongozi wetu ili vijana wetu wapate mahali pa kujifunza iwe eneo la kufanya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni suala la wananchi ambao mifugo yao imekamatwa muda mrefu. Nimesoma kitabu chote cha Waziri sijaona, mifugo ilishakamatwa zaidi ya ng'ombe 11,438, wafugaji hao walishashinda kesi mahakamani lakini hakuna kauli yoyote ya Serikali mpaka sasa hivi, kufanya hivyo ni kukiuka kabisa misingi na nguzo ya utawala bora na hasa utawala wa sheria. Kwa sababu kama watu wameshinda kesi mahakamani ni nini tena kinachoendelea? Serikali imeshindwa nini kuwafidia wafugaji hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la nne ni suala hili la Kijiji cha Nyatwali kule Bunda na Kijiji cha Gombo kule Malinyi. Wananchi hawa ilikuwa kazi sana kuwashawishi kukubali kupisha maeneo yao, leo wameshakubali kupisha maeneo kinachoshindikana ni nini kulipwa haki yao ili waende wakatengeneze maisha mapya? Wabunge wa maeneo hayo wamelalamika muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tano ni kuuawa kwa mamba mkubwa duniani. Tulipokea taarifa hapa tarehe 27 Disemba, 2023,

muwindaji mmoja bingwa kutoka Marekani alijitapa akiwa na mamba amemning'iniza juu ya mti na baadaye kuanza kumchuna mamba huyo akijitapa kwamba amefanikiwa kumuua mamba mwenye urefu mkubwa kuliko mamba wote duniani.

Mheshimiwa Spika, jambo hili lilileta taharuki sana hapa nchini lilipotokea na ilitangazwa katika vyombo vyetu vya habari na mitandao ya kijamii likaenea kila sehemu. Sasa bahati mbaya sana pia nimeliangalia kwenye hotuba ya Waziri sioni jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mamba wetu ambaye ana urefu wa sentimita 493.8 ni karibu mita tano. Mamba ni mrefu sana na ni kweli taarifa za kwamba huyu alikuwa ni mamba mrefu kuliko wote duniani hazijawahi kukanushwa na taasisi yoyote ndani ya nchi na nje ya nchi. Sasa najiuliza, kama tulikuwa na mamba mwenye urefu mkubwa kuliko mamba wote duniani aliruhusiwaje kuwindwa kwa utaratibu wa kawaida hapa nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri na *TAWA* walikubalije mamba huyu awindwe? Je, kweli huyu mamba ana thamani sawa na mamba wengine wa kawaida tu ambao unaweza ukatoa kibali akawindwa? Je, nchi yetu haikuwa na matumizi yoyote na huyo mamba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukitafuta vivutio vya watalii, kama tuna mamba mwenye urefu kuliko mamba wote duniani, kwanini huyo mamba asingewekewa vizimba, tukamjengea vizimba, tukajenga kituo cha utalii pale. Leo anaenda kuwindwa kwa kibali cha kawaida tu. Hata *TAWA* walipotaka kujibu hili swala, kwa taarifa yao tarehe 02 Januari, 2024 walitoa majibu mepesi sana wakasema; "*mamba huyo aliwindwa katika kitalu cha Lake Rukwa GR kwa kibali namba hicho cha tarehe 12, Agosti mpaka tarehe 19, Disemba, na kwamba, mamba huyo alikuwa na urefu huo uliotajwa ambao ni sentimita 493.*" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama huyu mamba, kwa sababu hawa mamba tunajua wanasimamiwa na ile Sheria ya Umoja wa Mataifa ya wale viumbe ambao wapo kwenye hatari ya kutoweka. Kwa hiyo, ina

maana kwamba *TAWIRI* walikuwa wanajua na vijana wetu wote walikuwa wanajua kwamba tuna mamba mwenye urefu mkubwa kuliko mamba wote duniani. Sasa huyu mamba aliendaje kuwindwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naona kwamba hizi zilikuwa ni njama baina ya watendaji wetu wasiokuwa waaminifu kula njama kwa ajili ya kulihujumu Taifa letu, sasa kama hayo yamefanyika, naomba hatua kali zichukuliwe na uchunguzi ufanyike juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesikia kengele, jambo la mwisho ni jambo ambalo limeripotiwa pia na Kamati juu ya ubimbikazaji wananchi wanaoishi kando kando ya hifadhi kesi. Manyanyaso ambayo wanapata, kupigwa, kuonewa na hadi kuuawa. Kamati imesema vizuri sana juu ya jambo hili na mimi nilileta ushahidi kwako baadhi ya watu ambao walipigwa wakauawa, wakateswa, wakanyang'anywa mifugo yao na ushahidi wangu uka-*prove* ndani ya Bunge kwamba ulikuwa ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu alitoa maagizo 12, juu ya kuzuia ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora na sheria za nchi kwa baadhi ya watumishi wetu wa hifadhi. Kamati inaenda inanukuu kwamba hata Mahakama nayo sasa imechoshwa na tabia ya Wahifadhi wanaowanyanyasa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imenukuu kule nyuma hukumu iliyotolewa na Jaji wa Mahakama Kuu, Kamazima Idd Kafanabo, ambaye alipokuwa anahukumu kesi na kumwachilia huru Richard Changei Ng'ombe anasema; "*Mahakama haiwezi kufumbia macho jambo hili linaloonekana kuzoeleka, kujirudia na kutofuata maadili ya kazi kunakofanywa na maafisa wengi wa uhifadhi na wengine katika haki jinai hasa katika ukamataji wa watuhumiwa na uchukuaji wa vielelezo.*" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mahakama nayo imechoshwa na watumishi wanaofanya manyanyaso haya. Sasa Kamati inasema pia

haijaelezwa kama kuna uchunguzi wowote uliofanywa na Wizara juu ya mambo haya. Kamati inasema hakuna hatua zozote zilizochukuliwa hadi sasa juu ya watu ambao wamekuwa wakionea wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Wizara ya Maliasili na Utalii kukaa kimya, Waziri Mkuu ametoa maagizo yake yakapuuzwa, wewe umeniagiza mimi nilete ushahidi, hakuna kilichotekelezwa. Kamati mpaka sasa hivi inaripoti hakuna kilichofanyika. Sasa kwa sababu wote tumedharauliwa, naomba kulishauri Bunge lifanye yafuatayo: -

Moja, Waheshimiwa Wabunge nawaomba leo tutoe fundisho, tuitake Serikali kupitia Waziri Mkuu kuwafukuza kazi watumishi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzia Waziri mpaka mfagizi wa ofisi. *(Makofi/Kicheko)*

Pili, Bunge liunde Kamati ya kuchunguza mambo haya kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hatuwezi kuendelea kuona wananchi wanafanyiwa haya wanayoendelea kufanyiwa sasa hivi. Ni lazima tufike mwisho, tuchukue hatua. Kamati ya Bunge iundwe, tuende tukachunguze maeneo yote ya uhifadhi na kwenda kubaini mambo haya ambayo wananchi wetu wamekuwa wakifanyiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kusambaa kwa mimea vamizi maeneo ya hifadhi. Jambo hili nimeona, ukisoma hotuba ya Waziri anazungumzia hekta ambazo zimeshughulikiwa mwaka huu kwa maana ya kung'oa hayo magugu vamizi ni hekta 3,776.57. Hekta hizo 3,700 ni ndogo sana ukilinganisha na uvamizi wa mimea katika hifadhi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hifadhi zetu zote zimevamiwa na uvamizi huu ni mkubwa. Tutabeba bunduki zote lakini hifadhi zetu zitateketea kwa sababu wanyama hawana malisho, watakosa maji, wanyama watakimbia mbuga zetu na kuja kwenye makazi ya watu na hata kwenda kwenye hifadhi za nchi zingine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutujengea kituo cha kisasa kabisa cha askari wa wanyamapori pale Nachingwea eneo la Nditi, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Maliasili na Utaalii kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee niwape pole sana wananchi wa Jimbo langu la Nachingwea waliopata kadhia mbalimbali kutokana na wanyama hawa wakali jamii ya tembo na maswaibu mengine yaliyotokea kutokana na mvua kubwa ya El Nino. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Serikali, naomba nizungumzie kidogo kwenye eneo hili la Ndovu. Jimbo langu la Nachingwea lina Kata 36 na Kata 20 zimevamiwa na wanyama wakali jamii ya tembo na nitayasema hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzia 2020/2021 tulipata kifo cha mwananchi mmoja, 2021/2022 tulipata kifo cha mwananchi mmoja na 2022/2023 tulipata vifo sita vilivyotokana na kuuawa na tembo. Mwaka 2023/2024 mpaka hii Juni, kuna vifo 10 vimetokea baada ya wananchi hao kuuawa na tembo. Kwa hiyo, ukiangalia hiyo *trend*

unaona kila mwaka kuna ongezeko la vifo vya wananchi vinavyotokana na kukanyagwa na tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupongeza kazi kubwa na nzuri ambayo inaendelea kufanywa na Serikali bado naiomba sana Wizara kuchukua juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba kifo tena kwenye Jimbo la Nachingwea kinachotokea baada ya kukanyagwa na tembo inakuwa basi, labda niseme tu, kama Mheshimiwa Waziri hatakuja hapa na mpango utakaoonesha namna atakavyokwenda kudhibiti tembo kule Nachingwea, nitarudi na shilingi yake kule Nachingwea kwa sababu wananchi wa Jimbo la Nachingwea wameniomba niwasemee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifo cha mwisho kimetokea tarehe 24, Mwezi wa Tano na kijana huyu alikuwa bado mtoto wa miaka 13. Kwa jina alikuwa anaitwa Antony Vumi Ndimba. Unaona kwamba bado tunapoteza nguvu kazi kubwa na ukienda kwenye maeneo hayo unaona namna watu walivyokata tamaa. Hata majirani zangu huku wananiambia wewe ni Mbunge unayewakilisha wananchi pamoja na ndovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa niiombe Serikali kuchukua hatua ili kukomesha kabisa vifo hivi ambavyo vinatokana na wanyama hao wakali jamii ya ndovu. Hata wananchi wa maeneo haya wengi wamekata tamaa ya kutoa ripoti ya yale wanayoyapata ikiwemo pamoja na uharibifu wa mazao na vitu vingine ambavyo vinatokea kwenye maeneo haya. Wamekata tamaa kwa sababu wanaona hatua hazichukuliwi kwa maana ya kukomesha kabisa wale wanyama kuonekana kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwa umri wangu mpaka nimefikia sasa nasogea karibu 50, miaka 40 yote sikuwahi kuona tembo kwenye maeneo haya. Kwa hiyo, kufikiri kwamba maeneo haya ni ushoroba wa tembo si sahihi! Maeneo haya siyo ushoroba wa tembo badala yake maeneo haya yamevamiwa na tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano kidogo, maeneo haya kabla ya hapo hawa tembo walikuwa hawaonekani kabisa huku. Kwa hiyo, ni uvamizi wa wanadamu na shughuli zao kwenye misitu kwenye hifadhi za hawa tembo ndiyo zimewafanya sasa waondoke kule wavamie kwenye maeneo ya makazi, ikiwemo na shughuli za ufugaji. Ni vizuri Serikali ikachukua jambo hili kwa uharaka wake ili kuweza kunusuru maisha ya hawa watu. Hata hizi takwimu tunazozisema siyo ajabu siyo sahihi kwa sababu kuna wananchi wengine wameshakata tamaa, hawawezi kabisa kutoa hizi ripoti badala yake hizi ni ripoti zile ambazo tayari tulishazifanyia kazi na tulizipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze kwenye kifuta jasho au kifuta machozi. Kwenye eneo hili nalo kuna muongozo ulitolewa na Wizara, kwa yule ambaye shamba lake linaharibiwa likiwa chini ya hekari moja halipwi na yule ambaye shamba lake linaharibiwa ikizidi zaidi ya hekari tano, zile hekari zinazozidi hazilipwi. Sasa hatuna sheria Tanzania inayomfanya kila mwananchi aidha alime zaidi ya hekari mbili au hekari tatu au zaidi ya hekari moja. Kwa hiyo, ni utaratibu wa kawaida. Ninamuomba Waziri, kama ni mwongozo huo muongozo sasa hauwatendei haki wananchi wetu. Futa huu mwongozo kwa sababu kimsingi unakwenda kuonea wananchi kwa sababu hakuna sheria inayomlazimisha mwananchi kulima zaidi ya hekari moja au pungufu ya hekari tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kwenye eneo hilo hilo, sisi kule kwenye Jimbo la Nachingwea tunafanya kazi kwa karibu sana na wenzetu wa *TAWA*, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Kamishna wa Uhifadhi wa *TAWA* kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya, pia ninampongeza sana Kamishna Msaidizi ambaye ni Kamanda wa Kanda kule Kusini, wanafanya kazi kubwa na nzuri, wanazo changamoto nyingi na mimi kama Mbunge nimekuwa nikishiriki mara kadhaa. Jambo la kwanza ni uchache wa watumishi wenyewe kwa maana ya hao askari na askari wa *VGS* kwa maana ya wale vijiji, kwenye eneo hili sasa na mimi niunge mkono lile pendekezo la Kamati, zile fedha, lile ongezeko la shilingi bilioni 19 sasa liende likafanye kazi kwenye maeneo haya kuwaongezea bajeti wenzetu wa *TAWA* ili waweze kufanya kazi yao ikiwa ni pamoja na kuboresha

maslahi yao. Tuende tukaboreshe maslahi yao ili walingane na majeshi mengine ya uhifadhi kama *TANAPA* na watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo ningeweza kutoa mapendekezo kadhaa ili wenzetu waweze kuyafanyia kazi. Pendekezo la kwanza nimeshasema kwamba *TAWA* ipewe kipaumbele kwa sababu vijiji vingi sana, Majimbo mengi yaliyo pembezoni tunahudumiwa na *TAWA*, kwa hiyo, hawa wapewe kipaumbele kwa maana ya kuajiri watumishi, askari wenyewe lakini pia na kuajiri wale askari wa vijiji kwa maana ya *VGS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kushirikiana na Halmashauri kuhakikisha kwamba vile vijiji vyote ambavyo vimeathirika na kadhia hii ya tembo tuwe na hawa askari ili likiwa linatokea jambo tuweze kupata usaidizi na waweze kuchukua hatua mara moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili ilishagonga, malizia.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, naunga mkono hoja lakini kama sijapata majibu ya namna tembo watakavyoondolewa kule Nachingwea, nitaondoka na shilingi ya Mheshimiwa Waziri kurudi nayo kule Nachingwea, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana kwetu kwa siku ya leo. Nitatangaza majina ya Wabunge ambao tutaanza nao mchana ama jioni tutakapokutana. Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray na wengine tutaendelea kuwataja kadri muda utakavyokuwa unakwenda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, mnatangaziwa kuwa Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi ambao wapo chini ya Wizara ya Fedha wapo kwenye Viwanja vya Bunge kwa ajili ya kutoa elimu na kupokea malalamiko yanayohusiana na huduma, kwa hiyo, mnakaribishwa kwenda huko.

Waheshimiwa Wabunge, pia mtaelekezwa taratibu na usimamizi wa Sheria za Kodi unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania - *TRA*. Maonesho haya yataanza leo na yatakwisha kesho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11 kamili jioni leo. *(Makofi)*

*(Saa 7.04 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa jioni hii kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Maliasili. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha mimi kusimama jioni hii kutoa mchango wangu. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watumishi wote walioko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, mimi jimbo langu, 60%, zamani nilikuwa nasema linazungukwa na Hifadhi ya *Selous*, sasa hivi kumegawanyika kuna Hifadhi ya Selous pamoja na *TANAPA* ile Hifadhi ya Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo naomba tu niende moja kwa moja nianze kuchangia kwa kadhia kubwa inayotupata sisi tunaozungukwa na hifadhi dhidi ya hawa wanyama waharibifu wanaoitwa tembo. Sitaitendea haki Wizara hii nisipolizungumza suala la tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, mtu yeyote wa Mikoa hii ya Lindi na Mtwara ukimsimamisha, atazungumzia suala hili la tembo. Tunaweza kulirudia kwa kila Mheshimiwa Mbunge atakayesimama ni kwa sababu ya uzito uliopo. Mimi nina kata 20 lakini miongoni mwa kata hizo, ziko kata zaidi ya 15 ambazo kwa kweli kila siku iendayo kwa Mungu tunaripoti kadhia hii ya tembo. Ipo Kata ya Kibutuka, Kata ya Nangano, Kata ya Mangirikiti, Kata ya Mkutano, Kata ya Mirui, Lilombe, Mlembwe, Liwale B, Makata, Ngongowele na Kata ya Mpigamiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi kata kila siku nina ripoti za wanyama hawa tembo. Kwa hiyo tunakuomba Mheshimiwa Waziri, tunakuomba sana sana ongeza juhudi. Mimi naiona nia njema ya Serikali kama vile tunavyoambiwa kuna mabomu, haya mabomu baridi ambayo yatatusaidia. Mimi namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutujengea kile kituo pale Ngumbu. Naomba pale Ngumbu pakafanyiwe utafiti kwa sababu Ngumbu tembo wakikaa pale, wanakaa mwaka mzima. Yaani tembo akiingia pale, hata kumtoa ni kwa shida. Kwa hiyo kuna mazingira ambayo pale Ngumbu pamoja na kituo kiko pale, lakini bado tembo wanasumbua. Kwa hiyo naiomba sana Serikali iende ikafanye utafiti pale kuona ni namna gani hawa wanyama tunavyoendelea kuathirika nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine, naomba niende kwenye Wizara hii inapozungumza utalii Kusini. Niliongea hili Bunge lililopita, Bunge la Kumi na Moja, Wizara hii Mheshimiwa Waziri utakapokuja ku-*wind up* jioni hii ya leo, utuambie unaposema utalii Mikoa ya Kusini, kwani Lindi na Mtwara iko Kanda ipi? Maana huwa haitajwi.

Mnaposema Utalii Kusini, Lindi na Mtwara huwa hazitajiwi. Mwaka juzi Bunge la Kumi na Moja, nilizungumza, palileta fedha kutoka *World Bank* kwa ajili ya kukuza utalii Kusini, lakini fedha ile haikuingia thumni Mkoa wa Lindi wala Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokuja kuuliza hapa, mkasema zimeenda Kanda za Juu Kusini na leo Mheshimiwa Dkt. Kabati pale alipochangia, nimemsikiliza, ameitaja mikoa ambayo ninyi mnaitambua kama iko Kusini. Akasema ni Mkoa wa Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, akamalizia na Ruvuma. Haijatajwa Lindi wala haijatajwa Mtwara, sasa utakapokuja hapa utuambie…

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** …Mkoa wa Lindi na Mtwara uko kwenye kanda ipi? Kwa nini…

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Aida Khenani.

**TAARIFA**

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa Taarifa mchangiaji, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati alizungumzia Nyanda za Juu Kusini ndiyo maana hakuzungumza habari ya Lindi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, siipokei, nimefuatilia sana ile Taarifa. Nyanda za Juu amekuja kutaja baadaye sana lakini alitaja Mikoa ya Kusini, akaitaja hiyo mikoa, baadaye akachomeka hilo neno Nyanda za Juu Kusini, hata ukifuata *Hansard* utaikuta. Hili jambo la kutokufikiria kwamba Kusini nako, yaani mimi nataka kujua tu, Wizara ya Maliasili, mnaposema Kanda ya Kusini inakuwaje Kanda ya Kusini haipo Lindi wala Mtwara? Au sisi tuko Kanda ya Pwani? Basi kama tuko Kanda ya Pwani mje mniambie

kwamba bwana, Lindi na Mtwara hatuitaji Kusini kwa sababu iko Kanda ya Pwani, hapo tutaweza kuelewa. *(Makofi*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye *point* nyingine ya mgogoro wa *WMA* ya Magingo pamoja na *TANAPA*. Mgogoro huu umekuja baada ya kuanzishwa *TANAPA*. Tulipokuwa *WMA* pamoja na *TAWA*, hatukuwa tukigombana kwa sababu wote tulikuwa tunafanya shughuli zinazofanana, lakini ilipoanzishwa *TANAPA* yaani kwa maana ilipoanzishwa Hifadhi ya Mwalimu Nyerere, iko migogoro pale, baadhi ya vitalu vimeondoka vimekwenda kwenye ile Hifadhi ya Mwalimu Nyerere. Mgogoro huo mimi nimeufuatilia sana ilifika mahali nilikwenda pale Wizarani, wakaniambia kuna Tume iliundwa na Mheshimiwa Rais na kipindi kile niliambiwa kwamba bado ripoti ile haijafika kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu tulikuwa tumebakiwa na kitalu kimoja kipo Morogoro kwenye Wilaya ya Kilombero. Tukimaliza kitalu hicho, tutakuwa tumemaliza kazi, tutampelekea Mheshimiwa Rais kwa ajili ya maamuzi ili tuweze kujua ni vijiji vingapi vinatakiwa viingie Hifadhi ya Mwalimu Nyerere au vijiji vingapi vimeachiwa na Hifadhi ya Mwalimu Nyerere ili shughuli nyingine ziweze kuendelea. Leo ni mwaka mzima umekatika, hatujapata ufumbuzi suala hili limefikia wapi mgogoro wa *WMA* ya Magingo pamoja na Hifadhi ya Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, tunazungumzia habari za malikale, Historia ya Majimaji haijatuacha nyuma sisi watu wa Liwale. Tunalo boma pale, Boma la Mjerumani boma ambalo limetumika kipindi ambacho watumwa walikuwa wananunuliwa kutoka Nyanda za Juu Kusini pamoja na Kusini (Mikoa ya Ruvuma, Mtwara), kabla hawajafikishwa Kilwa kwenye soko, walikuwa wanafikishwa Liwale. Kuna Boma la Mjerumani liko pale.

Mheshimiwa Spika, mimi nimelifuatilia lile boma, nilikuja kuuliza swali hapa, wakaniambia halmashauri imefanya jambo kulitengeneza lile. Mimi nataka kuwaambia kwa sababu ya uhaba wa mapato tuliyonayo ndani ya halmashauri, boma lile linakwenda kuteketea na historia ile inaenda kupotea. Kwa hiyo naomba watu wa malikale, hebu njooni Liwale mwangalie lile boma. Lile boma, ziko picha za

viongozi mbalimbali wa Vita ya Majimaji wako kwenye lile boma. Boma lile sifa yake kubwa, mawe yaliyojengwa ni matumbawe ambayo yametoka Kilwa, kilometa zaidi ya 230 wazee wetu walikuwa wanatikwa yale mawe kichwani kwenda kujenga lile boma pale Liwale. Kwa hiyo lina historia kubwa sana. Naomba sana, Mheshimiwa Waziri uje Liwale uje utembelee hili Boma la Mjerumani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, naomba niende kwenye kifuta machozi. Mheshimiwa Waziri, mimi nimeshauliza maswali zaidi ya matatu yanayohusiana na kifuta machozi. Kwanza kifuta machozi kile bado kimepitwa na wakati. Mimi tangu niko shule ya msingi, kile kifuta machozi kiwango ni hichohicho, leo tunazeeka miaka 60 kifuta machozi kiwango kimebaki palepale, lakini siyo tu kubaki palepale nacho hakifiki kwa wakati. Nacho ni sababu kubwa ukiona kifuta machozi kinapita kwenye *OC* ya Wizara. *OC* ya Wizara mnawagawia *TAWA*, *TAWA* zikifika kwenye *OC* yao wanaamua nini kipaumbele cha kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaweza kukuta *TAWA* wana madeni, …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imeshagonga…

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** … wakifika pale badala ya kupeleka zile fedha kwa wahusika, wanatumia. Kwa hiyo mimi naomba utafutwe utaratibu mwingine…

**SPIKA:** Haya, ahsante

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** …ili kifuta machozi kiwafikie walengwa.

**SPIKA:** Ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, astaghfirullah! Nakushukuru kwa nafasi. Mimi siwezi kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, tutagawanya ile ya mdogo wangu…

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Liberata Rutageruka Mulamula, Mheshimiwa Profesa Alois Ndakidemi ajiandae.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza naanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna alivyoendelea kuikuza hii sekta yetu ya utalii kupitia *Royol Tour*. Mheshimiwa Rais, kwa muda mfupi amewezesha watalii kuongezeka kwa kasi hapa nchini na tumeona faida ya *Royal Tour*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sekta hii ya utalii ndiyo sekta inayoongeza Pato letu la Taifa kwa 18%, lakini siyo hilo tu, kuchangia 25% katika Pato letu la Taifa kupitia fedha za kigeni. Ukisoma Ilani ya Uchaguzi 2020/2025 utaona kwamba Ilani yetu inaeleza kuwa itafikia watalii 5,000,000 kufikia 2025 kwa kila mwaka. Vilevile, tutakwenda kuongeza Pato letu la Taifa kufikia 2025 hadi dola za Kimarekani 6,000,000,000.

Mheshimiwa Spika, hayo yote yatawezekana endapo Serikali itashirikisha sekta binafsi kwa sababu tusiposhirikisha sekta binafsi, kwa hali ilivyo kwa sasa ni lazima tuwekeze kwenye ujenzi wa hoteli zenye nyota mbalimbali. Ninasema hivi kwa sababu, sasa hivi hoteli zetu zilizopo hazikidhi haja ya watalii wetu. Ukitembelea hoteli zetu utagundua kwamba bado kuna upungufu mkubwa kuanzia kwenye miundombinu ya hoteli lakini hata wahudumu waliopo katika hoteli zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nashauri tu bado kuna haja ya Wizara kushirikisha sekta binafsi ili kukuza zaidi hii sekta yetu ya utalii. Kwa kuzingatia hilo ni pamoja na kwamba vyuo vyetu vya utalii vinavyotoa *course* za utalii pamoja na vyuo vya *VETA* viboreshwe ili

wanafunzi wetu (vijana wetu) wanaosoma katika vyuo hivyo, wapate taaluma ya kutosha na waweze kuhudumia katika hizi hoteli zetu za kitalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bado ukiangalia hata miundombinu ya barabara zinazoelekea katika hifadhi zetu na hapa nitatolea mifano katika Hifadhi yetu ya Tarangire na Hifadhi ya Manyara. Ukienda katika Hifadhi ya Tarangire Geti lile la Kibaoni – Minjingu, Geti la Mamire, Geti lile la Sangaiwe, barabara hizi kuna wakati hazipitiki kabisa hivyo hukwamisha watalii kwenda kwenye hifadhi zetu za wanyama.

Mheshimiwa Spika, lakini ukienda hata kwenye geti la upande wa Manyara kupitia Mayoka, barabara ile kuna wakati inakatika kabisa haipitiki kwa hiyo watalii wanashindwa kufika katika maeneo haya. Ukiangalia barabara zetu hizi, hazitoki mbali na barabara kuu ni umbali mfupi sana. Kwa hiyo naomba Wizara iangalie namna ya kutengeneza zile barabara hata kwa kuweka kiwango cha lami ili watalii wanapokuja iwe rahisi sana kuingia kwenye hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini katika maeneo ninayotoka mimi kuna migogoro ambayo imechukua muda mrefu sana hasa migogoro kati ya *Tarangire National Park* na vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Tarangire. Mfano, tuna vijiji ambavyo vinazunguka Hifadhi ya Tarangire, kuna Kijiji cha Minjingu, Kijiji cha Ayamango, Kijiji cha Gedamar, Kijiji ya Kakoi, Kijiji cha Gijedabung. Iliundwa timu ya Waheshimiwa Mawaziri nane walikuja katika maeneo yetu, wakaangalia haya maeneo, wakafanya utafiti, lakini bado mpaka sasa mgogoro uko pale palepale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba Serikali ione namna gani ya kumaliza mgogoro huu kati ya hivi vijiji nilivyovitaja na Hifadhi ya Tarangire. Migogoro hii inapochukua muda mrefu, inafika hatua wananchi hawaishi hata kwa amani. Kwa hiyo naomba Taarifa ile ya Kamati ya Waheshimiwa Mawaziri nane iliyofanyika ipelekwe kule kwa wananchi ili wananchi wajue lao ni lipi na ambalo siyo lao ni lipi ili

kufanya wananchi waweze kuishi kwa amani na bila migogoro na hifadhi.

Mheshimiwa Spika, hii migogoro ya hifadhi na wananchi inapoendelea, ndiyo pale ambapo unakuta mapigano yanaanzishwa katika maeneo haya. Kwa hiyo ili kuendeleza pia ujirani mwema kwa sababu hivi vijiji vinazunguka maeneo ya hifadhi, ni vyema basi mgogoro huu ukatatuliwa ili wananchi waweze kuishi vizuri na hawa watu wa hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wenzangu pia wameshaliongelea kumekuwa na uvamizi wa wanyama waharibifu katika maeneo yetu. Mfano, eneo la Mamire pamoja na eneo la Mwada kumekuwa na wanyama wengi wanavamia mara kwa mara hasa kipindi ambacho mazao yameshaiva huko mashambani, wananchi wameendelea kupata hasara. Wakati mwingine hata wanyama wale wanapovamia yale maeneo, inachukua muda mrefu kuwarudisha wale wanyama kwenye hifadhi kwa maana ya kwamba hata taarifa ikitolewa, basi hawafiki kwa wakati kuwaondoa wale wanyama, jambo linalopelekea wale wanyama wanaenda kuleta madhara ikiwemo kuharibu mazao lakini pia na kujeruhi wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna hili suala la kifuta jasho na kifuta machozi na fidia, limekuwa na tatizo kubwa sana. Wenzangu wamelizungumzia na mimi nalisemea pia, kwamba kifuta jasho na kifuta machozi imekuwa ni tatizo kubwa. Hebu fikiri mtu ameharibiwa shamba lake la eka moja, mazao yaliyokwisha kukomaa shambani yameliwa, halafu unamletea kifuta jasho baada ya mwaka mmoja tena hela yenyewe ni shilingi 100,000. Hili jambo halikubaliki, naomba Serikali iangalie upya sheria zetu hizi ili kuona namna ya kuwasaidia wananchi kwa sababu wanapovamiwa, wananchi wanaendelea kuwa maskini na wanaendelea kuumia vibaya mno.

Mheshimiwa Spika, mimi nilishauri yawezekana kifuta jasho kinachukua muda mrefu kwa sababu kinatolewa na Wizara. Mimi nashauri kifuta jasho kitolewe na hifadhi yenyewe ili wakati mwingine hata wanyama wanapovamia maeneo yetu, wawe wepesi kwenda

kuwarudisha kwa sababu kitendo cha kuwacheleweshea kuwarudisha wale wanyama, ndiyo wanaendelea kutuletea madhara katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nina jambo lingine ambalo niliona nilishauri, ni kuhusu kurudisha 15% ambayo ilikuwepo ya mapato katika hifadhi zetu. Asilimia zile 15 zinaporudishwa kule zilikuwa zinasaidia sana kuchochea maendeleo hasa katika vijiji vile ambavyo vinazunguka hifadhi. Baada ya kuondoa zile 15%, hata ule ujirani mwema baina ya vijiji na hifadhi unapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi naomba 15% zile zirudishwe ili wananchi wanaozunguka maeneo yale, waendelee kufaidika na uhifadhi wa wanyamapori katika maeneo yetu. Ushauri wangu ni kwamba, asilimia ile ikirudishwa, isipelekwe kwamba ikatengeneze miradi, kwa sababu Serikali yetu ya Awamu ya Sita imeleta miradi ya kutosha katika maeneo yetu: miradi ya maji, miradi ya afya, miradi ya barabara. Kwa hiyo nilikuwa naomba ile fedha ipelekwe vijiji vile vinavyozunguka maeneo yale, lakini wananchi wawe wanakopeshwa. Wanapewa mafunzo, mfano mafunzo ya ufugaji nyuki, ufugaji wa kuku na kilimo cha mbogamboga, ili mwananchi moja kwa moja afaidike na zile fedha ambazo wanapelekewa katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la mwisho nisemee kuhusu ombi la wafanyabiashara wa utalii wakati wanapokata leseni zile za *TAWA*. Naomba gharama zote zile za leseni, zijumlishwe kwenye leseni moja badala ya mtu anapoomba leseni, anaambiwa alipe hapa, alipe hapa, alipe hapa. Kwa sababu fedha zote ni za Serikali, naomba kwamba gharama zote ziwekwe kwenye sehemu moja ili mtu anapolipa mara moja anakuwa amelipa kila kitu badala ya mtu kuhangaika kulipa hapa na hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Liberata Rutageruka Mulamula, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri ajiandae.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza natoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara wa kuvutia watalii wengi sana kuja nchini kupitia ziara zake mbalimbali kupitia ushiriki wake mahiri katika filamu ya *Royal Tour*.

Mheshimiwa Spika, pia tumefahamishwa kwamba kumekuwa na filamu mahususi *(Amazing Tanzania)* iliyozinduliwa hivi karibuni nchini China na asubuhi hii tumefahamishwa na Mheshimiwa ambaye alishiriki katika uzinduzi huo, Mheshimiwa Oliver Semuguruka ambaye huwa tunamwita nyara. Ameshuhudia kwamba kwa kweli ni ushahidi wa kutosha kwamba tumejiongeza na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mbunge) ambaye pia ni wifi yetu. Huwa nasema Kagera hatukosei tunachagua walio nona na wasomi na wako wengi humu. Kwa hiyo, nakupongeza sana kwa hotuba nzuri lakini pia nimpongeze Naibu Waziri wako Mheshimiwa Dunstan Kitandula, huwa namwita mwanadiplomasia *by association;* anajua kwa nini. Nampongeza pia Katibu Mkuu Abbas na Naibu Katibu Mkuu na Wakuu wote wa vitengo na taasisi kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi naomba niwapongeze Wizara kwa mwendo wao wa kasi wa kidijiti. Kwa mara ya kwanza tumepata hotuba kwa kutumia *QR Code,* hata Wizara ya Habari na Mawasiliano haikutumia hii. Kwa kweli kama ni teknolojia ya kidijiti mmejiongeza sana, hongera sana. Pia, tulivyopita kwenye mabanda ulikuwa unapata kama ni *Film* ya *Royal Tour* kama ni ramani ya utalii yote unaipata kwenye *QR Code;* hongera sana Mheshimiwa Waziri na timu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda niwapongeze kwa kuwezesha nchi yetu kutambuliwa katika Ripoti ya Baraza la Utalii na Masuala ya Safari Duniani *(World Travel Tourism Council)*. Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi 10 bora Duniani kwa uhimilivu wa maeneo ya kupokea watalii *(sustainability)* na mlimuona Mheshimiwa Angellah Kairuki alikuwepo wakati Tanzania inatangazwa kuwa miongoni mwa nchi 10 bora Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze katika yale ambayo wengi wameyasema kuongeza mazao ya utalii. Najua *historically* tumejikita zaidi kwenye kutembelea mbuga za wanyama. Hata hivyo, tunajua kwamba kuna fursa kubwa ya kukuza utalii wa fukwe na *hot springs.* Mheshimiwa Bilakwate hayupo hapa lakini ukienda Mtagata Kyerwa, Karagwe kuna *hot springs* ambazo zinawaleta sana watalii kutoka Japan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa nasema Wizara jamani mpanue wigo. Pia, tumepewa hiki kijitabu sijui kama ni sehemu ya Wizara. Naomba mkisome kina ujumbe mahususi, Tanzania ndicho chanzo cha baraka kwa mataifa mengine. Someni jinsi Tanzania ilivyobarikiwa. Nasema hivi Mheshimiwa Waziri anajua nimekua naisemea hii kwamba katika kupanua wigo wa vivutio vya watalii angalieni vituo vya Hija ile tunaita *faith-based tourism*. Bahati nzuri mimi natoka Mkoa ambao una vivutio hivyo vya Hija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Nyakijoga ambayo iko Mgana Kata ya Bwanja Wilaya ya Missenyi. Kwa kweli ukienda Nyakijoga pengine Kibeo ya Rwanda ambayo inaongelewa kila siku hailingani na hiyo Nyakijoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka huko nyuma kulikuwa na *documentary* iliyoandaliwa ilikuwa inaitwa, "Nipeleleke Nyakijoga." Iliandaliwa na Wanakagera na ilizinduliwa na Hayati Mzee Benjamin Mkapa. Naamini hiyo *film* ipo na Mheshimiwa Waziri mnaweza mkaiongeza ubora wake ikawa ni kuzitangaza hizi sehemu za Hija. Pia, huko Karagwe, Bukene, Minziro; Minziro kuna sehemu ambayo kwa kweli kila mwezi wa Januari panafurika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi *message* yangu kwa Wizara ni kwamba pamoja na kufurika watu wengi kutoka nchi za jirani na humu ndani nchini lakini miundombinu bado. Hamna sehemu ya kulala, watu ma mia na ma mia utakuta wanalala nje. Kwa hiyo, mkiweza kuvitangaza hivi vituo mtapata pia na wawekezaji kuwekeza katika upande vya *accommodation.*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuongelea kuhusu ushiriki; kuna Mbunge mmoja ameongelea ushiriki kuhusisha Sekta Binafsi. Mheshimiwa Angellah Kairuki, kule Bukoba unajua kuna wadau ambao wamekuwa wanajituma kutangaza utalii katika Kanda ya Ziwa. Kuna wakina Rutta William wa Bukoba *tours*, kuna Kiyovele; ndiyo karibu miaka 20 wanatangaza lakini hawapati *support* ya Wizara au taasisi. Hivyo, wadau hawa wamepanga kutakuwa na wasanii zaidi ya 100 wanatembelea Kagera na sehemu nyingine kama sehemu ya utalii lakini sijui kama mna habari hiyo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba nisisitize kwamba Mkoa wa Kagera ni *hub*. Tukiutumia vizuri ni Mkoa pekee ambao unapakana na nchi nne kabla hujaenda kwingine. Kwa hiyo, mkiweza kuiuza Kagera *as a hub* na Kanda ya Ziwa mtaona italeta matokeo chanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho niongelee kuhusu Chuo chetu cha Taifa cha Utalii kwamba kiimarishwe imesemwa sana. Nisisitize tu kwamba muwezeshe hiki Chuo cha Utalii kuanzisha ushirikiano na vyuo vya utalii vya Mataifa mengine yaliyopiga hatua. Najua mnafungua vyuo hivyo katika kanda Temeke, Tandika lakini mwende nje pia kuweza kupata katika ku-*train* watu wetu hasa katika *customer care* mnahitaji *input* ya vyuo vya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mwishoni niseme kuhusu lugha. Katika *tour guides* ukienda katika nchi yeyote umekuwa unazunguka na juzi nilikuona wakati unatembelea Kanisa lile maarufu kule Cairo ulivyofika umeona kwamba hiki kituo ni kituo cha imani na ni kituo cha utalii lakini kuhusu lugha nadhani kuna mtu umemsikia anaongea Kiswahili pale. Kwa hiyo, mimi nasema mjitahidi kwa vile tuwe tunahamasisha

nchi nyingi muweze kufundisha lugha mbalimbali. Akija Mchina mtalii akisikia *guide* anaongea Kichina 'Haaa' mtaona wengi tu. Kwa hiyo, mimi naomba muweke msisitizo katika kutumia hizo lugha simulizi kwa wageni kwa kutumia lugha hizo za fasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama sijasikia kengele, niseme kuhusu *retention*. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wa kuruhusu taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili kuwa na *retention* ya fedha wanazozalisha. Hatua hii itawezesha taasisi hizi kuboresha huduma zao na kutatua changamoto ambazo nimezitaja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imeishagonga.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema yote hayo naomba kuunga mkono hoja na kumpongeza wifi yetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Professor* Patrick Alois Ndakidemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa. Nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya. Mimi mchango wangu leo jioni hii utahusiana na Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro ni zawadi kubwa ambayo Mungu ametupa sisi Watanzania. Ni mlima mrefu kuliko yote Barani Afrika na mlima ambao katika vilele saba ambavyo vinafikika kwa urahisi Duniani, cha kwetu ni cha nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wataalamu wanasema kwamba Mlima Kilimanjaro ndiyo mlima mrahisi kupanda kuliko milima yote. Kwa mantiki hiyo tukitumia vizuri uwepo wa mlima huu tutaliongezea Taifa letu kipato cha kutosha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mlima Kilimanjaro una vitu vingi. Kuna *Kilimanjaro National Park* (Mbuga ya Wanyama) ambapo kuna wanyama wa kila aina kama vile ndege na vitu vingine. Kuna ndege kama 750 ambao wako pale Kilimanjaro, tuna Ziwa Chala ambalo liko ndani ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, tuna maporomoko ya maji ya *Materuni Water Falls,* maporomoko ya Marangu *Water Falls,* tuna mti mrefu kuliko miti yote barani Afrika ambao una meita 81.5, uko katika kijiji cha Tema kata ya Mbokomu na kuna *Kikuletwa hot springs*, watu wakitoka kupanda milima kule wanaenda Kikuletwa wanaoga basi mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na umaarufu wa mlima huu bado tuna changamoto kubwa kwenye mlima wetu. Barabara zinazopeleka watu kwenda kwenye maeneo haya ambapo ni watalii wanatembelea mlima wetu kwa mfano Barabara ya Umbwe – Geti, lako la kupitia Umbwe kwenda mlimani nimeishalia sana hapa Bungeni kwamba ni mbovu. Mtalii akienda, akirudi hatamwambia mwenzake apitie ile barabara kwa sababu ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kibororoni – Suduni mpaka Kidia tunaishukuru Serikali inajenga lakini tunaomba waongeze *speed* kwa sababu itakuwa inapeleka watu maarufu Mlimani Kilimanjaro. Barabara ya kwenda Materuni *Water Falls* ni mbaya na bado ujenzi wake unasuasua unakwenda pole pole sana. Kwenye huu mti mrefu ambapo ni nembo kubwa hakuna barabara nzuri kabisa na miundombinu pale siyo mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kuhusiana na barabra vijiji vyote karibia vyote vya Wilaya ya Siha, Hai, Vunjo, Rombo na mimi Moshi Vijijini vinavyopakana na ule mlima barabara siyo nzuri sana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ushauri wangu sasa. Najua kwenye *corporate social responsibility* kuna pesa ambayo inatoka, kama *TANROADS* au *TARURA* wameshindwa kutusaidia kutengeneza zile barabara na tunapata kipato kikubwa kutoka kwenye huu mlima; kwa nini zile pesa za *corporate social responsibility* zisitumike kutengeneza hizi barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ni lami tungekuwa tumeishamaliza siku nyingi sana badala kupeleka pesa mahali pengine ambapo hazirudi pale mlimani. Kwa hiyo, tunaomba pesa zirudi pale zitengeneze hizi barabara ili tuweze kunufaika na milima wetu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili kule Kilimanjaro ni idadi ndogo ya watalii wanaotembelea Mlima Kilimanjaro. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu na ile *film* yake ya *Royal Tour,* alihamasisha na watalii wameongezeka. Sasa wameshaanza kuongezeka; mwaka 2020/2021 watalii walikuwa 12,000 lakini mpaka Aprili mwaka huu watalii walikuwa wamefikia 53,000 kutokana ile *film* ya Mheshimiwa Rais, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kilimanjaro niwaambie ina uwezo mkubwa sana wa kutuingizia kipato cha kutosha na hawa watalii 53,000 ambao walikuja waliingizia Serikali shilingi bilioni 84. Sasa Mlima Kilimanjaro una uwezo wa kupokea watalii kati ya 200 mpaka 300 kwa mwaka lakini hapa unaona *the highest number* ambayo tumerekodi ni hii 53,000 ambayo imetokea baada ya Mheshimiwa Rais kutufanyia hii *film* ya *Royal Tour*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mapato haya hayaendani kabisa na hadhi kubwa ya Mlima Kilimanjaro. Mimi niishauri Serikali, tunachotaka ni kupeleka watalii kwa wingi waende pale Kilimanjaro na tupate pesa. Naomba niishauri Serikali irudi nyuma. Kuna suala zuri sana lilikuwa limeanzishwa la kutumia kiberenge kupeleka watalii kule Mlimani Kilimanjaro, lilikuwa ni wazo zuri lakini kwa sababu huwa kuna watu wanatuambia usifanye hiki kwa sababu zao Serikali ikasitisha ule utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano tulikuwa na Ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere la Kufua Umeme, walitupigia kelele acheni acheni. Hawakuwa na nia nzuri lakini tumejenga tunaona sasa hivi tunapata umeme. Tumeona hata Reli ya *TAZARA* walikuwa wanatunyima tusiijenge, lakini tukaamua tukawa na viongozi wakamua tukajenga reli yetu ya *TAZARA* mambo yanakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Serengeti walikuwa wanatunyima tusijenge barabara kupita pale. Sasa mimi sidhani kama kuna uharibifu wa mazingira kiasi hicho kwamba tutauharibu mlima. Ni kipande cha mita 10 tu kwenda mapaka pale mlimani mpaka juu kule ukilinganisha na eneo lote ambalo Kilimanjaro inayo. Mimi niwaombe ile *idea* ya ku-*introduce* kiberenge pale Kilimanjaro irudi, mwende mkakae na wadau…

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Manyanya.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilikuwa na muunga mkono kwamba kuweka kiberenge ni utaratibu ambao hautakuwa wa kwanza Tanzania. Nilivyoenda China, kutembelea kule *Great Wall,* juu kabisa kule watu wanaenda na kiberenge, wanaoamua wanaenda na miguu. Pia, siku za mwisho mwezi wa nane nilienda Israel kwenye Mlima wa Majaribu *(Temptation Mountain),* watu wanaenda na kiberenge kwa sababu kwenda kwa miguu ni shida lakini watu wanalipa hela na wanaenda. Kwa hiyo ni wazo zuri kabisa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nimefurahi nikaongea hata kabla hujaniruhusu. Nimeipokea kwa mikono miwili ahsante sana *Engineer* Manyanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiberenge kitatusaidia. Kuna watu wenye ulemavu wangependa sana wafike mahali nao wafurahie uwepo wa mlima wao, kuna wazee ambao hawataweza kwenda pale, kuna watu wengine wana pesa lakini *sporting* ya kupanda milima siyo *hobby* yao. Wao wanataka wapelekwe na kiberenge waangalie warudi. Kwa hiyo, tukifanya hivyo tutakuwa tumetenda haki. Kwa

sababu hata kwenye jengo la kuingia hapa Bungeni kuna maeneo maalum ya kuwasaidia watu wenye ulemavu na sisi tuwajali hawa wenzetu ili tuwapatie fursa nao waweze kuupanda ule mlima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme huu ni mradi wenye manufaa kwa Taifa letu tusiwasikilize eti watu wanasema hivi hapana. Serikali irudi kama ni mwekezaji tuwekeze sisi wenyewe ile mali ni yetu tuwekeze pale siyo…

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Inatokea wapi? Ahaaa! Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hussein Amar.

**TAARIFA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli hata mimi naunga mkono hilo suala la kiberenge ama viberenge kwa sababu hata sisi wenye uzito mkubwa ambao hatuwezi kutembea tutafanya utalii kwa kutumia hicho kiberenge, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili, nashukuru sana kaka yangu. Kwa hiyo, tufanye maamuzi wenyewe Wizara ikae chini tusiwape watu wengine kama ni wawekezaji wawe wawekezaji wa kwetu watoto wa nyumbani hapa. Tuweke kiberenge pale basi maisha yaendelee. Ninahakika kipato kitaongezeka na tutakuwa tumetendea haki ule Mlima Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu ajiandae.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema kwa kunifikisha muda kama huu na kusimama katika Bunge hili kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa sana ambayo anayofanya katika Sekta hii ya Utalii ambayo imekuwa na malalamiko mengi sana na wananchi wengi sana kupoteza maisha pamoja na wengine pia kupoteza mali zao kwa maana ya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze mimi huyu ni mwanangu ananiita mama mdogo ambaye ni mwanangu Mheshimiwa Angellah Kairuki. Huyu mama mwenzangu aliyetoka kuongea amesema ni ndugu yake mimi mwanangu mama yake ni dada yangu. Kwa hiyo, nimpongeze sana kwa kazi nzuri ambayo anafanya lakini nimpongeze Naibu Waziri Mheshimiwa Kitandula, nipongeze na viongozi wote katika hii Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi zangu mimi nitajikita katika maeneo mawili. Maeneo ya utalii hasa katika wanyama, tembo na misitu. Nimesimama mara nyingi sana katika Bunge lako hili nikiongelea hasa masuala ya tembo. Leo nasimama mbele ya Bunge hili kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa sana anayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu Wabunge, Mheshimiwa Rais halali, Watanzania, Mheshimiwa Rais halali. Mheshimiwa Rais anasikiliza jinsi wananchi wanavyolalamika kuhusu tembo na usiku mzima anakaa akiwaza nini afanye ili kutatua tatizo hili? Leo hii tumeona teknolojia mpya ya kuwafukuza tembo kwa mabomu ya baridi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia unaona jinsi gani watu wanajali nini cha kufanya ili kutatua tatizo hili? Siyo hili tu, wamekuwa na teknolojia nyingine ya kuhakikisha kwamba wanaweza kufanya

utaratibu wa kuwafuatilia tembo wapo wapi? Wamefungwa tembo 35 ambao ni viongozi kufuatilia makundi ya tembo. Hii yote ni jinsi gani unaangalia Wizara hii inajali. Nikupongeze sana Mheshimiwa Rais na nimpongeze sana Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, taarifa imeeleza kwamba…, samahani nimekuita Rais, nisamehe katika hilo ila sijakosea sana kwa sababu na wewe pia ni Rais wa Mabunge ya Dunia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na mchango wangu, kwanza niipongeze sana Wizara hii ya Maliasili na Utalii, ni Wizara ambayo kwa kweli ni nyeti. Wizara hii inafanya kazi usiku na mchana, lakini ninayo machache ya kuzungumza; teknolojia hizi ambazo mmezitumia kipindi hiki tukumbuke tembo ni mnyama ambaye ana akili sana, ni mnyama anajifunza na anajaribu kuangalia na anatengeneza mazingira ya kusoma. Kwa hiyo, tuangalie ni kwa nini tembo walikuja wakaingia mpaka kwenye makazi ya watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tembo mpaka kufika kwenye makazi ya watu ilikuwa ni kutafuta maji, kukosekana kwa maji katika meneo ya hifadhi ndiyo husababisha tembo kuharibu migomba ambayo ina maji, miwa, mpunga na sehemu zingine kama kule Mwanga tembo aliweza kula wali, kwa kuingiza mkonga wake kwenye nyumba za miti anakuta sufuria la wali anakula, kwa sababu amekosa maji kwenye hifadhi. Niiombe Wizara sasa hivi mhakikishe mnachimba mabwawa mengi maeneo ya hifadhi ili wale tembo wasije tena katika maeneo ambayo wananchi wanaishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea kuhusu tembo nitaongelea kuhusu misitu *TFS* (Wakala wa Misitu), Tanzania tuna misitu mingi sana uki-*google* utaona katika Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Same kuna Msitu wa Shengena ambao una miti 17 yenye uwezo wa kutibu ugonjwa wa *cancer*. Lakini ukiangalia utaona Same ni Wilaya ambayo inaongoza kwa *cancer,* miti hii ni ya asili ambayo watu hawajui thamani yake. Unakuta wengine wanaingia wanaukuta upo ndani ya msitu, wanakata kwa sababu hawajui thamani yake. Lakini

miti hii haipo tu Shengena, ipo katika Maporomoko ya Mlima Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miti hii pia inapatikana Rukwa, nini cha kufanya? Tunatambua *cancer* ni ugonjwa hatari sana nchini na haujapata tiba, hivyo ili tusaidie Watanzania niiombe Wizara kupitia maliasili wahakikishe wanafanya tafiti za kugundua miti hii ilipo na kuiotesha kwa wingi na kuendelea kuangalia misitu ambayo miti hii itastawi, ili tuweze kuiotesha kwa wingi liwe kama zao la biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Nchi ya Canada na Ujerumani kuna viwanda vinavyotengeneza dawa asilia, hivyo basi, kama Serikali kupitia misitu yetu tutaboresha miti hiyo kwa kuiotesha kwa wingi na kahamasisha wananchi kuiotesha kwa wingi na kuwa chanzo cha mapato kwa Taifa letu na tutapata fedha za kingeni.

Mheshimiwa Spika, pia badala ya kuuza nje tutahakikisha tunajenga viwanda vyetu nchini, tutawaita Wataalam wa Ujerumani na India waje kutufundisha jinsi ya kutengeneza dawa ya *cancer*. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeongeza Mapato ya Taifa letu na mwananchi mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi sina mengi zaidi, naunga mkono hoja. Watanzania tumpeni Mheshimiwa Rais maua yake halali kwa ajili ya Taifa hili la Tanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, atafutiwa na Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Hotuba ya Maliasili na Utalii, bajeti inayotaka bilioni 348.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuchangia Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kusikia kilio chetu Wabunge wa Kanda ya Ziwa (Shinyanga, Geita na Tabora), tumekuwa na kilio siku nyingi kuhusiana na hili Pori la Kigosi. Nikushukuru sana Waziri nimeona kwa mkono wako umesaini Tangazo la Serikali Na. 345 la tarehe 3 Mei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kutumia fursa hii kuwaambia wananchi walio kandokando na Pori la Kigosi linaenda kufunguliwa tarehe 3 Julai, 2024. Sasa niiombe Wizara ikatoe elimu kwenye hili pori kwa sababu limetoka kwenye pori kubwa limeenda *TFS,* nafahamu kuna sheria zake. Hivyo sasa, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri ni kazi kwenu kufanya haraka wananchi wetu wapewe elimu ili waendelee kulitumia hili pori kwa matumizi ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuwa hili Pori la Kigosi, limeniathiri pakubwa sana kwenye Wilaya ya Mbogwe ambayo ipo Kata ya Iponya, Kijiji cha Sango. Ukiangalia kulikuwa na mvutano mkubwa sana na watu hawa wa wanyamapori, lakini kwa sasa hivi kwa sababu limeshuka Wakala wa Misitu *(TFS),* Waziri nikuombe sana twende tukatoe elimu, ili watu waweze kufanya shughuli za uhifadhi wa nyuki, kilimo pamoja na mambo mengine yanayoruhusiwa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ipo Kata ya Bukandwe tokea mwaka 2021 nilikuwa naisemea kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ukurasa wa 52, tulifanya kampeni kwa maelekezo ya Chama Cha Mapinduzi kilichotuweka madarakani kwamba, tuinadi sera tutatenga heka zaidi ya 6,000 ili kusudi watu waende wakapate maeneo ya kuchangia pamoja na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kilio kikubwa sana kutokana na hili pori kwa Kata ya Masumbwe, Kijiji cha Mdoda, Mnanda Isebya, Nyashinge huko, Kijijiji cha Ilolanguru na Kanagwa. Kwa hiyo, nikuombe Waziri tutakapomaliza shughuli hizi za kupitisha bajeti zako tushirikiane kwa pamoja kwenda kutoa elimu kwa wananchi nini

kinatakiwa kufanywa, ili watu waweze kufanya kazi zao nyingine za *TFS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo yote haya niliyoyataja ya jimboni nitumie nafasi hii kuishauri Serikali…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, namuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa kusaini hiyo *GN* ya Kigosi, lakini yapo maeneo kama hayo katika Wilaya ya Sengerema kuna sehemu inaitwa Mchangani pia kuna sehemu nyingine Maswa *Game Reserve* kule.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam unagundua huzungumzi na Waziri unampa taarifa Mbunge mwenzio yule pale Mheshimiwa Maganga.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa Mheshimiwa Maganga kwamba, kuna maeneo hayo ya Maswa *Game Reserve,* pia kuna Manyoni, maeneo ya Itigi pia tunataka Mheshimiwa Waziri ayaangalie hayo yote yafunguliwe watu waendelee na shughuli zao, kama walivyofanya watu wa Masumve Mbogwe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, naipokea ila naomba nilindie muda ikiwezekana uniongezee kidogo kwa sababu nina ajenda…

**SPIKA:** Hapana, muda wako kautumia Mheshimiwa Tabasam kwa hiyo, mtamalizana baadaye. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba niishauri hii Wizara kwenye suala la mkaa; ninafahamu Mpango wa Serikali kulingana na shughuli za mkaa tunasema kwamba, tunaharibu mazingira pamoja na mambo mengine. Mheshimiwa Waziri mimi ningependa niwe muwazi watu wetu bado masikini, wengi tunaishi kwa maisha ya chini, kwa kuwa, umeaminiwa umekuwa Waziri dada yangu uwe na huruma ya wakinamama kwa sababu nyie mna huruma kubwa sana. Ningeomba, ikiwezekana mkabadilishe kanuni, kwa sababu watu hawa wanakabiliwa na changamoto kubwa ya kupigwa sana na mgambo wanaouza mkaa, lakini ukijakufuatilia wanafuata taratibu zote za kisheria wengine wanakata mpaka vibali.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha askari baadhi walioko barabarani hawajasomea haya mafunzo. Naomba niungane na kamati kabisa kwamba, bajeti inayoongezeka waende wakaajiriwe watu ili wawe na uchungu wakati mwingine kuumiza watu. Unakuta mtu ana kibali lakini kabla hajakamatwa anapata kipigo cha kufa mtu, matokeo yake baadaye wanagundua alikuwa na kibali, kisheria lakini ameshaumizwa mguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, fedha zinazoongezeka hapa kwenye hii bajeti wajiriwe askari ambao watapewa semina, jinsi ya kukamata watuhumiwa kwa kuzingatia haki za binadamu pamoja na mambo mengine ya kiusawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo suala lingine la upandaji miti, naomba nizungumze mbele ya Wabunge wenzangu; naona kama kumekuwa na maagizo wakati wa kupanda miti, inapandwa miti mingi lakini jinsi inavyopandwa hiyo miti naona tunaharibu pesa za walipa kodi. Maana wakati mwingine hiyo miti haikui, inaharibika na watu wametengeneza *clip*, wamepiga picha tumepanda miti na wamelipana posho. Hili suala nikuombe Mheshimiwa Waziri mliangalie kusudi ikiwezekana watu wa namna hiyo wanaoharibu kodi za wananchi halafu hawaisimamii vizuri miti, waweze kushughulikiwa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine, Mheshimiwa Waziri nizungumzie suala la Kanuni za Maliasili, sizifahamu zote lakini ni vyema ukazipita upya dada yangu ili kusudi ziwe rafiki. Ninashukuru sana kwa kutengeneza mabomu ya kufukuza tembo kwa binadamu; kama inawezekana kutengeneza mabomu ya kufukuza tembo, kwa nini zisitengenezwe bunduki nyingine za kutisha zisizoua wakati mtu anapita tu kwenye hifadhi anatishiwa, kuliko kulenga kupiga shaba za moto, kuua kwamba huyu ni jangili. Wakati mwingine wengi wanakutwa siyo majangili, ni mtu anapita kwa bahati mbaya hajui kwamba hii ni hifadhi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nitatolea mfano kwenye wilaya yangu, kuna geti la maliasili, lakini upande wa pili ni hifadhi na upande wa huku ni hifadhi, barabara kuu imepita katikati ya hifadhi. *(Makofi)*

*Kwa hiyo, ukimkuta mgambo amevuta bangi vizuri, hajali watu anasimamia sheria, ana-shoot watu anaumiza watu.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na Wizara yako hilo suala mliangalie upya, binadamu wengi wanaumia sana na maisha haya kiukweli hatulingani. Ni kweli tunajua Serikali ina mpango wa kuwezesha gesi sijui na nini, lakini kabla hamjapata vizuri majibu ya kuwapunguzia wananchi gesi asilia za kupunguza matumizi ya nishati, ni vyema sasa tukajua kabisa tuna watu ambao wanatumia mkaa wa kuokota na miti ya kuokota wanaishi na maisha yanaenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ushauri wangu ni huo, uziangalie upya kanuni, pia wakimbize wale wanaokuharibia Wizara yako, ukachukue hatua mapema ikiwezekana kuwafukuza kazi.

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono Hoja ya Mheshimiwa Luhaga Mpina kwamba, tuwafukuze Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na mwenzake msaidizi na sekta nzima. Mimi naomba mkafanye uchunguzi vizuri kwa sababu wabovu wanaowaharibia sekta wamo na wanafahamika. Kwa hiyo, ifanye tathmini na kuangalia upya wale

ambao hawaendani na Serikali na matakwa ya Mheshimiwa Rais waweze kusimamishwa ikiwezekana wafungwe kwa sababu wameumiza watu wengi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Maganga wakati ukichangia hapa ulisema kwamba, mgambo anakuwa amevuta *bangi* na kwa sababu hilo ni kosa kisheria hebu futa hayo maneno ya mgambo kuvuta *bangi*.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** *Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na kufuta lakini ni kweli kwamba mwaka 2021 tulikamata mgambo walikuwa 10 na walikuwa wameshaumiza mwananchi mmoja, tulikuta kweli wamevuta bangi na mpaka sasa hivi wamehukumiwa kufungwa*. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana lakini nafuta hiyo kauli. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, futa vizuri hayo maneno. *(Kicheko)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, basi maneno ya bangi nafuta, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka ajiandae.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Suluhu Hassan kwa kufanya vizuri sana katika sekta hii na ameongeza idadi kubwa ya utalii na hatimaye kuongeza pato kubwa kupitia utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nipende kutoa pole kwa wananchi wangu ambao wameuawa na tembo miezi miwili, mitatu iliyopita. Tarehe 23 Machi, 2024, aliuawa ndugu mmoja anaitwa Shaibu Abdallah Manokwe, ambaye alikuwa anaishi kwenye Kijiji cha Namakambale katika Kitongoji cha Nalupala, aliuawa na tembo. Lakini kama haitoshi tarehe 21 Mei, 2024, (tunazungumzia juzi tu) ndugu yetu Omary Abdallah Rashid aliuawa na tembo katika Kijiji cha Mbungulaji, Kata ya Kalulu. Kwa hiyo, utaona ni namna gani sisi Tunduru tulivyokuwa na changamoto kubwa ya tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niiombe Serikali kupitia Wizara kuweza kuweka mikakati Madhubuti, ili kusaidia hii changamoto isiwe kubwa:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza sisi kwenye wilaya yetu tuna eneo kubwa sana kwa maana ya kuwa na hekta za mraba 18,778; pia miundombinu siyo mizuri ya barabara na pia tunayo idadi ndogo sana ya Askari wa Wanyamapori. Tunao askari watano tu lakini mahitaji ya askari ni 20 na tunapungukiwa askari 15, hata hao 20 bado ni wachache. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kuishauri Serikali waongeze idadi ya askari, ili waweze kusaidia changamoto ile ya wanyama wakali wanapotokea kwenda kwenye makazi ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Wizara, tumeona kuna mpango wa kwenda kutoa mafunzo ya Askari wa Vijiji *(VGS)*. Huu mpango ni mzuri na ni jambo jema sana, tunaupongeza lakini tunayo maswali mawili machache kwa maana ya kwamba, kwenye vile vijiji vyetu tayari wapo askari wengine wa *VGS* ambao tayari walipata mafunzo lakini hawakuajiriwa na hatujawatumia mpaka hivi sasa. Je, sasa tunakwenda kutoa mafunzo kwa *VGS* wengine? Tafsiri yake ni nini? Mwisho wake ni nini? Wakishapata mafunzo je, wataajiriwa au watawekwa ili waweze kulipwa angalau kwa mikataba mifupi

waweze kusaidia pale tembo wanapotokea kwa haraka kabla askari wale wa *TANAPA na* wengine wanapokuja kurudisha, wawe wameshasaidia, kabla ya watu kutoka mbali na kuwafikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu Waziri atakapokuja ku-*wind up* hapa atueleze huu mpango wa *VGS* mwisho wake ni nini? Kwa sababu tayari tunao *VGS* wengine hawajaajiriwa na wamekaa tu hatuwafanyii kazi na tunakwenda kutoa mafunzo kwa wengine. Naomba kujua tutakapotoa mafunzo kwa hawa je, wale waliopata mafunzo na hawa watakaokwenda kufundishwa mwisho wake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika hili kama watatoa mafunzo kwa hao Askari wa *VGS* kwanza waanze kuchukuliwa wale ambao walipata mafunzo kwa muda mrefu na wapo vijijini; lakini la pili, wale watakaokwenda kufundishwa sasa hatimaye wapewe mkataba waajiriwe kwa mkataba wa muda mfupi, ili waweze kukaa kwenye vile vijiji kwa sababu *VGS* wanaitwa ni Askari wa Vijijini. Maana yake wapo kwenye vilevile vijiji ambavyo wananchi wetu wanaopata athari ya tembo wanaishi kwenye vile vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiwatumia hawa maana yake ni tembo watakapotokea na wao kwa haraka zaidi watakwenda kusaidia kabla askari hawajatoka mbali na madhara yakawa makubwa sana. Katika hili Mheshimiwa Waziri naomba uliwekee mkazo kweli kweli kwa sababu hili litakwenda kusaidia kupunguza hata gharama kubwa ya kwenda kulipa kifuta jasho na kifuta machozi. Kwa sababu tumeona mwaka jana sisi tulitumia zaidi ya bilioni 8, mwaka huu tumeona mmetenga zaidi ya bilioni 7, lakini tukiwalipa hawa askari wetu kwa posho ndogo ndogo hatuwezi kufikia kwenye bilioni 7 au 6 ambapo wanaweza kwenda kuokoa mazao yasiliwe kwa wingi na hatimaye kuokoa maisha ya wanadamu ambao wanapoteza maisha yao kuuwawa na tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia suala la pili tuna uchache wa vitendea kazi kama nilivyosema ukubwa wa Tunduru ulivyo lakini vitendeakazi ni

vichache sana. Wilaya kama ile kuwa na gari moja halafu na miundombinu ya barabara si mizuri siyo jambo sahihi sana. Kwa hiyo, niombe sana katika hili tuongezewe vitendeakazi kwa maana ya magari, tuongezewe bunduki kwani bunduki tulizonazo kule ambazo wanazozitumia ndugu zetu wale ni za zamani sana, kiasi kwamba wengine wakienda porini zinashindwa hata kufanya kazi kutokana na kuzeeka kwa zile bunduki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili. Wanatumia gharama kubwa kwa sababu, risasi wanazotumia kwa bunduki zile zina bei ghali na badala yake tuwapelekee bunduki za kisasa ambazo hata risasi zake ni za bei rahisi, ili waweze kurahisha kufanya kazi yao na kuwasaidia wanchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kifuta jasho na kifuta machozi, tunaishukuru sana Serikali na tunaipongeza Wizara. Hivi ninavyosema siku nne, tano, sita zilizopita kwenye Wilaya yangu ama kwenye jimbo langu tayari wananchi kule wamekuwa wanalipwa kifuta jasho na kifuta machozi, lakini katika hili ninaomba sana tena sana kwa sababu, waliokwenda kulipa kule ni watu ambao wametoka Wizarani, lakini wamekwenda kule wamepewa siku nne tu za kuweza kukamilisha malipo hayo na waweze kurudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa utaona kwa ukubwa wa Wilaya ile kuwapa watu siku nne wawe wamelipa kwenye vijiji vyote, hii imeleta adha kubwa kwenye jimbo langu kwa sababu, nimekuwa napokea simu mara kwa mara. Wengine wanalalamika kwamba, tunaambiwa twende tukapokelee Makao Makuu ya Kata. Mtu anatembea kilometa 20, kilomita 15 kufuata Makao Makuu ya Kata kwenda kufuata malipo yake ambapo sasa si sahihi na wengine wanashindwa kutoka eneo moja kwenda eneo lingine kufuata yale amalipo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba katika hili sasa Mheshimiwa Waziri, kama kuna uwezekano watu wale warudi tena waongezewe siku. Waende wakawalipe wengine ambao hawajalipwa ambao walikuwa

wanastahili kulipwa kwa sababu ya uchache wa siku walizopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, ninaomba nizungumzie suala la *WMA*. *WMA* ni hifadhi zinazosimamiwa na wanavijiji wenyewe. Pale nyuma walikuwa wanasimamia hifadhi zile, walikuwa wanapata pesa na hatimaye pesa zile zilikuwa zinasaidia kwenye vijiji husika kwa sababu, walikuwa wakipata zile pesa wanakwenda kusaidia kujenga zahanati, wanakwenda kusaidia kujenga matundu ya vyoo shuleni na wanakwenda kusaidia huduma muhimu za kijiji husika. Kwa hiyo, ilikuwa inatija kubwa sana, lakini baadaye pesa zile zilikuwa zinaondolewa na kwenda Hazina kwanza, halafu ndio wapangiwe asilimia yao irudishwe kule kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana imekuwa sasa toka zimeanza kwenda hazina, zile pesa zimekuwa hazirudi tena kwenye *WMA*. Kwa maana hiyo sasa, tunakwenda kuvunja moyo wa wananchi wale kutunza zile hifadhi zao za *WMA* na badala yake wanaona kwamba, haina tija kwa sababu, wanatunza kwa nguvu zao, kwa mali zao, lakini wakati mwingine wanapoteza muda wao na hakuna wananchokipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika hili. Ninaomba sasa kama kuna pesa ambazo zinapaswa kutoka Hazina kwenda *WMA* zirudishwe, kwa zile ambazo zilitolewa bila kupelekwa kule. Kwanza zipelekwe zile ambazo *WMA* wanadai, lakini la pili, kutengenezwe mfumo uleule kama wa zamani wa kwamba, pesa zile za *WMA* ziwasaidie wananchi wenyewe ambao wanatunza maeneo yale ya hifadhi, kama ilivyo kwa *TANAPA* na maeneo mengine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka. Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Mheshimiwa Waziri, tunaomba unapokuja kwenye hitimisho utuambie *TAWA,* Wilaya ya Nkansi, ni lini watapata gari nililoomba toka mwaka jana?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni suala la kifuta jasho na kifuta machozi. Jina lenyewe halifai, inaonekana kama ni *favor* kuwalipa Watanzania. Kwa hiyo, mimi ninaona kwamba, jina lenyewe haliakisi. Pamoja na kwamba, fidia na yenyewe siyo jina zuri, lakini ni bora fidia itaendana. Kwamba, wawalipe kulingana na kile walichopoteza, tofauti na hivi ambavyo ipo, inaitwa kifuta jasho na kifuta machozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna namna mnaweza kufuta machozi ya binadamu aliyepotea, halafu tunamlipa shilingi milioni moja mpaka shilingi milioni mbili. Kwa hiyo, jina lenyewe tu halifai, inaonekana tu kama ni *favor*. Mimi ninashauri tubadilishe jina hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili. Kanuni za Mwaka 2011, nimekuwa ninazungumza mara kadhaa na leo ninakwenda kushauri. Tumeona kuna mabadiliko kidogo, mulikuwa mnalipa eka moja shilingi 25,000 kutoka eneo la hifadhi kwa maana ya kilometa moja. Shilingi 25,000 kwa ekari, maandalizi ya eka moja ni sawa na shilingi 850,000. Kwa hiyo, mnaweza mkaona ni namna gani tunawadhulumu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamefanya marekebisho kutoka shilingi 25,000 sasa hivi wanazungumza shilingi 37,500. Ninaomba nizungumze kwa maumivu makali sana, Wizara hii inachangia kuwapa umasikini Watanzania. Haiwezekani na mimi ninatamani leo niwape shilingi 37,500 mkaninunulie magunia 30, tuone kama inawezekana. Serikali mnajua wapi mnanunua hayo mahindi kwa bei rahisi. Haiwezekani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo ni lazima tuwasaidie hawa watu, ili kuwasaidia. Hii pesa ambayo mnatenga hata nyongeza siyo suluhisho. Suluhisho ni kuhakikisha wanazuia wale wanyama wabaki kwenye hifdhi, hilo ndio suluhisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nishauri, ili nchi yetu isiingie kwenye lawama hii ambayo inatokea sasa hivi. Tumeshafanya mambo makubwa ni vizuri Serikali ianze kufikiri leo kuweka utaratibu na Sekta Binafsi kuwe na bima za maisha. Wale ndiyo wahusike na kuwalipa hao watu, wakae watengeneze utaratibu mzuri. Leo hata wapeleke iwe laki moja, hawataweza, lawama hizi hazitaisha. Ushauri wangu kwa nia njema ndiyo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wa pili. Nimeona hapa mnazungumzia sijui ndege, sijui mabomu baridi; mnazungumzia matokeo, tayari tembo wameshaenda kuathiri mazao ya watu, wameua watu. Tufikiri kuwazuia wale wanyama kabla hawajatoka kwenye hifadhi kwenda kufanya uhalifu. Hapo tutakuwa tunazungumzia suluhisho la jambo hili, haitawezekana kwa namna yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mipaka hii ya hifadhi pamoja na vijiji na maeneo ya wananchi mengine yaliwekwa kuanzia Mwaka 1948, idadi ya watu inaongezeka, ardhi ni ile ile. Ninashauri, Serikali imekuwa inahubiri hapa ndani, ooh wafugaji wafuge kisasa na sisi tuanze kufikiri kuhifadhi kisasa. Eneo dogo, lakini tuweke wanyama ambao ni wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninajiuliza, kwa nini tunasema mtu akifa, ameuawa na tembo, atalipwa shilingi milioni mbili, lakini tembo akiuawa na binadamu ni shilingi milioni 30? Hakuna dhamana, miaka 30 jela?

Mheshimiwa Spika, mimi ninashauri, ili kuondoa sura hii ya kwamba, nchi yetu haithamini wanyama kuliko binadamu, basi binadamu akiuawa na tembo alipwe mara mbili ya ile fedha ya tembo. Badala ya shilingi milioni 30 alipwe shilingi milioni 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini, gharama ile itatuumiza, tutakuja na mikakati sahihi ya kuzuia wanyama wasiende kuathiri Watanzania. Hii kuweka shilingi milioni mbili ni dharau kwa Watanzania. Kwanza hicho hicho kiwango mlichopanga hakiendi na hata kikienda kinaenda kwa kuchelewa, halafu bado eti unaita kifuta machozi. Utamfuta machozi ndugu yangu kwa shilingi milioni mbili? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mpango madhubuti wa hii Wizara, kwa ushauri mwema kabisa, kuna mambo mawili; tuzuie tembo wasitoke na kama wanapenda viazi, mpunga na mahindi, limeni mazao ya Serikali kwa sababu, tembo ni wa Serikali. Wale mazao ya Serikali, siyo kwenda kula mazao ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ndiyo hilo, wekeni utaratibu maalamu, kuwe na utaratibu wa Bima. Zile Sekta Binafsi ndiyo zihusike na hayo mambo na hilo ndiyo litakuwa suluhisho la hii migogoro wakati tunazungumza kuhusu maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani leo, toka mwaka 1948 watu walikuwa wangapi? Leo idadi ya watu imeongezeka, hii hifadhi tunaihifadhi, kwa ajili ya nani?

Mheshimiwa Spika, tunahifadhi, kwa ajili ya Watanzania. Kama ndivyo, maeneo ambayo kwa sasa hayana sababu ya kuwa hifadhi, wapeni Watanzania waendelee na masuala ya uzalishaji kuliko ambavyo iko sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni leo tunasema eti tumewapa wananchi mafunzo, eti wapige vuvuzela ndiyo wazuie tembo. Hawa tembo hata vuvuzela hawasikii kwa sababu, wameshazoea, hizo vuvuzela wanazisikia mpaka uwanjani. Sisi tunasema eti kwamba, wananchi wamevamia, hawajavamia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tembo sasa hivi wanaingia mpaka kwenye nyumba za watu. Kwa hiyo, ni lazima Serikali kuondoa hilo doa la

kwamba, inathamini wanyama kuliko binadamu. Walipwe mara mbili ya gharama ya tembo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula. Mtoa hoja ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha tena kurudi kwenye Bunge hili, baada ya zahama za Ijumaa Kuu ya Tarehe 29 ya Mwezi Machi ya risasi hizo za *AK147*. Hakika Bwana akiwa upande wako hakuna atakayekuwa juu yako. Ndicho ninachoweza kusema nikishumkuru Mungu wangu aliye hai. Siwezi kuendelea kusema zaidi juu ya hilo, ninaviachia Vyombo viendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninakushukuru wewe kwa mambo makubwa mawili, kwanza kwa kuniona na kunipa nafasi ya kusema, lakini pili kwa kunifariji wakati nilipopata zahama hizi. Pia, ninamshukuru Waziri Mkuu wa nchi yetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa pamoja na Naibu Waziri Mkuu kwa kunipa faraja siku ile ile baada ya kitendo kile cha kinyama kilichonitokea. Kupitia kwao ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu, vyombo vyake vya usalama vilinisaidia pia, kunipa ushirikiano mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba, nikiendelea kusema bila kufikisha shukrani zangu za dhati za Wana-Simanjiro kwa, Mheshimiwa Dkt. Samia, Rais wetu mpendwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wana-Simanjiro wataniuliza maswali mengi. Kazi aliyoifanya kwa muda huu mfupi wa uongozi wake haiwezi kulinganishwa na kipindi chochote katika historia ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Simanjiro leo wana faraja kubwa kutokana na kazi aliyofanya Rais katika Sekta ya Maji, Sekta ya Afya na katika Sekta ya Umeme. Tumepata miradi mikubwa ya kihistoria ambayo wafugaji wa Simanjiro na wakulima hawana

chaguo jingine Mwaka 2025 isipokuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais huyu hana wa kufananishwa naye katika Uchaguzi wa mwaka 2025, ndani ya chama wala nje ya chama. Tumuombee afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye hoja iliyoko mbele yetu kwa kuanza kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Kairuki, na Naibu Waziri kwa taarifa yao waliyoiwasilisha pamoja na Mwenyekiti. Pia ninawapongeza Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya *Comrade* Mheshimiwa Mnzava. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko jambo ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi sana hapa, nalo ni wimbi la wanyama kutoka katika maeneo yaliyohifadhiwa kuingia katika ardhi ya vijiji na kuleta athari kubwa sana kwa wananchi. Ni vizuri Wizara ya Maliasili na Utalii ikafanya utafiti na kueleza bayana ni nini kimesababisha wanyama katika miaka hii michache kuondoka katika maeneo yaliyohifadhiwa na kuhamia katika maeneo ya wananchi. Je, ni mimea vamizi? Je, wanyama wameongozeka sana? Tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Spika, wanyama wanaondoka ndani ya hifadhi. Ninaujua ukweli mmoja niliofanya utafiti, leo tembo hawawezi kukaa Tarangire kwa muda wa kutosha kwa sababu, malisho yao hayapo. Sasa wanyama wakishatoka nje ya hifadhi namna bora ya kuendeleza uhifadhi nje ya hifadhi, na huu ndiyo ushauri wangu leo, ni kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kukubali kwamba, wanyama wale wamekwenda katika maeneo ambayo hayakuhifadhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni maeneo ambayo ni ardhi za vijiji, lakini hukohuko kuna vitalu vya uwindaji, upigaji picha na shughuli za utalii katika maeneo ya vijiji. Sasa, umefika wakati ni lazima Wizara ikubali kugawana, Serikali ikubali kugawana mapato na vijiji kutokana na wananyama ambao wana shughuli za utalii zinazofanywa nje ya hifadhi na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, ukifanya hivyo, wananchi watapunguza makali ya athari za wanyama hawa kutokana na fedha hizo na nchi za jirani zimeshafanya hivyo. Maeneo yanayozunguka hifadhi ni vizuri kutengeneza *One Life Conservatives* za wananchi wenyewe ambao wataweka hoteli za kitalii wenyewe. Watapunguza shughuli za kilimo katika mipaka ya Hifadhi za Taifa, ila watatengeneza shughuli za utalii nje ya hifadhi. Ukifanya hivyo watanufaika kutokana na uhifadhi huo na athari zile kwa kweli, watakuwa hawazisikii kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko jambo lingine ambalo ni lazima tulizungumze bayana na hili litasaidia kuondoa ndoto ya kufikiri tunaweza kuendelea kugeuza ardhi za vijiji kuwa mapori tengefu au mapori ya akiba. Leo ipo nyaraka moja inayoendelea kuonekana katika mitandao ya kijamii, ambayo ni Taarifa ya Tathmini ya Hali ya Mapori Yetu na mapendekezo yaliyofanywa na wataalamu kwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Nina uhakika na nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Angellah Kairuki na nina imani sana na Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, taarifa hiyo ninahakika imefika kwenu, lakini ninahakika hamjaifanyia maamuzi. Jambo kubwa ambalo ninataka kuwashauri ni pokeeni ushauri wetu, ili baadaye msije mkauziwa mbuzi kwenye gunia ikaleta athari kubwa kwa wananchi wetu, kama nyaraka hiyo ipo kwenye mitandao.

Mheshimiwa Spika, juzi nimefurahi Waziri mmoja alivyoona barua moja katika mitandao ya kijamii aliomba Wizara zenye dhamana zifanye uchunguzi juu ya jambo hilo la fedheha ambalo limetangazwa kupitia barua hiyo. Tangu hili la Ripoti ya Tathmini ya Mapori Tengefu katika Kaskazini mwa Nchi…

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, sawa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nyaraka hiyo ambayo anaitaja haiko mezani kwangu, haijatolewa na chombo rasmi. Kwa hiyo, ninaomba wala tusiizungumzie kwa sababu, tunazidi kuleta taharuki kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, taratibu za Kiserikali zinajulikana, namna ya kutenga maeneo kama Mapori Tengefu inajulikana, kama itafika wakati huo na kuna tathmini hiyo itakuwa inaendelea, basi taratibu rasmi za Kiserikali zitafanya kazi. Ninamuomba Mheshimiwa Mbunge tusilijadili kwa sababu, ni kuendelea kuleta taharuki kwa wananchi wakati jambo hilo wala haliko rasmi na hata mezani kwangu mimi sijatoa nyaraka hiyo na hata haliko kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Taarifa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ninamheshimu sana Waziri, lakini kwa kweli, Mheshimiwa Waziri, jambo hili kwanza nasema siipokei na siipokei kwa sababu moja. Mchakato huu ulipoanza ulianzia Bungeni, fuatilia Taarifa ya Waziri katika Bajeti ya mwaka 2021/2022 ya kupandisha hadhi mapori hayo, akasema wanakusudia kupandisha hadhi. Wakaenda kutuma timu za wataalamu, zimekuja katika wilaya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zilipofika kwenye Wilaya tukatambulishwa kwamba, zipokeeni kwenye vijiji. Wameleta taarifa, bahati mbaya taarifa yao ilipoletwa kwa Waziri ika-*leak* na taarifa hiyo ni hii hapa, ipo, wananchi wote wanayo. Tukijifanya hatuioni unatuharibia kura katika Ukanda wa Kaskazini kwa sababu, wananchi wanayo na bahati mbaya taarifa siyo nzuri. Inapendekeza maeneo karibu yote ya wafugaji katika Wilaya hizo zingebadilishwa kuwa *Game Reserve*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka…

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo ni hata kama hiyo taarifa haijawa *open,* lakini imeshakuwa ahadharani. Ni vizuri mka…

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nimekaa.

**SPIKA:** Unaweza kunisaidia taarifa hiyo unayoisema hapo? Nisaidie niipate hiyo taarifa. *(Makofi)*

Hebu, haya kabidhi hiyo taarifa. Endelea na mchango wako.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, niendelee?

**SPIKA:** Malizia mchango wako.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ooh! Rai yangu kwa Serikali yangu ni kwa sababu, taarifa hii wananchi wanayo na wanaijadili, tukisema hatuioni ni vizuri Serikali mkaweka tamko tu kwamba, haya ni mapendekezo. Ndivyo tunavyowaambia wananchi, ni mapendekezo ya wataalamu, bado hayajafanyiwa maamuzi, bado Serikali haijafanyia maamuzi, lakini tukisema na tunajua unaweza kuyabadilisha, kama Waziri na Baraza la Mawaziri linaweza likabadilisha, siyo lazima likubaliane nayo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia leo kwenye hiyo taarifa, hata anakotoka Naibu Waziri, kule kwenye eneo la Umba, kule kwa Diwani Letinga kwenye kata yake moja kule na yenyewe inapendekezwa kuwa *Game Reserve*. Ukija Same upande wa Kalimawe unapendekezwa kuwa *Game Reserve*. Same Mashariki, Magharibi, upande wa Ruvu, Same inapendekezwa kuwa *Game Reserve,* upande wa Simanjiro, Ruvu Masai inapendekezwa kuwa *Game*

*Reserve,* Natron *Game Reserve*, Longido *Game Reserve* na Mto wa Mbu *Game Reserve*.

Mheshimiwa Spika, vijiji 80 katika Wilaya ya Monduli, Simanjiro na Ngorongoro vyote vinapendekezwa kuwa *Game Reserve*. Ninajaribu kusema na hiyo hawakutaja vijiji vyote. Waheshimiwa Mawaziri tafakarini hili, tusaidieni kwa sababu, uhalali wa CCM unatokana na CCM kuendelea kuwa mtetezi wa wananchi wakulima na wafanyakazi maskini wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hamuwezi kujificha kwenye kichaka hicho na kwa sababu taarifa yenyewe inasema itatekelezwa Mwaka 2025/2026. Hatari yake ni kwamba, usipotoa kauli wananchi wanaamini kwamba, tunanyamaza tupate kura kwanza halafu tuwanyang’anye ardhi zao wakati taarifa ni mapendekezo. *(Makofi)*

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ilishagonga. Sekunde 30 malizia.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninasema wazi kabisa kwamba, bajeti hii kwa masikitiko, kama Waziri hatatoa tamko linalotoa faraja kwa wananchi, siungi mkono na nitakusudia kutoa shilingi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MCHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kunijalia uzima na afya njema leo hii.

Mheshimiwa Spika, aidha natoa pongezi za dhati ya nafsi yangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuliongoza Taifa letu kwa weledi, uzalendo, ubunifu na ufanisi mkubwa sana. Pia, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Naibu Spika

na Waheshimiwa Wenyeviti wote kwa kuendesha vizuri sana vikao vya Bunge kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wenyeviti wa Bodi na watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nina sehemu chache za kuchangia. Tanzania ni moja kati ya nchi zilizobarikiwa vivutio vingi vya utalii sambamba na maliasili ambazo zinachangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, idadi ya watalii imeongezeka. Kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara husika pamoja na mapato yanayotokana na watalii waliozuru nchini, ni jambo la faraja sana kwetu. Hata hivyo, bado tuna mazao au vivutio vingi hatujavitumia vizuri au kuviongezea nguvu kama utalii wa michezo, utalii wa tiba asili, utalii wa malikale, utalii wa fukwe, bahari na kadhalika. Hivyo basi, naomba kuishauri Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na mafanikio makubwa waliyofanikiwa ni vyema kuiongezea uzito Idara ya Malikale na Idara ya Utalii kwa lengo la kukamilisha malengo ya idara hizo kwani zitatuongezea mapato zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba kuishauri Wizara iboreshe ushirikiano na Wizara ya Utalii na Malikale ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Utalii sio sekta ya muungano, lakini ushirikiano utasaidia kuongeza wageni wanaokwenda Zanzibar wasiishie Zanzibar, waje na Tanzania Bara kwani kuna vivutio vipo Zanzibar huku hakuna na vingine vipo huku Zanzibar havipo.

Mheshimiwa Spika, aidha kuboresha miundombinu katika maeneo yanayotumika kwa shughuli za kitalii na uhifadhi ni jambo la msingi. Baadhi ya maeneo yanakabiliwa na changamoto ya uchakavu na ubovu wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Hivyo basi, naunga mkono hoja asilimia

mia, nikiamini Ripoti ya Kamati itazingatiwa na kufanyiwa kazi kwa weledi na kuzingatia maslahi ya Taifa letu. Ahsante sana.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia yafuatayo; Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na TAMISEMI katika kuona namna nzuri ya kufanya kazi na Askari Wanyamapori walioko katika Halmashauri zetu za Majiji, Miji na Wilaya. Pia, kuwe na nafasi ya kuangalia upya uwindaji wa kienyeji, ili wananchi wavae umiliki wa hizo maliasili.

Mheshimiwa Spika, naomba nipongeze kwa ongezeko la idadi ya watalii na kuongezeka kwa mapato pamoja na kuimarika kwa ulinzi na usimamizi wa rasilimali za wanyamapori, lakini suala la mimea vamizi ni bora likafanyiwa kazi ili kunusuru kupotea kwa malisho. Aidha, kuwe na ujenzi wa lango la kuingilia katika Hifadhi ya Katavi, sambamba na kuvutia wawekezaji wa huduma za malazi.

Mheshimiwa Spika, utangazaji wa vivutio vya utalii. Nashauri kuwepo na mikakati ya kutambua na kutangaza vivutio vingi, ili kuongeza wigo wa mapato.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuwe na vipaumbele vichache tuweze kupanga, kusimamia na kupima matokeo, ili tuweze kakabiliana na ushindani na pia, tuwe sehemu ya washindi. Tuendelee kutangaza kidijitali *(DDMCC)* ili kuleta tija. Kutokana na uhaba wa huduma ya malazi ya watalii ni bora hoteli na *lodge* zikarejeshwa kwa wale walioshindwa kukidhi vigezo vya mkataba.

Mheshimiwa Spika, ipo nafasi ya *Diaspora* na Mabalozi katika kuutangaza utalii. Kwa kupitia fundisho la corona tuendelee kuutangaza utalii wa ndani sambamba na kuanzisha utalii wa *TBA*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo ameifanya

sekta hii ya utalli kuendelea kukua na kupaa kimaitaifa na hatimaye kuwa ni moja ya sekta inayochochea uchumi wa nchi yetu. Sekta hii imeendelea kukua siku hadi siku kwa sababu, imekuwa ikiongezewa Bajeti. Ni wajibu kwa Wizara kusimamia ipasavyo fedha wanazopata kwa kutatua changamoto za miundombinu ya barabara kwenye mbuga zetu za utalii ili kuvutia watalii wanaokuja kwa shughuli za utalii.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamechangia hapa Bungeni kuhusu umuhimu wa kutunza misitu yetu, lakini nasikitika kuona hivi. Mheshimiwa Waziri, ni kwa nini wameshindwa kufanya maamuzi ya kuwaondoa wavamizi wa Msitu wa Bondo? Hivi kuna maslahi ya nani? Kwa nini Waziri umeshindwa kuchukua hatua stahiki? Nimezungumza zaidi ya mara tano, lakini kwa makusudi wamedharau.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Kata ya Mswaki wameutunza msitu huu kwa miaka 40, lakini wamekuja wananchi kutoka Manyara na kufanya uharibifu mkubwa. Wananchi hao walikuwa na kila sababu ya kufanya shughuli za kilimo, lakini hawakufanya, sasa iweje Serikali hauchukui maamuzi ya kuwaondoa wavamizi hawa?

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali leo inipe majibu ya kuridhisha. Naunga mkono hoja.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi na mimi kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu ya Maliasili na Utalii. Naanza kwa kuwapongeza sana dada yangu Mheshimiwa Kairuki na kaka yangu Mheshimiwa Kitandula kwa kazi kubwa wanayofanya kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika nchi zilizobarikiwa Tanzania ni mojawapo, tuna vivutio vingi na vizuri duniani. Ni matarajio ya Watanzania kuwa, Wizara hii ikisimamiwa vizuri itatusaidia sana katika kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja ningependa kuishauri Wizara, ili kuhakikisha sekta hii inakwenda vizuri. Hatuwezi kukwepa

uwekezaji kwenye kutangaza vivutio tulivyonavyo ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tulijenga kituo cha utangazaji kwa njia ya kidigitali na lengo lilikuwa ni zuri sana la kusaidia kuwa na mipango ya kimkakati na kuwezesha kufanya maamuzi kutokana na taarifa zinazopatikana mubashara na kuhakikisha taarifa hizo zinawafikia *TTB* ndani na nje. Kituo hiki kilitumia zaidi ya shilingi bilioni 1.06 na kilikamilika tangu Aprili, 2022. Mpaka hivi leo kituo hiki hakitekelezi yale majukumu ya kutangaza utalii, kama ambayo sisi kama Watanzania tulitarajia, na matokeo yake tumeinyima sekta ya utalii faida ambazo zingetokana na utangazaji wa vivutio vyetu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, kwa nafasi yako uweze kuona je, kituo hiki kina umuhimu? Kama ndivyo, kwa nini kituo hiki hakitumiki kama kilivyokusudiwa?

Mheshimiwa Spika, *all in all* ninawapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya na ninatakia heri katika utekelezaji wa bajeti hii.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naanze kwa kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, nanza na masuala ya kiujumla; fedha zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Wizara inaomba shilingi bilioni 348.12 ikiwa fedha za maendeleo ni shilingi bilioni 97.24 na matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 250.88. Nakubaliana na ushauri wa kamati kuhusu matumizi ya nyongeza ya bajeti, shilingi bilioni 16, ili kuimarisha utafiti wa misitu na wanyama, kuongeza vivutio vya utalii na kuzidisha mapambano dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kuongeza bajeti ya *TAWA*.

Mheshimiwa Spika, pia, naipongeza Wizara na Taasisi zake kwa ukusanyaji mzuri wa mapato ambapo imefikia 97.12% ya mapato yote ya mwaka husika. Ni wazi kuwa, Wizara itavuka malengo. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Makumbusho ya Maraisi Dodoma. Mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni moja, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Makumbusho ya Marais wa Tanzania itakayojengwa Jijini Dodoma. Huu ni uamuzi mzuri wa kupongezwa kwani eneo hilo la Kumbukumbu ya Marais litatumika kama sehemu ya kujifunza, kufanya utafiti na kivutio cha utalii ndani na nje ya nchi. Pia, makumbusho hiyo itakuwa sehemu nzuri kwa wanafunzi kujifunza historia ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafugaji walioshinda kesi Mahakamani. Waziri katika hotuba yake na Taarifa ya Kamati haijaeleza chochote kuhusu hatua iliyofikiwa na Serikali katika kurejesha au kufidia mifugo ya wafugaji walioshinda kesi Mahakamani. Hii ni ishara kuwa, Serikali haijayafanyia kazi madai halali ya wafugaji hao yaliyowasilishwa Serikalini muda mrefu, licha ya wafugaji kulalamika na kukumbushia mara kwa mara. Sisi Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni tumekuwa tukiitaka Serikali kutekeleza hukumu ya Mahakama na kutenda haki kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijarejesha mifugo ya wafugaji walioshinda kesi Mahakamani ambapo, kwa kipindi cha Mwaka 2017 hadi Mei, 2023 ni jumla ya ng'ombe 11,438 punda 13 na kondoo tisa katika maeneo ya Hifadhi za *WMA, TAWA, TFS* na *TANAPA*. Mambo haya yanachochea chuki baina ya wananchi na Serikali yao na hii ni kwenda kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Sheria za nchi ambapo Mahakama ndio chombo cha mwisho cha utoaji haki. Je, ni nini kinachoifanya Serikali kupuuza utekelezaji wa hukumu ya Mahakama ambapo, pia, ni ukiukwaji wa misingi na nguzo za utawala bora na utawala wa Sheria?

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia kwa wananchi waliopisha uhifadhi. Timu ya Mawaziri nane ilibainisha baadhi ya vijiji vinavyotakiwa kuhama kupisha uhifadhi ambapo baadaye Mthamini Mkuu wa Serikali alifanya tathmini ya mali, ili kuwafidia wananchi hao pamoja na utayari wa wananchi hao kuhama katika maeneo hayo, lakini Serikali imeshindwa kuwalipa fidia, ili kupisha uhifadhi kama

ilivyoelekezwa na Serikali. Leo ni miaka miwili imepita, wananchi wa maeneo hayo wako njia panda, hawawezi kufanya maendelezo ya ardhi, mashamba na nyumba za makazi na biashara.

Mheshimiwa Spika, mfano katika Kata ya Nyatwali, Wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara, Kijiji cha Ngombo, Wilaya ya Malinyi, Mkoa wa Morogoro na maeneo mengine nchini, Serikali iliagiza vijiji hivyo kuhamishwa kupisha uhifadhi, lakini leo wananchi hawajafidiwa. Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na wananchi wa maeneo husika wanapaza sauti kila leo kuomba kufidiwa kama ilivyoahidiwa na Serikali. Naungana na viongozi na wananchi wa maeneo hayo kuiomba Serikali ilipe fidia kwa wananchi hao, ili waweze kuendelea na maisha yao mengine na Serikali kufikia malengo ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utafiti unaofanywa na *TAFORI* na *TAWIRI.* Kamati inakiri kuwa, Taasisi za Utafiti za *TAFORI* na *TAWIRI* hazikutengewa fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake na kama taasisi hizi hazina bajeti ya kutosha maana yake ni haziwezi kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kufanya utafiti wa namna bora ya uhifadhi na utalii endelevu. Hata hivyo, katika Mwaka 2023/2024 *TAWIRI* na *TAFORI* zilifanya tafiti 46 tu na kuratibu na kusimamia miradi ya utafiti 93 ya watafiti wa ndani na nje ya nchi. Pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Taasisi za Utafiti, lakini kasi ya kufanya utafiti ni ndogo na hivyo, kuwa na maeneo mengi ya kipaumbele na yenye changamoto ambayo hayajafanyiwa utafiti.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya matokeo ya utafiti ni madogo kwa kuwa, tafiti nyingi zimefichwa kwenye makabati na hawazipati walengwa na watumiaji wa tafiti hizo. Pia, hatuoni mkazo wa matumizi ya tafiti zinazofanywa na vijana wa *Masters* na *Ph.D,* ili kupanua wigo wa kufanya tafiti na kusaidia upatikanaji wa taarifa muhimu zitakazowezesha uhifadhi endelevu wa wanyamapori, misitu na kukuza utalii. Hotuba ya Waziri haijaeleza kama kuna kanzidata *(database)* inayowezesha kuzipata na kuzitumia tafiti 46 zilizofanywa na *TAWIRI* na *TAFORI* na tafiti 93 zilizofanywa na wadau, ili kuongeza matumizi ya matokeo ya utafiti na kukuza uhifadhi na utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuuawa kwa mamba mkubwa duniani, mali ya Tanzania. Tarehe 27 Disemba, 2023 ilisambaa picha jongefu *(video clip)* inayoonesha muwindaji/wawindaji bingwa kutoka Marekani, Josh na Sarah Bowmar, kudaiwa kumuua mamba mkubwa zaidi duniani nchini Tanzania. *Video* hiyo ilionesha mamba mkubwa amemning'inizwa juu ya mti na baadae kuchunwa hadharani. Josh aliitangazia dunia kuwa, amefanikiwa kumuua mamba mkubwa kuliko wote duniani kutoka nchini Tanzania kwa kutumia upinde na mshale. Taarifa hizi zilisambaa kwa kasi kubwa kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vingine vya habari ndani na nje ya nchi na kuleta taharuki kubwa nchini.

Mheshimiwa Spika, hapa kuna maswali mengi ya kujiuliza kama ifuatavyo; kwa nini tukio kubwa kama hili lililotokea katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Waziri wa Maliasili na Utalii ameshindwa kulitolea taarifa kwenye hotuba yake? Kwa nini taasisi zetu za *TAWA* na *TAWIRI* zilificha taarifa za kuwepo mamba mwenye urefu mkubwa duniani hadi tukatangaziwa na mwindaji Josh kutoka Marekani akiwa ameshamuua na kuondoka naye?

Mheshimiwa Spika, Muwindaji Josh kutoka Marekani alijuaje kuwa katika Kitalu cha *Lake Rukwa GR* kuna mamba mwenye urefu mkubwa kuliko mamba wote duniani? Thamani ya mamba huyo mwenye urefu wa takribani meta tano inalingana na mamba wa kawaida wanaoruhusiwa kuwindwa? Nchi yetu haikuwa na matumizi na huyu mamba hadi kitolewe kibali cha kuwindwa na kuuawa na mgeni kutoka Marekani? Je, ni fedha kiasi gani alizolipa muwindaji huyo kwa Serikali na kupewa kibali cha kumuwinda na kumuua mamba huyo?

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TAWA* baada ya kuwindwa na kuuawa kwa mamba huyo ilitoa majibu mepesi kupitia taarifa kwa umma ya tarehe 2 Januari, 2024 kuwa, mamba huyo aliwindwa katika Kitalu cha *Lake Rukwa GR* kwa Kibali Namba MP-0001792, kilichoanza tarehe 12 Agosti, 2023 hadi tarehe 9 Septemba, 2023 na kwamba, mamba huyo alikuwa na urefu wa futi 16.2 sawa na sentimeta 493.8 (takribani urefu wa meta tano).

Mheshimiwa Spika, ilitegemewa baada ya *TAWIRI* na *TAWA* kubaini kuwa, nchi yetu ina mamba mrefu kuliko mamba wote duniani angetangazwa kidunia na angejengewa kizimba, kuwekewa ulinzi na kuhifadhiwa kama sehemu ya kivutio kikubwa cha utalii ambapo wageni kutoka mataifa mbalimbali duniani wangefika kumuona na kuliingizia Taifa letu mapato na fedha nyingi za kigeni. Jambo hili limefanya watafiti na wanafunzi kukosa eneo la kujifunza na kufanya utafiti; leo wageni na watalii ambao waliopaswa kuja Tanzania kumuona mamba huyo mkubwa kuliko wote duniani wanalazimika kwenda nchini Marekani kwenye hifadhi ya muwindaji Josh kumuona akiwa amekaushwa na kumlipa mamilioni ya fedha.

Mheshimiwa Spika, ninajua *TAWA* na *TAWIRI* walikuwa na taarifa za kutosha kuhusu uwepo wa huyu mamba na mwindaji Josh hakwenda kitalu cha *Lake Rukwa GR* kwa kubahatisha. Hapa kuna harufu kubwa ya rushwa ambapo huenda baadhi ya Watendaji wa Serikali walikula njama kuipoteza rasilimali hiyo muhimu kwa Taifa letu na kujinufaisha binafsi.

Mheshimiwa Spika, pia, ifahamike kuwa, uwindaji wa mamba unasimamiwa kupitia Sheria za ndani na za Kimataifa chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo kwenye hatari ya kutoweka *(Convention on International Trade in Endangered Species of Wild Fauna and Flora-CITES)*. Pia, zipo taarifa kuwa, mwindaji Josh na mkewe wamewahi kuhukumiwa kwa uwindaji haramu nchini Marekani.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri mambo yafuatayo; kwanza Waziri wa Maliasili na Utalii aliambie ukweli Bunge juu ya sakata la kuwindwa na kuuawa kwa mamba huyu mrefu zaidi duniani na kupelekwa Marekani, huku nchi yetu usiku na mchana inatafuta vivutio vya utalii. Pili, Bunge liunde tume kuchunguza mkasa mzima wa kuwindwa na kuuawa kwa mamba mkubwa kuliko wote duniani na wote watakaobanika kuhusika na kashfa hiyo, wawajibishwe kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvamizi wa wanyamapori wakali. Kumekuwepo na matukio mengi ya wananchi kuuawa na wengine kupata ulemavu wa kudumu kutokana na athari za wanyama wakali wakiwemo tembo, viboko, nyati, chui, mamba, simba na kadhalika na kusababisha madhara mengine makubwa, ikiwemo kubomolewa kwa nyumba, mazao kuliwa yakiwa shambani na majumbani na wananchi kuachwa kwenye ufukara wa kutupwa.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Meatu ushahidi wa takwimu unaonesha kuwa, madhara ya uvamizi wa tembo ni mkubwa, leo ninapozungumza hapa Bungeni wamefikia watu 20 ambao wameuawa na wengine kumi wamejeruhiwa. Mashamba yaliyoharibiwa ni ekari 2,086 katika kaya 715, nyumba zilizobomolewa ni 480, mazao yaliyoshambuliwa majumbani ni magunia 1,500 sawa na tani 150. Mifugo iliyouawa ni ng'ombe tisa, kondoo saba na mbuzi 19, lakini pia, kitaifa umekuwa ukiripotiwa uvamizi wa tembo na wanyama wengine wakali kila kona ya nchi, hasa vijiji vinavyopakana na maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na uvamizi wa tembo na wanyama wakali wengine kwa kujenga vituo vya kudhibiti tembo, kuendesha doria, kuongeza maaskari na *VGS*. Vilevile ujenzi wa vizimba vya kuzuia mamba na viboko, ufungaji wa mikanda maalum ya mawasiliano *(GPS Satellite Collars),* uvunaji wa wanyama wakali na kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyama wakali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kifuta jasho na kifuta machozi. Wizara imefanya mapitio ya kanuni za kifuta jasho na kifuta machozi za Mwaka 2011 kwa kuongeza kiwango cha malipo. Hili ni jambo ambalo tulilipigia kelele muda mrefu na hivyo, hatua iliyofikiwa na Serikali ni ya kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto katika ulipaji wa kifuta jasho na kifuta machozi. Viwango vya kifuta machozi na kifuta jasho ni vidogo na haviendani na uhalisia. Pamoja na uamuzi wa Serikali wa kupandisha viwango bado viwango vilivyowekwa ni vidogo sana

havina uhalisia na haviendani na gharama za maisha za sasa. Pia, ifahamike kuwa, viwango vya kifuta machozi na kifuta jasho vilivyokuwepo viliwekwa miaka 14 iliyopita, leo gharama za maisha zimepanda, gharama za mazishi ziko juu, gharama za matibabu ziko juu, lakini pia, haiingii akilini ekari moja ya mazao ya mpunga, mahindi, vitunguu, nyanya, pamba na kadhalika vyenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni moja kufidiwa kwa shilingi 150,000 na ng'ombe kufidiwa kwa shilingi 75,000. Viwango hivi tuvikatae na tuitake Serikali kuweka viwango vinavyoendana na hali ya maisha ya sasa ikizingatia mfumuko mkubwa wa bei na ugumu wa maisha tulionao sasa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na kucheleweshwa kwa malipo ya kifuta machozi na kifuta jasho kwa wananchi walioathiriwa na wanyama wakali ambapo inachukua hadi miaka mitatu na vilevile Serikali imekuwa na malimbikizo ya madai ya wananchi kwa muda mrefu. Hotuba ya Waziri haijabainisha ni malimbikizo kiasi gani ya madai ya kifuta jasho na kifuta machozi yamefikia hadi sasa kwa nchi nzima. Ibara ya 50 ya hotuba ya Waziri inaonesha kuwa, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Mei, 2024 kiasi cha shilingi bilioni 2.4 zilikuwa zimelipwa kwa wananchi 10,552 waliopata madhara ya wanyamapori wakali, lakini haionesha ni kiasi gani bado kinadaiwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, mfano katika Jedwali Namba 7, Ukurasa wa 203, Wilaya ya Meatu inaonesha wamelipwa watu watano kiasi cha shilingi 4,500,000 wakati madai yaliyowasilishwa Serikalini kutoka Wilaya ya Meatu ni zaidi ya shilingi 118,775,000. Inashangaza pia, kuona baadhi ya Halmashauri nyingine zikilipwa zaidi ya shilingi milioni 370 na nyingine zikilipwa kiduchu dhidi ya madai halisi, ni vigezo gani vilitumika kufanya malipo hayo?

Waheshimiwa Wabunge, wananchi wetu wanateseka sana na madhila ya hawa wanyama wakali, tuitake Serikali kulipa kifuta machozi na kifuta jasho madai yote yaliyolimbikizwa na madai mapya kulipwa kwa wakati. Aidha, kifuta jasho kimekuwa hakitolewi kwa baadhi ya uharibifu kwani Sheria haitambui uharibifu wa nyumba, mazao yakiwa nyumbani na mali nyingine, lakini pia, haitoi fidia zaidi ya ekari tano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mkakati wa kupambana na wanyama wakali na waharibifu kumekuwepo na kukosa ufanisi kwa doria zinazoendeshwa na *TAWA, TANAPA* na *NCAA* katika kudhibiti wanyama wakali. Pamoja na doria zinazoendeshwa, lakini wanyama wakali wameendelea kuvamia makazi ya wananchi kutokana na mapungufu ya doria hizo ikiwemo kufanyika kwa msimu na sio kila siku. Vilevile, kukosa vifaa muhimu vya ulinzi, kukosa magari na mafuta, upungufu wa maaskari na *VGS* na ushirikishwaji hafifu wa wananchi waishio pembezoni mwa maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, bila kuimarisha doria katika mipaka na maingilio ya wanyamapori katika vijiji na makazi ya wananchi, vita ya uvamizi wa wanyama wakali hatuwezi kuishinda. Ununuzi wa helkopta mbili na *drone*, ufungaji wa mikanda maalumu ya mawasiliano *(GPS Satellite Collars)* vitasaidia kwa kiasi kidogo.

Mheshimiwa Spika, aidha naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga vituo viwili vya kudhibiti tembo katika Jimbo la Kisesa, ambapo vimejengwa katika Kijiji cha Malwilo na Kijiji cha Ng'hanga. Hili ni jambo zuri na la kupongezwa ingawa vituo hivi havina askari na *VGS* wa kutosha, mafuta, magari na vifaa vingine muhimu vya ulinzi hali inayosababisha uvamizi wa tembo kuendelea licha ya kuwepo vituo hivyo. Mwaka 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023 nililazimika kutafuta gari na kutenga kiasi cha shilingi 11,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya kusaidia udhibiti wa tembo kutoka Mfuko wa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kitaifa wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu uliowasilishwa na Serikali bado una mapungufu makubwa kwani, kwa sehemu kubwa unahusu maboresho ya huduma za hifadhi za kila siku. Mkakati hauoneshi ni vijiji vingapi vitakavyohusika na wala hauainishi mahitaji muhimu ya kutekeleza mkakati huo ikiwemo ajira za mkataba za *VGS,* mafuta, magari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati iliyopangwa na Wizara ya shilingi bilioni 45.1, kwa ajili ya kuboresha maeneo ya hifadhi katika

malisho, maji, vizimba na vifaa vingine muhimu ni lazima uandaliwe mkakati maalumu wa kuzuia tembo kuingia kwenye vijiji, mashamba na makazi ya wananchi. Mkakati huo ushirikishe wananchi, Serikali za Vijiji, Madiwani na Wabunge kwa kila Wilaya zilizoko pembezoni mwa maeneo ya hifadhi, ili kupata mahitaji halisi ya namna ya kudhibiti wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, pia, Serikali itenge fedha za kutosha kugharamia mkakati huu ambao utaweka ulinzi na doria za kila siku kuzuia tembo na wanyamapori wengine wakali kuingia kwenye vijiji na makazi ya wananchi. Aidha, kiundwe kitengo maalumu cha kushughulikia uvamizi wa wanyamapori wakali, ili kutofautisha shughuli za udhibiti na uhifadhi na huduma za jamii. Hivi sasa askari wa doria za ulinzi na uhifadhi pamoja na udhibiti wa ujangili ni haohao wanaotumika kufukuza tembo, kazi ambazo si rahisi kuzifanya kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipeleke magari katika Ofisi za Wanyamapori za Halmashauri za Wilaya zinazopakana na hifadhi ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, ili kuongeza nguvu za kupambana na wanyamapori wakali wanaoingia kwenye vijiji na makazi na kurahisisha ufanyaji wa tathmini ya uharibifu unaofanywa na wanyamapori. Pia, Wizara inunue mabomu baridi na kuyasambaza kwenye Halmashauri za pembezoni mwa hifadhi kote nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro baina ya hifadhi na watuamiaji wengine wa ardhi. Kumekuwepo na migogoro baina ya askari wa uhifadhi na wananchi, hususan waishio pembezoni mwa hifadhi, ambapo kumekuwepo na malalamiko kwamba, kwanza wananchi wanapokamatwa ndani ya hifadhi wamekuwa wakipigwa, kuteswa, kupatiwa ulemavu na kuuawa, lakini pia, kumekuwepo na matumizi makubwa ya nguvu pasipo na sababu. Pili, wahifadhi wamekuwa wakivamia wananchi majumbani na mashambani na kupora mali zao ikiwemo mifugo, mazao na fedha.

Mheshimiwa Spika, tatu ni, mipaka ya hifadhi kutanuliwa kiholela na wananchi kufukuzwa kwenye makazi yao kwa

kuchomewa nyumba zao, mifugo kupigwa risasi na kufyekwa mazao. Jambo la nne ni Maafisa wa Uhifadhi kuswaga mifugo kutoka vijijini na kuingizwa kwenye hifadhi, ili kutengeneza shinikizo la kupewa rushwa na mwanya wa kuuza mifugo hiyo kwa faida binafsi.

Mheshimiwa Spika, tano ni, mifugo kukamatwa na kunyimwa huduma muhimu kama maji, malisho, chanjo na dawa, hali inayosababisha mifugo mingi kufa ikiwa imeshikiliwa na Serikali na hata wananchi wanaposhinda kesi Mahakamani wanashindwa kukabidhiwa mifugo hiyo kwa kuwa haipo. Sita, mifugo kuuzwa kiholela ndani ya hifadhi badala ya soko la wazi kwenye minada ya wananchi. Mfano Mwaka 2023, ng'ombe waliuzwa kwa wastani wa shilingi 170,000 badala ya shilingi 1,500,000 kwa kila ng'ombe, kinyume na kifungu cha 114(2) cha Sheria ya Wanyamapori na Kanuni ya *The Animal Welfare (Impounded Animal) Regulations 2020* ambavyo vinataka mifugo iuzwe kwenye minada ya wazi kwa bei ya soko.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la saba ni, faini wanayotozwa wafugaji ya shilingi 100,000 kwa kila kichwa cha ng'ombe haipo kwenye Sheria, lakini nane ni, mifugo kukamatwa na kushikiliwa kama ushahidi bila kushirikishwa uongozi wa eneo husika, bila kuwashirikisha wafugaji wenyewe na bila kufanya uhakiki wa idadi ya mifugo inayokamatwa. Hali hii imesababisha mifugo kupotea, kuibwa na kuuzwa kiholela na jambo la tisa ni, kuvunjwa kwa Kanuni ya 9(1) *The Animal Welfare (Impounded Animal) Regulations 2020* na kifungu cha 106(1)(b) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake ya Mwaka 2022 zinataka ukamataji ni lazima ushuhudiwe na mashahidi wengine wakiwemo viongozi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla baadhi ya maafisa wa uhifadhi wamekuwa wakikiuka maadili ya kazi zao, haki za binadamu na utawala wa Sheria kwa kisingizio cha kusimamia Sheria za uhifadhi. Hali hii imesababisha madhara makubwa kwa wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, Wabunge kwa muda mrefu tumelalamikia jambo hili na hata tulipotakiwa kuleta ushahidi wa matukio hayo

tulifanya hivyo na taarifa zetu kuthibitishwa na Bunge kuwa, zilikuwa ni sahihi na za kweli. Waziri Mkuu alipoingilia kati na kutoa maagizo 12 hapa Bungeni Aprili, 2023 kwa mamlaka za uhifadhi kuendesha doria kwa kuzingatia haki za binadamu, utawala wa Sheria na kuwashirikisha wananchi naye alidharauliwa na *operation* zikaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mahakama Kuu ya Tanzania nayo imeingilia kati suala hili na kuonesha kukerwa na makosa ya kukiuka maadili ya kazi, haki za binadamu na utawala wa Sheria kunakofanywa na askari wa uhifadhi kupitia hukumu ya kesi, *Criminal Appeal No.40809 of 2023,* iliyosomwa Tarehe 24 Aprili, 2024. Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Musoma, Mheshimiwa Kamazima Idd Kafanabo, wakati anamuachilia huru mtuhumiwa Richard Changei Ng'ombe, mkazi wa Wilaya ya Serengeti alitoa onyo kwa kusema, na ninanukuu kama ilivyonukuliwa katika Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii; "Mahakama haiwezi kufumbia macho jambo hili linaloonekana kuzoeleka na kujirudia la kutofuata maadili ya kazi kunakofanywa na maafisa wengi wa uhifadhi na wengine katika haki jinai, hasa katika ukamataji wa watuhumiwa na uchukuaji wa vielelezo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kamati inakiri pia, kuwa, Wizara haijafanyia uchunguzi tuhuma hizo na wala haijachukua hatua zozote kwa baadhi ya askari wanaokiuka maadili ya kazi yao na kutenda kinyume cha Sheria ambao wanafahamika kwa majina na vyeo vyao ndani ya Jeshi Usu. Kitendo cha Wizara kutochukua hatua kwa wahusika ni ishara kuwa, uhalifu huu una baraka zote za viongozi wakuu wa Wizara kwa kuwa, Sheria zinaendelea kuvunjwa na wananchi wetu kupata mateso makubwa na kupoteza maisha Na Kwa kuwa, Bunge na Mahakama zimedharauliwa. Nashauri yafuatayo:-

(i) Waheshimiwa Wabunge, naomba leo tutoe fundisho, tuitake Serikali kupitia Waziri Mkuu kuwafukuza kazi watumishi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzia Waziri hadi mfagizi wa ofisi.

(ii) Bunge liunde Kamati Maalum kuchunguza na kubaini matukio yote ya ukiukwaji wa Sheria katika mikoa yote Tanzania na kupendekeza hatua stahiki za kuchukua kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kusambaa kwa mimea vamizi maeneo ya hifadhi. Utafiti wa *TAFORI* na *TAWIRI* unathibitisha kuwa, chanzo cha uharibifu wa mazingira, kuathiri afya ya udongo na ukosefu wa nyanda za malisho unachangiwa kwa kiwango kikubwa na kuenea kwa mimea vamizi *(Invasive plant species)* katika maeneo ya hifadhi. Kuenea kwa mimea hii vamizi kumekuwa chanzo cha wanyamapori kukimbia maeneo ya hifadhi na kwenda maeneo ya vijiji kutafuta maji na malisho.

Mheshimiwa Spika, mimea vamizi ilivyoenea katika hifadhi za *TAWA, TANAPA, NCAA, TFS* na *WMA* pamoja na Ranchi za Taifa za *NARCO* ni tishio kubwa la uhai na uendelevu wa hifadhi zetu na kama Serikali isipochukua hatua za dharura tutaua hifadhi hizi ambazo ni urithi tuliobarikiwa na Mwenyezi Mungu. Tutapoteza hadhi ya hifadhi zetu na kupungua idadi kubwa ya watalii nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni Wizara iling'oa mimea vamizi katika eneo lenye hekta 3,776.57. Hili ni eneo dogo sana ikilinganishwa na maeneo yaliyovamiwa na mimea vamizi, bado sioni mkakati madhubuti wa Serikali wa kupambana na kutokomeza mimea hii. Pia, kwa hali ilivyo sasa nilitegemea *NEMC* ingekuwa inafanya ukaguzi wa mazingira katika hifadhi zetu mara kwa mara *(Environmental Audit and Monitoring)*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchumi wa misitu na nyuki. Pamoja na *TFS* kufanya ufuatiliaji wa shughuli za uzalishaji na utunzaji wa taarifa za manzuki kwa kutumia mfumo *honey traceability* na kuhamasisha uzalishaji wa asali kwa kauli mbiu ya "Achia Shoka Tundika Mzinga", lakini hotuba ya Waziri haijaeleza hadi sasa wakala imesajili wazalishaji wangapi wa asali katika mfumo, wanazalisha kiasi gani na mauzo ya nta na asali nje ya nchi yana thamani gani katika Mwaka 2023/2024. Nini sababu ya Waziri kuficha takwimu hizi?

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 mauzo ya misitu nje ya nchi ambayo ni mbao, *veneer,* utomvu, mbegu, gundi, nguzo, karatasi, *MDF* na kadhalika yalikuwa ni shilingi bilioni 234.5 na nyuki na nta ni shilingi bilioni 34. Mauzo haya ni madogo sana ikilinganishwa na ukubwa wa rasilimali za misitu tulizonazo nchini.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya asali inatoroshwa na kuuzwa nje ya nchi na hivyo kupoteza ajira na mapato ya Serikali. Inakadiriwa zaidi ya tani 11,000 za asali zenye thamani ya shilingi bilioni 110 zinatoroshwa kila mwaka. Ninaamini kuwa, hili eneo la misitu na nyuki ni fursa kubwa ya kuongeza mauzo nje ya nchi, kukuza uchumi na kuongeza mapato ya Serikali, lakini kwa bahati mbaya sekta hii si kipaumbele cha Serikali. Wizara ya Maliasili na Utalii, *TAFORI* na *TFS* waandae mkakati wa kukuza sekta hii.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kuchukuaa nafasi hii kumshukuru Mungu kwa neema hii ya uhai. Aidha nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya. Sote ni mashahidii kupitia filamu yake kama *Royal Tour* ambayo imezaa matunda makubwa ikiwemo kuongezeka kwa watalii wengi nchini kwetu hali ambayo imeongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, bado Serikali ije na mpango wa kuwazuia tembo ambao wamekuwa ni janga kubwa na pia, kutoa elimu kwa wananchi juu ya kutunza uoto wa asili. Hii ni rasilimali kubwa na muhimu kwa nchi yetu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula na kumwambia mtoa hoja ajiandae, lakini wakati Mheshimiwa Kitandula atakapokuwa anachangia, Mheshimiwa Waziri nitakuletea hii taarifa uipitie kwa sababu, hapa mwisho inaonekana wanasema, "Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, hapa ndiyo mwisho wa wasilisho letu."

Wakiashiria kwamba, hili wasilisho lilikuwa linawasilishwa kwa Waziri. *(Makofi)*

Huku mwanzo wameelezea yale maelezo ya awali kwamba hii timu iliyoundwa iliundwa kutoka kwenye Wizara zipi na imeenda wapi na wapi. Kwa hiyo nitakuletea hapo uipitie halafu utaniambia, siyo lazima uje uhitimishe hapa kwa kujibu hoja hii lakini utaniambia mimi ina hali gani ili nijue namna ya kuamua hapa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dunstan Kitandula. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye imempendeza kuwepo hapa siku ya leo. Nitumie fursa hii vilevile kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kufanya kazi kwenye Wizara hii. Nirejee kuendelea kumhakikishia kwamba nitafanya kazi kwa uwezo wangu wote na kwa vipawa ambavyo amenijalia Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru vilevile Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa miongozo yao wanayotupa katika kutekeleza majukumu yetu. Nikushukuru wewe binafsi kwa jinsi ambavyo umekuwa ukitupa maelekezo mbalimbali, jinsi ya kufanya kazi katika Bunge letu Tukufu, nakushukuru sana. Kwa kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Angellah Kairuki kwa jinsi ambavyo amekuwa akinisaidia kunielekeza ili niweze kutimiza majukumu ya kumsaidia kazi katika Wizara hii, Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, wote kwa ujumla wenu kwa jinsi ambavyo tumekuwa tukishirikiana katika kufanya kazi ndani ya Bunge hili lakini vilevile kufanya kazi nje ya Bunge letu Tukufu katika kuwatumikia Watanzania, nawashukuru sana niwaombe ushirikiano huu uendelee. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu nawashukuru sana

ndugu zangu wa Mkinga kwa jinsi wanavyoendelea kunipa ushirikiano katika kutimiza majukumu haya ambayo nimepewa lakini vilevile kufanya kazi ya Jimbo letu la Mkinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepokea hoja nyingi kutoka kwa Kamati lakini vilevile kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge lakini kwa sababu ya muda ikupendeze kwamba wakati ninajibu nijibu kwa ujumla na kwamba kwenye *document* yetu ambayo Waheshimiwa Wabunge wataipata itaonesha mchango na swali la kila Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuokoa muda kama ambavyo umekuwa ukituelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo tumeipokea, ambayo nataka kujielekeza inahusiana na mambo ya mipaka, kupima maeneo, kufanya utambuzi na kuweka alama za maeneo hayo lakini vilevile tumetakiwa, tumepokea ushauri wa kufanya kazi kwa kushirikiana na Wizara nyingine za Kisekta katika kuweka mipaka. Niseme mambo haya tumeyapokea, tumepokea ushauri wa Kamati, tumepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na sisi tutaenda kufanya kazi hii kuhakikisha kwamba migogoro katika maeneo yetu inakwisha.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mifano tu kwamba jambo hili tumekuwa tukilifanya mathalani hadi Februari mwaka huu takribani maeneo 87 yamefanyiwa kazi, maeneo 68 yalikuwa ya *TFS*, maeneo 12 yalikuwa ya *TAWA* na maeneo saba yalikuwa ya *TANAPA*. Huku tumeweza kuweka mipaka, tumeweza kuweka vigingi na kuainisha mipaka hiyo kwa wananchi wetu ili kuweza kuondoa migogoro. Vilevile katika eneo hili tumeweza kuweka vigingi vyenye urefu wa meta 1.5 katika umbali wa meta 500, jitihada hizi tutaendelea nazo kuhakikisha kwamba tunaweka vigingi hivi ili wananchi waweze kuyaelewa maeneo haya na waweze kutoingia kwenda kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa kwa upana sana na Kamati yetu na Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia hapa ndani ni migogoro kati ya askari wetu wa

hifadhi na wananchi. Nataka niseme kwamba tumelisikia jambo hili, ushauri tumeupokea, tutatumia maarifa yote kuhakikisha kwamba tunakomesha migogoro hii. Nataka niwape tu *comfort* kwamba katika kushughulikia suala hili tayari tumeanza kuchukua hatua kwa askari wetu ambao wamekiuka miiko ya kazi zao, wapo ambao tumewafukuza kazi, wapo ambao tumewachukulia hatua nyingine za kinidhamu na hatutasita kuchukua hatua kwa askari wote ambao watakiuka taratibu zinazotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeshauriwa kutoa elimu ya kina kwa wananchi kuhusiana na umuhimu wa hifadhi zetu lakini jinsi ya kuendana na maeneo haya, tunawaahidi elimu hii tutaitoa, tumekuwa tukifanya hivyo lakini sasa tutafanya kwa nguvu kubwa zaidi na katika bajeti yetu hii tumeonesha, tumetenga mafungu ya fedha kwa ajili ya kwenda kufanya kazi hii, tuwahakikishie kwamba tunaenda kufanya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo eneo la vitendea kazi limezungumziwa kwa ukubwa sana na tumeshauriwa kuwa na mpango mkakati wa kuweza kuajiri wafanyakazi kwenye taasisi zetu ili tuondokane na utaratibu wa kuwa na askari wa muda. Kwa sababu utafiti wetu umeonesha kwamba askari wetu wengi wa muda ndiyo hao ambao wanakiuka miiko ya taratibu zao. Napenda kushukuru Serikali kwamba imetutengea fedha katika bajeti hii, tunayo fedha ya kuajiri askari wapya, tunayo fedha ya kuendelea kutoa mafunzo kwa askari wa vijijini na jambo hili tunaenda kulifanya kwa sababu hata sisi hatufurahishwi na migogoro hii inavyooendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imetuelekeza vilevile kwamba *TAWIRI* wapatiwe fedha ili waweze kufanya sensa ya wanyama wakali na waharibifu lakini na wanyama wote katika maeneo yetu 11 ya ekolojia katika nchi hii. Nafurahi kusema jambo hili tumelifanyia kazi kwa kiwango kikubwa na kwamba fedha imetengwa kwa ajili ya kwenda kufanya sensa ya wanyama katika nchi yetu kwenye ekolojia zetu zote 11. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge muwe na amani fedha hii ipo imetengwa na *TAWIRI* wanaenda kufanya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo eneo ambalo limezungumziwa kwamba kutokana na wingi wa idadi ya watalii wanaokuja nchini, nchi yetu sasa inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vyumba vya malazi, vilevile miundombinu kwenye maeneo yetu mengi imeharibika. Nataka kuwahakikishia kwamba jambo hili na lenyewe tumeliangalia kwa upana wake kwenye bajeti yetu lakini Kamati imekwenda mbali zaidi, imeshauri kwamba zile *hotel* ambazo zilikuwa zinamilikiwa na Serikali, ambazo wawekezaji wale wamekiuka masharti Serikali ichukue hatua za kurejesha *hotel* hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie kwamba Serikali imeanza kufanyia kazi jambo hilo. Tayari hoteli moja imerejeshwa lakini baada ya kurejeshwa aliye nyang'anywa hoteli ile amefungua kesi. Kwa hiyo tunahitaji umakini mkubwa katika kufanya jambo hili, tunaomba twende sote kwa pamoja tushirikiane kwenye jambo hili, tusije kwenda kwa jambo hili kwa pupa tukajikuta kwamba nchi yetu inaingizwa kwenye kesi na kulazimika kulipa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo kamati imelizungumza kwa nguvu kubwa ni kukiwezesha Kituo chetu cha *DDMCC* kiweze kufanya kazi inayokusudiwa. Nafurahi kusema kwamba tumelisikia jambo hili na Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kituo hiki na kwamba yale yaliyopendekezwa na Kamati yetu tumeyazingatia na Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha kule mbele basi tutaelewana kwenye eneo hili lakini nataka muwe na amani kwamba jambo hili tumelipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamezungumzia umuhimu wa kushughulikia au kuibua fursa nyingi za kiutalii, hususani kwenye maeneo ya utalii wa kiutamaduni na hili nalo tunaenda kulifanyia kazi. Yapo Mawazo mazuri sana tumeyapata humu ambayo tulikuwa tumeanza kuyafanyia kazi lakini Wabunge wametuboreshea fikra mpya ya eneo hili. Tuwahakikishie tunaenda kuifanyia kazi kwa sababu lengo letu sote ni kuhakikisha malengo yetu ya kuwa na idadi ya watalii milioni tano katika nchi hii tunayafikia. Niombe tuendelee kushirikiana, tuungane mkono ili jambo hili liweze kufanikiwa,

tukifanikiwa kwenye hili maana yake tunakuwa tumefanikiwa kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamehoji. Kumekuwa na maeneo ambayo maeneo ya wananchi yanatakiwa kuchukuliwa, kumekuwa kukifanyika mazoezi ya kufanya tathmini ili fidia itoke. Maeneo mengi tumekamilisha tathmini hizi lakini tunachelewa kulipa kwa sababu wakati mwingine wananchi wanakwenda kukata rufaa kufungua kesi kupinga maamuzi yale. Sasa kesi zinapotokea mnakuwa hamna jinsi manasubiri matokeo ya maamuzi ya Mahakama ili tuweze kwenda pamoja. Dada yangu Mheshimiwa Esther umeuliza jambo hili kwa uchungu mkubwa, nataka nikuhakikishie kwamba jambo hili tunaenda kulifanyia kazi ili tuhakikishe kwamba wananchi hawa na wengine katika maeneo mengine wanalipwa stahiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayo changamoto ambayo kama wabunge sasa tukae tuwaelimishe wananchi wetu. Tunapofanya tathmini hizi, tathmini hizi zinapofanyika na Mtathmini Mkuu wa Serikali zinafanyika kwa mujibu wa sheria tulizonazo. Kwa hiyo viwango vile ni kwa mujibu wa sheria, kwa hiyo kwenda kulipa nje ya viwango vile ambavyo vimewekwa kwa mujibu wa sheria wakati mwingine inakuwa ni changamoto, inakuwa haiwezekani. Kwa hiyo nitoe rai, wote kwa ujumla wetu tusemezane kwenye eneo hili, wananchi waweze kulipwa fidia stahiki kulingana na sheria zinavyosema. Tukienda kinyume tukawalipa kinyume na sheria zinavyosema maana yake tunaenda kuzalisha tena mgogoro mwingine wa kikanuni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hii hoja ya Mheshimiwa Ole-Sendeka kwa sababu Mheshimiwa Waziri anakuja kuhitimisha hapa na asije akalazimika kumjibu Mheshimiwa Mbunge, mimi nimeipitia kwa haraka na nimempatia Mheshimiwa Waziri anasema yeye hii taarifa

haifahamu hana taarifa nayo na ilivyoandikwa hapa Januari 2024 yeye hajawasilishiwa taarifa hii.

Sasa kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri maana yake kila kilichopo humu Mheshimiwa Ole-Sendeka kama kipo kule vijijini, kipo wilayani, kipo popote kilipo Wizara ya Maliasili na Utalii haihusiki. Kama nimeelewa vizuri Mheshimiwa Waziri, haihusiki kwa sababu huku ndani zimetajwa taasisi mbalimbali huku kwenye hii taarifa ya Mheshimiwa Ole-Sendeka. Zimetajwa taasisi ambazo zilihusika na kufanya haya na huku zipo na picha ambazo zimewekwa za ushirikishwaji wa wadau na wale wanaohusika maafisa wapo mbele pale lakini sasa inaonekana hii itakuwa ilijitengeneza kwa sura ambayo kwa kweli Serikali haina taarifa nayo. *(Makofi)*

Sasa kwa kuwa Serikali haina taarifa na jambo hili kuna namna mbili na kwa sababu Serikali haina taarifa lakini taarifa yenyewe inaonekana ni ya Serikali lakini kwa kuwa Serikali imeikana hii taarifa Mheshimiwa Ole-Sendeka nafikiri maadamu Serikali imeikana humu ndani, Bunge haliwezi kushughulika nayo taarifa hii isipokuwa na wewe pia sasa ukae nalo kama Mbunge kwamba taarifa hii Serikalini haipo na kwa hivyo mipango iliyotajwa humu yote haipo Serikalini. Nadhani umenielewa Mheshimiwa Mbunge ili usije ukaanza kuuliza maswali sasa yanayotokana na taarifa hii, umenielewa Mheshimiwa Ole-Sendeka? *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nimekuelewa nilikuwa nasema tu je, inatosha najua wewe ndiyo una *rule out* mwishoni lakini je, hatuwezi kupata *commitment* ikaingia kwenye *Hansard* ya Mheshimiwa Waziri ili kuikana hiyo taarifa ili watu wapate amani kule maana hali iliyopo kule ni mbaya, mbaya sana, tukishapata hiyo basi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa nafikiri maelezo ya awali alipotoa taarifa kwako ndicho alichomaanisha labda kama ni tofauti na hicho, nitampa nafasi aseme kabla sijamwita kuhitimisha hoja lakini nilivyomwelewa wewe wakati unasema kuhusu taarifa hii na taarifa aliyokupa wewe kwamba taarifa hii haijui na haitambui nafikiri alimaanisha hivyo

Mheshimiwa Waziri ama kuna jambo la tofauti ili uwe umelijibu kabla ya kuhitimisha hoja yako hapa mbele. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo haijasainiwa, taarifa hiyo na mimi niliiona kwenye mtandao wa *WhatsApp* wa Wabunge wa CCM. Ndiyo maana nikasema kwa taarifa rasmi hata kama kuna mchakato wa Kiserikali kuna taratibu zake, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya kuna taratibu zake. Jambo kama hilo kama lipo na kuna maamuzi yamefanyika mchakato wake utafikiwa, ndiyo maana nikasema Mheshimiwa Mbunge asilete taharuki kwa taarifa ambayo Wizara haijaitoa, naomba kuwasilisha. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimelazimika kusimama, taarifa hii karatasi ya juu ni kweli mtu anaweza kuwa ametoa kwenye mtandao nembo ya Serikali lakini imeandikwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii, taarifa ya awali ya tathmini ya mapori tengefu ya Kaskazini kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Januari 2024. Huku mbele haina kurasa, huku mbele kuna sehemu inasema kuundwa kwa timu ya kisekta, kutokana na hitaji hilo ambalo wamelitaja huku mwanzo, hitaji hilo la kufanya tathmini ya mapori tengefu Serikali iliunda timu ya wataalamu wa kisekta inayojumuisha wajumbe kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya *RAS* Manyara na Arusha, Ofisi ya Kamishina wa Ardhi Manyara na Arusha, Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya za Simanjiro na Monduli.

Njia zilizotumika kufanya tathmini, Waheshimiwa taarifa ni ndefu kidogo. Sasa Mheshimiwa Waziri, mimi yaani hii hoja ingekuwa imeisha ungesema hivi taarifa hii labda Serikalini bado hamjaifanyia maamuzi mnaendelea kuichakata lakini maelezo unayoyatoa ni kana kwamba hii taarifa haipo. Kama haipo sisi tuifute hapa kwamba haipo, kama itakuja ije basi mtaanza upya zoezi hili ama kama sivyo basi urekebishe maelezo yako kwamba taarifa hii mliwapa wataalamu, wataalamu hawajaileta bado kwenu, kwa kuwa hawajaileta bado kwenu mnaishangaa ipo huku nje kwa hivyo mnasubiri bado wataalamu

wawaletee taarifa. Kama hivyo sivyo sisi hapa ndani tuifute hii kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameileta na anaeleza maana yake itaingia kwenye *Hansard* wakati Serikali haina hii taarifa na haijamtuma kwa kweli mtu yeyote kwenda kufanya kazi hii, kama imemtuma semeni tumemtuma hatujapata bado taarifa hii kiofisi, kama hamkumtuma semeni hamjamtuma tujue hawa ni matapeli tufute taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, ndani ya Serikali kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, zipo taratibu ambazo zinatuongoza ili ku-*own* taarifa na kuziwasilisha ndani ya Bunge lako Tukufu. Alipozungumza Waziri wa Maliasili mwanzo aliweka wazi jambo hili, kama taarifa bado haipo kwenye mikono yake hiyo bado siyo taarifa rasmi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukiitazama taarifa yenyewe na kazi inayofanyika ni kazi ambayo inahitaji sekta kadhaa ambazo ni lazima zikae pamoja ndipo ziweze kufanya kazi kuwa na maamuzi na kuyawasilisha ndani ya Bunge lako Tukufu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri tusaidie, timu hii imewahi kuundwa? Ama haijawahi kuundwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwenye Ofisi yetu ya Waziri Mkuu, ambayo tunashughulika na uratibu wa timu hizo za pamoja na timu zinazosimamia mambo haya, bado haijafika kwetu na wala hatujawahi kuiunda kwa utaratibu huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kufika taarifa ni suala moja, timu imewahi kuundwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, hatujaunda timu hiyo.

**SPIKA:** Hamjaunda timu hii.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, sisi ndani ya Serikali kwa maana ya uratibu wa kuweza kuweka jambo hili likae sawa sawa, hatujawahi kuiunda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, timu hii imewahi kuundwa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nimeingia katika Wizara hii mwezi wa Tisa na mpaka Januari hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge, ametoa wasilisho lake mimi nilikuwa sijaunda timu hiyo, ndiyo maana nasema kama kuna tathmini zinaendelea kuna taratibu zake, ndiyo maana tukaendelea kumuomba Mheshimiwa Mbunge, kama likifanyiwa maamuzi na kama kitu hicho kipo, kitaletwa kwa utaratibu mahsusi wa Serikali na kama alivyoeleza Mheshimiwa Jenista pale, tunaomba Kiti chako ukituridhia jambo hili Mheshimiwa Mbunge alikubali kwamba si rasmi na kama hata lipo kwa sasa si rasmi.

**SPIKA:** Hee, haya jamani, haya maelezo yanayotolewa hayanisaidi mimi kufanya maamuzi hapa mbele. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, mimi ninaliomba sana Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Ole-Sendeka amesema, toka mwanzo Waziri ameliweka vizuri, hebu sisi tuendelee na haya mambo yote Serikalini na kama jambo hili lipo litaletwa rasmi na Watanzania watapewa taarifa rasmi.

Mheshimiwa Spika, tukiliacha hivi kama lilivyo kwa taarifa ambayo Serikali kupitia Wizara inasema siyo taarifa ya Wizara, tutatengeneza taharuki ambayo haipo. Alichosema Mheshimiwa Ole-Sendeka ni kutaka kuondoa taharuki, Waziri ameshasema kwamba jambo hili halipo. Kwa hiyo, tunaomba tu jambo hili lisiwe ni sehemu ya

kuliamulia humu ndani kwamba lipo na wakati Serikali imeshasema bado halipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Waziri wa TAMISEMI yupo hapa? Haya Mwenyekiti wa Kamati naona umesimama. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA- MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nimesimama tu nilisaidie Bunge lako, inawezekana maelezo anayoyasema Mheshimiwa Waziri ni sahihi kwamba, kama Serikali hawajafika mahali pa kuleta hilo jambo hapa ndani lakini sisi kwenye Kamati tunajua mambo mawili. Jambo la kwanza, wakati wa uwasilishaji wa bajeti ya mwaka 2022/2023 Waziri akiwa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Serikali ilitamka Bungeni kwamba ina kusudio la kufanya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, mwaka jana 2023 tulikuwa na mgogoro wa watu - wawekezaji wenye hoteli kwenye eneo la Mto wa Mbu, ambao wanatozwa tozo kwa eneo lile kama eneo la pori tengefu wakati wanaona limepoteza ile hadhi. Tulipozungumza na Serikali walituahidi kwamba, ipo timu inayofanya tathmini ya haya mapori tengefu ikikamilika watatuletea kwenye Kamati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ole-Sendeka, naomba uketi.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Sawa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimepokea barua hapa kutoka kwa Mheshimiwa Ole-Sendeka, hii barua imeandikwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Simanjiro, Ndugu Gracian Makota, sijui Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, huyu bado ni Mkurugenzi wa Simanjiro, Ndugu Gracian Makota bado ni Mkurugenzi?

Mheshimiwa Naibu Waziri, hebu nenda kidogo hapo nje mpigie simu muulize kuhusu hii barua ambayo aliwaandikia, nakuleta hii barua ili wewe ukamuulize. Barua imeandikwa kwa Afisa Mtendaji wa

Kijiji cha Olchoronyori tarehe 19 Juni, 2023. Tathmini ya maeneo yenye rasilimali za wanyamapori katika mapori ya Simanjiro - Naberera na Simanjiro - Kitiangare. Mkurugenzi akaseme aliandika hiyo barua au hapana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuelewane kwa sababu jambo hili bado sijaweza kulifanyia maamuzi kwa maelezo ninayoyasikia kutoka upande wa Serikali. Kwa sababu hiyo, naomba tuendelee na ratiba yetu, hili jambo tulipeleke mwishoni. Nadhani tumeelewana Waheshimiwa Wabunge? Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii kwa ajili ya kuhitimisha hoja yangu ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kipekee na kwa moyo wa unyenyekevu mkubwa niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini kusimamia Wizara hii. Ninampongeza Mheshimwia Rais, kwa namna anavyoendelea kuiongoza nchi yetu kwa umahiri mkubwa kwa amani, upendo na utulivu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru wewe binafsi kwa namna ambavyo umewezesha mjadala wa hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka huu wa fedha. Niendelee kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa namna ambavyo wamechambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara yetu kwa mwaka 2023/2024, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote walipata nafasi ya kuchangia kwa michango yao mizuri yenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara yetu. Vilevile, kuhakikisha kwamba sekta ya maliasili na utalii inaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Spika, Wizara imepokea na kuchambua michango kutoka kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, lakini pia kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge 58 ambapo kati ya hao Wabunge 56 wamechangia kwa kuzungumza na Wabunge wawili wamepata nafasi ya kuweza kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge, wote waliotoa maoni pamoja na Kamati yetu kwamba, maoni na ushauri wenu utazingatiwa katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia inapokea ushauri na maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote. Hoja na maswali ya Waheshimiwa Wabunge, yamejikita katika masuala mbalimbali ya Wizara. Ninaomba sasa ikikupendeza niweze kuwasilisha ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizowasilishwa na Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kamati kulikuwa kuna hoja ya kuboresha Kanuni na viwango vya fidia, kifuta machozi kwa wananchi kutokana na madhila mbalimbali yanayojitokeza kutokana na Wanyama wakali na waharibifu. Kuona namna ya kuzingatia hali halisi ya maisha na thamani ya uharibifu au madhara ambayo yametokea.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu tarehe 31 Mei, mwaka huu 2024, niliweza kutoa tangazo la Serikali Na. 440, kwa ajili ya kufanya marekebisho katika Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, katika marekebisho hayo tumeweza kufanya marekebisho kwa kuongeza viwango kwa asilimia 100 kwa majeraha ya kudumu pamoja na vifo vya binadamu. Vilevile, tumeweza kuongeza kwa 50% majeraha ya muda, uharibifu wa mazao pamoja na vifo kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii nipende tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, tumeanza na hatua hizi za awali tuweze kuona aina ya matukio na idadi yanavyojitokeza badala ya kwenda ghafla kwa kuongeza viwango vikubwa sana kabla hatujaona hali halisi ya ulipaji ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, watukubalie kwa sasa na bahati nzuri kwa kuwa Kanuni Waziri anakuwa na uwezo nao naiona hoja yenu Waheshimiwa Wabunge wote ni kweli kwa viwango hivi kutoka 1,000,000 kwa kifo kwenda kwa 2,000,000 bado haitoshi kuweza kufidia thamani halisi ya binadamu. Kwa hiyo, napenda tu kusema kwamba naiona hoja yenu Waheshimiwa Wabunge kabisa na ndiyo maana tukasema tuanze na viwango hivyo na ninamshukuru Waziri wa Fedha, kwa namna ambavyo Wizara yake iliweza kuridhia, lakini ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na kuendelea kutoa pole kwa wananchi wote na ndugu wote ambao wameweza kupata kadhia hii na kuweza kupoteza ndugu zao wapendwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja kwamba kwa kwa mazao yanayopungua ekari moja huko nyuma ilikuwa hailipwi, ninapenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge katika marekebisho haya niliyoyafanya kwa kutambua hilo hilo kwamba si kila mmoja ana uwezo wa kulima zaidi ya ekari moja. Kwa hiyo, tumeweka marekebisho na kwa sasa hata kama mtu ana pungufu ya ekari moja ataweza kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine ya Kamati kuhusiana na kurejeshwa kwa fedha za *WMA* ambazo zinadaiwa na jumuiya. Ninapenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati na Wabunge wengine waliochangia wamekuwa wakiifuatilia sana

hoja hii, napenda kuwahakikishia Kamati kwamba, tunaendelea kuhakikisha tunalipa fedha hizi na fedha zote zilizobakia tunaamini itakapofika tarehe 30 Juni, Wizara ya Fedha imetuahidi zote zitakuwa zimelipwa kwa wanufaika wa *WMAs'* hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba mfumo sasa badala ya fedha kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali za *WMA, TAWA* waweze kupewa na kuzirejesha moja kwa moja kupitia *WMA* zetu. Niishukuru sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na uongozi mzima wa Wizara ya Fedha walitukubalia, tunashukuru kwa uongozi wako, tulivyokuwa tukifanya mashauriano wakati wa Kamati ya Uongozi na Bajeti na suala hili tuliweza kulieleza vizuri na tutakapoanza tarehe 01 Julai, basi kwa hakika utaratibu huu utarudi kama ilivyokuwa zamani na itatuwezesha kuweza kuwalipa *WMAs* fedha zao kwa wakati ili waweze kuendeleza *WMAs'* zao waweze kuendeleza ulinzi, vilevile kuweza kuendeleza uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kuona ni kwa namna gani tunaendelea kutangaza au kuibua vivutio mbalimbali. Nipende kuwahakikishia Wajumbe wa Kamati, tutaendelea na mikakati mbalimbali ya kutambua na kutangaza vivutio vingine vya utalii. Vilevile, tunaendelea kushirikiana na Mikoa pamoja na Halmashauri zetu na kama Wizara kupitia bajeti ijayo ya mwaka 2024/2025 tumetenga fedha kwa ajili ya kushirikiana na Mikoa mbalimbali kwa ajili ya kuweza kubaini vivutio vipya.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye hoja nyingine ambazo Wajumbe wa Kamati walipendekeza na hasa katika suala zima la mgawanyo wa fedha zile nyongeza ya shilingi bilioni tisa, natambua suala hili lipo mezani kwako, Kamati wameweza kuwasilisha *addendum,* pia sisi tuweza kuzingatia na kutambua mapendekezo mazuri ambayo Kamati imeweza kuyaona kupitia Wajumbe wa Kamati na wengine wote walioweza kuchangia. Kwa hiyo, kama Serikali na kama Wizara tumeweza kufanya marekebisho na tumewasilisha *addendum* mezani kwako. Niwashukuru Waheshimiwa

Wajumbe wa Kamati, tunaamini nia ni nzuri na lengo ni kuona kwa namna gani sekta hii inaendelea kuimarika na kukuwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine ya Mheshimiwa Olelekaita pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine ambao walitamani kujua fedha hizi za *WMA* zinaendelea kutoka kwa wakati. Kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Priscus Tarimo pamoja na Mheshimiwa Cecilia Paresso na haswa kuhusiana na ada ya leseni ya biashara za utalii au *TTBL* kwa upande wa mawakala wa kupandisha watalii milimani, ilipendekezwa kutoka dola 2,000 iweze kupunguzwa hadi dola 1,000.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Priscus Tarimo na Mheshimiwa Mrisho Gambo, nilipata nafasi ya kufanya kikao na Waongoza Utalii na niliridhia mapendekezo yao ikiwa ni pamoja na hili la kupunguza ada hii ya wanaopandisha watalii Mlimani kutoka dola 2,000 badala ya kwenda dola 500, tulikubaliana tuanze na dola 1,000 kwanza, wakati tunaendelea kuangalia hali inavyokwenda. Mabadiliko haya yataanza Julai, 2024 kabla ya mwaka wa fedha haujaisha nitatoa mabadiliko au marekebisho katika Kanuni zinazosimamia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine kwamba, wafanyakazi wanaofanya kazi katika hifadhi zetu hasa kwa wale wanaotoa huduma mbalimbali kwamba, wamekuwa wakilipishwa viingilio na kwamba, utaratibu uweze kuangaliwa upya. Kwa upande wa wafanyakazi wote ambao wanafanya kazi katika kambi za kudumu, *lodges* lakini na zile *permanent camps* hawa hawatozwi viingilio vyovyote, lakini kwa magari yanayotumika katika huduma za malazi pia wamekuwa hawatozwi gharama yoyote ya viingilio, isipokuwa wanalipa tozo ya mwaka mara moja kwa kuzingatia ukubwa wa gari.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuisikia hii hoja na kwa kutambua kwamba, wengi ambao wamekuwa wakilipishwa ni wale ambao wanaenda katika *seasonal camps* ni hoja ambayo pia tumeipokea na tutaenda kuiangalia kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na kuna hoja ya ada ya leseni ya biashara za utalii *TTBL* kwa Waongoza Utalii au *Tour Guide* na ilikuwa inapendekezwa kiwango hiki huwa kililikuwa kinatozwa ni dola 50 kwa mwaka. Mapendekezo ya Mheshimiwa Mrisho Gambo, ilikuwa kwamba ada hii itozwe kwa miaka mitatu na iwe ni kiwango cha shilingi isiyozidi 70,000.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, nipende pia kusema hoja hii ilikuwa ni moja ya hoja pia ambayo ilijitokeza nilipokutana na Chama cha Waongoza Utalii na katika makubaliano yetu tulikubaliana kwamba, kwanza, tutaanza kutoza ada hizi kwa shilingi za kitanzania, lakini la pili tutaipunguza badala ya kwenda shilingi 70,000 itakuwa ni shilingi 100,000 na tozo italipwa 100,000 na itadumu kwa miaka mitatu. Kwa hiyo, tumeweza kuizingatia kwamba, italipwa kwa miaka mitatu au itadumu kwa miaka mitatu, lakini itakuwa ni kwa shilingi 100,000.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hoja pia ya upungufu wa huduma za malazi, nipende kuendelea kuwahakikishi Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mkakati wetu wa kuona ni kwa namna gani tunaongeza idadi ya vitanda. Vilevile, tunaendelea kupongeza wale wote ambao wamewekeza katika sekta yetu ya utalii. Kwa kuweka hoteli za aina mbalimbali na nyota mbalimbali na kama Serikali tumeendelea kupunguza gharama haswa kwa upande wa ada za leseni kwa wale ambao wanafanya shughuli hii.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea pia kuandaa makongamo mbalimbali kwa ajili ya kuweza kuvutia Wawekezaji watakao wekeza katika huduma za malazi. Vilevile, kwa upande wa *TANAPA* pamoja na Ngorongoro na Taasisi zetu nyingine za uhifadhi na kwenyewe pia wamendelea kuvutia Wawekezaji katika maeneo ya hifadhi ili watu waweze kuja kuwekeza kwa ajili ya kuongeza idadi ya vitanda.

Mheshimiwa Spika, tumendelea pia kuboresha au kujenga viwanja vya ndege, kwa sasa tunaendelea na ujenzi wa viwanja vya

ndege vinne kwa upande wa Mikumi, kwa upande wa Nyerere, vilevile kwa upande wa Hifadhi yetu ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia ili kuhakikisha kwamba, tunaenda na soko letu la utalii, pia kuhakikisha kwamba, huduma inayotolewa inaenda na viwango vinavyohitajika na watalii wanaokuja nchini. Tumeendelea vilevile kuboresha vyuo vinavyotoa taaluma ya utalii na ukarimu ikiwe Chuo chetu cha Taifa cha Utalii, Chuo chetu cha Mweka. Vilevile, Kituo chetu cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga ili kuendelea kuhakikisha kwamba, tunazalisha wataalamu wenye weledi, lakini watakaokidhi mahitaji ya soko, kwenye eneo hili nimesikia Wabunge wengi wakilizungumzia akiwema Mheshimiwa Martha Gwau, vilevile Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara na Wabunge wengine ambao wamelisemea kwa uzito mkubwa, tutaendelea pia kuongeza wigo wa mazao ya utalii kwa kufungua maeneo mapya yenye vivutio vya utalii ikiwemo kusini ili kuleta mtawanyiko mzuri zaidi wa watalii katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja pia nadhani ilikuwa ya Mheshimiwa Mrisho Gambo, ambaye alitamani kujua ni faida gani ambazo zimepatikana kutokana na tozo ya *TDL* ya kuendeleza utalii. Nipende kumhakikisha Mheshimiwa Mrisho Gambo na Waheshimiwa Wabunge, wengine tozo hii imekuwa ya manufaa makubwa sana na ukiangalia imeweza kufanya kazi kubwa sana katika kuongeza idadi ya utalii. Kupitia kazi iliyofanyika ya kuboresha huduma za malazi katika sekta ya utalii, wataalum wetu wameweza kupata nafasi kupitia *TDL* kuweza kupanga sehemu za huduma za malazi katika viwango vya ubora wa nyota, hadi sasa wameweza kupanga huduma za malazi takribani 308 kuanzia nyota moja hadi nyota tano.

Mheshimiwa Spika, vilevile, tumeendelea kupitia tozo hii ya *TDL,* kuweza kuitumia katika kuimarisha mafunzo katika Chuo chetu cha Taifa cha Utalii na haswa katika fani za utalii na ukarimu kwenye ngazi ya cheti na *diploma*. Wanafunzi wanaodahiliwa kiwango

kimeongezeka kutoka wanafunzi 311 hadi kufikia wanafunzi 550 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, pia kupitia tozo hii tumeweza kubaini vivutio vipya vya utalii ili kuweza kupanua zaidi wigo wa mazao ya utalii nchini na kupunguza utegemezi wa utalii wa wanyamapori. Vilevile, tumeweza kuitumia tozo hii ya kuendeleza utalii ya *TDL* katika kuimarisha ukusanyaji wa takwimu kwa wakati lakini pia kufanya utafiti wa watalii ambao wamekuwa wakija nchini na pindi wanapoondoka nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia kuna hoja ya maslahi ya wapagazi na wapishi yaweze kuangaliwa. Nipende kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Priscus Tarimo na wengine tunapokea ushauri huu na tayari Wizara ya Kazi, Wakala wa Usafiri wa Utalii *(TATO)* pamoja na *TLTO* waliweza kukaa na Wizara ya Kazi na kuweza kuona ni nini kiweze kufanyika katika kuboresha maslahi ya wapagazi.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuanzia Januari 2025, Wizara ya Kazi imeshashauriana na *TATO* na wadau wetu waongoza watalii pamoja na wapagazi na wapishi. Tunaamini viwango kamili vitaweza kutolewa kwa ajili ya ujira wa wapagazi hawa, wapishi na vilevile kuangalia kwa upande wa waongoza utalii ni nini haswa kinaweza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Festo Sanga na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao walitamani kujua baada ya kurudisha utaratibu wa Ngorongoro na *TANAPA* kuweza kubakisha fedha na kuweza kuzitumia kwa ajili ya shughuli zao na kuendeleza miundombinu ya hifadhi endapo fedha hizi zitatumika ipasavyo lakini kuona ni kwa namna gani kutakuwa na udhibiti ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kumhakikishia Mheshimiwa Sanga na Waheshimiwa Wabunge wengine wote tunapokea ushauri huu, tutauzinagtia na tutaendelea kukiimarisha kitengo chetu cha ukaguzi

wa ndani Wizarani lakini pia katika Taasisi yetu ya *TANAPA* na Ngorongoro na Taasisi zingine. Pia, tutashirikisha kitengo chetu cha ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha kwamba tunadhibiti matumizi. Sambamba na hilo tutahakikisha taasisi husika pia zinaimarisha mifumo yake ya ukusanyaji wa mapato lakini pia matumizi ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja kuhusiana na kuboresha mfumo wa malipo ya kifuta jasho. Tumeanza majaribio katika Halmashauri za Wilaya 10 kupitia mfumo wetu wa *Problem Animal Information System.* Tunaamini mfumo huu utaweza kutusaidia kuleta ufanisi zaidi ili tuweze kupokea taarifa za matukio yanayojitokeza kwa mfumo wa kielekroniki.

Mheshimiwa Spika, tunaanza na halmashauri hizo 10 na tutaendelea kuboresha kwa kadri tutakavyoona yale ambayo tutayabaini katika halmashauri hizo. Pia, tunajua mchakato ni mrefu sana, nako pia tutaendelea kuupitia ili kuweza kuuboresha na kuweza kupunguza hatua zinazotakiwa kutekelezwa au kufikiwa mpaka mtu anapoweza kupata malipo yale ya kifuta jasho na kifuta machozi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya *WMAs* mbalimbali. Wananchi wamekuwa wakiwasilisha mapendekezo ya kuanzishwa *WMAs* mpya tukitambua umuhimu wa *WMAs* hizi katika kushirikishwa lakini pia katika suala zima la uhifadhi wa wanyamapori lakini vilevile na namna ambavyo wananchi wanaweza wakanufaika na rasilimali hizo. Nipende kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kufanyia kazi na muda si mrefu zile ambazo zinasubiri kuidhinishwa basi zitakuwa zimeidhinishwa ndani ya muda si mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Daimu Mpakate na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali hasa katika maslahi ya askari wetu wa Jeshi la Uhifadhi kuona ni kwa namna gani katika taasisi zetu ndani ya Wizara ya Maliasili pasiwe na kupishana sana katika viwango mbalimbali vya mishahara. Nipende kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tumepokea ushauri huu, tutaendelea kulifanyia kazi suala hili ili kuhakikisha kwamba tofauti zinaondoka za mishahara kwa askari wetu na haswa ukitambua kwamba wote

wanafanya kazi ambayo ni ngumu na nzito na ni muhimu sana nafasi yao katika suala zima la uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa Ofisi ya Rais Utumishi ili kuona ni kwa namna gani suala hili litaweza kuhitimishwa ili kuwa na mishahara ambayo inafanana. Pia, kulikuwa kuna hoja ya malipo ya *VGS* kwa wakati. Nipende kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tutafuatilia kwa upande wa kule Tunduru Kusini na katika maeneo mengine kwa wale ambao wanadai posho mbalimbali ambao hawajalipwa na tutaweza kupeleka mapema kabla ya mwaka wa fedha haujakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Shally Raymond kwa namna gani tunashirikisha wanawake katika kuwapatia fursa mbalimbali za utalii. Vilevile, hoja hii ilijitokeza kwa Mheshimiwa Janeth Mahawanga pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine. Nipende tu kulihakikishia Bunge lako kupitia Chama cha Wamiliki wa Kampuni za Utalii Wanawake *(TAUTO)* lakini vilevile Chama cha Waongoza Utalii Wanawake na vikundi mbalimbali tutaendelea kuwashirikisha katika makongamano na mikutano mbalimbali ili waweze kujua fursa mbalimbali ambazo zipo katika utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hilo tu na katika maliasili ikiwemo suala zima la ufugaji nyuki na uongezaji thamani asali, tukitambua kwamba ni maeneo ambayo yana mnyororo mrefu lakini pia yanachangia katika pato la Serikali, yanatuletea fedha nyingi za kigeni na pia yana mchango mkubwa wa kuongeza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Margaret Sitta kuhusiana na malipo ya *WMA* yake ya Uyumbu. Nipende kumhakikishia kama nilivyojibu katika majibu yangu ya awali, wale wote ambao wana madeni kupitia *WMA* zao wanatudai kama Serikali fedha hizo ifikapo tarehe 30 Juni zitakuwa zimekwishalipwa.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Sitta ambaye alitoa pendekezo au alitoa ombi la wananchi wake hasa wafugaji nyuki kuweza kupewa eneo la takribani *square kilometer* 5.5

katika Hifadhi ya Mto Ugalla. Nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Margaret Sitta kwamba kwa mujibu wa Sheria za Hifadhi za Taifa hairuhusiwi kufuga nyuki. Hata hivyo tunaipokea hoja hii, tutaendelea kuichakata na kuweza kuona kama kuna eneo mbadala la kuweza kuwapatia ili wananchi wake waweze kuendeleza shughuli hizo za ufugaji nyuki tukitambua Wanaurambo na Wanatabora wamekuwa ni watu ambao wanafuga nyuki vizuri sana na imekuwa ikituingizia pato katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Sitta kuhusiana na ahadi ambayo ilitolewa kwa ajili ya kupeleka mashine ya kuchakata mazao ya nyuki. Nipende kumhakikishia Mheshimiwa Margaret Sitta kupitia mfuko wetu wa misitu kwa mwaka 2024/2025 tutaweza kununua mitambo ya kuchakata mazao ya nyuki na tutaisimika katika jengo alilolipendekeza la kikundi hicho ili kuweza kuinua uchumi wa wananchi wake na kuweza kuimarisha uhifadhi wa misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja kuhusiana na Mgogoro wa Msitu wa Tongwe Mashariki ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Moshi Kakoso. Natambua faida na manufaa ambayo walikuwa wakiyapata kama halmashauri. Nipende kumhakikishia Mheshimiwa Kakoso, Kamati ya Wataalamu inakamilisha utaratibu na mchakato wa kisheria wa marekebisho ya mipaka na wadau wameweza kushirikishwa vizuri. Tunaamini muda si mrefu utakapokamilika ndani ya miezi michache basi wataweza kujulishwa na wataweza kurudia katika kazi za awali ambazo walikuwa wakizifanya.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Amsabi ambaye alipendekeza Wizara kuchukua jukumu la udhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwani Halmashauri za Wilaya hazina uwezo. Nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kama Wizara ya Maliasili na Utalii tutaendelea kushirikisha halmashauri zote nchini haswa katika zoezi la kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Tutaendelea kutoa mafunzo, tutaendelea kutoa vifaa vya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kuwa lengo letu kama Serikali ni kuwafikia wananchi

wote kwa haraka katika kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha udhibiti wa wanyamapori kwa mwaka ujao wa fedha 2024/2025 tumepanga kununua pikipiki 39 kwa ajili ya Maafisa Wanyamapori wa Wilaya na Askari wa Jeshi la Uhifadhi ili kuweza kuwaongezea ufanisi zaidi haswa wanapofanya doria za mwitikio wa haraka.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo katika bajeti ijayo tumepanga kujenga vizimba 50 kwa ajili ya kuzuia mamba na viboko katika wilaya mbalimbali nchini. Pia, tutaendelea kuwatumia ipasavyo askari wetu wanyamapori wa vijiji ambao kwa kweli tunawashukuru sana kwani bila wao zoezi hili lingekuwa ni gumu sana na wakati wote katika mwitikio wa haraka wamekuwa tayari kuweza kushirikiana na wananchi na Serikali katika kutatua kadhia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tutaweza kununua helikopta mbili, tutanunua mikanda 100 ya mawasiliano kwa ajili ya kufuatilia mienendo ya tembo na pia tutachimba mabwawa 30 ndani ya hifadhi zetu ili kuwezesha wanyamapori kutumia muda mwingi zaidi ndani ya hifadhi hususan katika kipindi ambacho kuna upungufu wa maji wakati wa kiangazi na hatimaye tunaamini hii itatusaidia sana kupunguza tembo na wanyama wengine wakali kutoka nje ya hifadhi kutafuta maji na kuleta madhara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Deo Mwanyika na ameeleza vizuri kuhusiana na mpango ule mkakati ambao tunao kama Serikali hasa katika kuongeza thamani katika mazao ya misitu iliyohandisiwa *(EWP)*. Niendelee kumhakikisia Mheshimiwa Mwanyika eneo hili tunaendelea kulifanyia kazi lakini pia kwa upande wa mazao ya vinia pamoja na mazao mengine ya misitu ambayo tumekuwa tukiendelea kutoa vibali.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba ni kweli mwezi Juni nyongeza ile ya muda kuweza kupeleka nje mazao hayo inaisha. Kwa hiyo tutaendelea kulipitia kwa ujumla na tutashirikisha wadau wetu.

Lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kulinda wazalishaji wa ndani lakini vilevile kuweza kufanya vikao mbalimbali na taasisi za kifedha ili kuona ni kwa namna gani sasa wanawawezesha pia wawekezaji wa ndani wanaojishughulisha na mazao ya misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Martha Gwau ambaye alitamani kuanzisha madawati mbalimbali au Maafisa Waambata katika Balozi zetu ili waweze kuendelea kuhamasisha zaidi masuala yetu ya utalii. Pia, waweze kutangaza zaidi vivutio vya utalii vilivyomo nchini mwetu, kwani ukitambua kwamba haya ni masoko muhimu ya utalii. Tumeanza hatua hizi kupitia taasisi yetu ya Bodi ya Utalii na Wizara ya Mambo ya nje. Kwa kuanzia tumeanza na Ofisi yetu ya Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza ambao wameshaajiri Afisa Dawati la Utalii na tunaamini pia katika masoko mengine na Balozi zetu Marekani na kwenyewe pia wataweza kulifanyia kazi suala hili na tunashukuru kwa mchango huu mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, kulikuwa kuna hoja nyingine ya kuboresha huduma kwa wateja na hasa watalii wetu lengo likiwa ni kwamba watalii wetu badala ya kuja mara moja basi waweze kuja mara nyingi, anapokuja mwaka huu ikiwezekana pia na mwaka kesho aweze kuja. Kwenye eneo hili alitolea pia ushauri kuona ni kwa namna gani *VETA* na vyuo vingine ambavyo navyo vinatoa mafunzo ya utalii tuweze kuvidhibiti na kuviratibu. Nipende kusema kuwa ushauri huo tunaupokea na tutaendelea kushauriana na kushirikiana na Wizara yetu ya Elimu ili kuhakikisha kwamba ubora wa elimu inayotolewa na *VETA* pamoja na vyuo vingine vinavyotoa mafunzo ya utalii basi viweze kuwa ni vya hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kulikuwa kuna hoja ya kuona ni kwa namna gani tunaendelea kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Elimu na nyinginezo. Nipende kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kushirikiana na Wizara yetu ya Elimu. Kwa kuanzia sasa hivi tunaanza mtaala wa masomo ya utalii kuanzia kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne. Vilevile kutakuwa na

mchepuo au tahasusi inayohusisha pia somo la utalii kwa kidato cha tano na kidato cha sita. Kwa sasa Wizara yetu ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Elimu tunaendelea kufanyia kazi mtaala huo na tunamshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais aliweza kuridhia mapendekezo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na mapendekezo ya kuona ni kwa namna gani Wizara, *TTB* pamoja na *TIC* tunaweza kushirikiana kwa kuona ni kwa namna gani tunaweza kuhamasisha vikundi vya wanawake na vijana kuweza kushiriki katika shughuli mbalimbali za utalii. Nipende kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kuwashirikisha katika maeneo yote ya maliasili na utalii ikiwemo pia hata katika programu yetu ile ya miaka 10 ya ufugaji nyuki ambayo tunaamini itaweza kuajiri zaidi ya wananchi 400,000 na itakuwa ni programu ya miaka 10.

Mheshimiwa Spika, tayari tuna matarajio kwa miaka hiyo 10 itatugharimu takribani shilingi bilioni 770. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tutawashirikisha katika programu hiyo na tutajitahidi kwa kadri tutakavyoweza wananchi katika maeneo yenu waweze kushiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Kabati ya kuona ni kwa namna gani maeneo ya malikale yanatumika vizuri na alitolea mfano wa gereza lile la Kihesa Mgagani. Pia, wengine wote akiwemo Mheshimiwa Kisangi na wengine tutaendelea kuona ni kwa namna gani tunayatambua maeneo mapya ya malikale lakini vilevile kuendelea kuboresha maeneo yote ya malikale ambayo tunayo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Mhagama kuhusiana na kuanzisha *WMA* ya Ifinga. Nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mhagama kwamba tumefikia katika hatua za mwisho na muda si mrefu tutaweza kukamilisha *Ifinga WMA*.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Mhagama alipendekeza tuweze kushirikiana na halmashauri yake na hasa kuweza kugharamia

*resource zone management plan*. Nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mhagama kwenye bajeti ijayo, Wizara ya Maliasili na Utalii tumetenga shilingi milioni 60 kwa ajili ya kugharamia nyaraka hiyo na nyaraka nyingine za muhimu ili kuiwezesha Jumuiya hii ya Ifinga iweze kufanya kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa lile eneo la *Industrial Processing Zone* ya *wood products* na lenyewe pia tutaendelea kukaa na halmashauri kuweza kuona ni kwa namna gani tutaweza kushirikiana ili kuhakikisha kwamba wanatekeleza wajibu wao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Kama ilivyo ada tutaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*.........................................Sh. 6,495,666,550

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na kuna majina mengi sana ya Waheshimiwa Wabunge hapa ambao wanaomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Sijui tutaweza kuyafikia mangapi lakini majina yapo mengi. Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu aliyotoa. Lakini bado ameongelea *EWP* kwa ujumla wake na hatua ambazo wanategemea kuzichukua, *focus* kubwa wakati nachangia na bado nina *concern* kubwa, nilikuwa nimeomba kuwe na mkakati mahususi wa haraka wa kwenda maeneo haya ambayo wakulima wadogo wa miti wanafanya biashara na kampuni za nje za Kichina ambazo kwa kweli zinaendelea kuwatia umaskini, na hiyo inatokana na kwamba biashara hii haipo *regulated* hata kidogo imeachwa kuwa kama soko huria na holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilimuomba sana Waziri, kwa sababu Wizara hii bado ina *mandate* ya kwenye mambo ya misitu na *concern* nyinyine kubwa ilikuwa ni kwamba kwa yanayotokea tunaendelea ku-*deport* miti, tunaendelea ku-*cause environmental degradation*, tunaendelea kuonesha kwamba hatuna upandaji wa miti ambao ni *sustainable* kwa sababu China au wawekezaji *interest* yao wamekaa wanangojea miti iletwe, ichakatwe iondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitegemea angetoa majibu mazuri zaidi ya kuonesha mkakati ambao wanaweza wakaufanya katika muda mfupi wa kuunda timu ndogo, kutuma kwenda kufanya *analysis* ya jambo hili kabla hawaja-*renew* vibali vya *EWP* kwa hawa wawekezaji wa Kichina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata majibu ya kuridhisha bado nitapenda kuomba Bunge lako lini-*support* katika hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea hoja ya Mheshimiwa Mwanyika, kama nilivyoeleza kupitia ule Mpango kazi wa *EWP*, tutaendelea kutekeleza lakini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwenye hili tutashirikiana na halmashauri husika katika eneo lake kusimamia na kuhamasisha matumizi endelevu ya malighafi ya magogo na vilevile kuhamasisha upandaji wa miti ili kuweza kulinda mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tutaona ni kwa namna gani tutaendelea kulinda maslahi ya wakulima wetu na haswa binafsi. Pia, tutahakikisha usalama na maslahi bora kwa wafanyakazi wanaofanya kazi katika viwanda hivyo anavyovielezea Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, suala hili tutalifanyia kazi na tutashirikiana na kumpatia taarifa ya namna tutakavyolitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ameketi kuashiria ameelewa. Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, Tanzania tunayo sera ya malikale ya Mwaka 2008 ambayo inatambua mabaki ya wanadamu na hata wanyama kama vile *dinosaur* ni sehemu ya urithi wa nchi yetu. Lakini kwa kiwango kikubwa baadhi ya malikale hizi ziko nje ya nchi ikiwemo Nchi ya Ujerumani na kwa maana hiyo Watanzania hatujaona kama tunanufaika na mali kale hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba malikale hizi ikiwa ni pamoja na Mjusi *Dinosaur* wa Ujerumani anarudishwa Tanzania? Naomba ufafanuzi na nisipopata maelezo ya kuridhisha kutoka kwa Serikali, nitaomba nitoe hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ninamshukuru Mheshimiwa Kassinge na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamekuwa wakifuatilia suala hili la urejeshwaji wa malikale na hata katika mchango wa Ijumaa, Waheshimiwa Wabunge wengi pia waliligusia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Kassinge na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba, kama mtakumbuka Mheshimiwa Rais wa Ujerumani alifanya ziara ya Kiserikali Tanzania na aliweza kufanya pia mazungumzo na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mheshimiwa Rais wa Ujerumani alipata nafasi ya kwenda kutembelea Mkoa wa Ruvuma kupitia eneo lile la Makumbusho yetu ya Majimaji na aliendа kuangalia yale makaburi ya waliofariki wakati ule. Lakini kupitia mazungumzo waliyoyafanya na Mheshimiwa Rais ilikubalika sasa tuanze mchakato wa kuweza kurejesha malikale hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wegine, tumeshaanza taratibu kupitia Wizara yetu ya Mambo ya Nje kupitia taratibu za kidiplomasia tunaendelea kulifuatilia suala hili na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwa wavumilivu au kuwa watulivu wakati Serikali ikilifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeunda Kamati mbalimbali za kitaifa ikiwemo Kamati ya wataalam, Kamati ya Makatibu Wakuu na Mawaziri, pia tunayo Kamati ya Taifa ya Majadiliano ambayo sasa itaweza kwenda kujadiliana na wenzetu wa Ujerumani ili kuhakikisha kwamba tunapata kila kitu ambacho kiliweza kuchukuliwa kama vile miili, *dinosaur* wetu pamoja na malikale zingine mbalimbali ambazo zilichukuliwa wakati ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati hizo kuundwa, tuendelee pia kupitia wataalam kufanya tafiti zaidi ili kuweza kujua ni mali kiasi gani sasa na mikusanyo iko nje ya nchi. Unaweza ukafikiri unafuatilia vichache kumbe ziko nyingi zaidi katika vyuo mbalimbali vya elimu, Makumbusho za huko Ujerumani na katika taasisi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hili pia tunafuatilia katika nchi zingine, lakini tumeanza kwanza na Ujerumani. Sambamba na hili pia tunatafuta uzoefu, tunaangalia uzoefu wa wenzetu wa New Zealand walifanyaje na uzoefu wa wenzetu wa Namibia walifanyaje ili sisi tutakapofanya majadiliano basi mchakato wetu uweze kuwa ni bora zaidi na tuweze kupata kile ambacho Tanzania inakikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika nchi yetu kumekuwa na aina mbalimbali za utalii lakini katika masikio ya Tanzania tunasikia mara nyingi ni utalii wa mbuga za wanyama, fukwe na malikale. Lakini hatujazisikia vizuri aina nyingine za utalii ziliendeshwa katika nchi yetu. Nilikuwa nataka kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, je, Serikali yetu imejipanga vipi sasa katika kuhakikisha wanaanzisha aina mbalimbali za utalii katika nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kwa hali ilivyo sasa aina za utalii unaofanyika nchini uko *very narrow*. Serikali imeliona hili na ndani ya Serikali sasa tumejipanga kupanua wigo wa aina ya utalii ambao tunaweza kufanya kwenye nchi yetu ili uweze kunufaisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza kufanya tafiti kwenye maeneo ya misitu tuone ni jinsi gani misitu inaweza kutumika kufanya mambo ya utalii. Tunaanza kuangalia kwenye maeneo haya ya

fukwe, kuboresha zaidi na kuona ni kwa namna gani tunaweza kuvitumia visiwa vyetu. Pia kuangalia maeneo ya tamaduni zetu, ni jinsi gani tunaweza kutumia tamaduni ili ziweze kutumika kwa. Lakini vilevile utalii wa matamasha mbalimbali; hata utalii wa matamasha ya vyakula kwenye miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maeneo ambayo tunataka kujikita ili tuweze kuona ni jinsi gani tunaweza kutumia rasilimali hizo. Kwa mfano, kwa Dodoma, wote tunafahamu kwamba Dodoma ndiyo eneo ambalo unaweza kulima zabibu mara mbili kwa mwaka. Tunataka kuitumia fursa hii kujielekeza ili kuona ni jinsi gani tunaweza kuitumia fursa hiyo ili tuweze kuongeza fursa za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa tukiwa ndani ya Bunge tumefanya utafiki kwa jinsi ambavyo tunaweza kuanzisha tamasha la ulaji wa nyamapori katika nchi yetu, mwitikio tulioupata ni mkubwa sana. Kwa hiyo, ndani ya Serikali tutatumia mbinu mbalimbali ili kuibua aina nyingi za utalii ili sekta hii iweze kuimarika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ni kwamba nimemsikia hapa Mheshimiwa Waziri akizungumzia suala la kuajiri wafanyakazi wa *TAWA* kwa ajili ya kukabiliana na Wanyama wakali wanaoingia katika maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Kanda ya Ziwa hususan katika Wilaya ya Sengerema Jimbo la Buchosa na Sengerema, tumekuwa na tatizo kubwa la mamba. Sasa nimesikia hapa hata mwenzetu mmoja alikuwa anachangia kuhusu mamba kuuwawa. Sisi Sengerema tuna hii shida, hao wawindaji wanaopewa vibali basi waje wavune hawa mamba waliopo Sengerema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninataka ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kama hatakubali kuleta kituo cha walinzi wa

wanyamapori katika Wilaya ya Sengerema, mimi nitakamata shilingi kwa sababu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam...

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, walinzi wako Bunda...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Naam.

**MWENYEKITI:** Hapa ni kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi ni kuhusu jambo mahususi la kisera.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Sasa kujenga kituo kwenye Jimbo la Sengerama linakuwa haliko hapa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana siyo jimbo, ni kwamba watumishi wale kwa sababu wako nchi nzima...

**MWENYEKITI:** Umechanganya mambo mengi, hapo unasema kituo kisipojengwa, wale wanaoajiriwa, watu waje wavune. Sasa hapo unataka ufafanuzi kutoka Mheshimiwa Waziri kwenye hoja ipi?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, amesema Rukwa watapelekwa katika hayo maeneo ya kupunguza hao wanyama wakali. Lakini kuna haya maeneo kama Rukwa na sisi Kanda ya Ziwa, tuliomba kituo kama hicho na walituahidi hicho kituo kitajengwa Sengerema ili wavune mamba tulio nao, tuna mamba wengi...

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa unataka ujibiwe hilo kama swali au... *(Kicheko)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafanyakazi wa *TAWA*. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya. Naona kuna mahali hatujaelewana lakini Mheshimiwa Waziri amelchukua hoja yako kwa hiyo ataifanyia kazi. Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya hoja za Kamati alivyokuwa nazijibu lakini nina jambo moja kwenye suala la zile fedha bilioni 19 ambazo kama Kamati tulipendekeza kuwepo na mabadiliko ya matumizi kwa maana ya fedha ziende kwenye maendeleo na fedha zingine kiasi ziende kwenye *OC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema, ameshaleta *addendum* kwa Mheshimiwa Spika. Sasa kwa kuwa sisi ndiyo Bunge na sisi kama Kamati tulileta mapendelezo mbele ya Bunge na hawa ndiyo Waheshimiwa Wabunge. Hivyo basi, ninaomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri; ni mabadiliko yapi yaliyofanyika ili Waheshimiwa Wabunge wote tufahamu na kama tutakuwa hatujapata mabadiliko hayo ninakusudia kushika shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimepata mabadiliko ya kwenye jedwali, ndiyo Kiswahili? Maana kuchanganya changanya mambo hapa. Haya, nimepata mabadiliko ya matumizi ya zile fedha ambayo yameletwa na Mheshimiwa Waziri. Wakati huo huo nimepokea pia mapendekezo ya mabadiliko kutoka kwa Mheshimiwa Timotheo Mnzava na haya mabadiliko yako tofauti kabisa. Yaani ya Mheshimiwa Mnzava na ya Mheshimiwa Waziri yako tofauti, ya Mheshimiwa Mnzava yanazungumzia ile bilioni 19 yote lakini ya Mheshimiwa Waziri yanazungumzia bilioni tano. *(Kicheko)*

Kwa hiyo basi, haya mabadiliko aliyoyaleta Waziri na ambayo yameletwa na Mheshimiwa Timotheo Mnzava, yote yataelekea Kamati ya Bajeti, ili kipindi hiki cha mashauriano tufike mahali ambapo upande wa Serikali utaleta ya kwao na upande wa Mheshimiwa

Mwenyekiti sasa wa Kamati kwa sababu na yeye atakuwa mjumbe wa Kamati ya Bajeti wakati huo, tutaweza sasa kushauriana vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa sasa yale mabadiliko yaliyokuwa yanapendekezwa kwenye bilioni 19 ya kutoka Serikalini na ya kutoka kwa Mheshimiwa Mnzava, yote yanaelekea Kamati ya Bajeti. Kwa hiyo, hata hayo aliyosema Mheshimiwa Waziri na aliyoyaleta hapa mezani yote nimeyapokea na ninayapeleka Kamati ya Bajeti kwa hiyo, hapa hatutayajadili leo hayo mabadiliko. *(Makofi)*

Haya, Mheshimiwa Sanga subiri kidogo maana hapa naambiwa kuna *addendum* juu ya *addendum*, ngoja niletewe zote hapa mbele.

Mheshimiwa Waziri, sasa hapo tutachanganyiana mambo, Mheshimiwa Jenista utulie kidogo. Mheshimiwa Waziri, kuna mabadiliko ambayo ulileta tarehe 31 Mei, 2024?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya mabadiliko hayo yalikuwa ni kabla Taarifa ya Kamati haijawasilishwa Bungeni na tulikuwa tumewasilisha Wizara ya Fedha ili waweze kuturidhia mapendelezo ya mabadiliko. Lakini baada ya mapendelezo ya Kamati walivyochangia Taarifa yao hapa, kwa hiyo, ile ilikuwa *withdrawn* na Wizara ya Fedha, lakini *addendum* pekee ambayo tunayo kwa sasa ni ile ambayo na wewe utakuwa umewasilishiwa ndani ya siku mbili hizi na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, kwa hiyo, mabadiliko haya ya Tarehe 31 Mei, tunayaondoa; mmeomba yaondolewe? Haya, haya tunayaondoa kwa hiyo, tumebaki na yale ambayo naelekeza sasa yaelekee Kamati ya Bajeti, siyo? *(Makofi)*

Kwa utaratibu sasa wa Kanuni zetu kwa sababu hilo la kuelekeza Kamati ya Bajeti nitalisema wakati Bunge limerejea lakini katika ngazi hii kwa sababu ndiyo tunataka kupitisha mafungu, mafungu haya yatapita pamoja, maana inabidi nielezee vizuri. Mafungu haya

yatapita pamoja na bilioni 19 ili isiwe imepungua kwenye fedha za jumla za Wizara ambazo Bunge linapitisha. Matumizi ya bilioni 19 ndiyo yanapelekwa kwenye Kamati ya Bajeti kwa ajili ya mgawanyo, nadhani tumeelewana vizuri. *(Makofi)*

Sasa kwenye kuielekeza Kamati ya Bajeti kulitazama hizo, nitazungumza nikiwa pale juu, Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelekezo uliyoyatoa nakubali kwamba tutasubiri maelekezo yako mengine. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia mchana, nilihoji juu ya mamba wetu mrefu mwenye zaidi ya sentimita 493.8 ambaye ni mamba wa kwanza kwa urefu duniani. Nikaeleza bayana kwamba aliwindwa na huyo Mwindaji Josh katika Kitalu cha *Lake Rukwa GR*. Nikasema kabisa mamba huyu na mimi bado naamini Taasisi yetu ya *TAWA* na *TAWIRI* na kwa sababu hawa mamba wako kwenye *group* lile la wale wanyama wanaoangaliwa kwa jicho la pekee kwa maana wako *CITES*. Kwa hiyo, ina maana kwamba *TAWIRI* muda wote wanafanya utafiti juu yao, hivyo inaonesha Taasisi zetu za zote Serikali zilijua Tanzania ina mamba mrefu kuliko mamba wote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndiyo kukawa na changamoto hiyo, kwa nini kama tuna mamba mrefu kuliko mamba wote duniani ambacho ni kivutio kikubwa cha utalii katika nchi yetu, aende kuwindwa katika uwindaji wa kawaida badala ya kutengenezwa kiwe kivutio cha utalii hapa nchini kwetu ili tuweze kupata fedha za kigeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, nisaidie jambo moja, kwenye kile kibali cha huyu mgeni ama mtalii wa uwindaji kuwinda huyo mamba mrefu, kilikuwa ni mahususi kwa ajili ya mamba mrefu ama

kilikuwa ni cha kuwinda mamba halafu akajikuta amempata huyo mamba mrefu? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kibali kile ni cha kuwinda tu mamba.

**MWENYEKITI:** Aanhaa, nichakuwinda tu mamba.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo mgogoro ulipoanzia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mpina kwamba mwezi Desemba, 2023 sisi tuliona *video* fupi ambayo ilisambazwa na mwindaji. Baada ya kuiona *video* hiyo na kuona kumekuwa na taharuki kwa wananchi wetu, tulitoa tamko tarehe 2 Januari, 2024 kuhusiana na uwindaji huo na endapo ulizingatia sheria husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba uwindaji wa mamba huyo ambaye anadai ni mkubwa zaidi duniani ulizingatia sheria zilizopo na ulizingatia matakwa na vigezo vyote vya Mkataba wetu wa Kimataifa wa Wanyamapori na mimea iliyo hatarini kutoweka *CITES*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nipende pia kutoa taarifa kwamba, tabia au sifa za wawindaji wengi mara nyingi hupenda kujisifia mara wanapomaliza uwindaji wao, kuonesha kwamba wamevunja *record* zao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa mujibu wa taarifa na takwimu za *Safari Club International*, mamba mkubwa ambaye amewahi kuwindwa duniani alikuwa na urefu siyo huo anaoutaja Mheshimiwa Mpina. Alikuwa na urefu wa futi 18.7 ukimlinganisha na mamba huyu ambaye Mheshimiwa Mpina anamtaja aliyekuwa na urefu wa futi 16.2. Hivyo, ni wazi kwamba wapo mamba wakubwa

zaidi waliovunwa zaidi ya huyo ambaye Mheshimiwa Mpina anamtaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mpina na wengine, Serikali tutaendelea kutangaza utalii wa uwindaji katika nchi. Vilevile, kwa kutambua kwamba tunazo nyara nzuri, tutaendelea kufanya uwekezaji katika maeneo yetu ya mapori ya akiba na maeneo ya uwindaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, naona umesimama.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono ili tuijadili hoja hii mahususi. Kwanza, Mheshimiwa Waziri hapa anazungumzia yule mamba mwenye sentimita 561 aliyewindwa kule Ethiopia, ni mwaka 2005. Kwa hiyo, alipowindwa huyo wa kwetu ndiyo akafikiwa kuwa namba moja duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, huyu Mwindaji Josh aliwahi kukamatwa kule Marekani kwa uwindaji haramu kwa hiyo hana usafi wowote ule na la tatu... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ngoja, ngoja. Sasa hapo unataka kupeleka mjadala kwingine kabisa, ukituweka hapa kwenye kujadili usafi wa mtu tena itakuwa mtihani. Mheshimiwa nakupa sekunde 30 malizia hoja yako.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kutokana na suala hili lilivyokaa ambavyo inaonekana kabisa kwamba, kuna mambo ambayo siyo ya kawaida. Inawezekana kabisa baadhi ya watendaji wetu wa Serikali walikula njama na hao wawindaji haramu na hao wawindaji walikula njama na wawindaji na kusababisha hiki chanzo ambacho kingekuwa kivutio kikubwa cha utalii hapa nchini kwetu kuwindwa kiholela na kuchukuliwa na kwenda... *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina wewe si unatoka kwenye maeneo ya uwindaji, yule mwindaji angeweza kujua kwamba, huyu ni mrefu kabla hajamuwinda? Alikuwa na uwezo huo?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema hapa kwamba, huyu mwindaji amepelekwa mahususi na wataalamu wetu mpaka kwenda kumuwinda yule mamba. Ndiyo maana nikasema kwamba... *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina haya, toa hoja yako. Toa hoja yako.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge ikiwezekana Bunge lote zima mniunge mkono tujadili hii hoja mahususi. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya, umeungwa mkono na watu hawajafika 10.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezidi, tumezidi, tumezidi...

**MWENYEKITI:** Hamjafika 10. Mmeanza kuongezeka baada ya… Nilipogeuka huku mlikuwa mmesimama watatu, ndiyo. Mlisimama hapa watatu, yule wa nne alafu tano, sita, saba, ndiyo utaratibu sasa, kama mlikuwa mnasikilizia mimi nawasaidiaje kwa mfano?

Mheshimiwa Esther Nicholous Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tumeendelea kushuhudia wanyama wakali wakifanya madhila mbalimbali kwa binadamu, kwa mifugo na kwa mazao, lakini kifuta jasho ambacho kinatolewa kimekuwa ni kidogo sana pamoja na kwamba, Wizara imefanya marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kufanya tafiti, kabla ilikuwa binadamu akiuwawa walikuwa wanalipa shilingi milioni moja, sasa hivi,

kuanzia Julai itakuwa shilingi milioni mbili, akipata ulemavu wa kudumu sasa hivi atakuwa analipwa laki tano na akipata ulemavu *temporary* analipwa laki tatu. Ng'ombe akiuwawa eti wanalipa shilingi 75,000 wakati ng'ombe akiingia hifadhini wanatoza faini zaidi ya shilingi laki moja, laki moja na nusu mpaka laki mbili na nusu mpaka milioni, haina hata uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuta mfugaji ana ng'ombe wake, labda ana thamani ya shilingi milioni moja, unamlipa shilingi 75,000. Nikajaribu kuangalia nchi ya Namibia ambayo ina tembo wengi, pale kwa mfano tembo akisababisha kifo wanalipa dola 15,000 takribani shilingi milioni 40 inafika, akipata *permanent disability* analipwa dola 5,000 kama shilingi milioni 13 hivi, akipata *temporary disability* analipwa dola 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwetu, ukijaribu kuangalia pia, Sheria za kuwalinda hawa Wanyama, tembo akiuwawa ni shilingi milioni 30. Sasa hii inakuwa inaleta sintofahamu baina ya binadamu Watanzania, ndiyo maana hata Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia hapa, wanaona kama vile tunathamini zaidi Wanyama kuliko binadamu. Nikajaribu hata kupitia Sheria zetu za bima, mtu akiwa amefariki wanalipa siyo chini ya shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sijaridhika nitashika shilingi. Nataka *commitment* ya Serikali ya kuleta mabadiliko ya Sheria ya Wanyamapori ya 2009 ambayo ita-*incorporate fine, specifically* baada ya kufanya tafiti i-*incorporate fine* na mapungufu mengine yote ambayo yanaonekana sasahivi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya tafiti kwa nchi wanachama, ili Watanzania waweze kulipwa fidia stahiki na siyo *compensation*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia hoja ya Mheshimiwa Esther Matiko. Kama ambavyo nimetangulia kusema katika maelezo yangu wakati najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Naafiki kwamba, ni kweli, kiwango hiki hakitoshi, lakini nikasema uwezo wa sasa wa Serikali kulipa ni huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaangalia taratibu nyingine, kama twende kwenye mfumo wa bima. Je, unafanyaje kazi na kadhalika na kadhalika. Kwa sasa tuombe Waheshimiwa Wabunge waridhie twende na viwango hivi ambavyo tumevitangaza tarehe 31 Mwezi wa Tano wakati tukiendelea na tafiti kuweza kuona ni mfumo gani bora ambao, walau utaweza kutoa kiwango ambacho kitakuwa kimeboreshwa zaidi na kinaweza kuwa kimeendana na hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa nimuombe Mheshimiwa Mbunge na wengine, hoja hii twende nayo kwa mujibu wa kanuni hizi ambazo tumezitoa sasa, tulizoziboresha tarehe 31 Mwezi wa Tano. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, naona umesimama?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja au haya malalamiko yamekuwa ni ya muda mrefu sana na tumekuwa nikilalamika sana humu, sikupata tu muda ningeweza kupitia. Mathalani, tunajua Watanzania wengi wanakaa pembezoni mwa hifadhi, lakini katika Kanuni ya Mheshimiwa Waziri anasema Mtanzania anayeishi ndani ya nusu kilomita hatafidiwa kwa chochote pale ambapo wanyama hawa wakienda kufanya madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Watanzania wanaishi pembezoni kabisa na wanafanya kilimo. Wanaishi pale, wanafuga, wanafanya shughuli nyingine zote.

**MWENYEKITI:** Haya, malizia hoja yako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijaridhika. Naomba kutoa hoja, ili Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono tu-

*discuss* kwa kina, Serikali ichukue, ione kwamba, ni hoja ambayo inatakiwa kufanyiwa kazi kwa makini zaidi kuliko hizi *rate* ambazo wanatoa saivi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, mbona mmesimama kabla?

Haya Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Wabaki wamesimama wale wa kuomba kuchangia. Watachangia Waheshimiwa Wabunge wachache kwa hivyo, wale mliohama viti vyenu, nashindwa kujua vizuri, naona hii miwani inahitaji msaada.

Mheshimiwa Mpina wewe si umetoka kuongea sasa hivi! Wewe umetoka kuongea sasa hivi, ngoja wapate nafasi wengine.

Waheshimiwa Wabunge, dakika ni moja. Mheshimiwa Francis, atafuatiwa na Mheshimiwa Kandege. Mheshimiwa Tecla Ungele ajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jambo hili...

**MWENYEKITI:** Samahani, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni la muhimu sana, Sheria hii ya kuwapa watu kifuta jasho na kifuta machozi imekuwa ni ya ukandamizaji kwa muda mrefu. Tungeomba Sheria ije kwa dharura, tuijadili katika Bunge hili, ili wananchi wa Tanzania wapate haki zao. Tunavyoongea sasa hivi wapo wananchi ambao wamepoteza maisha na wengine mali zao zimepotea, hawajui ni lini watapata hizo haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninao mfano hai. Kwenye Kata yangu ya Mwangeza wananchi wamepoteza maisha na mazao yamepotea, mpaka leo hawajui watalipwa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Haya, kengele imeshagonga. Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelazimika kusimama kuunga mkono hoja. Mimi ni kati ya watu ambao wamepata madhila makubwa sana kwa mpiga kura wangu ambaye alikuwa yupo shambani kwake, shamba la ulezi, akafuatwa na tembo akakanyagwa-kanyagwa. Ni katika Wilaya ya Kalambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa taarifa kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, *response* iliyokuwepo ni wameenda wao kama wao, lakini hakuna chochote ambacho kingewatia matumaini wananchi wa Kalambo kwamba, hili limetokea. Wana kazi ya kuhakikisha kwamba, tunalinda wanyama hawa, lakini na sisi siyo kwamba, ni *threat* na tusipate chochote kutoka Serikalini. Ni wakati muafaka, kama ambavyo alitangulia kusema mwenzangu, ije Sheria kwa udharura wake kwa kuthamini watu wetu, ili tuweze kupata fidia stahiki, ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Ungele, atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mheshimiwa Kuchauka ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika changamoto kubwa inayotuathiri Mkoa wa Lindi ni suala la vifo na ulemavu wa kudumu utokanao na wanyama. Uhai wa mwanadamu ukishatoka haurudi, hata hiyo fidia tunayoomba, hata hicho kifuta machozi tunachoomba siyo kwamba, kifanye jambo fulani, hakuna kitakacholingana na uhai wa mwanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba suala hili Sheria iletwe hapa, ili kuwepo na ongezeko kwa kiasi hiki kitakacholipwa kwa familia hii inayobaki. Ahsante. *(Makofi)*

**MWEYEKITI:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mheshimiwa Kuchauka. Mheshimiwa Bulaya ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Uhifadhi ni lazima uwe na gharama na gharama mojawapo ni lazima iwe kuwalipa fidia watu wanaopata madhara kutokana na athari zinazotokana na wanyama hao. Wakati wa kuleta Sheria izingatie aina zote za wanyama wanaoleta athari, si tembo peke yake. Mfano tu ni kwamba, kuna ngedere pia, nao huleta madhara makubwa na wanawafilisi wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngedere wa siku hizi wengine wamekuwa kama watu, wanavuna kabisa halafu wanakusanya wanaondokanayo. Kama tukiacha hivi mwananchi anakosa kabisa mazao na hii ipo hata kwenye Jimbo langu pale Kilolo. Kwa hiyo, mimi naunga mkono kwamba, Sheria iletwe haraka, ili wananchi waweze kupata fidia kutokana na zile athari wanazozipata ambazo zinasababishwa na hawa wanyama wakali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Bulaya. Mheshimiwa Timetheo Mnzava. Ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja. Hiyo Sheria iletwe haraka ifanywe mapitio kwa sababu, kwanza tunazungumzia umbali kutoka shambani na ulipo, bado umbali ule nao unasababisha. Pia aina ya mazao; inawezekanaje mimi nimeliwa mpunga wangu, nilipwe sawa na mtu aliyelipwa korosho? Unajua korosho ni zao kubwa au mwingine ni muembe au mnazi kwa hiyo, sheria ije tuone, tuchambue hata aina ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani aliyeliwa mpunga alipwe sawa na aliyeliwa korosho na pia, umbali kwamba, kila unapokaribia hifadhi ndivyo unavyokosa fedha. Wakati huohuo kuna maeneo yetu ambayo yalikuwa *WMA* yamechukuliwa na hifadhi. Utakuta tayari hifadhi inakaribia watu, sasa sisi inatukaribia halafu inatunyima mafao. Mimi naomba Sheria iletwe haraka sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Timotheo Mnzava ajiandae. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Haya mambo watu hawawezi kutuelewa, yani mwananchi akiua tembo ni shilingi milioni 30, halafu tunakuja kujisifia hapa eti tumeongeza shilingi milioni mbili kwa mtu ambaye amefariki, familia yake haiwezi tena kusomesha watoto. Tunakuja kujinasibu hapa tumemuongeza mtu ambaye amekatika viungo vyake, alikuwa anaenda kulima, mnasema badala ya laki saba mnampa milioni moja, lakini hawezi tena kufanya kazi kujipatia kipato chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo hatuwezi kuruhusu. Tunatengeneza mazingira ya wananchi wachukie hifadhi zao na waone Serikali hii inajali sana wanyama kuliko wao. Ni wakati muafaka wa kuwatendea haki Watanzania kwa kuleta Sheria ya kuhakikisha wananchi wa nchi hii wanalindwa kama ambavyo mnalinda wanyama wa Taifa hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Timetheo Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Mheshimiwa Dkt. Jafo ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Utaratibu wa kulipa kifuta jasho na kifuta machozi ulikuwa na changamoto mbili, moja ni viwango na mbili ni ucheleweshwaji wa kifuta machozi chenyewe na sababu kubwa ya ucheleweshaji wake ni mchakato huu. Kulikuwa na mlolongo mrefu sana kuanzia uhakiki mpaka mtu kuja kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeshauri tu nimwombe Mheshimiwa Matiko amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi, lakini Mheshimiwa Waziri afanye *commitment* kwa sababu, hizi ni kanuni ambazo kuzibadilisha ni rahisi kwake. Baada ya muda Mheshimiwa Waziri akazipitie upya, ili aangalie hivi viwango, lakini tuangalie na

namna ya kuboresha huu mchakato, ili usichukue muda mrefu wananchi wetu walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku kwa sababu, changamoto hii ni kubwa ni vyema Serikali ikaiona kwa ukubwa huu. Tuongeze nguvu kwenye kuzuia wanyama hawa wasiende kwenye mazao na maeneo ya wananchi, tusibaki tu na kung'ang'ania peke yake tuweke nguvu kubwa kwenye kuzuia wanyama hawa wasiende kwenye maeneo ya wananchi. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, atafuatiwa na Mheshimiwa Jafo halafu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kwenye hoja hii na umuhimu wake. Pili, niungane na muongeaji aliyepita na aliyetangulia kwamba, kimsingi hakuna fidia ambayo italingana kiwango na maisha ya mwanadamu. Maisha ya mwanadamu hayalinganishwi na fedha yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi tumetengeneza, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema, hiyo ni *token*, lakini tumepokea hoja hizi. Sisi, kama Serikali, tutaendelea kujadiliana na hasa tukiweka umahususi kwenye namna ya kuzuia masuala haya tukitoa na elimu pia, kwa wananchi wenyewe. Haya mambo hayahusishi Serikali tu yanahusisha pia, na *sensitivity* ya wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki hii, siku mbili zilizopita, tembo alikatiza pale kijijini kwangu na akatokea mwanakijiji akamsogelea apige *selfie* hivi na kwa kweli, amepoteza maisha kizembe namna hiyo, akakanyagwakanyagwa na tembo. Tutatengeneza kanuni tuongeze nguvu kwenye kuzuia kwa wale ambao wanakuwa kazini, lakini pia, hili jambo ni lazima kuendelea kuweka *sensitivity*.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, nani anayesema Taarifa?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa. Nipo hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa samahani, muda wake umekwisha.

Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Mheshimiwa Waziri jiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hoja aliyoongea dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko ni hoja ya msingi, pamoja na Mheshimiwa Ester Bulaya. Nakumbuka hoja hii ilitoka Mwaka 2011, ilikuwa ikijadiliwa na ninakumbuka Kanuni za awali zilikuwa ni Kanuni za Mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi baada ya muda mrefu sana tumeona Serikali ime-*respond* na kuja na Kanuni mpya za Mwaka 2024, hii inaonekana kwamba, Serikali ipo tayari katika eneo hilo. Mimi namwomba dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko kwamba, aone hii nia njema ya Serikali. Serikali imeshaanza kufanya jambo hili, lakini hata hivyo, Serikali itafanya tafiti za kutosha lengo kubwa ni kuona kwamba, jinsi gani hili tatizo litaweza kutatuliwa vizuri, kitafiti zaidi, hata kama ni kwa Sheria au Kanuni kubadilishwa basi tufike katika wakati ambao wataweza kuona kwamba, Serikali imetimiza haja yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Esther Matiko kwamba, arudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri, ili twende mbele, kwa ajili ya kufanya tafiti na kulishughulikia suala hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge mbalimbali walioweza kuchangia hoja hii. Kama ambavyo nimeeleza na pia, kama ambavyo hata Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ameeleza, kwanza tumeanza kwa maboresho ya jedwali lile la nne

kwa kuangalia viwango hivi, kwa kuanzia, kutokana na hali ya uwezo wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni Waheshimiwa Wabunge watakuwa wameona adhma ya Serikali na Wizara. Huko nyuma ilikuwa ni chini ya eka moja mtu alikuwa hawezi kulipwa, tumeweza kulizingatia. Vile vile kama mtakumbuka pia, tumeshaanza majadiliano na shirika letu la bima kuweza ku- *explore* na tunaendelea kuangalia bima nyingine, lakini mtakumbuka hata Mheshimiwa Kaboyoka alieleza, nadhani ilikuwa ni wiki hii hii, kupitia kamati ya *PAC* mamlaka yetu ya udhibiti wa bima, *TIRA* pia, ilienda kwenye Kamati na waliweza kujadiliana suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kusema suala hili ni suala ambalo linahitaji tafakuri ya kina. Tunaendelea kuwaomba Waheshimiwa Wabunge watupe nafasi wakati tunalitafiti. Kenya wanaendelea kulitafakari kupitia bima ndogo au *micro insurance,* Nepal nao pia, wameanza kupitia bima ndogo, lakini vile vile wenzetu wa Namibia nao pia, wameanza kulitafakari kupitia Kamati yao ya Maliasili ya Bunge lao la Namibia na wanaendelea kuangalia uzoefu wa kwetu tunafanyaje, lakini na wao kama wakiamua kwenda kwenye bima inakuwaje? Naomba tupewe nafasi tuendelee kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili je, bima hiyo anailipa nani? Je, anailipa Serikali kwa idadi ya matukio mangapi na kadhalika na kadhalika? Ikitokea anailipa mwananchi ambaye labda ana mazao yake, taratibu ziweje? Ndiyo masuala ambayo tunaenda kuyaangalia huko kupitia mamlaka zetu za bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi kwamba, walipe wananchi, lakini napenda kusema kwamba, taratibu za kibima zina taratibu zake. Kwa hiyo, tutakapoenda kufanya majadiliano, kama inawezekana, tutasikia mamlaka na taasisi za bima zitasemaje? Kama linawezekana, je, nini kifanyike, ili kuwezesha suala hili? Upande wa mchakato mrefu nilieleza pia, katika majibu yangu, tunaliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaanza majaribio katika zile halmshauri za wilaya kumi. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa mchakato huu unakuwa mfupi ipasavyo kumwondolea mwananchi kadhia na hasa huyu ambaye amepata madhila katika mazao yake lakini pia athari zingine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo tumekuwa na nia njema ya kubadili kanuni hizi mwezi huu wa tano nia njema bado iko pale pale tutaendelea kufanya mapitio ya kina na kuwashirikisha wadau mbalimbali na Wabunge wenyewe pia wakiwemo ili kuweza kuona ni kwa namna gani tuweze kuboresha kanuni hizi likiwemo na suala la nini kilipwe? Kiwango kiboreshwe kwa namna gani na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na niombe Waheshimiwa Wabunge watukubalie kwa hali ilivyo, sasa wanirudishie shilingi yangu, Mheshimiwa Matiko, tupe nafasi tuendelee kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umenichanganya kidogo hapo kwenye bima, wakulipa ni nani, kwani sasa hivi fidia analipa nani?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia inalipwa na Serikali. Nimelisemea hivyo kwa sababu ukiangalia nchi zingine za wenzetu ambao wameanza mchakato huu wa kutumia mfumo wa bima, wapo ambao mwananchi mwenyewe anajilipia bima ili ikitokea matukio ya namna hiyo basi bima inalipa. Kwa hiyo, sijasema kwamba Serikali inaenda kwenye mfumo huo bali nimesema ziko hizo *scenarios,* ndiyo maana nikasema tunavyokaa na mashauriano na wenzetu ili kupata uzoefu ili iweze kujulikana tutaenda kwenye mfumo gani na kwa utaratibu wa aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, hitimisha hoja yako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasisitiza mabadiliko ya sheria yaletwe ambayo yatatamka bayana fidia na siyo kifuta jasho. Fidia ambazo tutazijadili hapa tuziweke za viwango vikubwa. Nimetoa mfano wa Namibia, Namibia inalipa karibia milioni 40, sasa imepelekea Serikali iweze kuzuia tembo wasije kwa wananchi na wale wana tembo wengi sana. Wamejenga *electric fence over sixty percent* ya hifadhi yao. Kwa hiyo, wakilipa kiwango kikubwa watajizuia iko ni kama vile mtu anaogopa kuua mnyama maana yake gharama iko kubwa. Sasa hivi milioni mbili, milioni ngapi wanaacha tu, tembo wanakuja tu lakini *once* ikienda juu Serikali itakuwa *committed* itahakikisha wanyama hawaji kuwaua Watanzania huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nakurudishia shilingi yako ila hakikisha unaleta mabadiliko ya sheria ili ijadiliwe tuweze kuwalinda Watanzania na tuweze kuhakikisha wanyama wanabaki kule, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa jambo hili liko kwenye kanuni na sisi tunayo Kamati yetu ya Sheria Ndogo. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameshatoa yale maelezo ya awali, kama kutakuwa na umuhimu kweli wa kuleta sheria basi Kamati yetu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iangalie pengine ni vifungu gani ambavyo vitamwezesha zaidi Mheshimiwa Waziri kuweza kutengeneza hizo kanuni lakini tukisema kwamba vile viwango tuje tuviweke hapa ndani na mchakato ule wa mabadiliko ya sheria nadhani sote tunaufahamu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo nadhani kwa upande wa vifungu vya sheria ambavyo vinahitaji mabadiliko Kamati yetu ivitazame, lakini tumwache Mheshimiwa Waziri kwa kuwa zile ni kanuni akabadilishe kanuni kulingana na yale mawazo ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyasema na kwa huo utafiti ambao wao wanaenda kuufanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa uhitaji wa sheria, Kamati yetu itazame ni vifungu gani vitahitajika lakini viwango bado tuendelee huku kwenye kanuni kwa sababu tunao uwezo wa kuziita hizo kanuni

kama tunaona zina changamoto, tukaiambia Kamati yetu ya Sheria Ndogo itazame. Hilo lilikuwa linahusu viwango.

Mheshimiwa Waziri, hii sasa ya ucheleweshaji na kwa sababu ndiyo tuko hapa kwenye bajeti, kwa kweli hapendezi. Mtu afariki halafu watu waanze kukimbizana na kufuatilia na inajulikana kabisa kwa sababu watu wa maliasili wapo pia kila mahali. Hii Taarifa ikishakuja watu walipwe kama rambirambi inavyolipwa, rambirambi ikikaa miezi sasa inakuwa tena haina maana.

Kwa hiyo, kwenye hili la kuchelewesha pengine na lenyewe unapoenda kubadili kanuni jiwekeeni na ninyi wenyewe muda wa kulipa mule ndani ili wananchi wasiwe wanasubiri kwa muda mrefu kwa kisingizio cha kufanya tathmini wakati inajulikana mtu ameumia, ameenda hospitali kakatika, mtu ameumia au amefariki wameshazikwa, sasa hapo tena kidogo inakuwa inaleta changamoto. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa mujibu wa kanuni zetu kama nilivyosema majina bado yapo mengi hapa mbele lakini kanuni zetu zinataka nikishaongeza ile nusu saa ikibaki dakika kumi tunaingia kwenye mafungu. Kwa hiyo, sasa wale ambao hawakupata nafasi nadhani baadhi ya hoja zenu mtakuwa mmeshazisikia Wabunge wakisema kwenye hoja zingine.

Sasa namsikia mtu anasema bado, ni kwa sababu hoja moja inachukua muda kidogo. Kwa hiyo, hatutaweza kuzifikia hizo dakika zetu na kwa kweli zimebaki dakika kumi na ngapi hivi ndio za kusoma mafungu zenyewe.

Katibu tusomee mafungu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI – MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management* ……………..............….……Sh. 6,495,666,550
Kifungu 1002 - *Finance and Account Unit*……........………Sh. 1,258,276,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*…......................Sh. 1,661,282,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*…..........Sh. 591,548,988
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*……………........……………Sh. 676,784,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*…..............Sh. 911,798,044
Kifungu 1007 - *Legal Services Unit*……….........……………Sh. 608,102,240
Kifungu 1008 – *Management Information Systems Unit*....................................................Sh.1,058,061,000
Kifungu 1009 - *Research and Training Unit*…….................Sh. 38,184,195,431
Kifungu 1010 - *Paramilitary Coordination Unit*…….............Sh. 1,452,664,000
*Kifungu 1011 - Monitoring and Evaluation Unit*...................Sh.873,105,924
Kifungu 2001 - *Wildlife* ...........................................…………Sh. 108,550,306,213
Kifungu 3001 - *Forestry and Beekeeping*……........………Sh. 59,438,490,396
Kifungu 4001 - *Tourism* ………………..........………….....…Sh. 16,784,567,699
Kifungu 4002 - *Antiquities Unit*…………………….........…Sh. 12,339,234,515

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kabla sijalihoji Bunge haya mafungu tutakayosoma kwenye hizi fedha za maendeleo na hizi za kawaida, ile bilioni 19 imo?

**MBUNGE FULANI:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI**:

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……...........…Sh. 3,501,044,606
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……...............…..Sh. 40,972,672,655
Kifungu 2001 – *Wildlife*……..........…..............................…..Sh. 44,421,966,921
Kifungu 3001 – *Forestry and Beekeeping*……….............…Sh. 4,155,520,945
Kifungu 4001 – *Tourism* ……………………........…………..…Sh. 4,190,130,873

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Mtoa hoja taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge baada ya kuwahoji na Wabunge waliowengi kusema ndio, natumia fursa hii kutangaza rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kupitishwa rasmi na Bunge huko, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ile ambayo imeweza kupata pongezi kutoka kwa Wabunge lakini pia kwa kuzipokea changamoto mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezisema hapa ambazo ziko chini ya Wizara hii na tunawatakia kila la kheri kwenye kushughulikia changamoto hizo lakini pia kutekeza mipango ambayo mmejiwekea kwenye bajeti hii ambayo imepitishwa na Bunge, tunawatakia kila la kheri.

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri ya kuisimamia Wizara hii na kuhakikisha inatekeleza yale ambayo yako chini yake. Tunawashukuru sana. Pia Wabunge wote ambao mmepata nafasi ya kuchangia katika hoja hii, tunawashukuru kwa mawazo yote mliyoyatoa kama mlivyomsikia Mheshimiwa Naibu

Waziri, lakini pia Mheshimiwa Waziri wakieleza hapa kuhusu hoja zenu, pamoja na kwamba wataleta majibu lakini wameeleza kwamba yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyachangia wameyachukua kwa uzito na watayafanyia kazi. Kwa hiyo, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo kuna mambo mawili, la kwanza ni lile ambalo alichangia Mheshimiwa Charles Kajege leo asubuhi kuhusu madai ya aliyekuwa Jaji ama Jaji Mstaafu Mwesiumo ambaye mwaka 1998 alituhumiwa na mambo fulani hivi, lakini mwaka 2017 akaonekana kwamba hakuwa na hatia na 2018 akafungua kesi ya madai dhidi ya Serikali na kabla hukumu haijatoka Serikali na Mheshimiwa Jaji Mstaafu wakakubaliana kuhusu malipo na kiasi na ile hati ya makubaliano ikaenda kusajiliwa Mahakamani. Sasa Jaji amekuwa akifuatilia tangu mwaka huo mpaka sasa Serikali haijamlipa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa utaratibu wetu wa kawaida si kawaida ya Bunge na wala si utaratibu kwa Bunge ukiacha Serikali ambayo tumepewa kazi ya kuishauri lakini pia kuisimamia, si kazi ya Bunge kujadili kwa kweli majukumu ya mihimili mingine ukiacha Serikali, kwa sababu tumepewa kazi hiyo Kikatiba na kwa sababu jambo hili limeshatoka upande wa Mahakama liko upande wa Serikali na upande wa Serikali nyaraka zilizopo hapa mbele baada ya Mheshimiwa Mbunge kuniletea zinaashiria kumekuwa na mawasiliano kati ya taasisi hizi za Serikali, Wakili Mkuu wa Serikali, Wizara ya Fedha, Wizara ya Maliasili na Utalii na pia za Mahakama zipo na baadaye alipoona malipo yake yamechelewa akarudi tena kwa Wakili Mkuu wa Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali kwenye barua yake ya mwisho aliyomwandikia Mheshimiwa Jaji, yako maneno yanasema hivi; "Kwa kifupi suala lako linakwamishwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na siyo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali."

Waheshimiwa Wabunge, ni kazi yetu kuisimamia Serikali na kuishauri Serikali, jambo hili limechukua muda mrefu kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge huwa wanaleta hoja za wananchi wengine ambao pengine wamecheleweshewa madai yao sehemu mbalimbali

huwa wanayaleta kwenu na hili limeletwa kwa sura hii. Serikali lichukueni jambo hili mlipeni pesa zake maadamu mlikubaliana naye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tukisema hivi haimaanishi litaenda *endless* maana sasa inaweza ikaja tena mwakani Mheshimiwa Mbunge anaweza akasimama tena akasema lile jambo bado. Sasa naamini wakati huo ninyi pia jipangeni kwa sura ambayo Bunge halitaonekana linarejea jambo hili tena kulisikia kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge. Nafikiri kufikia hapo tutakuwa tumeshaelewana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ni hili ambalo Mheshimiwa Ole-Sendeka alikuwa akichangia hapa na bado tulikuwa tukielezana hapa, sasa nikawa bado sijafanya maamuzi na hata sasa inaniwia ngumu kidogo japokuwa kwa taarifa hizi alizozileta Mheshimiwa Ole-Sendeka hapa inaniwia vigumu sana kufikiri kwamba Serikali haijaunda timu hii.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo kwa sababu taarifa hii Serikali haijapelekewa rasmi, sasa hayo ni mimi ninasema, Serikali haijapelekewa rasmi kwa sababu kwa barua zilizopo alizoleta Mheshimiwa Ole-Sendeka zinaashiria kulikuwa na mawasiliano kati ya hizi Ofisi za Serikali. Sasa Serikali yenyewe iende ikajiridhishe na hayo kwa sababu sina sababu ya kusema barua hizi ni za kughushi kwa sababu nilimtuma Naibu Waziri pale nje na hajawapata hao wahusika wote, sijui kwa nini hajawapata wote lakini inaniwia ngumu kidogo kusema barua hizi kama ni za kughushi ama si za kughushi. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu sina uwezo huo wa kusema kama ni za kughushi ama sio za kughushi na maadamu kimeandaliwa kitu kama hiki sitaki kufikiri kwamba kiliandaliwa kutoka hewani. Serikali kafanyieni kazi madai ya Mheshimiwa Mbunge na mwone namna ambavyo hiyo... Hii Taarifa sina hakika kama mnayo nakala, kama hamna naweza kuwapa hii. Someni wale Wajumbe waliokuwemo mule kwa sababu picha zao zipo watazameni ili sasa

walete hii taarifa Serikalini ili ninyi sasa mchukue zile hatua ambazo huwa mnachukua kama Serikali linapotokea jambo kama hilo.

Mheshimiwa Ole-Sendeka, kwa hiyo kwa jambo hili tutaishia hapa kwa leo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, jambo la mwisho ni lile ambalo nilisema wakati tuko kwenye Kamati ya Matumizi huwa kanuni zetu huwa zinataka Kamati ya Bajeti ielekezwe wakati Bunge likiwa limerejea. Kwa hiyo, naielekeza Kamati ya Bajeti kulitazama jambo hili ambalo linaletwa kwenu na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Mtazame ule mgawanyo wa matumizi ya shilingi bilioni 19 kama hoja ya Kamati ilivyokuwa na upande wa Serikali watapata nafasi ya kueleza kwa upande wao na maamuzi yatafanyika wakati huo.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.16 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 4 Juni 2024, Saa Tatu Asubuhi)*